

MWINGILIANO TANZU KATIKA *MODERN* TAARABU-MIPASHO

MURIMI, Jackline Njeri

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMIFU KATIKA KISWAHILI,
IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA
KATIKA CHUO KIKUU CHA MOI, ELDORET.**

NOVEMBA, 2016

Ungamo la Mtahiniwa

Tasnifu hii kuhusu mwingiliano tanzu katika *Modern* Taarabu-Mipasho ni kazi yangu mwenyewe na wala haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kinginecho ili kutimiza

baadhi ya mahitaji ya shahada yoyote. Ni marufuku kuitolesha kazi hii nzima au sehemu yake yoyote bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi _____ Tarehe _____

MURIMI JACKLINE NJERI
SASS/D.PHIL/KIS/O3/13

IDHINI YA WASIMAMIZI

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya utahini kwa idhini na ridhaa yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo kikuu cha Moi, Eldoret.

Sahihi _____ Tarehe _____

DKT.SAMUEL MOSETI OBUCHI
IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA
CHUO KIKUU CHA MOI, ELDORET
S.L.P 3900,
ELDORET, KENYA.

Sahihi _____ Tarehe _____

DKT. MARK MOSOL KANDAGOR.
IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA
CHUO KIKUU CHA MOI, ELDORET
S.L.P 3900,
ELDORET, KENYA.

Tabaruku

Kwa babangu mpendwa mzee James Kirungii Murimi na mjukuu wangu Ivanna Njeri

Taraaji.

Shukrani

Ningependa kumshukuru Rabuka kwa kunipa pumzi na ari ya kuiandika hii kazi. Pili, natoa shukurani za dhati kwa wasimamizi wangu Dkt. Samwel Moseti Obuchi na Dkt

Mark Mosol Kandagor kwa uelekezi wao mufti ulioniwezesha kuifanya kazi hii. Asanteni sana kwa kuisoma kazi hii, kunihimiza nakunishauri bila ya kuchoka kila nilipohitaji ushauri wenu. Aidha, nawashukuru wahadhiri wangu wote na Chuo Kikuu cha Moi na hasa Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika kwa kunipa fursa ya kujijenga kitaaluma. Tatu, natoa shukurani zangu za kipekee kwa Dkt. Edwin Masinde Wanyonyi, mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa ukarimu wako na ari yako ya kuikuza lugha hii tukufu ya Kiswahili na kunikuza kitaaluma.

Kwa wazamifu wenzangu wa mwaka wa 2013; Angela Sawe, Samson Otwere, Nixon Migiro, Toboso Mahero, Isaac Kisiroche na David Bowen, nasema asanteni sana kwa ushirikiano, umoja, bidii na uchangamfu wenu. Mungu awakirikimie haja za mioyo yenu. Hatimaye ningependa kuwashukuru wanangu wapendwa Borris Lukorito Katasi, Rita Wanja Katasi na Brenda Waitherero Katasi kwa kunivumilia na kunihimiza kila nilipokuwa nikiifanya kazi hii. Mungu awazidishie neema mkaweze kufaulu maishani mwenu.

Ikisiri

Taarab ni muziki wenye umaarufu mkubwa katika Afrika Mashariki kwa zaidi ya karne moja. Muziki wa taarab umepata mabadiliko makubwa na kusababisha kuwepo kwa aina mbili kuu za Taarab: Taarab Asili na *Modern* Taarab. Utafiti huu ulihakiki mwingiliano tanzu katika Taarab-Mipasho. Malengo ya utafiti huu yalikuwa ni pamoja na kujadili mwingiliano tanzu kama unavyojitokeza katika miainisho ya tanzu za fasihi simulizi, kuchanganua miktadha mbalimbali ya mwingiliano tanzu katika muziki wa Taarab ya Mipasho na kutathmini dhima ya mwingiliano tanzu katika muziki wa Taarab ya Mipasho. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya mwingilianomatini iliyoasisiwa na Julia Kristeva (1960) baada ya kuizua kutokana na nadharia ya Mikhail Bakhtin ya Usemazano. Kutokana na nadharia ya mwingilianomatini, mtafiti ameitumia

kushughulikia mwingiliano tanzu katika Taarab-Mipasho. Nadharia ya umuundo ilishirikishwa ili kutoa mwelekeo zaidi kuhusu uanishaji wa tanzu za fasihi simulizi kama ilivyopendekezwa na Finnegan. Pia nadharia hii ilitumika katika kufafanulia uhuru na ubunifu wa mtunzi wa kuingiza vipengele vipya katika kazi. Utafiti huu ulichukua muundo wa kimaelezo. Ukusanyaji data ulihusisha usikilizaji, utazamaji na unukuzi daftarini wa nyimbo za Taarab ya Mipasho ili kupata mistari, vifungu vya maneno na stanza zilizobainisha mwingiliano tanzu. Sampuli ya utafiti ilikuwa nyimbo 32 za muziki wa Taarab ya Mipasho ambazo ziliteuliwa kumaksudi. Uchanganuzi na uwasilishaji wa data ulitolewa kwa njia ya maelezo ya kina yaliyohusisha udondoaji na ufafanuzi wa mistari, vifungu vya maneno na stanza zenye kudhihirisha mwingiliano tanzu kutoka kwa data asili. Matokeo ya utafiti yalibainisha udhaifu mkubwa katika mbinu zinazotumiwa kuainisha tanzu za fasihi simulizi. Aidha, mwingilianotanzu mkubwa ulibainika katika uwasilishaji wa muziki wa *Modern Taarab* ya Mipasho uliorejelewa. Muziki wa Mipasho ulitekeleza dhima ya kuelimisha, kuhifadhi utamaduni, kuburudisha pamoja na kudhihirisha upekee wa msanii miongoni mwa dhima nyingine. Utafiti huu unawachochea wahakiki wengine wa fasihi simulizi katika kufanya uchunguzi zaidi katika mitindo mingine ya nyimbo za *modern taarab* kwa misingi ya nadharia mbalimbali za fasihi. Aidha, kutokana na utafiti huu, ilitarajiwa kuwa watafiti wataweza kulinganisha na kulinganua mitindo tofauti ya taarab. Hatimaye, mtafiti anapendekeza tafiti zaidi zifanywe ili miongoni mwa mengine, kusuluhisha mgogoro kuhusu taarab ya mipasho, uanishaji wa tanzu za fasihi simulizi na waandishi katika miainisho ya utanzu wa nyimbo uwezekano wa kujumuisha nyimbo za taarab miongoni mwa vipera vya utanzu wa nyimbo katika awamu zote za usomi na uhakiki wa fasihi simulizi kwani muziki wa taarab na hasa mipasho bado unahitaji utafiti zaidi.

Abstract

Multigenerism in Modern Taarab Music-Mipasho

Taarab has been a very popular music genre within East Africa for more than a century. In recently times, Taarab music has undergone some drastic changes leading to two main branches which are *Taarab Asili* and Modern Taarab. The purpose of this study was to investigate multigenerism in Modern *Taarab-Mipasho* music. The objectives of this study are: to critic the mixing of various genres as portrayed in the classification of oral literature genres, to analyze the mixing of various oral literature genres in the *Taarab-Mipasho* and to evaluate the place of interdependence of genres in *Taarab-Mipasho*. The study was guided by the theory of intertextuality advanced by Julia Kristeva in the sixties after developing it from the theory of Dialogism advanced by Mikhael Bakhtin. In this research, intertextuality was used to tackle interactive style of genres in *Taarab-Mipasho*. Structural Theory was incorporated to shed more light on classification of genres in oral literature as recommended by Finnegan and also to determine the extent at which freedom

and creativity were displayed by artists through the involvement of others components in their work. The study adopted a descriptive design. Data collection was by way of observation whereby selected songs were viewed, listened to with specific attention to lines, words and stanzas portraying genres' interaction. The targeted sample for this study was 32 *Taarab-Mipasho* songs which were selected purposively. Data analysis and presentation were done by way of detailed word description inferred from the lines, words and stanzas displaying the interaction of genres from the raw data. The research findings indicated a great weakness in the methods used in classifying genres in oral literature. Also, multigenerism was very evident in the Modern *Taarab-Mipasho* involved in this study. *Mipasho* songs played the role of educating, conserving cultural heritage, entertaining, and displaying artists' uniqueness amongst others. Finally, the research recommended further research to resolve issues on classification of oral literature genres and the possibility of including of taarab songs in the songs genre in the classification of oral literature genres at all levels of learning. Also, more studies should be carried out on other styles of modern Taarab using other theories of oral literature and by way of comparing and contrasting the different styles of modern taarab.

Yaliyomo

Ungamo la Mtahiniwa.....	ii
Tabaruku.....	iii
Shukrani.....	iv
Ikisiri.....	v
Abstract.....	vi
Yaliyomo.....	vii
Ufafanuzi wa Istilahi.....	x
SURA YA KWANZA.....	ii
1.0 Utangulizi.....	1
1 .1 Usuli wa Suala la utafiti.....	1
1.2 Utanzu wa Modern Taarabu-Mipasho.....	9
1.3 Suala la Utafiti.....	14
1.4 Malengo ya Utafiti.....	15

1.5 Nadharia Tete.....	15
1.6 Umuhimu wa Utafiti.....	16
1.7 Nadharia za Utafiti.....	16
1.7.1 Nadharia ya Mwingilianomatini.....	17
1.7.2 Nadharia ya Umuundo.....	19
1.8 Misingi ya Uteuzi wa Suala la Utafiti.....	22
1.9 Upeo wa Utafiti.....	23
1.10 Yaliyoandikwa kuhusu Taarabu na Mwingilianomatini.....	24
1.11 Masuala ya Kimaadili.....	32
1.12 Mbinu za Utafiti.....	33
1.13 Muundo wa Utafiti.....	33
1.14 Ukusanyaji wa Data.....	34
1.15 Usampulishaji.....	35
1.16 Vifaa vya Utafiti.....	36
1.17 Uchanganuzi wa Data.....	37
1.18 Hitimisho.....	38
SURA YA PILI.....	39
UAINISHAJI WA TANZU ZA FASIHI SIMULIZI YA KISWAHILI.....	39
2.0 Utangulizi.....	39
2.1 Misingi ya Uainishaji wa Tanzu za Fasihi Simulizi ya Kiswahili.....	39
2.1.1 Majina ya Tanzu au Vipera.....	40
2.1.2 Mianza ya Tanzu.....	40
2.1.3 Miishio ya Tanzu.....	40
2.1.4 Lugha iliyotumika.....	41
2.1.5 Maudhui.....	41
2.1.6 Jinsi ya Utendaji.....	42
2.1.7 Watendaji/Wasanii.....	42
2.1.8 Ala ya Utendaji.....	43
2.1.9 Msingi wa Wakati.....	44
2.1.10 Msingi wa Mahali Maalumu.....	44
2.2 Mwingiliano tanzu katika Uainishaji wa Tanzu za Fasihi Simulizi ya Kiswahili.....	45
2.3 Nyimbo / Ushairi Simulizi wa Kiswahili.....	52
2.4 Hitimisho.....	56
SURA YA TATU.....	57
MIKTADHA MBALIMBALI YA MWINGILIANO TANZU KATIKA MODERN TAARABU MIPASHO.....	57
3.0 Utangulizi.....	57

3.1 Mwingiliano wa Utanzu <i>Modern</i> Taarabu- Mipasho na Maigizo.....	57
3.2 Mwingiliano tanzu kati ya <i>Modern</i> Taarabu - Mipasho na Utanzu wa Semi.....	68
3.2.1 Utanzu wa Semi- Kipera cha Methali.....	68
3.2.2 Utanzu wa Semi- Kipera cha Nahau.....	72
3.2.3 Utanzu wa Semi- kipera cha Mafumbo.....	79
3.2.4 Utanzu wa Semi- Kipera cha Lakabu.....	90
3.3 Mwingiliano kati ya <i>Modern</i> Taarabu-Mipasho na Ushairi Simulizi-Majigambo.....	96
3.3.2 Fomula ya Ufunguzi na Fomula ya Kufunga.....	108
3.3.3 Kipera cha Khurafa.....	114
3.4 Mwingiliano kati ya <i>Modern</i> Taarabu-Mipasho na Utanzu wa Mazungumzo- Kipera cha Mawaidha.....	119
3.5 Aina nyingine za Nyimbo katika <i>Modern</i> Taarabu- Mipasho.....	124
3.5.1 Sindimba katika <i>Modern</i> Taarabu-Mipasho.....	124
3.5.2 Sebene katika <i>Modern</i> Taarabu-Mipasho.....	126
3.5.3 Chakacha katika <i>Modern</i> Taarabu-Mipasho.....	127
3.5.4 Goma katika <i>Modern</i> Taarabu-Mipasho.....	128
3.5.5 Lelemama katika <i>Modern</i> Taarabu-Mipasho.....	129
3.5.6 Bembelezi katika <i>Modern</i> Taarabu -Mipasho.....	130
3.5.7 Ngonjera katika <i>Modern</i> Taarabu -Mipasho.....	131
3.6 Malumbano ya Washindani katika <i>Modern</i> Taarabu-Mipasho.....	136
SURA YA NNE.....	143
DHIMA YA MWINGILIANO TANZU KATIKA <i>MODERN</i> TAARABU-MIPASHO.....	143
4.0 Utangulizi.....	143
4.1 Kupima Ubingwa wa Mhusika.....	143
4.2 Kutumbuiza na Kuchangamsha Jamii.....	144
4.3 Kuhifadhi na Kuendeleza Utamaduni.....	145
4.4 Kuleta Uhalisia.....	145
4.5 Kuleta Mtiririko wa Ujumbe.....	146
4.6 Kuimarisha Mamlaka ya Matini.....	147
4.7 Kufikirisha na Kumakinisha.....	147
4.8 Kudhihirisha Upekee wa Mhusika.....	148
4.9 Kupanua Uwanda wa Kina cha Maudhui.....	149
4.10 Kujitambulisha kwa Fanani.....	150
4.11 Kukuza na Kuimarisha Lugha.....	151
4.12 Kuihamasisha Jamii.....	151
4.13 Nyenzo ya Kuelewa Hisia na Mitazamo ya Watu.....	152
4.14 Hitimisho.....	154

SURA YA TANO.....	156
MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO.....	156
5.0 Utangulizi.....	156
5.1 Muhtasari wa Tasnifu.....	156
5.2 Matokeo ya Utafiti.....	160
5.2.2 Miktadha Mbalimbali ya Mwingiliano tanzu katika <i>Modern</i> Taarabu-Mipasho	161
5.2.3 Dhima ya Mwingiliano tanzu katika <i>Modern</i> Taarabu- Mipasho.....	164
5.3 Mapendekezo.....	165
MAREJELEO.....	166
KIAMBATISHO: NYIMBO ZA TAARABU.....	171

Ufafanuzi wa Istilahi

Modern Taarabu: Mojawapo wa aina mbili kuu za Taarabu. Pia ina maana ya Taarabu ya Kisasa. Muziki wa *Modern Taarabu* huchezwa kwa mtindo unaoakisi uchezaji wa densi za kisasa, hutumia ala chache na za nguvu, huhusisha waimbaji wa kike na kiume na kucheza kwenye kumbi za burudani na kushughulikia uwanda mpana wa maudhui tofauti na ilivyokuwa kati ka Taarabu Asili. Muziki huu umeweza kukubalika na kupata umaarufu mkubwa sana na kuwa na wafuasi wengi wenye asili tofauti sehemu mbalimbali ulimwenguni.

Mipasho: Aina ya *Modern Taarabu* yenye kumaanisha ‘kueleza au kupasha habari nzito kwa njia ya kimapumbo’. Kupasha aidha humaanisha kueleza habari kwa njia ya matusi, majibizano au kwa malumbano.

Mwingiliano tanzu: Dhana ya mwingiliano tanzu imetumika kurejelea mfululizo wa maneno, mawazo na vifungu vya habari katika kazi za kifasihi ambayo ni pamoja na tanzu na matini mbalimbali zilivyoingiliana na mbinu zingine za kisanaa katika kuboresha uwasilishaji wa ujumbe katika nyimbo za Taarabu zilizorejelewa.

Sidii: Kifaa maalumu cha kuhifadhia nyimbo. (Kwa lugha ya Kiingereza-“CD” ni Compact Disk).

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi

Taarabu ni muziki wenye umaarufu mkubwa katika Afrika Mashariki kwa zaidi ya karne moja. Hata hivyo, muziki wa Taarabu umepata mabadiliko makubwa katika miaka ya tisini kutokana na ukuaji na ufanisi mkubwa wa *Modern* Taarabu na kusababisha kuwepo kwa aina mbili kuu za Taarabu: Taarabu Asili na *Modern* Taarabu. Mabadiliko katika muziki huu yanafungamana na maisha na maendeleo ya jamii ambayo ndiyo chanzo cha fasihi. Sura hii ya kwanza imeshughulikia usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, nadharia tete na umuhimu wa utafiti. Aidha, imeshughulikia nadharia ya utafiti na upeo wa utafiti.

1.1 Usuli wa Suala la utafiti

Neno Taarabu lina asili yake katika lugha ya Kiarabu na hunyambuliwa hivi: *Taariba*; *Yatiribu*; *Taraba*. Maneno haya yote yana maana ya ‘*raha*’, ‘*starehe*’, *furaha*, ‘*burudani*’ au ‘*kuingia ndani ya muziki*’ (Kiekgaard, 1996; Askew, 2002). Nyimbo za Taarabu huimbwa kwa lengo la kutumbuiza na kuwasilisha maudhui kupitia aghalabu kwa matumizi ya mafumbo. Kinge’i na Kisovi (2005) wanasema kuwa nyimbo za Waswahili za Taarabu huimbwa katika sherehe za kuwakaribisha wageni, harusini na kwenye mikutano ya kisiasa miongoni mwa sherehe zingine katika jamii hiyo.

Kuna mitazamo miwili kuhusu asili ya muziki wa Taarabu katika Afrika Mashariki. Mwamzandi (2002) anafafanua kwamba, mitazamo hii inatagemea wanaosema. Mtazamo mmoja unashikilia kuwa asili ya Taarabu ni Misri. Kwa mujibu wa Khatib (1992) na Askew (2002), asili ya Taarabu ni Sultan wa Zanzibar Seyyid Barghash (1870-1888) ambaye aliwaalika wanamuziki wa Taarabu kutoka Misri ili waje wamchezee

muziki wao yeye na watu wake katika jumba la kifalme (Beit-el-Ajaib). Baadaye alimpeleka Misri mwanamuziki Mohammed Ibrahim ili aweze kujifunza ustadi wa nyimbo za Taarabu na pindi tu aliporejea Zanzibar, alipanda mbegu ya Taarabu Afrika Mashariki. Mohammed Ibrahim aliunda chama cha watribu cha nyumba ya mfalme. Sultan Seyyid Bargash alitimiza mahitaji yote ya kikundi hiki na hivyo kikundi hiki hakikuruhusiwa kucheza nyimbo zake kwingineko isipokuwa katika ikulu ya mfalme pekee. Wanachama wengine wa kikundi hiki ni pamoja na Ajmi Bin Abdalla, Mussa Bulushi ambaye alikuwa mwalimu wa Siti Binti Saad, Shaib Abeid na Mohammad Llyas miongoni mwa wengine (Khatib 1992). Nyimbo zao zote ziliimbwa kwa Kiarabu. Mtazamo huu wa asili ya Taarabu unajikita katika imani kuwa kila kilicho kizuri kililetwa kutoka nje ya Afrika.

Hata hivyo, kuna mtazamo wa pili unaoshikilia kuwa Taarabu ni sanaa iliyotokana na mwingiliano wa utamaduni wa Waswahili na tamaduni nyingine mbalimbali (Graebner, 1990; Kirkegaard, 1996; Askew, 1997; Ntarangwi, 1998; Khamis, 2001). Aidha, muziki wa Taarabu umeathiriwa pakubwa na utamaduni wa Kihindi kama inavyodhihirika katika miundo ya baadhi ya tamaduni maarufu za Waswahili. Hili linadhihirika katika filamu za Kihindi ambazo huakisi msingi thabiti wa toni za baadhi ya nyimbo za Taarabu zinazovutia sana mjini Mombasa (Beez na Kolbusa, 2003). Kwa mujibu wa watafiti hawa, wengi wa wageni kutoka Uarabuni, Uchina, Misri na Indonesia waliozuru pwani ya Afrika Mashariki (Zanj) waliathiriwa na utamaduni wao ambao ni pamoja na muziki na ala za kuchezea muziki huo. Baada ya kutambua kuwa wangepumzika katika pwani hii kwa muda, walianza kujitumbuiza kwa nyimbo zao na wenyeji wa pwani ile wakapata kutumbuizwa pia kwa ala na muziki huo wa kigeni. Kirkegaard (1996) anaendelea kusema kuwa hapo ndipo muziki wa Taarabu uliibuka kutokana na mtangamano kati ya utamaduni wa Kibantu na ule wa Kiislamu. Kwa mujibu wa mtazamo huu, nyimbo za

Taarabu zina asili yake katika Afrika Mashariki na hasa pwani ya Kenya. Mji wa Lamu ambao umokaskazini mwa Kenya ndio unaohusishwa na kitovu cha nyimbo za Taarabu kabla ya nyimbo hizi kusambaa na kuenea kwingineko mathalan visiwa vya Pemba. Hivyo basi, Taarabu ilikua katika Afrika Mashariki kutokana na mwingiliano wa mitindo ya miziki ya kiasili na miziki ya watu wenye tamaduni za Ulaya, Kiajemi na Marekani waliotagusana na Waswahili.

Akitoa mchango wake kama mojawapo wa wafuasi wa mtazamo huu, Ntarangwi (1998) anashadidia kuwa nyimbo za Taarabu zina uhusiano mkubwa na muziki wa Kibangala ambao kwa muda mrefu ulichezwa na kuwa maarufu kisiwani Lamu kabla ya Taarabu kuanzishwa kisiwani Zanzibar. Mwanachama na mwanamuziki wa kikundi cha Taarabu Zanzibar; *Ikhwani safaa*, Sheikh Abeid aliyeishi kati ya miaka ya 1890-1974 alikiri kufunzwa nyimbo za Taarabu kwa mitindo ya Kilamu (Topp, 1992). Mtazamo huu unashikiliwa na wengi wa wasomi wa Kiafrika ambao kwa pamoja wanaendeleza dhana kuwa hata Afrika imekuwa na utamaduni mzuri ambao umepanuka kwa kuingiliana na kuathiriana na tamaduni zingine ulimwenguni. Muziki wa Taarabu umekuwa na historia ya kuwa na aina nyingi za Taarabu kama vile Taarabu ya Zanzibar, Taarabu ya Dar-es-Salaam, Taarabu ya Mombasa na Taarabu ya Tanga. Mpaka leo mabadiliko katika uwasilishaji wa Taarabu yangali yanaendelea. Taarabu imekuwa pia ni ya kucheza na si kusikiliza ujumbe tu kama ilivyokuwa zamani. Hivyo kuna uwezekano kuwa muziki wa Taarabu katika Afrika Mashariki ulikuwa na mitindo mingi tofauti ya uchezaji na majina tofauti kadri ulivyokua na kuenea.

Graebner (1990) anaeleza kuwa kuna aina mbili za Taarabu asili. Kwanza ni Taarabu ya wanawake ambayo hadhira yake ni wanawake pekee. Taarabu hii huchezwa kwa mtindo wa kiasili wa ngoma ya wanawake wa Kiswahili. Aghalabu uchezaji wa Taarabu hii ni kwenye harusi. Pia, hujulikana kama *Taarabu ya Kiswahili*. Aina ya pili ya Taarabu ni ile

ijulikanayo kama *Taarabu ya Wanaume*. Taarabu hii huhusisha wanaume pekee katika uchezaji wake na huchezwa vile vile kwenye harusi kama ilivyo ile ya wanawake. Jina lingine la aina hii ya Taarabu ni *Taarabu ya Kiarabu* kutokana na namna ilivyokopa mitindo mingi ya miziki ya asili ya Kiarabu.

Utendaji wa ushairi miongoni mwa Waswahili una historia ndefu mno inayokisiwa kuwepo katika karne ya kumi na sita wakati ambapo kumbukumbu za utendaji wa sanaa ya Waswahili ilichipuka. Askew (1997) anasema kuwa Waswahili wameainisha ushairi wao katika miainisho mitatu: *shairi* (shairi lenye mishororo minne katika kila ubeti), *utenzi* (shairi refu lenye mishororo mitatu au minne katika kila ubeti na ambalo huwa limetungwa kama utendi) na *wimbo* (shairi lenye mishororo mitatu lililotungwa ili liimbike). Taarabu imeainishwa katika aina ya tatu ya wimbo wenye mishororo mitatu katika kila ubeti na mshororo wa nne ujulikanao kama *kiitikio*, *kipokeo*, au *kibwagizo*. Hata hivyo, kwa mujibu wa wanajadi wa Taarabu, kuna Taraab aina moja tu ambayo hufuata mtindo wa mapigo ya taratibu huku wasikilizaji wake wakiwa wametulia na kusikiliza wakiwa wameketi kitako. Tofauti na maoni haya ni yale ya wanamapinduzi ambao wanasema kuwa kuna Taarabu ya sasa ambayo imeiga midundo mipya na mabadiliko katika uchezaji ngoma na mavazi ya wasanii. Hili limesababishwa na haja ya muziki huu kubadilika kadri wakati ulivyozidi kubadilika kiuchumi, kisiasa na kijamii (Khatib, 1981).

Khamis (2005) anaeleza kuwa kuna mihula minne katika historia ya Taarabu. Muhula wa kwanza ni kuanzia mwaka wa 1905 hadi 1920. Huu ndio wakati ambapo Sultan Seyyid Bargash alikuwa mtawala wa Zanzibar. Taarabu iliimbwa katika ikulu yake kwa lugha ya Kiarabu kama ilivyokuwa imeigwa kutoka Misri. Ntarangwi (2001) anasema kuwa muziki wa Taarabu uliletwa Zanzibar mnamo 1870 na kikundi cha wanamuziki kutoka Misri kilichokuwa kimealikwa na Sultan Barghash kuimba ikuluni mwake. Katika

kipindi hiki, Zanzibar ilikuwa ngome muhimu ya kibiashara chini ya utawala wa Kiarabu wa Sultani wa Oman. Nyimbo za Taarabu katika nyakati hizo zilitumiwa katika kuwatumbuiza viongozi wenye asili ya Kiarabu, wafanyibiashara na mabepari.

Sultan Sayyid Bargash aliishi maisha ya anasa na alipenda raha na starehe sana. Baada ya kufanikiwa katika wajibu wake huu, Mohammed alirudi ikulini mwa Barghash, na baadaye akawa mshairi wa kibinafsi wa Barghash. Mohammed pia aliwafunza marafiki zake kucheza ganuni, ujuzi walioutumia baadaye walipoanzisha kikundi cha kwanza cha Taarabu kilichojulikana kama *Nadi Ikhwani Safaa*, mwaka 1905 kule Zanzibar (Topp 1992).

Ntarangwi (2001) anaeleza kuwa kutoka Zanzibar, Taarabu ilisambaa kwingineko katika mwambao wa Afrika Mashariki ikiwemo Mombasa na Lamu. Kea (2006) anadahili kuwa maudhui katika nyimbo za Taarabu zilizoimbwa katika ikulu ya mfalme yalihusu kuomba dua ya mapenzi kati ya Sultan na Malkia, kumwomba Sultan maisha marefu katika utawala wake, kusifu maumbile huku nyimbo zingine zikiimbwa kwa nia ya kumchangamsha na kumchekesha mfalme. Wakati ule, watu wa tabaka la juu walivaa mavazi yao nadhifu na kuketi vitini wakingoja kutumbuizwa na kikundi hiki cha *Nadi Ikhwani Safaa* (Owen, 2010).

Muhula wa pili unahusisha kipindi cha mwaka wa 1920 hadi 1940. Katika muhula huo, lugha ya Kiswahili ilitumika katika nyimbo za Taarabu baada ya enzi ya utawala wa Sultan Barghash kufikia kikomo. Mabadiliko ya muziki wa Taarabu yalipelekea kubadilika kwa hadhi ya nyimbo hizi kutoka kuwa nyimbo za watu wa tabaka la juu katika jamii hadi kuwa nyimbo za wachochole. Mabadiliko haya yalikusishwa na mhusika wa Taarabu aliyesifika sana Zanzibar na nchi za nje, Siti binti Saad (Askew, 2002). Utendaji wa Taarabu ulianza kuwafikia watu wengine mbali na watawala na

matajiri baada ya kuwepo kwa utendaji hai wa bendi mbele ya umma na pia kuwepo kwa mbinu ya kurekodi nyimbo hizi. Watu wa tabaka la kati waliweza kuzinunua na kuzisikiza nyimbo za Taarabu. Huu ndio wakati ambao Siti Binti Saad, aliyeishi miaka ya 1880-1950, alianza kuimba Taarabu akitumia lugha ya Kiswahili kule Zanzibar na Tanzania.

Siti alifanikiwa kuimba nyimbo nyingi sana za Kiarabu na Kiswahili katika santuri na sahani. Khamis (2002) anadahili kuwa Taarabu wakati huo iliweza kuenea hata zaidi kwani Siti alikuwa na uwezo wa kuimba kwa lugha za Kihindi, Kiarabu na Kiswahili. Uwezo huu wa kuchanganya lugha tofauti tofauti katika uimbaji wake uliweza kumpa Siti sifa, umaarufu na hadhi visiwani na kulikokuwa na utamaduni mseto wa Kiarabu na Kiswahili. Hii ndiyo sababu iliyomfanya Khatib (1992) kudai kuwa kwa Waafrika wengi, Taarabu kwao ilianza na Siti. Aidha, Siti alianzisha aina ya Taarabu iliyojulikana kama *Womens' Taarabu* ambayo ilikopa sana kutoka utamaduni wa nyimbo za Waswahili na za Kihindi. Siti aliifanya Taarabu kuwa ya Kiafrika kwa kuimba kwa Kiswahili na kuitoa nje ya kasri la kifalme kwa kuiwasilisha kwa watu wa kawaida (Owen, 2010).

Muhula wa tatu unajikita katika mwaka wa 1950 hadi 1960 ambapo Taarabu iliweza kuwa huru zaidi kutokana na kuwepo kwa upeperushaji wake katika mawimbi ya redio mbalimbali. Muziki wa Taarabu uliweza kusambaa sana katika awamu hii. Muhula wa nne ulikuwa kuanzia mwaka wa 1970 hadi sasa. Katika kipindi hiki, kumekuwa na ufanisi mkubwa zaidi wa Taarabu uliochangiwa na kuwepo kwa runinga, video, tepurekoda, mtandao miongoni mwa vifaa vingine vya kisasa vya kielektroniki. Taarabu imeweza kuenea hadi Msumbiji, Afrika Mashariki, sehemu za Maziwa Makuu kama vile Congo, Afrika Kaskazini, Magharibi na Mashariki, Bahrain, Yemeni, Saudi Arabia, Uturuki na Bara Hindi. Isitoshe, Khamis (2002)

anaongezea kuwa mabadiliko katika uimbaji na utendaji yanayoonekana katika muziki wa *Modern* Taarabu yamesababishwa na haja ya kuubadilisha muziki huu ili uweze kuambatana na mitindo na aina ya muziki wa kisasa.

Utendaji wa Muziki wa Taarabu umekopa mengi kutoka tanzu nyingine za muziki kama ilivyojadiliwa na watafiti wengine wakiwemo Campbell (1976, 1983) na Franken (1986). Katika utendaji wake, Taarabu imeingiza utendaji wa tanzu zingine za Waswahili kama vile *vugo*, *msondo*, na *chakacha*. Wamitila (2003) katika kielelezo chake cha *Ngoma za Waswahili* ameonyesha *vugo* kama ngoma katika jamii ya Waswahili ambayo huchezwa na wanawake waliokomaa. Hii ni ngoma inayochezwa na wanawake wa Kibajuni.

Kama ilivyo *vugo*, *msondo* ni utanzu uliopata jina lake kutokana na ngoma ya kitamaduni inayotumika katika muziki huu. Katika mji wa Mombasa na Pemba, wanaume kwa wanawake huchezwa ngoma ya *msondo* katika sherehe za harusi (Wamitila, 2003). Watendaji wa *msondo* huunda nusu duara wakitazamana na wacheza ngoma huku wakiacha nafasi baina yao. Mistari mifupi mifupi ya nyimbo huimbwa kwa kurudiwarudiwa huku wanawake katika hadhira wakicheza kwa mtindo wa *msondo* pamoja na wa *chakacha*. Wapiga ngoma huzipiga kwa mtindo wa mapigo kumi na mbili. Chakacha nayo ni ya pili kwa umaarufu baada ya Taarabu katika muziki wa Waswahili. Huchezwa na wasichana usiku kucha kama kilele cha sherehe za harusi ya Waswahili. Katika *chakacha*, ngoma ya *msondo* huwa ala muhimu miongoni mwa zingine kama *vumi* na *chapuo*. Ni nadra sana kwa tanzu hizi tatu kucheza kila moja kivyake bila kuingiliana, suala ambalo linachangia kuwepo kwa mwingiliano wa tanzu mbalimbali za nyimbo.

Kando na kuhusisha tanzu hizi tofauti za nyimbo za Waswahili, Taarabu huhusisha tanzu za nyimbo za tamaduni tofauti tofauti kutoka janibu zingine kama vile Amerika ya Kusini, Bara Hindi na mitindo ya Kiarabu katika utendaji wake. Hata hivyo mwingiliano tanzu kati ya nyimbo hizi kutoka tamaduni tofauti na zile za Taarabu ni suala ambalo halijashughulikiwa katika tafiti za Taarabu ambazo zimewahi kufanywa hapo awali. Pia suala la namna tanzu nyingine zilivyoingiliana na *Modern* Taarabu-Mipasho bado ni suala ambalo halijashughulikiwa na tafiti nyingine nilizopitia katika mapitio ya maandishi.

1.2 Utanzu wa Modern Taarabu- Mipasho

Jamii inapobadilika kiwakati, fasihi pia hubadilika kwa sababu chimbuko lake ni mazingira halisi ya jamii. Hii ndiyo hali waliyokumbana nayo wasanii wa muziki wa taarabu pale walipoamua kuipa Taarabu Asili kisogo na kujiingiza katika *Modern* Taarabu. Askew (2000) anasema kwamba mwamko mpya wa kujitegemea na ushindani uliibuka katika jamii ambapo waliokuwa makini waliona umuhimu mkubwa wa Taarabu katika kujikuzi kiuchumi. Wasanii wa Taarabu walitalii uwezekano wa kubadilisha mtindo wa Taarabu kutoka hali yake asili ya muziki mwororo wenye kutumia vyombo vichache na wenye kuwasilisha hisia za kimapenzi. Badala yake waliona haja ya kuhusisha ala chache tena zenye nguvu zaidi, kuongeza kasi ya uchezaji wake na kiwango cha mvuto wake ili kuivutia hadhira. Mabadiliko hayo aidha yalikusisha kuwepo kwa kikundi cha idadi ndogo ya waimbaji na wachezaji wa ala. Vivyo hivyo, mtindo wa uchezaji wa ala ulibadilika kutoka mtindo wa kitamaduni hadi wa Kimagharibi na hivyo kubuni mtindo mpya wa kucheza ambao ulikuwa nadra sana katika nyimbo za Taarabu asili.

Licha ya kutafuta kipato, uhamaji wa wasanii wa Taarabu kutoka Taarabu asili pia ulisababishwa na kudidimia kwa Taarabu ya Wanawake. Kama anavyosema msimamizi wa mhusika mkongwe wa taarabu Bi Kidude, gharama ya juu ya kuwakodi waimbaji ndiyo iliyochangia Taarabu ya wanawake kufa na wasanii wake kujiunga na bendi za *Modern* Taarabu. Kwa mujibu wa Khamis (2001) kujitenga kwa *Modern* Taarabu kulisababishwa na haja ya wasanii wa Taarabu kuboresha maisha yao kupitia kwa kipato bora anachorejelea kama *maslahi*. Wakati mwingine wasanii walilazimika kuanzisha bendi au makundi yao na mitindo mipya yenye kuvutia ili kujihakikishia kipato (*maslahi*) pale walipokosa.

Taarabu asili ni ya mwendo wa polepole, nyororo, yenye kudhihirisha hisia za kimapenzi na isiyo na lengo la biashara. Hivi sasa Taarabu iliyochipuka ya *Modern* Taarabu, tofauti na Taarabu asilia inayotumia ala kama vile udi, ganuni, violini, gitaa ya stima na zeze chini, violini kubwa na kodiani, *Modern* Taarabu hutumia gita ya stima, kinanda, zeze kubwa kwa sababu ya kutoa muziki uliolainika (Khamis, 2001). *Modern* Taarabu vile vile huhusisha wanaume kadhaa katika kutunga nyimbo, kucheza ala kama vile kinanda, gitaa, ala za besi huku wanawake wakiongoza kuimba muziki pamoja na kwaya.

Muziki wa *Modern* Taarabu una sifa zifuatazo : ufaraguzi, mawanda na uwezo wa kubadilika ambao huukubalia kutumia vyombo mbalimbali vya kishairi, sifa inayoubainisha na nyimbo zingine kutoka Afrika Mashariki. Aidha, Khamis (2001) anaeleza kuwa muziki wa *Modern* Taarabu kwa kiwango kikubwa umekopa mengi kutoka muziki wa Taarabu asili kama vile; miondoko ya mwili ya haraka, minenguo ya viuno na makalio hasa kwa wanawake ambayo ni ishara tosha ya uhuru kamili walionao waimbaji mbalimbali na hali ilivyokuwa katika Taarabu Asili iliyozingatia utamaduni wa Waswahili uliodhibiti alivyohusika mwanamke katika utendaji wake hadharani. Aidha,

kuongezea mbinu ya majazi kwa matumizi ya msamiati kama vile 'pajero', 'US dollar', 'mobile telephone' (kisimu cha mkono), dhahabu, nguo za bei ghali na viatu na usawiri wa wanawake ambao daima huwa tayari kutongozwa na watalii au wenyeji na uchanganyaji na uhamishaji ndimi vimechangia pakubwa katika kufaulisha muziki huu wa *Modern* Taarabu. Isitoshe, mauzo na utendaji hadharani umeongezeka. *Modern* Taarabu pia hubainika kupitia kwa mabadiliko katika mtindo wa waimbaji na kiitikio.

Bendi za *Modern* Taarabu huimba nyimbo zao katika kumbi mbalimbali za burudani na starehe Beez na Kolbusa, (2003). Uchache wa ala za muziki na idadi ya waimbaji katika *Modern* Taarabu hukusudiwa kuiwezesha bendi kusafiri kwa urahisi na kwa mapana na kuongezea kiasi cha faida wanayopata. Hadhira katika *Modern* Taarabu huwa tendi kwani hutarajiwa kucheza muziki huu unapoimbwa.

Kwa mujibu wa Traore (2004) muziki wa Taarabu umepata mabadiliko makubwa katika miaka ya tisini kutokana na ukuaji na ufanisi mkubwa wa *Modern* Taarabu. Kuanzia miaka ya 1980, hasa baada ya vita vya Tanzania dhidi ya utawala wa Idi Amin Uganda, uchumi wa Tanzania ulianza kudorora kwa kasi sana na kuanza kuelekea kwa mfumo wa kibepari. Polepole, ilianza kubainika kuwa chama tawala kilipoteza mamlaka yake juu ya asasi zake zote na hasa zile za kitamaduni ambazo zilikuwa zimesimamia utendaji wa nyimbo za Taarabu. Katika makala yake, Traore (2004) amejadili kwa mapana uwiano na jinsi nyimbo za Taarabu zilivyoathiriana na kanga. Pia alizungumzia suala la uriwaya kama linavyojitokeza katika muziki wa Taarabu. Mabadiliko haya ya mtindo wa Taarabu pia yalimaanisha kuwa hadhira yake ingekuwa mpya na hali sasa ingechukua mwelekeo wa kuhudumia umma zaidi na wala sio kuwaburudisha watawala na matajiri kama ilivyokuwa hapo awali katika muziki wa Taarabu asili.

Watunzi wa *Modern* Taarabu wanafahamu namna nyimbo zao zilivyobadilika na kuathiri hisia za hadhira yao kama anavyobainisha Traore (2004:79)

[Nyimbo], za sasa ni very transparent, wazi, zamani walikuwa wanaficha wanatumia nyimbo za mafumbo. Unaweza kumsifu ndege wako vile anavyoruka na kutua na vipi kumbe unamsifu mtu. Sasa kikubwa nilichokigundua mimi ni kwamba zamani walikuwa wanaficha walikuwa wanatumia lugha ya sitiari. Lakini siku hizi wanaweka waziwazi kuelezea kila kitu.

Mipasho ni kipera cha *Modern* Taarabu, jina ambalo linamaanisha ‘nyimbo zenye urushianaji wa matusi na mabishano kupitia kwa utendaji wake’ (Khamis, 2002). Matusi yanayoendelezwa katika nyimbo za *Modern* Taarabu-Mipasho japo kwa mafumbo yameonekana kuwakera wafuasi wa Taarabu asili ambao wanaona hali hii kama upotovu wa kimaadili na heshima iliyosisitizwa katika Taarabu Asili (Traore, 2004). Ufafanuzi mwingine ni kuwa jina *mipasho* linatokana na kitenzi cha Kiswahili *pasha*, chenye maana ya ‘kusababisha kupata’, ingawa katika muktadha huu kile anachopata mtu ni matusi na kejeli! Beez na Kolbusa (2007:36) anatoa maana ya mipasho kwa kusema hivi:

(...) ni kupashana kwa kinamna fulani, kwamba nataka kumpasha mtu jambo hili pasipo kuleta ugomvi. Ila tu watu wajue kwamba nampasha nani. ...mipasho ni kitu ... cha kupeana neno laivu lakini pasipo kuweza wewe kulijibu kwa sababu kitu ambacho anakupashia wewe pale katumia redio huwezi kumwambia kwa nini unanifanyia fumbo kwa neno hili.

Matusi hayo yamesisitizwa zaidi na matumizi makubwa na ya kuvuta nadhari za kimapenzi kupitia kwa minenguo ya viuno na miondoko ya viungo vya wanawake wanapokuwa wanacheza nyimbo za mipasho zinapoimbwa. Muziki huu hunuiwa kuwasilisha masuala ambayo ni vigumu kuyawasilisha katika hali ya kawaida. Hili linadhihirika katika maelezo yafuatayo ya Beez na Kolbusa (2007:36)

(...) kwa sababu mipasho ni fumbo sasa fumbo unapoamua kufanya fumbo ina maana nyimbo za zamani mipasho ilikuwa ni fumbo sasa siku hizi wanapasua kabisa ‘nitakung’oa jino, nitakufanyia nini, mwanamke gani shepu huna?! Ukijitazama kama ni wewe ndiyo shepu huna, kwa hiyo unaelewa kwamba hiyo nyimbo nimeambiwa mimi. Unawaambia watu kitu ambacho kinakukera lakini

hawana ushaidi na hawawezi kukushtaki kwa sababu wewe umecheza muziki wewe unajihisi hiyo ni hiyari yako umeshapashwa.

Hata hivyo ufafanuzi mwafaka wa mipasho ni kama ulivyotolewa na Beez na Kolbusa (2007) ambaye anasema kuwa neno hili mipasho limetolewa katika maana ya msingi ya kimsamiati na limepewa maana ya ziada yenye kumaanisha kusema ukweli; au kusema bila ya kuogopa ili mhusika anayepashwa au anayesemwa aupate ujumbe wake vizuri sana na umuadilishe, umuelimishe au kumuadabisha. Ili kufanikiwa kuwasilisha ujumbe kwa njia nzuri na kutimiza majukumu yake mengine, hatuna budi kuchanganua namna wasanii mbalimbali wa muziki wa mipasho walivyohusisha mtindo wa mwingiliano tanzu katika kazi zao na kutathmini ufaafu wa matumizi ya mtindo huu wa mwingiliano tanzu kama mojawapo ya sifa kuu za fasihi simulizi ya Kiswahili. Aina nyingine za *Modern Taarabu* ni pamoja na *Rusha-roho*¹ na *Taa-rap* ambayo ni mseto wa Taarabu na mtindo wa rapu ni tofauti mno na aina zingine zote za Taarabu tulizotaja katika matumizi ya ala, mahadhi, kasi, uimbaji na ukuruba wake kwa mtindo wa muziki wa rapu.

Katika utamaduni wa Kiafrika, nyimbo ziliimbwa kwa kujumuisha utendaji na miondoko ya viungo mbalimbali vya mwili mathalan mkono, kichwa na kiuno kutegemea jamii husika. Hadhira katika mipasho huwa tendi kwani hutarajiwa kucheza muziki huu unapoimbwa. Katika jamii ya Waswahili ambapo *Modern Taarabu* huimbwa, sehemu za mwili zinazotumika zaidi katika utendaji ni pamoja na viuno, mikono na miguu. Katika utendaji wa nyimbo za Taarabu, baadhi ya mistari huimbwa na kiongozi anayethibiti nyimbo zile huku waimbaji wengine wakiimba sehemu zingine za nyimbo zile. Mbinu hii ya takriri ndiyo humithilisha sifa za nyimbo za *Modern Taarabu* na zile za ushairi.

¹**Rusha roho:** Ndio mtindo wa hivi punde wa Taarabu uliokusudiwa vyombo vya habari kwa ajili ya kucheza tu. Hamna utendaji hai wa bendi ila muziki uliorekodiwa huchezwa na hadhira yenye wanawake pekee.

Kulingana na Wamitila (2008) dhamira na maudhui havijitokezi tu katika kazi ya kifasihi bali ni zao la mahusiano na maingiliano ya vipengele na mbinu kadha katika kazi inayohusika. Uelewekaji wa dhamira kwa njia kamilifu unategemea maudhui na wasanii, sauti ya msimulizi, mandhari, msuko, mtazamo, mtindo, mwingiliano tanzu na mengineyo. Nyimbo za *Modern Taarabu* huwa na maudhui kurejelea shughuli mbalimbali za maisha kama vile kazi, vita, maadili, malezi na mafanikio.

Aidha, matumizi ya tamathali nyingi ni sifa nyingine muhimu katika nyimbo za *Modern Taarabu* na hutumiwa kudhihaki tabia isiyokubalika na inayokiuka desturi za kijamii. Aidha, nyimbo za *Modern Taarabu* husifu, hukashifu, husuta na huonya dhidi ya wanaoonekana kuwa ni maadui wa mtu binafsi au jamii. Jumbe katika nyimbo hizi zinatokana na uzoefu wa maisha, itikadi, mitagusano katika jamii na maisha yanayoenziwa. Isitoshe, ujumbe huweza kuonyesha aina ya uhusiano uliopo kati ya jamii na asasi za kiutamaduni, mitindo ya mahusiano au matukio yanayofaa kukumbukwa. Mwisho, tabia za ulafi, uvivu, umbea, uvumi na matendo mabaya ya uasherati hushambuliwa katika nyimbo hizi. Nyimbo hizi huwa na umbo la mistari ambayo hukaririwa kwa kuzingatia madhumuni ya mhusika. Finnegan (2012) anasisitiza kuwa mbinu ya takriri katika nyimbo za Kiafrika ni nguzo muhimu sana. Hivyo basi, utafiti huu uliona hii kama fursa ya kipekee ya kulipa umuhimu suala la mwingiliano tanzu na namna unavyojitokeza katika *Modern Taarabu-Mipasho*. Suala la utafiti ambalo limefafanuliwa katika sehemu ifuatayo.

1.3 Suala la Utafiti

Mwingiliano tanzu una umuhimu mkubwa katika kuwasilisha ujumbe uliodhamiriwa na mtunzi kwa hadhira. Aidha, matumizi mwafaka ya mtindo wa mwingiliano tanzu hufanya muundo wa kazi ya fasihi kuivutia hadhira lengwa kando na kutekeleza majukumu

mengine muhimu. Licha ya masuala anuwai kushughulikiwa katika tafiti zilizofanywa kuhusu muziki wa Taarabu, imebainika kuwa ama suala la mwingiliano tanzu na dhima yake katika muziki wa *Modern Taarabu-Mipasho* halijashughulikiwa kabisa au hata pale linapojitokeza, limekuwa ni kwa kutajwa tu. Hivyo basi, utafiti huu ulizingatia namna tanzu anuwai zilivyoingiliana katika uwasilishaji wa ujumbe kwenye muziki wa mipasho pamoja na kutathmini dhima ya mwingiliano tanzu katika muziki wa *Modern Taarabu-Mipasho*.

1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulielekezwa na malengo yafuatayo:

1. Kujadili mwingiliano tanzu katika uainishaji wa tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili.
2. Kuchanganua miktadha mbalimbali ya mwingiliano tanzu katika muziki wa *Modern Taarabu-Mipasho*.
3. Kutathmini dhima ya mwingiliano tanzu katika muziki wa *Modern Taarabu-Mipasho*.

1.5 Nadharia Tete

Utafiti huu uliongozwa na nadharia tete zifuatazo:

1. Kuna mwingiliano tanzu katika uainishaji wa tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili.
2. Miktadha mbalimbali imedhihirisha mwingiliano tanzu katika muziki wa *Modern Taarabu-Mipasho*.
3. Mwingiliano tanzu katika muziki wa *Modern Taarabu-Mipasho* unatekeleza dhima mbalimbali.

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ulinuiwa kuwachochea wahakiki katika kufanya uchunguzi zaidi katika tanzu kwa kuzingatia nadharia ya mwingiliano tanzu. Vile vile, kutokana na utafiti huu,

ilitarajiwa kuwa wapenzi na watafiti wengine wataweza kuchochewa na kumakinikia zaidi nyimbo za Taarabu. Isitoshe, utafiti huu ulinua kuwahamasisha wahusika wote kama vile wasomi na hasa waandishi katika miainisho ya utanzu wa nyimbo ili wamakinike na kuweza kujumuisha nyimbo za Taarabu miongoni mwa vipera vya utanzu wa nyimbo katika awamu zote za usomi na uhakiki wa fasihi simulizi. Vile vile, uchunguzi wa utafiti huu haukupata ithibati yoyote ya kuonyesha kuwa kuna utafiti wowote uliokwisha kufanywa kuhusu *Modern* Taarabu-Mipasho kwa kutumia nadharia ya mwingiliano tanzu.

1.7 Nadharia za Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili; Nadharia ya mwingilianomatini na nadharia ya umuundo. Katika utafiti huu, nadharia ya mwingilianomatini ilitumika katika kushughulikia mwingiliano tanzu katika *Modern* Taarabu-Mipasho mintarafu lengo la kwanza na la pili katika utafiti huu. Kwa mujibu wa nadharia ya umuundo, utafiti huu ulipata fursa ya kumakinika katika kujadili lengo la pili la utafiti huu ambalo ni kujadili miktadha mbalimbali ya mwingiliano tanzu katika *Modern* Taarabu-Mipasho kutokana na uhuru wa ubunaji alionao mhusika wakati wa uwasilishaji wa ujumbe. Aidha, nadharia hii ilitumika katika kutathmini dhima ya mwingiliano tanzu katika *Modern* Taarabu-Mipasho. Katika sehemu ifuatayo, nafasi ya nadharia ya mwingilianomatini katika utafiti huu umeshughulikiwa.

1.7.1 Nadharia ya Mwingilianomatini

Mwingilianomatini ni istilahi ambayo asili yake ni neno la Kiyunani *intertexto* lenye maana ya ‘usokotaji wakati wa usukaji’ (Tafsiri yetu). Istilahi hii iliasisiwa na Mfaransa Julia Kristeva mnamo miaka ya sitini baada ya kuikuza kutokana na nadharia ya Mikhail

Bakhtin² ya Usemezano (Bakhtin, 1994). Bakhtin (1981) aliamini kuwa utanzu wa fasihi una uwezo wa kuingiza vipengele vya tanzu zingine lakini ukabakia na sifa zake kama utanzu. Vivyo hivyo, Bakhtin anasema kuwa utanzu wa fasihi kuwa na vipengele vingine ndani yake hakuondoi hadhi ya utanzu huo. Aidha anazidi kusema kwamba msingi mkuu wa nadharia ya mtindo wa mwingiliano matini umo katika jinsi kazi za kifasihi zinavyohusiana, kuumbana na hata kuchangamana. Mulila (2005) anadahili kuwa mwingilianomatini ni ugiligili unaopatikana baina ya tanzu mbalimbali za fasihi ya Kiswahili unaosababisha ugumu katika kutofautisha au kutenganisha tanzu hizi mbalimbali za fasihi simulizi ya Kiswahili. Kristeva anasema kuwa kazi za kifasihi huingiliana na kuhusiana katika kile kinachoweza kuitwa mwanda wa kimwingiliano-matini. Aidha Kristeva alisema kuwa mtindo wa mwingiliano matini ni matokeo ya kazi ya mwandishi mmoja na uhusiano wa kazi ile na kazi zingine na miundo ya lugha iliyotumika.

Kutokana na nadharia ya mwingilianomatini, mtafiti amepanua maana na matumizi yake katika kushughulikia mwingiliano tanzu katika fasihi simulizi ya Kiswahili. Kama alivyofasili Senkoro (2011), mwingiliano tanzu ni mbinu ambayo huonyesha kutumiwa kwa utanzu mmoja wa fasihi katika kutolea au kuwasilisha utanzu mwingine. Kwa mfano, si jambo geni kukuta wimbo au kipande cha wimbo ndani ya ngano au hadithi. Hivyo basi mwingiliano tanzu ni ule uwepo wa sifa mbalimbali za utanzu mmoja au zaidi katika kazi fulani ya fasihi kama vile matumizi ya nyimbo, matumizi ya barua, ngoma, masimulizi ya hadithi ndani ya hadithi, misemo, nahau, majibizano, vichekesho, picha na michoro na kadhalika.

²Njogu na Wafula (2007), wanamtaja mwendelezaji wa nadharia hii kuwa ni Mikhail M. Bakhtin ambaye alikuwa mwanaisimu na mhakiki wa kazi za fasihi aliyeishi kati ya mwaka 1895- 1975.

Bakhtin (1981) ameanisha mwingilianomatini katika aina mbalimbali kwa kurejelea: jinsi matini au kazi za kifasihi huhusiana na kazi nyinginezo zilizoitangulia kwa kiasi kikubwa, mwingilianomatini za fasihi simulizi katika viwango tofauti vya kazi ile kama vile fani na usawiri wa wahusika, mwingiliano wa tanzu za fasihi simulizi na athari zake hasi au chanya kwenye mtindo wa kazi inayohusika, mwingilianomatini na muktadha ambao una uhusiano wa kuchochea mahusiano fulani kati ya kazi zinazohusika na hatimaye ni mwingilianomatimi wa fasihi simulizi na uwasilishaji ambao huonyesha jinsi uhusiano kati ya utanzu mmoja na nyingine huweza kuathiri maana na dhamira ya kazi inayorejelewa. Kati ya miainisho hii yote aina mbili za mwisho alizotaja ndizo zilizorejelewa katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu aina hizi mbili zimebeba yaliyomo katika malengo ya utafiti huu hasa lengo la kwanza na la pili.

Wanjala (2015) anasema kuwa mwingiliano tanzu hushikilia kuwa kazi ya fasihi huumbwa kwa kuvunja mipaka ya kitanzu kwa lengo la kuibuka na kazi bora zaidi. Kusudi kuu la nadharia hii ni kutupilia mbali uchambuzi wa kila utanzu wa kifasihi kivyake kwa msingi kuwa hakuna utanzu wowote mmoja ule ambao unaweza kujisimamia bila kutagusana na tanzu zingine katika utendakazi wake na ukafaulu kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa. Utenganishaji tanzu ulishadidiwa sana katika uainishaji wa Ki-Aristotle ambapo tanzu zingine zilipojitokeza katika uchambuzi wa kazi fulani, tanzu hizi zilichambuliwa kivyake kama mojawapo ya fani katika kazi husika. Mwingiliano tanzu una mihimili ifuatayo:

Kwanza, mwingiliano tanzu katika kazi yoyote ya fasihi husababishwa na mchakato wa mwingilianomatini ambao huiwezesha kazi husika kukopa, kubashiri, kunukuu, kuiga na hata kurejelea tanzu zingine ama katika fani au maudhui bila kuzingatia mipaka dhahania ya kitanzu. Katika utafiti huu, ukokotaji wa matini mbalimbali kutoka kwa nyimbo za

Modern Taarabu-Mipasho ulitumika katika uchanganuzi, uwasilishaji na ufasiri wa data ili kujadili miktadha mbalimbali ambapo mwingiliano tanzu ulijitokeza.

Pili, wakati mwingine mwingiliano tanzu huu hubainishwa kabisa na wataalamu wa fasihi simulizi kama mtindo wa kawaida katika kumbo za fasihi. Ili hadhira ya fasihi ielewe kazi yoyote ya fasihi lazima ihusishe vipengele vingine nje ya muktadha wa usomaji au usimulizi ule (Mshengyezi, 2003). Katika kuafikia malengo ya utafiti huu, nadharia ya umuundo ilishirikishwa ili kutoa mwelekeo zaidi kuhusu dhana ya mwingiliano tanzu na dhima yake katika fasihi simulizi na namna inavyojidhihirisha katika *Modern Taarabu-Mipasho*. Ufafanuzi zaidi kuhusu nadharia ya umuundo umetolewa katika sehemu ifuatayo.

1.7.2 Nadharia ya Umuundo

Scholes (1974) anaelezea kwamba msingi wa umuundo ni urasimu na hivyo kutilia mkazo umuhimu ulioko kati ya nadharia hizi mbili. Umuundo uliibuka katika miaka ya (1940-1950) hasa kutokana na jitihada za wanaisimu wa shule ya Prague (Wamitila, 2002). Lyons (1981) na Lodge (2005) wanahusisha chimbuko la nadharia ya umuundo na Ferdinand de Saussure ambaye hutambuliwa kuwa mwasisi wa isimuleo. Umuundo unapinga wazo la kijadi linalodai kwamba fasihi ni tokeo la mchango wa maudhui na fani. Hii ni kumaanisha kuwa kuna mambo mengine zaidi yanayochangia fasihi.

Katika kazi za fasihi, Umuundo humwelekeza mhakiki katika kuchunguza kazi ya sanaa kwa kuangalia vipengele vya ndani vya kazi hiyo. Vipengele hivi ndivyo huunganishwa ili kuunda kazi iliyokamilika japo kila kipengele pia huwa kina umuhimu wake. Wanaumuundo wanasisitiza kuwa kuna vipengele vinavyochangia ujenzi wa kazi ya sanaa na kuwa vipengele hivyo vinahusiana na kutegemeana ili kukamilisha kazi nzima. Aidha, walisema kuwa uzuri wa kazi ya fasihi hutegemea mambo kama ufungamano wa

sehemu mbalimbali za kazi hiyo. Waliamini kuwa dunia ni muundo mmoja usioweza kugawika katika vitengo vidogo vidogo tofauti. Dunia haikuumbwa kutokana na viungo mbalimbali vilivyotengana bali vinavyoingiliana na hivyo basi havitengeki kamwe. Hii miundo inapaswa kufikiriwa kijumla (Scholes, 1974; Hawkes, 1977; Culler, 2003). Kwa jumla, kama ambavyo muundo wa lugha ni mfumo, muundo wa fasihi simulizi ya Kiswahili una vipengele vinavyotegemeana na vinavyoelezwa katika muktadha wa vipengele vingine. Hili ni suala lililoadiliwa katika utafiti huu kwa kuzingatia namna tanzu tofauti zilivyoingiliana kama viungo mbalimbali katika kuboresha uwasilishaji wa ujumbe kwenye nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho*.

Pili, kulingana na nadharia hii ya Umuundo, ni muhimu kuchunguza iwapo tanzu za fasihi simulizi zinaafiki matarajio ya umuundo kwa kuangazia vipengele vinavyojenga tanzu hizo na uhusiano uliopo baina ya tanzu hizo. Finnegan (2012) anapendekeza utumiaji wa nadharia hii katika uhakiki wa tanzu za fasihi simulizi na hivyo nadharia hii ilitumika katika utafiti huu kuhakiki mwingiliano tanzu katika *Modern Taarabu-Mipasho*.

Tatu, nadharia ya umuundo inatoa uhuru kwa mtunzi kuwa mbunifu kwa kuingiza vipengele vipya katika kazi, mradi tu azingatie muundo wa kimsingi wa mfumo huo. Mwelekeo huu huingiza ujumi katika fasihi katika kupitisha ujumbe kwa urahisi maana kazi inakuwa ya kuvutia. Kwa mfano, mianza maalum katika hadithi huingiza mvuto wa kuteka nathari ya hadhira na kuifanya kuchangamkia kazi hiyo. Suala hili hutekelezwa na fomula ya ufunguzi na fomula ya kufunga katika *Modern Taarabu-Mipasho*.

Mwisho, nadharia ya umuundo huwafanya wasanii kuwa makini katika utunzi wao kwa sababu jinsi kazi inavyowasilishwa pia ni muhimu katika usanii. Si fahari ya usanii kuandaa kazi chapwa kimuundo kwa madai kuwa ujumbe ndicho kipengele cha kuwekewa uzito. Hivyo kwa msingi huu, utafiti huu ulijadili kufaulu kwa wasanii wa

Modern Taarabu-Mipasho kwa kutathmini jinsi walivyotekeleza uwasilishaji wa nyimbo zao na namna walivyotumia mwingiliano tanzu katika kuimarisha nyimbo hizo na kuzifanya ziwe za kuvutia ili kuondoa hali ya uchapwa.

Katika utafiti huu, mtafiti aliongozwa na nadharia ya mwingilianomatini na ile ya umuundo kuhakiki jinsi tanzu mbalimbali za fasihi simulizi zilivyoingiliana, zilivyoumbana na kuchangamana katika kuboresha uwasilishaji wa ujumbe katika *Modern* Taarabu-Mipasho. Aidha, nadharia hizi zilitoa mwongozo kwa mtafiti katika kufahamu kwamba, kazi ya mipasho inavyowasilishwa huhitaji ujuzi mwingi ili isiwe chapwa. Isitoshe, nadharia hizi zimetumiwa kuchanganua mwingiliano wa muziki wa mipasho na tanzu nyingine za nyimbo mathalan chakacha, bembelezi, sebene na sidimba.

1.8 Misingi ya Uteuzi wa Suala la Utafiti

Licha ya kuwepo kwa tafiti za fasihi simulizi kuhusu utanzu wa nyimbo na za muziki wa Taarabu kwa ujumla, mtafiti hakupata kukumbana na kazi za tafiti zozote zile kuhusu mtindo wa mwingiliano tanzu katika muziki wa *Modern* Taarabu. Aidha, uhakiki wa mtindo wa mwingiliano tanzu uliowahi kufanywa ulihusisha tanzu zingine za fasihi andishi kama vile riwaya (Rono, 2013) na uhakiki wa ngano katika fasihi simulizi uliofanywa na Oyoyo (2013) vile vile mwingiliano tanzu katika fasihi simulizi ya Kiafrika kwa mfano embalu na mwaka kongwa (Wanjala, 2015). Hivyo basi, mtafiti aliona haja ya kufanya utafiti kuhusu mwingiliano tanzu katika muziki wa *modern* Taarabu- mipasho ili kujaza mwanya uliojitokeza na kutathmini nafasi yake katika mawasiliano mapana ya jamii.

Vile vile kuna tanzu nyingi sana za fasihi simulizi. Hata hivyo utafiti huu umeshughulikia baadhi ya vipera katika utanzu wa semi, maigizo, ngomezi, masimulizi na ushairi

simulizi ambavyo viilidhihirika zaidi katika utendaji wa nyimbo zilizoshirikishwa katika utafiti huu.

Aidha, katika siku za hivi karibuni, wasanii wa *Modern Taarabu Mipasho* wameweza kuimarisha zaidi utendaji wao katika njia ya video za hali ya juu. Utendaji huu ni kiungo muhimu sana katika kufaulisha malengo ya utafiti huu hasa lile la kudhihirisha utanzu wa maigizo katika *Modern Taarabu-Mipasho*. Katika nyimbo hizo, ni nyimbo 31 za *Modern Taarabu-Mipasho* zilizotumiwa katika uchanganuzi wa data. Nyimbo hizi zilikuwa viwakilisho vya namna neno, mafungu ya maneno, sentensi au aya mbalimbali zilionukuliwa zilivyodhihirisha mwingiliano tanzu katika muziki wa *Modern Taarabu-Mipasho*. Aidha, utafiti huu uliegemea nadharia ya mwingilianomatini kama iliyoendelezwa na Julia Kristeva na ile ya umuundo kama mwongozo wa utafiti huu.

Hatimaye utafiti huu ulijikita katika nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho* licha ya kuwa kuna aina nyingi za nyimbo za Waswahili kama vile: Taarabu Asili, Chakacha, Lelemama, Mduara miongoni mwa nyingine.

1. 9 Upeo wa Utafiti

Nyimbo za Taarabu zimeimbwa na waimbaji binafsi na hata vikundi vingi katika mwambao wa Afrika Mashariki. Aidha, kuna Taarabu Asili na *Modern Taarabu*. Kutokana na aina tofauti za Taarabu na wingi wa nyimbo hali kadhalika waimbaji, ni vigumu kutafitia kwa kina nyimbo zote za Taarabu na pia waimbaji wote walioimba Taarabu. Hivyo basi utafiti huu ulijikita katika nyimbo za *Modern Taarabu* kutoka Zanzibar za makundi yafuatayo:

1. Jahazi *Modern Taarabu*
2. *East African Melody*
4. *Tanzania One Theatre (T.O.T)*

5. Zanzibar *Stars Modern* Taarabu.

Uteuzi huu ulifanywa kimaksudi kwa misingi ifuatayo:

Kwanza, *Modern* Taarabu-Mipasho kutoka nchini Zanzibar ni muziki wenye umaarufu mkubwa Afrika Mashariki na hasa humu nchini Kenya ambapo huchezwa na vyombo mbalimbali vya habari. Hii ni kutokana na wasanii wa nyimbo hizi kuwa na tajriba pana ya utungaji na uimbaji na kushughulikia maudhui mengi katika nyimbo zao za Taarabu.

Pili, kwa malengo ya utafiti huu, kanda za *Modern* Taarabu-Mipasho kutoka Zanzibar ziliweza kupatikana katika maduka yanayoziua kwani zimesambaa kote nchini Kenya.

1.10 Yaliyoandikwa kuhusu Taarabu na Mwingilianomatini

Miongoni mwa yaliyoandikwa kuhusu Taarabu yanapatikana katika utafiti wa awali wa King’ei (1992) ambaye alichunguza nafasi ya Taarabu katika lugha, utamaduni na mawasiliano katika jamii mnamo miaka ya 1963-1990. Baada ya kuchanganua maudhui mbalimbali katika nyimbo za Taarabu kama vile siasa, taswira ya mwanamke na mazingira mbalimbali ambamo uimbaji wa nyimbo za Taarabu umejikita, King’ei anashikilia ule mtazamo wa kwanza tuliorejelea katika usuli wa suala la utafiti huu kuwa asili ya Taarabu ni makundi mbalimbali ya muziki huu yaliyoundwa na Seyyid Bargash wakati wa utawala wake. Hata hivyo King’ei anakiri kwamba haijulikani ni namna na wakati upi ambao muziki wa Taarabu uliweza kusambaa katika pwani ya Afrika Mashariki. Maoni yake haya yanatoa mchango muhimu kwa utafiti huu kuhusu asili ya nyimbo za Taarabu.

Katika mojawapo ya tafiti zake, Ntarangwi (1998) ameshughulikia nyimbo za Taarabu, uana na dini kwa msingi wa utamaduni wa Waswahili. Katika utafiti huo, Ntarangwi alichunguza namna muziki wa Taarabu hutumika katika kubeba vipengele vya kitamaduni vya dini na uana. Baadaye katika utafiti mwingine Ntarangwi (2001)

amelenga kushughulikia historia ya Taarabu, muktadha wa utendaji wake pamoja na kuendeleza masuala ya kijinsia katika muziki wa Taarabu. Utafiti wake uliufaidi utafiti huu pakubwa kwa kutoa msingi na habari za kina kuhusu historia na utendaji wa muziki wa Taarabu.

Suala la ni nani alitunga wimbo fulani wa Taarabu, kwa nini, lini na maana iliyokusudiwa huwa halijulikani na wengi ila kinachopewa umuhimu ni maana inayohusishwa na wimbo husika katika muktadha wa jamii husika. Hivyo, maana ya wimbo yaweza kuwa tofauti kama ilivyofasiriwa na hadhira ya Nairobi ikilinganishwa na tafsiri ya wimbo uleule na hadhira ya Dodoma. Kama anavyosema Ntarangwi (2001), wimbo wa Taarabu ‘Vidonge’, ulioimbwa na ‘Malika’ ulikubalika, ukawa kwa nyimbo kumi bora kwa miezi miwili mtawalia mwaka wa 1993 na kupata maana tofauti katika miktadha mbalimbali na watu kutoka maeneo ya bara ya Kenya hata bila ya wao kufahamu maana asilia ya wimbo huo. Hivyo, nguvu za wimbo wa Taarabu imo katika maana inayowasilishwa kwa hadhira katika muktadha maalum na wala sio maana asilia kama ilivyokusudiwa wakati wa utunzi wake. Hali hii inaweza kuimarishwa zaidi kupitia kwa mwingiliano tanzu katika uwasilishaji wa nyimbo za Taarabu. Ni bayana kuwa nyimbo nyingi za Taarabu huwa hazimrejelei mtu au matukio maalum na hivyo zinaweza kukubalika katika hali na tafsiri mbalimbali.

Katika kiwango cha utendaji, matumizi na ubadilishaji toni na kiimbo katika nyimbo za Taarabu huwa na nafasi muhimu ya kuwasilisha na kuzalisha ujumbe. Aidha, miondoko ya mwili na ishara mbalimbali za mhusika wa nyimbo za Taarabu huchangia sana katika kutoa maana ya wimbo unaoimbwa. Isitoshe, hadhira ya nyimbo za Taarabu nayo huchangia sana katika kutoa maana ya wimbo pale wanapoimba, wanapocheza, wanapochagua waimbiwe wimbo fulani maalum au wanapowatuza waimbaji. Kawaida,

mtu mmoja katika hadhira anaweza kusimama, kuimba, kucheza na kisha kumtuza mhusika wa chaguo lake kabla ya kurudi alikotoka mwanzo, hivyo kuonyesha uwepo wake au kujihusisha kwake na ule wimbo. Hadhira iliyosalia hufasiri maana iliyokusudiwa na yule mmoja wao hasa pale anaporudia mishororo maalum kwa sauti au anapomtazama yule anayerejelewa katika wimbo husika (Ntarangwi, 2001).

Nyimbo za Taarabu ambazo hukashifu upotovu wa kimaadili katika jamii huchezwa kwa midundo ya kasi na mirindimo mitatu ambayo huchezwa kwa kuingiliana (Khamis, 2001). Mtindo huu unafanana na ule wa "women's Taarabu" nchini Zanzibar ambapo midundo inayohusishwa na wanawake huambatanishwa na matini zinazotumia lugha nzito yenye wingi wa matusi kwa madhumuni ya kukejeli anayerejelewa machoni pa jamii (Topp, 1993). Kinyume chake ni nyimbo zenye maudhui yanayomrejelea Mungu au mpenzi ambapo huchezwa kwa midundo taratibu ya mwendo wa pole. Uchezaji wa ala na jinsi zinavyochezwa ni kipengele kingine muhimu katika uainishaji wa mtindo na muundo wa muziki wa Taarabu. Aidha, idadi ya waimbaji (waimbao mmoja mmoja au wote kwa pamoja), wa ubeti mmoja au nyingi hutumika kuainishia aina ya Taarabu. Awali katika Taarabu kulikuwa na kikundi cha waimbaji 10 au 20 walioimba kwa kupokezana huku wakizungikia vitini au wakizunguka kwa nanma ya mviringo kwa mtindo wa Taarabu ya *Kidumbaki*.

Khamis (2001) katika mojawapo ya makala yake yenye anwani *Redefining Taarabu In Relation to Local and Global Influences*, ameeleza kwa kina awamu mbalimbali katika historia na mabadiliko ya muziki wa Taarabu. Aidha, Khamis ameanisha upekee na sifa mbalimbali zinazopatikana katika muziki wa *Modern Taarabu-Mipasho* baada ya kuangazia Taarabu asili. Kwa maoni yake, ni vigumu kuuchukua muziki wa Taarabu na kuufungia katika ufafanuzi mmoja tu kwani muziki huu umeathirika pakubwa kutokana

na uhuru unaoletwa na mwingiliano na vyombo vya habari. Hivyo, muziki wa Taarabu unahitaji kufafanuliwa upya kwa kuzingatia muktadha mpana ulioletwa na mabadiliko ya kiteknolojia. Kutokana na makala haya ya Khamis, utafiti huu uliweza kunufaika kupata habari kuhusu historia na mabadiliko ya Taarabu pamoja na sifa za *Modern Taarabu-Mipasho*.

Mtafiti mwingine aliyepata kushughulikia Taarabu ni Askew (2002). Yeye alifanya utafiti kuhusu mitindo ya utunzi kwa kuangazia suala la mabadiliko katika uwasilishaji wa nyimbo za Taarabu. Utafiti wake ulijikita katika mwingiliano wa nyimbo za Taarabu nchini Tanzania ambapo aliangazia matumizi ya mafumbo, vishindo na mipasho katika uwasilishaji wa ujumbe wa kisiasa. Haya aliyoangazia Askew yana umuhimu mkubwa kwa utafiti huu kwani katika kiwango kimoja, tafiti zote mbili zilinua kuangazia namna ya kuboresha uwasilishaji wa ujumbe kupitia mwingiliano wa vipengele vingine na muziki wa Taarabu. Timammy (2002) ameshughulikia aina mbalimbali za nyimbo za harusi za Waswahili wa Mombasa kwa kutumia uhakiki wa kimtindo. Utafiti wa Timammy umeshughulikia Taarabu kwa ujumla kwa kuiangalia kama utanzu wa nyimbo tofauti na utafiti huu ambao umejikita katika Taarabu aina ya mipasho.

Mwamzandi (2002) katika utafiti wake amedhihirisha jinsi Taarabu inavyotumia kipengele cha usemezano kama kifaa cha mawasiliano. Hata hivyo, yeye ametazama Taarabu kwa msingi wa utanzu wa ushairi na kuchanganua semi zilivyotumika katika kuwasilisha ujumbe katika muziki wa Taarabu kwa msingi wa mila na itikadi za jamii ya Waswahili wa Mombasa. Utafiti wake unatofautiana na utafiti huu kimalengo ambao kimsingi, unatazama mwingiliano tanzu katika *Modern Taarabu-Mipasho*. Aidha, katika utafiti huo alishughulikia Taarabu kwa msingi wa utanzu wa ushairi ilhali utafiti huu umeshughulikia *Modern Taarabu-Mipasho* kwa msingi wa utanzu wa nyimbo katika fasihi simulizi kwa kuchukulia kuwa nyimbo ni kile kinachoimbwa na hivyo nyimbo ni

dhana pana inayojumuisha tanzu nyingi za kinathari ambazo huweza kuingia katika kundi la nyimbo pindi tu zinapoimbwa. Hatamaye, sampuli yake ilirejelea jamii ya Waswahili kutoka Mombasa ilhali sampuli ya utafiti huu ni muziki wa *Modern Taarabu-Mipasho* kutoka Zanzibar. Hata hivyo, jamii hizi zinapatikana mwambao mwa Pwani na hivyo kuna uwezekano wa tamaduni zao kufanana.

Utafiti mwingine uliogusia utanzu wa Taarabu ni ule wa *Kibiriti Ngoma* uliofanywa na Beez na Kolbusa (2003). Utafiti huu umezungumzia suala la Taarabu na historia yake na hata uchezaji wake. La muhimu kwa utafiti huu kutokana na utafiti huo ni mjadala ulioendelezwa kuhusu *Modern Taarabu*, aina ya mipasho. Kwa mujibu wao, nyimbo za Taarabu ni mkusanyiko wa masuala yote muhimu katika maisha ya mwanadamu. Taarabu ni muhimu kwani ni ufafanuzi wa maisha. Utafiti wao ulifaidi utafiti huu katika kupata ufafanuzi kuhusu mipasho na utendaji wake mjini Dar es salaam. Hata hivyo, tofauti na utafiti huu, utafiti wao ulizingatia dhima ya mawasiliano katika *Modern Taarabu* kwa kujikita katika mgogoro baina ya wanawake wawili katika wimbo wa Taarabu wa 'Kibiriti Ngoma'. Isitoshe, waliufanyia utafiti wao Dar es Salaam, Tanzania ilhali utafiti huu ulifanyiwa nchini Kenya. Pia tofauti na malengo katika utafiti wao, utafiti huu ulihusisha nyimbo kadhaa za *Modern Taarabu-Mipasho* katika kutathmini dhima ya muziki huu.

Traore (2004) naye alifanya utafiti kuhusu nyimbo za Taarabu na kuchapisha makala ya *Continuity and Change in Zanzibar Taarabu Performance and Poetry*. Katika makala haya, yeye ameshughulikia uhusiano uliopo kati ya nyimbo za Taarabu na maandishi katika kanga. Pia, ameeleza umuhimu wa vazi la kanga kwa wahusika mbalimbali na vyama vya kisiasa kama chombo cha kuwasilishia ujumbe wa aina mbalimbali. Kanga ni vazi la kimsingi kwa wakaazi wa Pwani. Hivyo, maandishi katika kanga hizi husafiri kwa

haraka sana kadri wavaliaje wake wanavyosafiri na kutangamana na wenzao. Akitumia wimbo wa *Tutabanana hapa hapa*, Traore (2004) ameonyesha namna muziki wa mipasho unavyotumiwa kupasha habari. Amezungumzia kuhusu mabadiliko katika muziki wa Taarabu kutoka Taarabu Asili hadi *Modern* Taarabu na kufafanua kuhusu *Modern* Taarabu-Mipasho. Utafiti wa Traore ulinisaidia kufahamu zaidi kuhusu historia ya muziki wa Taarabu na mabadiliko yake. Pia ulimwezesha mtafiti wa utafiti huu kufahamu zaidi kuhusu Taarabu aina ya mipasho ilivyozuka na baadhi ya sifa zake.

King'ei na Kisovi (2005) katika utafiti wao wamezungumzia kwa kina kuhusu historia ya Taarabu. Kwa mujibu wa maelezo yao, nyimbo za Taarabu zinapatikana katika ushairi wa Waswahili. Nyimbo hizi zilitungwa kwa kusudi la kuimbwa katika sherehe mbalimbali za Waswahili ambazo ni pamoja na harusi, mikutano ya kisiasa na kuwakaribisha wageni miongoni mwa shughuli nyingine. Aidha, wameeleza kuwa hapo mwanzoni maudhui katika nyimbo za Taarabu yalilenga masuala ya kimapenzi, utani na mahusiano ya kijamii kati ya wapenzi na mahasidi. Hata hivyo, kuanzia mwaka wa 1980 maudhui yanayoshughulikiwa na nyimbo za Taarabu yamebadilika na kushughulikia masuala yanayohusu jamii nzima kiuchumi, kisiasa, kidini na kimaadili. Pia, wamefafanua mabadiliko katika vifaa vinavyotumika katika uchezaji wa muziki wa Taarabu. Utafiti wao uliufaa utafiti huu katika kuweka msingi kuhusu historia na mabadiliko ya nyimbo za Taarabu hali ambayo imepelekea kuzuka kwa *Modern* Taarabu, muziki ambao umeshughulikiwa katika utafiti huu.

Kea (2006) alitafitia usemezano katika nyimbo za Taarabu ambapo alichunguza athari za muktadha na mazingira katika utunzi na uimbaji wa nyimbo za Taarabu. Pia, alilenga kuonyesha namna usemezano unavyojidhihirisha katika nyimbo za Taarabu na kufafanua uhusiano uliopo kati ya malumbano katika nyimbo za Taarabu na usemezano. Utafiti wa Kea hasa pale anapochambua historia ya nyimbo za Taarabu na utendakazi wake pamoja

na alivyoshughulikia sampuli yake ya utafiti zilikuwa habari zilizoufaidi utafiti huu. Hata hivyo, mada, malengo na nadharia yake ya utafiti zilikuwa tofauti na yale ya utafiti huu na hivyo kujenga ari ya kutaka kuendeleza utafiti huu.

Owen (2010) alifanya utafiti kuhusu athari za muziki wa Taarabu kwa jamii zinazoishi Lamu na Matadoni nchini Kenya. Mbali na kueleza historia ya Taarabu, Owen katika utafiti huo ameangazia mchango wa tamaduni na shughuli za kijamii za jamii za Lamu na Matadoni kwa muziki wa Taarabu, ikilinganishwa na ilivyo katika miji mikubwa kama vile Zanzibar. Aidha, aliangazia nafasi ya muziki wa Taarabu kama chombo cha kuzifunza jamii za Lamu na Matadoni masuala ya kielimu, kisiasa, kidini na kijamii. Mojawapo ya matokeo ya utafiti wake ni kuwa muziki wa Taarabu ulitekeleza dhima ya kuwapa wananchi wa kawaida burudani ambayo haikuwa ghali kama ilivyokuwa na burudani za mijini. Pia, alipata kuwa muziki wa Taarabu ulikuwa kama njia mojawapo ya kuwapa wanajamii fursa ya kutakasa nyoyo zao na kuepuka shinikizo linalotokana na hali ngumu ya maisha ya kila siku. Utafiti wa Owen unachangia utafiti huu katika kuangazia muziki wa *Modern Taarabu-Mipasho* na dhima mbalimbali zinazotekelezwa na muziki huu katika jamii.

Macha (2013) ameshughulikia matumizi ya mtindo wa mwingilianomatini kwenye tendi. Madhumuni yake yalikuwa ni kutaka kujua kama tendi za Kiswahili huwa na mwingilianomatini na kubainisha vipengele vinayoingiliana katika utanzu wa tendi na dhima yake. Tofauti na utafiti wetu, Macha alishughulikia utanzu wa tendi katika utafiti wake ilhali utafiti huu umejikita katika utanzu wa nyimbo za *Modern Taarabu Mipasho*. Hata hivyo, utafiti wake uliufaa utafiti huu katika kushughulikia dhima ya mwingiliano tanzu katika *Modern Taarabu-Mipasho* kwa kujifahamisha na alivyoshughulikia dhima ya mwingilianomatini katika tendi. Vivyo hivyo, utafiti huu umeongozwa na nadharia ya

mwingiliano tanzu kutoka kwa nadharia ya mwingilianomatini ambayo ilitumika katika utafiti wake.

Kenguru (2013) ameangazia suala la mwingilianomatini kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi akizingatia historia na mazingira, wahusika na tamathali za semi. Utafiti huu umerejelea utafiti wake katika kushughulikia mwingiliano tanzu kwa kuangalia ambavyo yeye ameweza kubainisha mwingiliano matini katika kazi yake. Hata hivyo, utafiti wake unatofautiana na utafiti huu pale anapolenga kuainisha fasihi andishi na kujikita katika vipengele vya historia, wahusika na tamathali za semi katika utafiti wake huku utafiti huu ukiegemea nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho*. Pia yeye aliongozwa na nadharia ya vikale huku utafiti huu ukiongozwa na nadharia ya mwingilianomatini.

Wanjala (2015) ameshughulikia mwingiliano tanzu katika fasihi simulizi ya Kiafrika kwa kurejelea *Embalu* na *Mwaka Kongwa*. Wanjala alilenga kudhihirisha nafasi ya fanani, hadhira na muktadha wa utendaji katika ujenzi wa mwingiliano tanzu na kupambanua ni kwa namna gani vivigha katika mivigha ya *Embalu* na *Mwaka Kongwa* huelekeza uteuzi na utolewaji wa tanzu maalumu katika ujenzi wa mwingiliano tanzu. Ingawa sampuli, mojawapo ya nadharia na vifaa vya utafiti alivyotumia ni tofauti na vilivyotumika katika utafiti huu, umuhimu wa utafiti wake katika utafiti huu unatokana na namna alivyoshughulikia historia ya uainishaji wa tanzu za fasihi simulizi na nadharia ya mwingiliano tanzu. Wanjala katika utafiti huo amesisitiza umuhimu wa kuchunguza tanzu za fasihi simulizi ya Kiafrika kwa mfumo wa mwingiliano wake badala ya kuzishughulikia kwa kuuwekea kila utanzu mipaka bayana. Hii ni kwa sababu katika uwasilishaji wakati wa utendaji wake, utanzu mmoja huweza kutumia tanzu nyingine kwa kukusudia au kutokusudia hali ambayo matokeo yake ni ufanisi wa uwasilishaji wa ujumbe uliokusudiwa.

Hivyo, ni bayana kuwa muziki wa Taarabu una historia ndefu ambapo mabadiliko yameweza kupatikana wakati *Modern Taarabu* ilipoibuka. Mengi ya yaliyoangaziwa na watafiti mbalimbali kuhusu muziki wa Taarabu yamedhihirisha kuwa kuna tofauti ya kimalengo, sampuli, ukusanyaji data na hata uwasilishaji wa data katika tafiti zao na utafiti huu. Kazi za watafiti hawa tofauti tofauti ziliufaa utafiti huu kwani zilitoa msingi bora wa kushughulikia malengo ya utafiti huu. Sehemu inayofuata itaangazia masuala ya kimaadili yalivyozingatiwa katika utekelezaji wa utafiti huu.

1.11 Masuala ya Kimaadili

Ili kuwasilisha matokeo yaliyo sahihi na yanayoaminika, mtafiti alizingatia maadili ya kiutafiti kama ilivyopendekezwa na wataalamu mbalimbali wakiwemo Mugenda na Mugenda (1993) na Kothari (2003). Mojawapo ya suala la kimaadili alilozingatia mtafiti ni kuhakikisha kuwa alinunua kanda za *Modern Taarabu-Mipasho* ambazo ni halali na ambazo zimeidhinishwa. Hii ni kwa sababu ya kulinda haki na maslahi ya wasanii wa nyimbo hizi kwa kuwachangia kifedha ili waendeleze kipawa chao. Aidha, kanda halali zinamhakikishia mtafiti uwasilishaji wa nyimbo ulio na sauti na picha safi na shwari. Hili ni muhimu katika kupata data iliyo sahihi wakati wa ukusanyaji wa data. Aidha, ukusanyaji na uchanganuzi wa data uliidhinishwa na wasimamizi wa mtafiti pamoja na Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret. Hatimaye, mtafiti alipata kibali cha kufanya utafiti wake kutoka kwa Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, kabla ya kwenda nyanjani, hili likiwa ni hitaji mojawapo muhimu katika kuhalalisha utafiti wowote. Sehemu ifuatayo, imeshughulikia mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu.

1.12 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii imezingatia mbinu za utafiti kwa kujikita katika ufafanuzi wa muundo wa utafiti, ukusanyaji wa data, sampuli ya utafiti na vifaa vya utafiti. Mbinu za utafiti

zimekusudiwa kutoa mwelekeo katika kuafikia malengo ya utafiti huu. Kiutekelezaji, utafiti huu ulifanywa kwa kutumia sehemu mbili kuu: maktabani na nyanjani. Sehemu hizi zilichangiana na kukamilishana na kupata data toshelevu kwa utafiti huu.

1.13 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulichukua muundo wa kimaeezo. Kwa mujibu wa Hughes (1989), Merrian (1998) na Bryman (2001), utafiti wa kimaeezo huwa bora katika kutoa maelezo mengi na ya kina kutoka kwa chanzo cha habari. Aidha, utafiti wa kimaeezo hutoa maelezo halisi ya jinsi jambo lilivyo (Mugenda na Mugenda, 1999). Pia, muundo wa kimaeezo unafaa zaidi katika kupata taarifa za tafiti za fasihi simulizi za Kiafrika ambazo huwasilishwa kwa njia ya mdomo pamoja na kutazama utendaji wa wasanii. Muundo huu ulifaa utafiti huu katika ukusanyaji na uwasilishaji wa data ambao ulihusisha utazamaji na usikilizaji wa kanda za mipasho katika kupata maneno kwenye nyimbo hizo. Data iliyotumiwa katika utafiti huu ilikuwa ya kimaandishi ambayo ilitokana na nyimbo za Taarabu zilizonukuliwa baada ya mtafiti kutazama na kusikiza kanda za nyimbo za *Modern Taarabu*.

1.14 Ukusanyaji wa Data

Data ya utafiti huu ilikusanywa kutoka sehemu mbili: Maktabani na nyanjani. Ziara ya mtafiti katika maktaba za vyuo vikuu mbalimbali pamoja na mtandao ilimwezesha mtafiti kupekua na kupata matini kuhusu muziki wa Taarabu na nadharia ya utafiti huu. Tilitumia sampuli makusudi katika kuteua sampuli ya data ya utafiti huu kwa sababu tulilenga kupata nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho* zenye kudhihirisha mwingiliano tanzu. Utafiti nyanjani ulijumuisha kuzuru maeneo mbalimbali ambapo kuna maduka yanayouza kanda za video na kanda za nyimbo za Taarabu ambazo zimerekodiwa. Pia, utafiti nyanjani uliwezesha uteuzi wa nyimbo ambazo zilitumika katika utafiti huu.

Mbinu ya uteuzi wa data ya sampuli makusudi ilitumiwa katika kukusanya kanda za *Modern Taarabu-Mipasho* kwa kuzingatia mada ya utafiti. Aidha, mtafiti alizingatia anwani ya kanda zile katika kumwongoza alipokuwa nyanjani akiteua kanda ambazo angenunua kwa nia ya kuzihusisha kwenye data ya utafiti huu. Hatua iliyofuatia ilikuwa kusikiliza kanda za muziki wa *Modern Taarabu-Mipasho* katika tepurekoda na kuzitazama kanda za nyimbo hizo katika video ili kubaini maleba yaliyotumika, miondoko mbalimbali katika uwasilishaji, muktadha wa utendaji miongoni mwa masuala mengine yenye kuendeleza sifa za mwingiliano tanzu. Nyimbo hizo zilinakiliwa katika daftari kama zilivyokuwa na kuhifadhiwa katika maandishi ili kuweza kukokotoa matini zilizodhihirisha mwingiliano tanzu. Aidha, nyimbo zilizotumika katika kazi hii zilinakiliwa kwa madhumuni ya kuzijumuisha katika sehemu ya kiambatisho kama ithibati.

1.15 Usampulishaji

Katika utafiti huu, sampuli imetumiwa kumaanisha kanda za nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho*. Sampuli ilitumiwa katika utafiti huu ili kuepuka kuchunguza nyimbo zote za Taarabu na waimbaji wote wa Taarabu kutokana na idadi yao kuwa kubwa sana. Sampuli ilitokana na jumuiya pana ya nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho* zinazoimbwa Zanzibar. Nyimbo za Taarabu ziliteuliwa kwa nia ya kuzisikiza huku zingine zikitazamwa ili kuafikia malengo ya utafiti huu. Uteuzi wa kwanza katika baadhi ya nyimbo ulifanywa kwa kurejelea anwani za nyimbo hizo ambazo zilikuwa kama kidokezo cha yaliyomo katika nyimbo husika. Sampuli ilijumuisha nyimbo za mipasho zilizoimbwa na watu binafsi na zile zilizoimbwa na vikundi mbalimbali vya mipasho.

Uteuzi wa muziki wa *Modern Taarabu-Mipasho* uliorejelewa ulikuwa ni wa sampuli makusudi. Mugenda na Mugenda (1999) wanasema kuwa uteuzi wa sampuli makusudi

unafaa katika utafiti wenye muundo wa kimaelezo ambao lengo lake kuu ni kupata habari/data kwa msingi ya malengo ya utafiti husika. Kwa msingi huu basi, nyimbo 32 zilitumika katika kupata data ya utafiti huu. Nyimbo zilizohusishwa katika utafiti huu ni zile zilizosheheni mwingiliano tanzu ambao ni kiini cha malengo ya utafiti huu. Ingawa asili ya *Modern Taarabu* na bendi zinazocheza muziki huu ni mwambao wa Pwani ya Afrika Mashariki, nyimbo hizi zinapatikana katika maduka ya kuuza muziki ambayo yanapatikana kote nchini Kenya. Mtafiti alizinunua nyimbo zilizotumiwa katika utafiti huu kutoka maduka yanayouza muziki. Hii ilikuwa ni baada ya kusikiliza na kuzitazama nyimbo 105 za *Modern Taarabu* kwa makini hadi akafikia kuteua kimakusudi nyimbo 32 za *Modern Taarabu-Mipasho* ambazo zilikuwa na matini zilizodhihirisha kuwepo kwa mwingiliano tanzu. Hii ilikuwa ni asilimia 30 ya nyimbo zote alizosikiza mtafiti na ambazo zilidhihirisha mwingiliano tanzu, asilimia ambayo inapendekezwa na Mugenda na Mugenda (1999). Mbinu hii pia inakubalika na wataalamu wa utafiti ambao ni pamoja na Kothari (2004) ambaye anafafanua kuwa inawezekana kupata matokeo halali kwa kuchunguza sehemu ndogo ya jumuiya ya sampuli husika mradi tu inawakilisha malengo ya utafiti ya jumuiya pana. Mtafiti alihisi kuwa idadi hii ya nyimbo ilifaa kwani kama anavyokiri Wanjala (2015) mwingiliano tanzu haubadiliki kutokana na wingi au uchache wa tanzu ila kile kinachotendeka kukiwa na wingi wa sampuli ni urudufishaji ambao huchukua muda mrefu pamoja na kuwa kazi ndefu.

1.16 Vifaa vya Utafiti

Katika utafiti huu, kwanza, usomaji wa kina ulifanywa maktabani kuhusu nadharia ya utafiti kutoka vitabu, majarida na machapisho mbalimbali katika maktaba na kupitia kwa mtandao ili kupata msingi imara kuhusu mada ya utafiti. Aidha, data asili za kazi zinazojadili habari zote zinazohusu historia na maendeleo ya nyimbo za Taarabu, waimbaji wa Taarabu na maandishi mengine yoyote yaliyoambatana kimaudhui na

kidhamira na utafiti huu yalirejelewa katika kuimarisha hoja za uchunguzi. Pia, mtafiti alinufaika mno kutokana na marejeleo mengine ya vitabu na nukuu zinazohusiana na utafiti huu aliyozima kutoka kwa wasimamizi wake, wahadhiri wa vyuo vingine na hata marafiki. Habari zote zilizorejelewa zilinakiliwa katika daftari na kwenye tarakilishi kisha data asili yote ikatumika baadaye katika uchanganuzi wa data.

Pili, mtafiti alizisikiza nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho* na kuziteua zile zilizokuwa zimebainisha mwingiliano tanzu kulingana na malengo ya utafiti huu. Kisha, mtafiti alizitazama kanda za nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho* ili kubaini tanzu ambazo hazikudhihirika kwa kusikilizwa kama vile utanzu wa maigizo. Beti zote za nyimbo zilizosikizwa na kutazamwa zilinakiliwa kama zilivyokuwa katika daftari na zikaweza kutumika katika uchanganuzi wa data. Aidha, mtafiti alizichanganua kwa kina habari asili kutoka kwa makala zingine kama vile majarida na tafiti zingine pamoja na mtandaoni kuhusiana na *Modern Taarabu-Mipasho* ili kumwezesha kuboresha msingi wake wa ufahamu wa mada hii ya utafiti.

1.17 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data kutokana na nyimbo za Taarabu zilizokuwa zimeteuliwa awali ulifanywa kama ilivyokuwa imependekezwa katika sehemu ya vifaa vya utafiti. Uchanganuzi wa data ulifanywa na kuhaririwa kuanzia mwanzo hadi mwisho wa utafiti. Uwasilishaji wa matokeo kutokana na data iliyochanganuliwa ulitolewa kwa njia ya maandishi na majedwali yaliyoambatana na maelezo ya moja kwa moja kwa msingi wa marejeleo ya data yaliyofanywa kutoka nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho* zilizoteuliwa. Hata hivyo, ni vijisehemu tu vya tanzu kwa kurejelea maneno, virai, vishazi, sentensi, aya na vifungu vya habari katika muziki teule wa *Modern Taarabu-Mipasho* ndivyo vilivyowasilishwa ili kusisitiza uwepo na umuhimu wa mwingiliano

tanzu katika *Modern* Taarabu-Mipasho. Kuhusu hili, Wanjala (2015) anasema kuwa utanzu ndani ya mwingine hudhihirika tu kupitia kwa fani na maudhui yake. Sababu ni kuwa maneno au yanayonukuliwa huwa sio kamilifu. Badala yake mhusika hunukuu vipande vya maneno alivyoviteua kwa makini kimaksudi. Hivyo katika utafiti huu, mtafiti aliepuka kurejelea tanzu katika upana wake wakati wa uchanganuzi kwani baadhi yake ni pana kiasi cha kutokuwa na mipaka maalumu. Data iliyokusanywa na kunakiliwa imeambatishwa mwishoni mwa tasnifu hii.

1.18 Hitimisho

Katika sura hii, mtafiti amejadili usuli wa suala la utafiti ambapo amefafanua kuwa kuna mitazamo miwili mikuu kuhusu asili ya Taarabu. Aidha, ameeleza namna *Modern* Taarabu-Mipasho ilivyotofautiana na Taarabu asili kimaudhui na hata kiutendaji. Uwasilishaji na maudhui katika nyimbo za *Modern* Taarabu-Mipasho yamezipa umaarufu ambao umeziwezesha kutamba kote pwani na hata bara katika mataifa mbalimbali ulimwenguni. Pia, ameshughulikia malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo wa utafiti na maadili ya kiutafiti yaliyozingatiwa katika utekelezaji wa utafiti huu. Hatimaye, amejadili yaliyoandikwa kuhusu Taarabu kabla ya kufafanua mbinu za utafiti zilizotumika katika kukusanya, kuchanganua, kufasiri na kuwasilisha data. Sura inayofuata imeshughulikia lengo la kwanza la utafiti huu ambalo ni kujadli mwingiliano tanzu katika uainishaji wa tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili.

SURA YA PILI

UAINISHAJI WA TANZU ZA FASIHI SIMULIZI YA KISWAHILI

2.0 Utangulizi

Sura ya pili imejikita katika kujadili lengo la kwanza la utafiti huu ambalo ni kujadili mwingiliano tanzu katika uainishaji wa tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili mintarafu ya nadharia ya Umuundo ili kuweka msingi imara wa kujadili lengo la tatu la utafiti huu hapo baadaye. Aidha, katika kushughulikia uainishaji wa tanzu za fasihi simulizi, sura hii imeshughulikia ushairi simulizi kama utanzu wa fasihi simulizi ya Kiswahili kwa kuwa nyimbo za Taarabu zimewekwa katika utanzu huu katika uainishaji huo. Hatimaye, ufafanuzi kuhusu muziki wa *Modern* Taarabu umetolewa kabla ya kuuchanganua katika ya sura ya tatu.

2.1 Misingi ya Uainishaji wa Tanzu za Fasihi Simulizi ya Kiswahili

Ngure (2003) na Muiruri (2006) wamefafanua uainishaji kuwa ni ugawaji wa vipera vya fasihi simulizi na uwekaji wake katika makundi mbalimbali kwa msingi wa vigezo maalumu. Hata hivyo, tatizo la uainishaji kama anavyodahili Ndungo (2006) ni kuwa tanzu wanazozifahamu au kuzifikiria watafiti mawazoni mwao kabla ya kwenda nyanjani hazilingani na tanzu zinazopatikana katika jamii wanazoenda kutafitia. Hali hii imesababishwa na kukosekana kwa nadharia zinazoongoza ugawaji wa tanzu za Fasihi Simulizi ya Kiswahili ambapo wataalamu wengi wamekuwa wakitumia vigezo mbalimbali katika kuainisha tanzu na vipera vya fasihi simulizi. Miongoni mwa misingi ya uainishaji huu kama anavyosema Muiruri (2006) ni pamoja na:

2.1.1 Majina ya Tanzu au Vipera

Kila utanzu na kipera huwa na jina ambalo ni tofauti na tanzu au vipera vingine.

Mifano ya majina haya ya tanzu ni kama vile utanzu wa hadithi, semi, mazungumzo maigizo nyimbo/ ushairi simulizi na ngomezi.

2.1.2 Mianza ya Tanzu.

Tanzu na vipera tofauti tofauti vina namna yake ya pekee ya kuanza. Kutokana na mianza hii, tunapata utanzu wa hadithi na kipera cha vitendawili katika utanzu wa semi.

Mifano; Utanzu wa hadithi/masimulizi

-Msimulizi: Hadithi! Hadithi!

Hadhira : Hadithi njoo!

Utanzu wa semi, kipera cha vitendawili-Mtegaji: Kitendawili!

Hadhira: Tega!

2.1.3 Miishio ya Tanzu

Kama tulivyorejelea uainishaji kwa msingi wa mianza, vivyo hivyo kuna uainishaji wa tanzu kwa msingi wa miishio. Kila utanzu na hata kipera huwa na namna maalumu ya kuhitimisha. Kwa mfano katika utanzu wa hadithi/ masimulizi, tamati inaweza kuwa “ ... wakaishi raha mustarehe”.

Katika kutamatisha kitendawili, mtegaji husema; “...nilienda Moyale (au mji mwingine wowote), watu wa huko wakaniambia nje niwasalimu. Je, mmepokea? Jibu ni...” Hapa mtegaji hutoa jibu.

2.1.4 Lugha iliyotumika

Msingi huu wa uainishaji hutumika kuainisha kwa kuchunguza tamathali za semi zilizotumika katika vitendawili na methali na kisha kuzigawa katika makundi mbalimbali. Kwa mfano:

Methali za istiari- Ujana ni moshi...
- Dunia msumeno hukata mbele na nyuma.

2.1.5 Maudhui

Kutokana na msingi huu, tunaweza kupata yaliyomo katika kazi husika ya fasihi simulizi yakitumika kuainisha. Mfano;

Utanzu wa nyimbo - Hodiya (nyimbo za kazi), Nyiso (nyimbo za tohara)

-Mbolezi (nyimbo za kuliwaza waliofiwa)

-Nyimbo za arusi, siasa, mapenzi miongoni mwa nyingine.

Utanzu wa semi- methali kwa kurejelea ujumbe ni kama vile;

Methali za majaliwa- Liandikwalo halifutiki

Methali za makanyo- Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

Utanzu wa ushairi – kifunga nyama, majigambo

Utanzu wa masimulizi – Ngano za mtanziko ambazo maudhui yake ni ile hali ya mvutano unaotokana na kuwepo kwa hali mbili au zaidi kinzani au tatanishi zinazowahitaji wasanii kufanya uamuzi baina ya hali hizo.

2.1.6 Jinsi ya Utendaji

Mifano ni katika utanzu wa hadithi ambao pia unajulikana kama masimulizi. Utanzu huu ulipata jina kutokana na kwamba huwasilishwa kwa njia ya kusimuliwa. Pia, maghani yamepata jina lake kutokana na kwamba huwasilishwa kwa njia ya kughaniwa.

2.1.7 Watendaji/Wasanii

Msingi huu hujikita katika msingi kuwa kila utanzu huhusishwa na watendaji wa hali, jinsia na umri fulani. Mfano ni nyimbo za watoto ambazo watendaji wake hutarajiwa kuwa watoto ingawa wakati mwingine huimbwa na watu ambao si watoto kwa sababu na miktadha tofauti tofauti. Pia, nyimbo za kitamaduni zinaweza kuainishwa kwa msingi wa jinsia. Kwa mfano katika jamii ya Waswahili, chakacha huchezwa na wanawake na vijana huku vugo ikichezwa na wanawake waliokomaa (Wamitila, 2003). Vile vile, kuna masimulizi aina ya khurafa ambayo yamepata jina kutokana na wahusika wake kuwa wanyama huku mighani ikiwa na wahusika ambao ni mashujaa. Ngano za mazimwi zimepata jina lake kutokana na wahusika wake kuwa ni mazimwi ambayo ni viumbe wenye uwezo mkubwa kuliko binadamu wa kawaida na pia husemekana kutisha sana. Pia, malumbano ya utani yameainishwa kwa msingi kuwa wanaohusika wanatarajiwa kuwa watani. Katika uwasilishaji wake, utani una kanuni za hali na namna ya kutokea. Mojawapo ya kanuni ni kwamba wanaotania lazima wawe ni watu wenye uhusiano na ukuruba mzuri kwa kurejelea utamaduni na ada kwani utani una mipaka yake. Hufanywa baina ya watu wanaofahamu lugha na jamii yao vyema.

2.1.8 Ala ya Utendaji

Katika msingi huu, vifaa vinavyotumika kuwasilishia utanzu au kipera fulani hutumika katika kukipa jina. Mfano ni ngoma ya *Isikuti* kutoka jamii ya Abaluhya kutoka sehemu

za Magharabi mwa nchi ya Kenya. Ngoma hii imepata jina lake kutokana na ala ya kienyeji ambayo ni ngoma inayochezwa kwa mtindo maalumu. Hivyo, *Isikuti* ni jina lenye maana mbili: aina maalumu ya uchezaji inayojulikana kama *isikuti* na ala maalumu ijulikanayo vile vile kama *isikuti* ambayo huchezwa kwa mtindo wa aina yake. Vivyo hivyo, kama ilivyofafanuliwa katika sura ya kwanza, sehemu ya usuli wa suala la utafiti, katika jamii ya Waswahili kuna msondo ambao ni utanzu uliopata jina lake kutokana na ngoma ya kitamaduni inayotumika katika muziki huu. Watendaji wa msondo huunda nusu duara wakitazamana na wacheza ngoma kwa mtindo wa msondo pamoja na wa chakacha.

Aidha, katika jamii ya Waswahili kuna utanzu wa Vugo, muziki ambao hujikita katika maandamano kutoka kwa bwana harusi hadi kwa bibi harusi kwa kusudi la kuwasilisha mahari na sherehe nyinginezo. Utendaji wa muziki huu huhusisha upigaji wa pembe za nyati ambazo zinajulikana kama *vugo* kwa kutumia vijiti kwa mdundo wa mapigo matatu ambao huambatana na milio ya ngoma. Kwa mujibu wa Bazmaleh (2006) vugo huchezwa na wanawake wakiwa wameshika pembe na kigongo kidogo cha kupigia pembe. Pembe hupigwa kufuata mlilo wa ngoma na mara moja moja huinuliwa juu kichwani zikipigwa kwa nguvu huku wakiimba mashairi mengi mazuri. Aidha, mistari mifupi ya nyimbo za kitamaduni zilizochanganywa na vipande vya nyimbo za Taarabu kwa ustadi mkubwa na wataalamu wa nyimbo za Taarabu huimbwa kwa kurudiwa rudiwa katika maandamano haya (Franken, 1986).

2.1.9 Msingi wa Wakati

Tanzu na vipera katika fasihi simulizi huhusishwa na wakati wa kipindi maalumu. Mfano ni katika utanzu wa nyimbo ambapo kuna kipera cha nyiso, nyimbo zinazorejelea wakati wa jando, hodiya, nyimbo zinazorejelea wakati wa kazi na nyimbo za vita kwa msingi

kwamba hutendeka wakati wa vita. Pia, kuna kipera cha sogu ambacho hurejelea mazungumzo wakati wa mapumziko.

2.1.10 Msingi wa Mahali Maalumu

Fasihi Simulizi imeweza kuainishwa kwa msingi wa mahali inatendeka. Kwa mfano ikiwa nyimbo zitaimbwa jandoni basi zitaiwa nyiso ; zikiimbwa matangani zitaitwa mbolezi ; na zikiimbwa harusini zitaitwa nyimbo za harusi. Kutokana na misingi hii, ni bayana kuwa vigezo vya kuainisha tanzu na vipera katika fasihi simulizi ya Kiswahili na katika jamii za Kiafrika ni vingi na tofauti tofauti kama walivyo waainishaji.

Licha ya kuwepo kwa misingi hii yote ya uainishaji, bado utata upo kuhusu misingi ya kuzingatwa wakati wa kushughulikia tanzu na vipera vyote vya fasihi simulizi ya Kiswahili. Swali ni kuwa ni uainishaji upi ulio mkamilifu, wa kuhusisha misingi yote au baadhi ya misingi na kwa nini ? Tatizo hili linakuwa changamano zaidi kutokana na suala la tanzu mbalimbali kuvunja mipaka yake na kuingiliana katika uwasilishaji wa kazi za fasihi simulizi ya Kiswahili, suala ambalo limeshughulikiwa katika utafiti huu. Mgogoro huu unazidi kudhihirika katika sehemu inayofuata ambayo itaangazia suala la uainishaji wa tanzu za fasihi simulizi lilivyoshughulikiwa na watu mbalimbali.

2.2 Mwingiliano tanzu katika Uainishaji wa Tanzu za Fasihi Simulizi ya Kiswahili

Mwingiliano tanzu hurejelea namna utanzu ulivyotagusana na tanzu zingine na matini yote kwa ujumla ili kuboresha uwasilishaji wa ujumbe. Kama anavyosema Mulokozi (1989) hakuna utanzu wowote ule uliojitosheleza ila tanzu huingiliana na tanzu zingine ili kufaulisha uwasilishaji wa ujumbe. Mwingiliano tanzu hutumiwa na msanii kwa kujua au kwa kutojua. Dhana ya mwingiliano tanzu inaondoa mipaka ya kazi husika na kuiweka wazi kutazamwa kwa kuzingatia jinsi ilivyojumuisha mitindo na mbinu mbalimbali kwa

mfumo uliosukwa taratibu ili kuwasilisha ujumbe wake. Wamitila (2008) anadahili kuwa mwingiliano tanzu katika kazi moja hutoa nafasi kubwa ya mhusika kujieleza barabara.

Utanzu³ wa Taarabu ni zao la fasihi simulizi ya Kiswahili ambao ni fasihi simulizi ya Kiafrika. Hii ina maana kwamba sifa zake za kiutendaji zinajikita katika utendaji wa tanzu zingine za fasihi simulizi ya Kiswahili. Mojawapo ya sifa hizi ni hali ya mwingiliano wa tanzu ambao hutumika na wasanii kwa kujua au kwa kutojua. Katika mapitio ya majarida, makala na vitabu mbalimbali, mtafiti hakukumbana na maandishi yaliyojikita waziwazi na kuzungumzia suala la mwingiliano tanzu katika *Modern Taarabu-Mipasho*. Hivyo, ni vyema kuangazia namna tanzu mbalimbali zilivyoainishwa na watu mbalimbali ili kupata msingi imara wa kujadili tanzu hizi zilivyoingiliana katika *Modern Taarabu-Mipasho*.

Historia ya uainishaji wa tanzu za fasihi simulizi ulimwenguni inahusisha vipindi tofauti na athari zake katika miainisho hii. Wanjala (2015) anasema kuwa uainishaji wa tanzu za fasihi simulizi ulimwenguni ulianza katikati mwa karne ya kumi ukiongozwa na mtazamo wa Ki-Aristotle. Mtazamo wa Ki-Aristotle ulinawiri zaidi katika kipindi cha urasmi-mkongwe na baadaye katika urasmi-mpya katika fasihi za kilimwengu. Wageni, wakiwemo watawala wa Kikoloni, Wamishenari na Wanaathropolojia walijihusisha na utafiti wa fasihi ya lugha za Kiafrika bila ya kuelewa vyema. Katika kipindi hiki, Bara la Afrika lilidhaniwa kutokuwa na fasihi na hivyo utafiti wa fasihi wa lugha za Kiafrika ulifanywa kwa lengo la kupata na kuhifadhi fasihi hii. Uhakiki wa aina hii (Ki-aristotle) huziwekea tanzu mipaka bayana.

Mtazamo huu ndio uliotumiwa na wageni kama vile Finnegan miaka ya sabini na kuweza kuzianisha tanzu za fasihi simulizi ya Kiafrika bila kuzingatia mwingiliano tanzu na

³Utanzu ni istilahi inayotumiwa kuelezea au kurejelea aina ya kazi mbalimbali za kifasihi. Inawezekana utanzu mkuu kuwa na vitanzu vingine mbalimbali. Kwa mfano, tanzu kuu za fasihi andishi ni riwaya, tamthilia, ushairi, hadithi fupi, wasifu, tawasifu na tarihi (Wamitila (2003). Kipera ni kikundi au kipengele cha fasihi simulizi kilichowekwa pamoja kwa sababu ya uwiano wake kimtindo, kiuwasilishaji, kimuundo na ki-mada.

kuweka mipaka baina ya tanzu hizo. Baadaye katika karne ya ishirini, wasomi na wanafasihi wa kwanza Waafrika wakiwemo P’Bitek, Ngugi Wa Thiong’o, Taban Lo Liyong’ walipata mafunzo kutoka kwa Wanaathropolojia kwa msingi wa uainishaji wa Ki-Aristotle. Hata hivyo, mtazamo huu unaenda kinyume kabisa na hali halisi ilivyo katika *Modern Taarabu-Mipasho*. *Modern Taarabu-Mipasho* hufuata mfumo wa tanzu tofauti tofauti kuumbana, kuchangiana na kuingiliana kama ilivyo na dhana ya mwingiliano tanzu. Haya ni maoni muhimu katika utafiti huu katika kutoa ufahamu wa uainishaji wa tanzu na vipera mbalimbali katika fasihi simulizi ya Kiswahili kwa mujibu wa wataalamu tofauti tofauti.

Uainishaji wa tanzu za Fasihi Simulizi ya Kiafrika na hasa ya Kiswahili umeshughulikiwa na wataalamu mbalimbali. Mmoja wa wataalamu hawa ni Mulokozi (1989) ambaye ameanisha tanzu sita za fasihi simulizi kama ifuatavyo: Mazungumzo, masimulizi, hadithi, semi, ushairi simulizi, na Maigizo. Hata hivyo, ingawa amejitahidi kuelezea na kuzigawa tanzu na vipera vya fasihi simulizi kwa kuzingatia vigezo vyote viwili, yaani umbile na tabia ya kazi inayohusika na kigezo cha muktadha na namna ya uwasilishaji wake kwa hadhira, anakiri kuwa bado hakuna wataalamu walioshughulikia suala hili kwa undani zaidi kwani tanzu za fasihi simulizi hutofautiana kati ya jamii na jamii. Vivyo hivyo, vigezo vyote hivi vinaweza kuingiliana. Kwa mfano, kigezo cha kidhima, kama vile kuonya au kuelimisha huweza kuonekana katika tanzu zaidi ya moja au hata katika vipera mbalimbali.

Mulokozi pia ametaja nyiso kama mfano wa tumbuizo ilhali si nyiso zote hutumbuiza. Vile vile, kigezo alichotumia cha namna ya uwasilishaji huweza kuingiliana kutoka utanzu mmoja hadi mwingine. Kwa mfano, katika utanzu wa masimulizi na mazungumzo namna ya kuwasilisha inaweza kufanana ilihali kimsingi hizi ni tanzu mbili tofauti. Pamoja na hayo, inakuwa vigumu kuona tofauti zilizopo baina ya tanzu wakati kigezo

cha wahusika kinapotumika. Kigezo hiki huweza kuingiliana katika utanzu mmoja na mwingine. Kwa mfano, unaweza kuwa na hadithi yenye wanyama, binadamu, mizimu na kadhalika.

Kwa jumla, uainishaji wa tanzu na vipera vya fasihi simulizi kama vilivyoainishwa na Mulokozi vinaingiliana kifani na kimaudhui hali inayochangiwa na mwingiliano tanzu katika fasihi ya Kiswahili na hili ni suala ambalo utafiti huu ulilenga kushughulikia. Hoja hii inasisitizwa na Mulokozi (1999) anaposema kuwa changamoto kubwa imo katika uainishaji wa vipera katika tanzu tofauti tofauti kutokana na uwezo wa vipera hivi kuvuka utanzu mmoja na kuingia katika utanzu mwingine. Anataja mfano wa ngano ambayo kwanza inaweza kubadilikabadilika kutoka kuwa tarihi, kisasili, khurafa, hekaya na mighani kwa wakati mmoja. Kama anavyoshadidia Wanjala (2015) maana na muundo wowote ule wa utanzu wa fasihi simulizi hubadilika kutegemea mutadha na matumizi yake katika jamii husika. Hali hii inadhihirisha mwingiliano tanzu na hivyo kuwa msingi bora unaoshadidia suala la utafiti huu.

Katika kufafanua athari hasi za kuweka mipaka baina ya tanzu za fasihi simulizi katika uainishaji wake, Senkoro (1996) anadhihirisha kuwa mipaka hii ni ya kidhahania. Kwa maelezo yake, sio kila wakati nyimbo za bembelezi ambazo ni za watoto huwa zimelenga watoto pekee. Wakati mwingine nyimbo zile huweza kuimbiwa watoto lakini maudhui yake yakawalenga watu wazima. Hali hii ni dhihirisho la ugumu wa kuziainsha tanzu mbalimbali kutokana na mwingiliano wake.

Matokeo ya utafiti wa Wainaina (2002) kuhusu visasili katika jamii ya Wakikuyu yalidhihirisha ufaafu wa kuishughulikia fasihi simulizi kama mfumo kamili bila kutenganisha tanzu zake kwa kuziwekea mipaka. Hivyo, ujumbe katika fasihi simulizi hukamilika katika mfumo mzima wa uwasilishaji ambao ni mwingiliano tanzu na wala

sio katika kuzitenga tanzu kwa misingi ya mipaka ya uainishaji wa mtafiti. Wainaina alitumia nadharia ya umuundo katika utafiti wake ili kudhihirisha mwingiliano tanzu katika ngano za visasili. Nadharia hii pia imetumika katika utafiti huu kusisitiza mwingiliano tanzu kutokana na namna inavyosisitiza kuangalia kazi ya kifasihi kwa kushughulikia jinsi vipengele vyake mbalimbali vilivyoingiliana katika kukamilishana kwenye uwasilishaji wake.

Katika makala yake moja yenye anwani “Majadiliano ya Tanzu katika Ushairi wa Kiswahili’ Mwamzandi (2002) alitanua dhana ya majadiliano kumaanisha semi tofauti zilivyowania kusikika katika shairi la ‘Mnazi: Vuta N’kuvute” kutoka diwani ya *Sauti ya Dhiki*. Katika makala hiyo, Mwamzandi alichunguza maingiliano ya tanzu za ushairi na tamthilia kwa kujikita katika vipengele vya kimaigizo, lugha ya kishairi, ploti, wahusika na mandhari ili kuonyesha suala nyeti la dhana ya tanzu. Katika kuhitimisha makala hii Mwamzandi (2002: 163) anasema kuwa:

“...ukweli kwamba hakuna tanzu isiyobadilika. Juhudi za mhusika ndizo humpelekea kuteua fani mahsusi itakayosadifu ujumbe wake.”

Hoja hii inaakisi hali ilivyo katika nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho* ambapo tanzu huingiliana na kubadilikabadilika wakati wa uwasilishaji wa ujumbe. Katika makala yake, alipata kuonyesha namna tanzu wa mashairi na tamthilia zinavyoweza kusuhubiana. Usuhuba huu katika utafiti huu unaleta dhana ya mwingiliano tanzu katika uwasilishaji wa nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho*.

Ngure (2003) ameanisha fasihi simulizi katika kile anachorejelea kama vipera vitatu vikuu:Utambaji/usimulizi ambao unajumuisha vijipera vingine mathalan ngano/hadithi, mighani, hekaya, visa vya kijanja, ngano za matanziko, visa-viini, khurafa/kharafa, visa vya mazimwi na miviga. Pili, ni tanzu fupi ambazo zina vijipera kama vile misemo, vitanza ndimi, mawaidha, vichekesho, malumbano ya utani, sogu na vitendawili. Tatu, ni

kipera cha ushairi-simulizi chenye vijipera kama vile: ukariri, ushairi wa kishujaa, nyimbo, malumbano/ulumbi na mighani. Kutokana na muainisho huu, Ngure amegawa fasihi simulizi katika migao mitatu tu kwa lengo la kurahisisha maelezo katika kitabu chake. Hata hivyo uainishaji wake una utata pale anaporejela migao mikuu kama vipera badala ya tanzu.

Maelezo aliyoyatoa Ngure (2003) kuhusu migao hii ni finyu mno kiasi cha kutojumuisha vipera na tanzu zote za fasihi simulizi kama vile utanzu wa ngomezi ambao haukutajwa kamwe katika muainisho huu. Aidha, kama anavyodahili Wanjala (2015), Ngure hakuelezea ufupi wa tanzu zake fupi. Huenda ikawa hali hii ilisababishwa na utata wa mipaka baina ya tanzu kutokana na tanzu hizi kuingiliana sana katika utendakazi wake. Mchango wa Ngure ni muhimu kwa utafiti wetu kwani unachangia kudhihirisha namna tanzu za fasihi simulizi ya Waswahili zimeingiliana kiasi cha kutobainisha mipaka yake.

Wamitila (2003) ameanisha fasihi simulizi katika tanzu nne kuu: hadithi/ simulizi, maigizo, ushairi na semi/tanzu bainifu. Yeye ametoa muanisho kwa msingi wa lugha iliyotumiwa katika uwasilishaji. Mchango wake mkuu katika utafiti huu ni maelezo yake kuwa mwingiliano kati ya vitendawili na methali sio wa ajabu. Vitendawili huweza kuwa katika muundo wa methali kwa maana kuwa kuna methali ambazo huchukuliwa pia kama vitendawili. Aidha, anakiri kuwa tunaweza kuuona mwingiliano huo tuangaliapo tanzu nyinginezo. Mwingiliano wa methali na vitendawili unadhihirishwa na mifano ifuatayo: Kitendawili: *Kuku wangu ametagia miibani*, jibu: *nanasi*. Methali: *Usiwe nanasi kutagia miibani*. Kitendawili: *Nina kishindo kikuu*. Jibu: *Kimya*. Methali: *Kimya kingi kina mshindo mkuu*. Pia, ameanisha kipera cha ngonjera katika utanzu wa maigizo na ushairi. Hali hii ni thibitisho la ilivyo vigumu kutenganisha baadhi ya vipera vya Fasihi Simulizi ya Waswahili kutokana na kuingiliana kwake katika muundo, dhima na utendakazi wake.

Muiruri (2006) ameanisha fasihi simulizi katika tanzu saba ambazo ni: hadithi, nyimbo, ushairi-simulizi, semi, mazungumzo, maigizo na ngomezi. Hata hivyo, anakiri ugumu uliopo katika kutenganisha nyimbo na ushairi-simulizi. Anasema kuwa tanzu hizi mbili zinafaa kuwekwa katika utanzu mmoja-nyimbo/ushairi-simulizi. Hali hii ni dhihirisho la mwingiliano tanzu unavyosababisha ugumu katika kuainisha tanzu na vipera mbalimbali vya fasihi simulizi kwani utendaji na uwasilishaji wake unalingana na kuingiliana sana. Pia, amefafanua kuwa nyimbo huhusiana na kuingiliana sana na tanzu mbalimbali za fasihi simulizi kwa kujumuisha matumizi ya utanzu wa semi, lugha ya mafumbo, methali, nahau na misemo. Aidha, baadhi ya nyimbo hutumia lakabu na misimu.

Tanzu zingine alizoorodhesha Muiruri (2006) ni pamoja na matumizi ya maigizo ambayo huhusisha ishara, miondoko ya mwili na maleba katika nyimbo. Isitoshe, utanzu wa ngomezi na matumizi ya ala zingine za muziki pia amezitaja kuwa muhimu katika kufanikisha utanzu wa nyimbo. Utanzu wa mazungumzo nao ameumetaja kama unaotumika katika kutoa nasaha pamoja na kudhihirisha ulumbi katika utanzu wa nyimbo. Muiruri (2006) anaendelea kusema kuwa baadhi ya nyimbo hutumia mbinu simulizi ambazo hutumika zaidi katika utambaji. Uainishaji na ufafanuzi huu ni muhimu sana katika kutoa msingi mwafaka wa utafiti huu unaotoa mwelekeo wa kuhakiki namna tanzu mbalimbali za fasihi simulizi zinavyoingiliana katika muziki wa *Modern Taarabu*.

Katika matokeo ya utafiti wake, Kenguru (2013) alibainisha kuwa ingawaje fasihi imeweza kugawanywa katika fasihi andishi na fasihi simulizi, mgawanyiko huu una dosari zinazotokana na ukweli kwamba fasihi andishi ina athari nyingi kutokana na kuingiliana na fasihi simulizi kwa hivyo mgawanyiko huu haustahili kuchukuliwa kama mpaka ambao hauwezi kuvukwa. Hoja hii inashadidia umuhimu wa kuchunguza muziki wa *Modern Taarabu-Mipasho* kwa kuzingatia mwingiliano tanzu ambao ni suala lisiloweza kuepukika.

Wanjala (2015) amejadili mwingiliano tanzu katika fasihi ya Kiafrika. Kulingana na maelezo yake, mwingiliano tanzu umeweza kudhihirika katika uwasilishaji wa nyimbo kutegemea jamii, muktadha, jukwaa na malengo yake. Mfano ni katika muktadha wa maombolezo ambapo kupitia kwa miviga, fanani anaweza kudhihirisha utanzu wa majigambo, mawaidha, ngonjera miongoni mwa nyingine.

Ingawa waandishi hawa wote wanaelekea kukubaliana kuhusu kuwepo kwa tanzu kama vile nyimbo, mashairi, ushairi simulizi na masimulizi, ni bayana kwamba kutokana na mapitio haya, uanishaji wao unatofautiana. Utafiti huu umeeleza sababu za tofauti hizi katika misingi ya uainishaji pamoja na tanzu kuingiliana kwa kiasi kikubwa hivi kwamba ilikuwa vigumu kuziwekea mipaka maalumu. Aidha, utafiti huu umetambua uwezo wa tanzu za fasihi simulizi kuingiliana sana na kubadilikabadilika kifani, kimaumbo na hata kimaudhui kwa kutegemea muktadha na namna ya uwasilishaji wake. Kwa mfano, ngano iliyopo katika masimulizi ni tofauti na ngano iliyopo katika maghani. Ufahamu huu ni muhimu katika utafiti huu katika kummakinisha mtafiti anaposhughulikia *Modern Taarabu-Mipasho*, azingatie namna tanzu na vipera mbalimbali vilivyoingiliana katika kupata uwasilishaji bora na kamili.

2.3 Nyimbo / Ushairi Simulizi wa Kiswahili

Finnegan (1977) na Sengo (1978) wanaeleza kuwa nyimbo zilianza pale tu binadamu alipoanza kupambana dhidi ya mazingira yake katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali. Mazigwa (1991) anafafanua kwamba nyimbo kama kipengele kimojawapo cha fasihi simulizi ni hazina ambayo huhifadhi na kusambaza mawazo juu ya maisha ya binadamu na maendeleo yake. Kurejelea Taarabu kama nyimbo katika utafiti huu kunatokana na maoni ya Timammy (2002) kuwa wimbo ni tamko lenye mahadhi na yenye ubeti mmoja au zaidi iliyokamilika kimaana katika muktadha. Aidha, anasema

kuwa wimbo ni fani inayowasilishwa kwa njia ya mdomo na ambayo ina mpangilio maalum wa kipekee tofauti na fani zingine za fasihi kama tamthilia na riwaya. Katika Taarabu, kila ubeti huwakilisha ujumbe ambao umekamilika. Maelezo haya ni muhimu kwa utafiti huu katika kuhakiki mtindo wa mwingiliano tanzu katika *Modern Taarabu-Mipasho* kwa kuzingatia kuwa Taarabu ni nyimbo zenye beti zilizokamilisha ujumbe wake.

Ufaraguzi ni sifa muhimu katika nyimbo za Waswahili. Waimbaji huwa na uhuru wa kufaragua wimbo fulani ili ukidhi mahitaji ya muktadha au sherehe tofauti na ile iliyotungiwa awali. Nyimbo kama vile za kusuta huweza kufanyiwa ufaraguzi na kutumika katika muktadha mwingine tofauti. Hali hii pia inajitokeza katika nyimbo za Kiafrika kama inavyodhihirishwa na watafiti mbalimbali. Kwa mfano Mwakasaka (1977) ambaye alifanya utafiti wa nyimbo katika kabila la Wanyakyusa, aliona kuwa sanaa ya kutunga nyimbo inahitaji kipaji maalumu, ujuzi wa kuwasilisha mawazo kiufundi na matumizi makubwa ya picha. Pia anasema kwamba wakati mwingine nyimbo huandamana na vifaa vya kimuziki.

Maelezo ya mtafiti huyu yalifaa utafiti huu katika kufafanua umuhimu wa muziki wa Taarabu katika jamii. Aidha, maoni yake kuhusu umuhimu wa mhusika kuwa na kipawa maalum, ujuzi na mawazo katika kufanikisha uwasilishaji ujumbe yanalipa uzito suala la utafiti huu. Utafiti huu unatarajia kuwa ujuzi wa kipawa maalumu anaozungumzia Mwakasaka katika nyimbo utaweza kushughulikiwa kupitia kwa kuhakiki mwingiliano tanzu katika *Modern Taarabu-Mipasho*.

Kutokana na juhudi za uainishaji wa tanzu za fasihi simulizi ya Waswahili, imedhihirika kuna utanzu wa ushairi simulizi ambao asili yake ni nyimbo. Muziki wa Taarabu umewekwa katika utanzu wa mashairi simulizi/nyimbo ya fasihi simulizi ya Kiswahili.

Kwa kuzingatia uainishaji huu, ni muhimu kuuzungumzia utanzu huu wa ushairi simulizi na au nyimbo katika sehemu hii ili kuweza kuweka ufahamu ufaao kuhusu sifa na uwasilishaji wa nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho* katika utafiti huu. Ngure (2003) anaeleza kuwa ushairi simulizi una pande mbili muhimu : msemaji na msikilizaji. Msemaji hana budi kuhakikisha kuwa amechochea hisia, ameamsha ari, ametoa msisimuko, amemzindua msikilizaji na kumwathiri na yale anayosema. Pia, anatilia mkazo umuhimu wa kuwepo kwa ufundi maalum katika uwasilishaji ili kufaulisha malengo ya ushairi simulizi. Hoja hii ni muhimu katika utafiti huu kwani ni mojawapo ya nguzo za mwingiliano tanzu.

Nyimbo kama mojawapo ya tanzu muhimu za fasihi simulizi katika jamii ya Waswahili hutumika katika shughuli mbalimbali za kitamaduni. Miongoni mwa shughuli hizi ni kazi, michezo, mapumziko pamoja na sherehe tofauti tofauti. Isitoshe, umuhimu wa nyimbo hujitokeza katika sherehe mbalimbali za Waswahili kama vile mtoto anapozaliwa, mtoto anapopewa jina, wakati wa jando na unyago na katika harusi. Licha ya kuburudisha, nyimbo katika jamii ya Waswahili huwa na dhima ya kushauri, kuhimiza, kuliwaza, kuelimisha, kusuta na hata kuhifadhi mila na utamaduni wa jamii miongoni mwa dhima zake zingine nyingi. Kwa kufanya hivyo, nyimbo huweza kutoa mafunzo mbalimbali kama vile kuonya, kukosoa na kuadilisha jamii. Vivyo hivyo, nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho* ni muhimu kwa jamii katika kuiwezesha kukabiliana na changamoto mbalimbali anazokumbana nazo katika maisha ya kila siku.

Nyimbo za ushairi simulizi huweza kubeba maudhui mbalimbali kuhusu maisha, utamaduni, siasa, dini, elimu na mazingira ya jamii husika. Aidha, huweza kuwasilisha hisia mbalimbali zinazomkumba binadamu maishani ambazo ni pamoja na furaha, huzuni, ucheshi miongoni mwa nyingine. Isitoshe, Muiruri (2006) anasema kuwa nyimbo za ushairi simulizi zinaweza kushirikisha mbinu za kimaigizo zinazohusisha toni, ishara

na miondoko mbalimbali katika utendaji. Sifa hii ni miongoni mwa tunayoyashughulikia katika utafiti huu. Aidha, katika utendaji wake nyimbo za ushairi simulizi huhusisha viambata vingine kama vile maleba hali kadhalika ala mbalimbali za muziki. Maelezo haya yaliyotolewa na wataalamu mbalimbali kuhusu utanzu wa ushairi simulizi yanagusia muziki wa *Modern Taarabu-Mipasho* moja kwa moja kwani umo katika utanzu huu. Lililosalia katika utafiti huu ni kubainisha sifa zilizotajwa kuhusu ushairi simulizi katika muziki wa *Modern Taarabu-Mipasho* katika sehemu ya uchanganuzi wa data ya utafiti huu.

Kwa mujibu wa Finnegan (2012) sifa nyingine muhimu ya nyimbo za fasihi simulizi ni kuwepo kwa mhusika katika uimbaji wa nyimbo ili kuwasilisha ujumbe wa mhusika. Mhusika ana uamuzi wa kuelekeza wimbo kwa njia mbalimbali kama vile kuzungumza na hadhira katikati ya wimbo baada ya kusitisha wimbo ili kuteka nadhari yao na kuupitisha ujumbe sawasawa. Aidha, anaweza kuuliza hadhira icheze wimbo ule na kuimba pamoja naye. Kutokana na maelezo haya kuhusu nyimbo ni wazi kwamba nyimbo hutekeleza majukumu mbalimbali katika shughuli za maisha ya kila siku ya maisha ya mwanadamu. Hata hivyo, watafiti wote katika tafiti zao hawakubainisha mwingiliano tanzu katika nyimbo za Taarabu ya mipsho, suala ambalo limeshughulikiwa katika utafiti huu.

2.4 Hitimisho

Sura hii imeangazia maandishi mbalimbali ya watafiti wengine kuhusu taarabu na nadharia ya mwingiliano tanzu kutokana na uainishaji wa tanzu mbalimbali. Miainisho ya awali ya tanzu haikuzingatia mwingiliano tanzu unaopatikana katika utendaji wa tanzu hizi. Kila utanzu uliangaliwa kivyake kwa kuwekewa mipaka mahsusi. Pia kutokana na uainishaji huu, kuna utanzu wa ushairi simulizi pamoja na sifa zake ambamo nyimbo za

Modern Taarabu-Mipasho zinapatikana. Katika sura inayofuata, ninachanganua miktadha mbalimbali ya mwingiliano tanzu katika Modern Taarabu-Mipasho.

SURA YA TATU

MIKTADHA MBALIMBALI YA MWINGILIANO TANZU KATIKA MODERN TAARABU MIPASHO

3.0 Utangulizi

Sura hii imejikita katika uchanganuzi wa data, uwasilishaji na maelezo kuhusu miktadha ambamo tanzu mbalimbali zimejitokeza na kuingiliana katika nyimbo za *Modern* Taarabu-Mipasho zilizonukuliwa. Miongoni mwa mwingiliano tanzu uliojadiliwa katika sura hii ni baina ya *Modern* Taarabu-Mipasho na tanzu za maigizo, semi, mazungumzo, masimulizi, ushairi simulizi, na aina nyingine za nyimbo. Mwingiliano tanzu huu

umejadiliwa kwa kurejelea baadhi ya vipera vilivyojitokeza katika tanzu husika. Data iliyokusanywa katika utafiti huu ilihaririwa kuanzia mwanzo hadi mwisho wa utafiti ili kuichuja na kuhifadhi habari zilizokuwa na umuhimu katika utafiti huu. Uchanganuzi wa mwingiliano tanzu kutoka nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho* zilizokuwa zimeteuliwa na kunukuliwa umetolewa kwa njia ya maelezo ya kina na ya moja kwa moja. Ukokotaji wa mistari, mafungu ya maneno na beti mbalimbali zilizodhihirisha mwingiliano wa tanzu mbalimbali katika nyimbo zilizoteuliwa umehusishwa katika uchanganuzi wa data. Ufuatao ni uchanganuzi kuhusu utanzu wa maigizo katika *Modern Taarabu-Mipasho*.

3.1 Mwingiliano wa Utanzu *Modern Taarabu- Mipasho* na Maigizo

Utanzu wa maigizo⁴ umeingiliana na ule wa nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho* zilizorejelewa katika utafiti huu kwa njia tofauti hususan maleba tofauti tofauti yaliyovaliwa, matumizi ya ishara na ishara za nyuso na hali kadhalika miondoko mbalimbali ya mwili. Wasanii katika maigizo huiga mambo yanayopatikana na namna yanavyoonekana katika jamii. Maigizo kama kipengele cha sanaa ya maonyesho huwa na sifa kama vile dhana inayotendeka, jukwaa, watendaji, hadhira, muktadha wa kisanii wenye ubunifu na kusudio la kisanii. Maigizo hutumia maleba maalumu kama vizuizui. Katika maigizo, matendo yaigizwayo na wasanii huwa si halisi kwa sababu wahusika wa kifasihi huwa si watendaji halisi ila hujitwika uhusika kwa muda tu kwa kusudi la kuwasilisha ujumbe ambao ungewasilishwa na wahusika halisi katika jamii. Katika *Modern Taarabu-Mipasho*, mhusika aghalabu huigiza matini ya nyimbo zake katika uimbaji wake ili kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe.

⁴Kwa mujibu wa Mulokozi (1996) na Muiruri (2006: 71), maigizo ni utanzu wa fasihi simulizi wenye mpangilio wa maneno ambayo huambatana na utendaji wa wasanii. Maigizo ni sanaa inayotumia watendaji kuiga tabia au matendo ya watu na viumbe wengine ili kuburudisha na kutoa ujumbe fulani. Mulokozi anasema kuwa maigizo ya Kiafrika huambatana na ngoma, mtambaji wa hadithi au matendo ya kimila.

Katika *Modern Taarabu-Mipasho*, maigizo yamefanywa kulingana na maudhui mbalimbali kama yalivyojitokeza katika nyimbo husika (mfano umetolewa katika kiambatisho **3-MC-Mpenzi Chocolate**- Mzee Yusuf). Mhusika katika utendaji wake ameigiza wimbo huu kwa kutumia ndege aina ya helikopta kuonyesha ufalme wake wa mapenzi. Aidha, katika uigizaji huu, Mzee Yusuf anadhihirisha uigizaji wa kifilamu ambapo anapoanza kuimba anatua kutoka kwa ndege. Amejitoa katika ulimwengu wake wa utamaduni wa Mwafrika na kuingia katika ulimwengu wa uigizaji wa Kimagharibi. Usafiri kwa ndege si wa kawaida kwa watu wachochole. Usafiri wa aina hii ni wa wachache ambao wanajiweza kifedha. Hili ni dhihirisho kuwa yeye kweli kama mfalme wa mapenzi ana uwezo wa kifedha. Ameabiri helikopta tayari kuondoka ili afike na kutua uwanjani palipo na hadhira yake inayomsubiri kwa hamu kumsikiliza akiwasilisha nyimbo zake za mipasho.

Mzee Yusuf amedhihirisha mwingiliano kati ya utanzu wa filamu, maigizo na *Modern Taarabu-Mipasho* akiwa katika ndege aina ya helikopta. Uigizaji huu pia ni namna ya kuonyesha mawazo yake ya kisasa ambapo anatumia usafiri wa kisasa, hali ambayo inaambatana na aina ya nyimbo anazoimba-*Modern Taarabu-Mipasho* ambazo zimejitenga kutoka Taarabu asili yenye kufuata utendaji na uwasilishaji wa kitamaduni. Aidha, Mzee Yusuf ameigiza akiwa amealia mavazi ya kifalme au Sultan huku akihudumiwa na wafanyikazi kadhaa katika uigizaji wake ili kuonyesha utukufu na haiba inayoambatana na maisha ya kifalme. Amevaa vazi laini la sari na kuzungukwa na mapambo mbalimbali katika chumba chake. Maudhui makuu katika wimbo huu ni mapenzi motomoto anayopewa mhusika na mpenzi wake ambaye anammiminia sifa telelele. Kukiwa na joto, mpenziwe anamtuliza kwa kumpepea na kukiwa na baridi kali, mpenziwe anampa joto. Anaigiza akilakiwa na kusaidiwa kubeba mizigo mizito, hata

akifuliwa nguo zake chafu na hata kupuuliziwa na kulishwa kama anavyofanyiwa mtoto kutokana na mapenzi mengi kwake.

Katika muktadha wa wimbo huu wa *Modern Taarabu-Mipasho*, mhusika amejawa na bashasha na ndipo anaamua kumpa mpenzi wake chokoleti na tende kudhihirisha mapenzi matamu anayopata. Aidha, analinganisha uzuri wa mapenzi anayopata na utamu wa chokoleti na tende. Hali hii ni dhahirisho la ufahamu wa mhusika kuhusu mambo ambayo hutendeka katika ulimwengu wa kimapenzi. Kwa kawaida, watu wanapopendana hudhihirisha mapenzi yao kwa namna nyingi tofauti. Miongoni mwake ni kule kubusiana na kukumbatiana, kulakiana na kusaidiana katika majukumu mbalimbali kama vile kukuna nazi na hata kufua nguo.

Ukunaji nazi na ufuaji nguo ni kazi za wanawake katika utamaduni wa Waswahili. Kwa mwanamume kufanya kazi hizi basi itakuwa ni kwa hiari yake na kwa sababu zake binafsi. Hata hivyo, kufanya kazi hizi hakutaidunisha nafsi ya yule mwanamume kwani atakuwa amechagua yeye mwenyewe kufanya hivi. Mwanamke anayesaidiwa kufanya kazi hizi hufurahia na kuhisi amependwa na yule mpenzi wake. Katika muktadha wa wimbo huu, Mzee Yusuf aliamua kufanya kazi hizi kutokana na mapenzi mazuri ya kuridhisha aliyokuwa amepata kutoka kwa mpenzi wake. Mpenzi wake aliweza kumpikia chakula kitamu na kisha kumlisha. Katika muktadha wa utendaji wa Taarabu hii, Mzee Yusuf alimuuliza mpenzi wake ataje lolote alilotaka kufanyiwa naye angefanya ndipo mpenzi wake akaamuuliza amsaidie kukuna nazi. Kisha, Mhusika huyu anaigiza akimsaidia mkewe kufua nguo kama njia nyingine ya kuonyesha penzi lake kwake. Mwanamume wa Kiafrika akionekana akifanya kazi kama hii ya kukuna nazi, baadhi ya watu humwona kama ambaye ametawaliwa na mkewe ambapo husemwa kuwa ‘amekaliwa na mkewe’.

Aidha, wapenzi huweza kutumia majina ya kuvutia na ya kilakabu kwa wapenzi wao katika kujaribu kuelezea hisia zao za kimapenzi. Sababu ni kuwa ni muhali kuweza kuzielezea hisia za kimapenzi kwa kutumia maneno ya moja kwa moja. Badala yake, maneno yenye kuleta athari za mguso na hisia za kimapenzi hutumika. Mfano: **3-Mc - 6-‘Yeye ndiye Chocolate wangu’**. *Chocolate* ni kitafunio ambacho huwa na sukari na kakau na ambacho huyeyuka kinapotiwa mdomoni. Ladha yake ni tamu kwelikweli na yenye harufu ya kuvutia. Aidha, anayeelezea hisia zake za kimapenzi hutumia maneno yanayodhihirisha kusalitika kwake kimapenzi kama ilivyobainika katika kiambatisho kifuatacho. **3-Mc**

- 10 Unaponukia udi, malaika hunisimama mie’
 21 Ye ndio kila kitu kwangu, mpenzi chocolate
 22 Ye ndio binti wangu sisikizi yoyote,
 23 Kama ni tamu,
 24 Nairamba, alivyotia,
 24 Kama ni hamu,
 25 Naipenda , aniswabilia`
 26 Ananitia nakshi, nakshi mahamumu,
 27 Kumwacha sitaki, nitajidhulumu.
 28 Kidonda tamu nzi ndo hufia,
 29 Hapa patamu ndio maana nimetulia
 30 Dhahari wazimu champari nimevua
 31 Ananitia nakshi, nakshi mahamumu

(3-MC)

Kutokana na kifungu hiki, mhusika huyu yuko radhi kupenda mpenziwe kwa namna zote zile wala hatabanduka kamwe. Haoni haja ya kusikiza maneno ya watu wengine kuhusu mapenzi yao. Heri afie pale kama nzi kidondani! Matendo na maneno katika wimbo huu yanadhihirisha kuwa mtu akishapenda ni vigumu kumgeuza nia kwa lolote lile kama anavyodhihirisha Mzee Yusuf. Mhusika huyu anaigiza ufalme wake wa kimapenzi katika himaya yake ya kidhahania. Baadaye, Mzee Yusuf anamalizia kwa kuigiza akirejea katika kupaa na kuondoka kwa ndege iliyomleta alipoanza. Katika sehemu hii, ile ishara maarufu inayoashiria mwisho wa uigizaji katika filamu, **‘THE END’** inaonyeshwa na uimbaji unakamilikia pale.

Mfano mwingine wa mwingiliano tanzu wa maigizo na *Modern Taarabu-Mipasho* umo katika kiambatisho ***6-Fs-Full Stop*** - Taarabu iliyoimbwa naye Khadija Kopa. Mhusika huyu anatoa onyo na kutaka mambo kadhaa yakome. Miongoni mwa anayopendekeza yakome ni pamoja na wafitini wanaoingilia ndoa za watu, vijana wanaoshiriki mapenzi kiholelaholela na wanawake wanaojivunia utamaduni wa kigeni. Katika uimbaji huu Khadija Kopa ameonyeshwa akinyoosha mkono wake kila anapotaja neno ‘*fullstop*’ kama ishara ya ‘kutia kikomo’. Aidha, ametumia neno ‘*Fullstop*’ ili kusisitiza ujumbe wake wa kutaka masuala anayotaja yakomeshwe mara moja.

Katika kuwakomesha wafitini, Khadija Kopa ametumia moto unaowaka sana na kuwaonya wasiuguse wasije wakaungua. Moto huu ni ishara ya hatari iliyomo kwa watu wale wafitini wanaoingilia ndoa za watu, wanawake wanaojivunia utamaduni wa kigeni na vijana wanaoshiriki mapenzi kiholelaholela. Pia, katika wimbo huu, mmeigizwa tabia mbaya ya wanawake wanaopigania mabwana. Ili kudhihirisha msimamo wake kuhusu kudumisha mila na utamaduni wa Kiafrika, mhusika huyu na wanaoigiza naye wanavalia khanga na shanga na kubeba vibuyu. Haya ni maleba ambayo huvaliwa katika utamaduni wa Kiafrika. Pia, uchezaji wao katika wimbo huu ni wa kitamaduni kulingana na utendaji wa nyimbo katika fasihi simulizi ya Kiafrika. Hali hii imeshadidia msimamo wa Khadija Kopa wa kudumisha utamaduni na kuasi mkengeuko unaoambatana na tabia ya kigeni. Amewaongoza vijana ambao ni wachezaji wake katika kuvaa na kucheza kwa njia ya utamaduni wa Kiafrika.

Mwingiliano tanzu mwingine kati ya utanzu wa maigizo na *Modern Taarabu-Mipasho* unapatikana kwenye kiambatisho ***20-UJ-Utalijua Jiji***- Afua Suleiman. Baadhi ya sehemu zilizoigizwa ni pale mhusika anapomsuta mwanamke mwenzake kwa kumwambia maneno yafuatayo:

26. Unaningoja njiani, madhila kunifanyia

27. *Usitake ushindani, hunishindi nakwambia*
 28. *Mimi naletewa ndani, wewe watanga na njia*
 29. *Magomeni buguruni, ndara zakukatikia.*

(20-UJ)

Uigizaji wa sehemu hii unaonyesha wanawake wawili wakipigana baada ya mmoja kumvizia mwenzake njiani. Hii ni hali ambayo hutokea hasa baina ya wanawake washindani wa mapenzi. Mwanamke ambaye amedhulumiwa kimapenzi atafanya lolote kupigania penzi hilo hata kama ni kumvizia mbishi wake vichochoroni ili amfunze adabu kwa kumchapa. Vita hivyo huwa ni vya ghafla kwa anayevamiwa. Wanawake wanaopigana hutumia viungo vyao vya mwili kama vile mikono, miguu na hata meno katika kuwaadhibu wenzao. Aghalabu, vita vya aina hii huleta aibu kubwa pale wanawake wanaopigana wanapoangushana kiholela huku wakiraruliana nguo hivyo kuonyesha uchi wao.

Mashambulizi ya aina hii pia huwa na madhara mengi kwa wapiganao kwani huacha maumivu ya mwili pale wanapokwaruzana ngozi kwa kucha zao au wanapoumana kwa meno. Aidha, hupata majeraha ya nafsi zao kutokana na uchungu waliopata pale wanapopigana. Mahusiano baina yao huweza kuharibika kabisa kutokana na uhasama wa kimapenzi. Hii ndiyo hali inayompata mwanamke wa kwanza wakati anapoviziwa na mbishi wake anayeonekana kuwa na hamaki nyingi kutokana na hali ya mateso ya kimapenzi aliyopitia. Anabururwa huku akizabwa makofi yanayofuatana kwa mfululizo.

Katika muktadha huu, Afua Suleiman anaonekana kujigamba kuwa hashindikiki katika uwanja wa mapenzi. Kisha anajigamba kuwa yeye huletewa kila kitu nyumbani ambapo katika uigizaji wa kanda hii anaonekana akiletewa mavazi kama vile khanga na mwanamume husika. Anamsuta mwanamke mpinzani wake ambaye katika kanda hii anaonekana akihangaika kutafuta hadi ndara zinakatika. Ndara kukatika ni ishara ya kutembea kwa muda mrefu katika hali ya kuhangaika akitafuta riziki. Huu ni uendelezaji

wa vita vya maneno baada ya mhusika kuvamiwa kwa kuviziwa njiani. Inamlazimu amsute mpinzani wake wa mapenzi kwa maneno yaliyojaa kejeli, ya kumdunisha, kumdharau na kuumumiza moyo ili amwachie mpenzi wanayebishania. Mwanamke huyu anaonekana akiwa tayari kabisa kulinda himaya yake ya kimapenzi aliyoinyakua kutoka kwa mwanamke mwenzake kwa namna yoyote ile inayowezekana hata ikiwa ni kwa meno na ukucha.

Mwanamke aliyenyang'anywa mpenzi kwa kubaki na machungu anaweza kuamua kutafuta wapenzi wengine kama alivyofanya mrejelewa katika mpasho huu. Hii ni njia moja ya kulipiza kisasi kwa mwanamume ambaye ni mpenzi wake kwa kuleta machungu kwa mwanamume pale atakapomwona na mwanamume mwingine. Pia, ni njia ya kujipatia kipato alichokosa kutokana na kutoshughulikiwa na mwanamume aliyemwacha. Pale tu anapoingia katika mtego huu, wanaume humtumia kama kiburudisho lakini baadaye wakamsema kila anapopita kutokana na tabia yake ya kuwa uasherati. Haya yamesemwa kama inavyodhihirika katika mishororo ifuatayo:

- 30. *Wasela wa vijiwani, nafuu wajipatia*
- 31. *Uroda kwa foleni, kwako wajipendelea*
- 32. *Wewe gumzo mjini, watu wanahadithia*
- 33. *Umeachika ndoani, kwa yako mbaya tabia.*
- 34. *Unaogea jikoni, bafuni unapikia*

(20-UJ)

Mwanamke mwigizaji haachi kumsuta mwenzake kuhusu tabia yake mbaya. Kawaida, chakula hupikiwa jikoni. Mazingira ya jikoni yanatarajiwa kuwa safi kwa ajili ya usalama wa kiafya kwa wanaotarajiwa kula chakula kilichopikiwa humo. Hivyo, hali ya mwanamke huyu kupikia bafuni ni ya kutatanisha na haifai hata kidogo. Bafuni watu huenda kuoga. Basi iweje chakula kikapikiwa bafuni na kuoga kukatendeka jikoni? Tabia kama hii haikubaliki popote kwa kiumbe razini. Matamshi ya usutaji kama haya hutumiwa na wanawake kuchongoana ili kuonyesha uzuri na ubora wao uliowapelekea

kuteuliwa na mwanamume dhidi ya wanawake wenzao. Mengi huwa yamepigwa chuku ili kumpaka tope mpinzani asipate nafasi yoyote katika maisha ya mwanaume wanayemng'ang'ania.

Katika muktadha ulioigizwa, mwanamke anayejisifu anamkejeli mwenzake kuwa hafai kitu, hapendeki ila anajiuza kwa wanaume ambao wanaonekana wakiwa wamepanga foleni nje ya chumba kidogo wakiwa wameketi kwenye benchi kila mmoja wao akisubiri zamu yake. Hii ndiyo hali ya mipasho, matusi yanaendelezwa bayana bila aibu. Mwanamke mrejelewa anaonekana akitoka nje na kibatari mkononi akiwaita ndani wanaume waliosubiri mmoja baada ya mwingine ili kushiriki ngono nao. Hatimaye, anakuwa gumzo mtaani ambapo watu wanaonekana wakimsema pale anapopita kutokana na tabia yake mbaya ya usherati. Isitoshe, mwanamke huyu ambaye anarejelewa kama 'mshamba' anaonekana katika kanda hii akipikia bafuni huku akiogea jikoni. Huenda ikawa hii ndiyo sababu ya mwanamume wanayebishania kumkataa na kuwatafuta mwanamke mwingine mwenye ujuzi wa mapishi, kujitunza na kumtunza mume. Pia, huenda ikawa ni hali ya kumharibia sifa mwanamke mtajwa ili apoteze hamu ya kuzozania mpenzi na mwanamke husika.

Aidha, katika wimbo huu, mambo ya uganga na maswala ya kishirikina yameigizwa. Mhusika anamkejeli mwanamke mwenzake kuwa katu hamwezi hata akienda kwa waganga na waganguzi na kuwa atamaliza mizizi bure kwani kumlea mume kwataka ujuzi. Mhusika anadhihirisha ufahamu wa vita vya kimapenzi na mazingira yake ambapo wanaobishania mpenzi huweza kuendana hata kwa waganga kama njia moja ya kumpata mpenzi wanayebishania kama ilivyowekwa wazi na kifungu kifuatacho:

37Utamaliza mizizi, waganga na waganguzi

38Talasimu na hirizi, ongeza na vipodozi`

39Kwake hupati nafasi, mimi ndio yake pumzi

(20-UJ)

Mhusika amefungamanisha uigizaji huu na uimbaji wa *Modern Taarabu-Mipasho* na kuufanya ujumbe wake uvutie na uwe na uhalisia. Hii ni hali mojawapo ambapo mwingiliano tanzu umedhihirika ukiboresha uwasilishaji wa ujumbe.

Mwingiliano tanzu umedhihirika tena kwenye uigizaji katika kiambatisho **15-UKSU-**

Umejuaje Kama Si Umbea- ulioimbwa na Mwanaidi Shaaban.

*34Milango uliyofunga, gonga misumari gonga, fanya ukuta ujenge pia,
35Weka mtu wa kuchunga, hutaniona kusonga, sasa Mungu kanifungulia,
36Ulie ukining'ong'a, ati mi wa moja kanga, hali ishanibadilikia,
37Jahazi kutoka Manga, kwangu limetia nanga, neema sasa nailalia.
38Hebu domo lako funga, kwangu mimi hutachonga, jua Mungu, ameshanilipia
(15-UKSU)*

Katika uigizaji huu, Mwanaidi Shabaan anaonekana akiwa katika jahazi ambalo limetia nanga. Yeye ndiye abiria pekee katika jahazi hili. Huu ni uigizaji wa safari ya maisha yake. Katika mkondo huu wa maisha, kila mja ana hadithi yake. Kuna wale watu ambao huzaliwa katika utajiri na wala hawaujui umaskini ni nini ila kwa kulisikia neno hilo tu. Hata hivyo, kuna watu ambao maisha yao tangu utotoni huwa ni ya taabu, mashaka na matatizo tele yenye kudhihirishwa na umaskini. Katika muktadha wa kifungu kilichonukuliwa hapo juu, mhusika ni miongoni mwa wale walioishi maisha ya umaskini kwa muda mrefu lakini ghafla wakaamka wakiwa wamefanikiwa. Mhusika anaeleza namna alivyobarikwa naye maulana na kujazwa na neema. Kimsingi, katika wimbo huu mhusika anazungumzia baraka tele alizopata katika maisha yake baada ya kupitia changamoto nyingi hapo awali. Anasifu kuwa ametoka katika lindi la umaskini na sasa ni tajiri kutokana na neema ya Mungu. Ndiyo maana akarejelea kuwa wambea walimsema kuwa yeye ni wa kanga moja kama ilivyo katika mstari ufuatao-

36. Ulie ukining'ong'a, ati mi wa moja kanga, hali ishanibadilikia. (15-UKSU)

Kanga ni vazi ambalo kwa kawaida katika mazingira ya pwani huvaliwa na wanawake. Mwanamke maskini aghalabu atatambuliwa kwa kuvalia kanga ile ile moja kila siku

huku aliye tajiri atabadilisha kanga kwani ana nyingi. Vazi hili la kanga huwa na maua na nakshi tofauti tofauti ambayo hulifanya livutie. Isitoshe, kanga huwa inatumiwa katika mawasiliano kwenye ujumbe ambao huwa umeandikwa kwa kurejelea maswala mbalimbali. Wanawake hujipamba kwa kanga zenye kuvutia katika sherehe mbalimbali za Waswahili. Katika kiambatisho tulichonukuu hapo juu, mhusika amefanikwa kutoka kuwa wa kanga moja na sasa ana kanga nyingi kuashiria kwamba maisha yake yamebadilika na kuwa tajiri. Mungu amemkumbuka mhusika kama alivyodokeza katika ukokotaji ufuatao:

37. Jahazi kutoka Manga, kwangu limetia nanga, neema sasa nailalia. (15-UKSU)

Kwa kawaida jahazi kutia nanga humaanisha kuwa limefika na safari imefikia hatima yake. Katika maisha ya kawaida, kila mja ana safari yake. Safari hii inaweza huwa na mikondo tofauti katika nyakati tofauti. Mikondo hii wakati mwingine huwa ni ya karaha lakini wakati mwingine ikawa ni ya baraka. Hii ndiyo maana Waswahili wakasema kuwa ‘Hujafa hujaumbika’. Hivyo, katika muktadha huu, jahazi la neema limetia nanga katika maisha ya mhusika huyu na kufanikisha maisha yake. Hii ni baada ya yeye kupitia hali yake ya karaha. Sasa kipindi cha baraka katika maisha yake kimewadia.

Matumizi ya jahazi katika uigizaji huu yanaonyesha kuwa mhusika anayafahamu mazingira yake. Usafiri wa sehemu ile mara nyingi huhusisha vyombo vya kusafiri baharini ambavyo hupitia na kutia nanga katika visiwa mbalimbali vilivyomo. Mhusika anaonekana akiwa ameshika makafi ya kuendeshea mashua, hali inayoashiria kudhibiti usukani wa maisha yake. Maisha yake hayana msukosuko tena, yamekwisha tulia sasa. Huu ni uigizaji ambao umeingiliana, kusukana na kukamilishana na utanzu wa *Modern Taarabu-Mipasho* katika kuboresha uwasilishaji wa ujumbe. Baada ya kuangazia utanzu wa maigizo katika sehemu hii, sehemu ifuatayo, itajadili mwingiliano tanzu kati ya utanzu wa semi na *Modern Taarabu - Mipasho* katika utendaji.

3.2 Mwingiliano tanzu kati ya *Modern* Taarabu - Mipasho na Utanzu wa Semi

Katika muziki wa *Modern* Taarabu-Mipasho, watunzi wameweza kudhihirisha utajiri mkubwa wa lugha na ubunifu kwa kutumia aina mbalimbali za semi⁵. Mifano ya semi tulizojadili kama zilivyoingiliana na utanzu wa maigizo na *Modern* Taarabu-Mipasho katika utafiti huu ni pamoja na methali, misemo, mafumbo na lakabu. Ufuatao ni uchanganuzi wa mwingiliano tanzu kati ya semi na *Modern* Taarabu-Mipasho

3.2.1 Utanzu wa Semi- Kipera cha Methali

Methali zimeingiliana na *Modern* Taarabu-Mipasho kama ilivyowekwa bayana na kiambatisho kifuatacho:

21- *WGO*- *Wagombanao*- Mzee Yusuf & Khadija Yusuf - Jahazi *Modern* Taarabu

1. *Kiitikio: Poleni wote wenye roho zoefu za majungu,*
2. *Mzee: Wagombanao,*
3. *Kiitikio: Ndio wapatanao,*
4. *Khadija: Walisema,*
5. *Kiitikio: Walimwengu.*
 - a. *Inshallah Salama, Sote twaomba salama.*
 - b. *Kwenu wote wenye chawa, msotuombea salama.*

(21-WGO)

Wagombanao, ndio wapatanao katika kiambatisho hiki ni methali ambayo imetumika kutoa ujumbe kwa mahasidi kuwa licha ya fitina na uzushi wao kuhusu kutengana kwao (waimbaji), sasa wamepatana na wanaendelea mbele na maisha yao. Kwa kawaida watu wanaogombana huwa na hamaki nyingi. Wakati wa kugombana hisia hupanda na watu wakakosana kiasi cha kutotaka kusemezana. Hatimaye, huingia hali ya utulivu wanapomaliza kugombana ambapo sasa wanaweza kuwaza kwa njia razini zaidi. Pale ndipo watakapogundua chanzo cha ugomvi wao. Katika muktadha wa kiambatisho kilichorejelewa katika mfano huu, baada ya kugombana, waimbaji walitulia katika hali ya

⁵Mulokozi (1996) anafafanua semi kama kauli au tungo fupifupi za kisanaaa zilizobeba maaana na mafunzo muhimu ya kijamii; ufafanuzi unaowiana na ule wa M'Ngaruti (2008). Aidha, utanzu wa semi husheheni vipera kama vile methali, vitendawili, mafumbo, misimu, lakabu na kauli-tauria. Licha ya kutoa ufafanuzi sawia na huu wa Mulokozi kuhusu semi, Muiruri (2006:45) katika ufafanuzi wake anaongezea kuwa utanzu wa semi huwasilisha ujumbe kwa njia fiche au yenye mkato. Pia, semi huhusisha taswira, tamathali za usemi na ishara katika kuwasilisha ujumbe.

kujichunguza na ndipo wakapata kutambua chanzo cha ugomvi wao. Waimbaji hawa wanaamua kuchukua hatua ya kusameheana na kuridhiana ili wasonge mbele na usanii wao uliokuwa umetia fora. Hakuna litakalawatenganisha tena. Wamegundua njama za mahasidi wao. Sasa wameamua kutupilia mbali uhasimu wao kwani wagombanao ndio wapatanao. Methali nyingine imetumika katika **22-TKT-Tuachen** **kama Tulivyo-Mohammed Ally.**

35Kimalizio;

36. *Majungu yenu ya bure, wenzangu* Mumedoda.
 37. *Fitina zenu za bure, wenzangu* Mumedoda.
 38. *Majungu yenu ni bure* Mumedoda.
 39. *Kanyaga Kobo*
 40. *Kwetu ndio kwanza mkoko unaalika maua.*
 41. *Nyie msitutie joto* Mtasumbua.
 42. *Kanyaga . Kobo*

(22-TKT)

Katika kiambatisho hiki kwenye kimalizio, mhusika anateta kuhusu watu wanavyolifitini penzi lao. Anawashauri wawaache jinsi walivyo katika penzi lao kwani ndio sasa penzi hilo linaanza kushika kasi pale anaposema **40. Ndio kwanza mkoko unaalika maua.** Mkoko huanza kuonyesha kunawiri na kukua kwake pale maua yanapoanza kuchanua. Kabla ya hapo ni vigumu kuona uzuri wa mkoko. ⁶Methali hii imetumiwa kuwanyamizisha wafitini ambao walikuwa wameanza kuongelea jambo lisilowahusu kwa kuwaambia kwamba, mambo bado, watulie waone uzuri zaidi wa lile linalowakera ukijidhihirisha. Katika kiambatisho hiki mhusika anawasuta wafitini wao kuwa wanawasumbua na hata hawajaona lolote. Wanajisumbua na kujitesa bure na maneno na majungu yao ambayo hayataathiri penzi lao. Yaani, ni mapema mno kwa hao wafitini

6

Methali ni kifungu cha maneno yanayobuniwa na kutumiwa kwa ufasaha wenye kuficha maana inayokusudiwa. Hutumia maneno machache katika kufumbia ujumbe mzito au hekima fulani (Muiruri,2006:47). Hata hivyo, Wamitila (2003) anaeleza methali kama nahau wa kimapokeo ambao una muundo fulani mahsusi, unaokumbukika na unaokusudiwa kuelekeza, kuadibu, kusuta, kulaumu na kushauri. Umapokeo katika methali ni muhimu sana kwani methali hupokezwa katika jamii. Umapokeo huu ni ishara kuwa methali husika inafahamika, kukubalika na kuidhinishwa na jamii kwani huwa ni mali ya jamii.

kuanza kulifitini penzi lao. Maudhi yake kuhusu fitina za wafitini wake anazionyesha pale anapopendekeza wazikanyage na kuzimaliza zile fitina (5.Kanyaga, Koboa).

Katika kiambatisho **8-UHH- Utaniona Hivi Hivi - Fatma Mahmoud** tunapata mfano mwingine ambapo methali imetumika na kuingiliana na utanzu wa *Modern Taarabu-Mipasho* kama ilivyodhihirika katika kifuatacho.

28. *Jabali Mungu anaona, si hofu zenu sina fundo,*
 29. *Hivi hivi mtaniona, si hofu vyenu vishindo,*
 30. *La kusema mimi sina, na moyoni sina fundo,*
 31. *Kaniongoza subahana, taratibu wangu mwendo,*
 29. *.Ada ya mja hunena, humpa nani kitendo.*

(8-UHH)

Kupitia kwa methali hii, mhusika anateta namna upole na uungwana wake ulivyochukuliwa visivyo hali ambayo ilimpelekea kudharauliwa. Anashitakia hali hii kwa Mungu ambaye ndiye mwenye nguvu za kuyaona matendo yote ya mwanadamu pale anaposema ***Jabali Mungu anaona, si hofu zenu sina fundo.*** Kama kiumbe mcha Mungu, amewasamehe wote waliomkosea na hana uchungu wowote tena moyoni mwake kwani Mungu amempa amani.

Baadaye anasema yeye hatakubali kudhalilishwa tena kwani nguvu zake zinatoka kwa Mungu. Matendo yake yanatosha kudhihirisha hili ndio maana ananena kuwa ada ya mja hunena ... Isitoshe, mhusika anadhihirisha hali ya machungu aliyoyapitia ambayo yamemfunza kutomwamini binadamu yeyote kamwe. Anaeleza hali yake hii kwa kutumia methali ***Muugwana akivuliwa nguo hasimami, huchutama*** kama ilivyo katika kiambatisho kifuatacho:

36. *Msimamo ndio huo, Mungu anatosha sana,*
 37. *Mungwana akivuliwa nguo, hasimami, huchutama,*
 38. *Mungu anaona, si hofu zenu sina fundo,*
 39. *Hivi hivi mtaniona, si hofu vyenu vishindo.*

(8-UHH)

Methali hii imetumika kwa maana kuwa muungwana akiaibishwa ambapo ni kama amevuliwa nguo na kuachwa uchi, hujihadhari kuficha uchi wake kwa kutosimama. Badala yake huchutama. Katika maisha ya kawaida, mtu akishaaibishwa na wenzake, huwa makini zaidi na wale anaojikusisha nao ili asiabishwe tena. Kuchutama kunaweza kuwa ni kujitenga au kutojikusisha na shughuli zinazohusu watu wasioaminika. Pia ni kuchukua tahadhari kabla ya hatari katika kile anachokifanya mwathiriwa ili kujinusuru kutokana na madhara yake.

Mwingiliano tanzu kati ya methali *Mla mla leo...* na *Modern Taarabu-Mipasho* umebainika katika kiambatisho **25- MB- Mambo bado- Fatma Yusuf**, kifuatacho:

- 23. *Wanaonichukia hasara kwao, wanajikata maini,*
- 24. *Wanaoninunia imekula kwao, mazali hamnipi pumzi sini*
- 25. *Mla mla leo, namfaidi mie, nyie yenu yamekwisha,*
- 26. *Punguzeni choyo, bata boy ninaye, nakula naye maisha.*
- 27. *Mkubali matokeo, siachani naye, mnajipandisha presha.*

(25-MB)

Katika kiambatisho hiki, methali hii ya ***mla ni mla leo mla jana kalani*** imetumiwa na mhusika kuwanyamazisha wanaomwonea kinyongo kwa ufanisi alioupata katika kazi yake. Anasema kuwa riziki yake inatoka kwa Mungu. Hana haja tena na fitina za waja. Yeye anafaidi kwa kupata tija yake leo licha ya wivu wao. Hili ni muhimu kwani kama ilivyo na methali ya *mla ni mla leo mla jana kalani*, kwake yeye ni afueni anapopata tija yake leo. Ya jana na kesho yamo mikononi mwake Maulana. Anawasuta wote wenye wivu kwa mafanikio yake ya kupata mpenzi anayemrejelea kama ***Bata Boy***. Anawaeleza wakome kujisumbua bure na wakubali ukweli wa mambo kuhusu mafanikio yake ya leo.

Kupitia kwa mifano hii ya methali, ni dhahiri kuwa utendaji katika utanzu wa *Modern Taarabu-Mipasho* umeweza kuhusisha methali katika uwasilishaji wa ujumbe wake. Methali zimo katika utanzu wa semi katika fasihi simulizi ya Kiswahili. Hivyo, tanzu hizi mbili zimeweza kuingiliana na kukamilishana katika kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe

uliokusudiwa. Sehemu inayofuata itaangazia jinsi misemo ilivyojitokeza na kuingiliana na *Modern Taarabu-Mipasho* katika utendaji wake.

3.2.2 Utanzu wa Semi- Kipera cha Nahau

Misemo kwa mujibu wa Muiruri (2006) ni mafungu yanayotumiwa na jamii fulani kwa namna maalumu ili kutoa maadili. Mafungu haya ya maneno huwa na maana fiche ambayo haielekei kuafikiana na maana halisi iliyohusishwa kwenye vifungu vyenyewe. Misemo ni kauli ambazo huelezea ukweli fulani. Misemo iliyodhihirisha mwingiliano na *Modern Taarabu-Mipasho* ni kama vile: 18. Wanipikia majungu ambao umewekwa wazi katika kiambatisho kifuatacho **1-KCR- Kijiba cha Roho.**

- 17. *Unachonga sana fulani, kuharibu jina langu,*
- 18. *Kwa mashoga majirani, wanipikia majungu,*
- 19. *Unachonga sana fulani, Mungu atakulaani,*
- 20. *Una nini rohoni, una jelas mwenzangu,*

(I-KCR)

Mlalamishi katika kiambatisho hiki ni mwanamke ambaye anamkashifu mpinzani wake kwa kumsemasema kwa watu na hasa majirani. Kama tulivyoona katika mipasho mingine, maudhui yaleyale ya wanawake kuzozania wanaume yamerudiwa sana. Mlalamishi anamsuta mpinzani wake kuwa ana kinyongo na ushuba wake na yule mwanamume mrejelewa. Anamshauri aache roho yake mbaya ama atakufa kwa wivu na kuzikwa nao. Huu ni nahau ambao umeingizwa katika kiambatisho hiki ili kuwasilisha maudhui ya wivu ambao mlalamishi anahisi kuonewa na mwanamke mwenzake. Aidha, mhusika anaeleza hisia zake kwa wanayebishania naye mpenzi katika kifungu kifuatacho

- 35. *Aidha ninamchuma, nachanulia mjini,*
- 36. *Ndo hayo yanokuchoma, yanokukata maini,*
- 37. *Unafanya kila jambo, kila jambo, unitoe duniani*
- 38. *Ni bure zako hujuma, huniwezi mwafulani.*

(I-KCR)

Yanokukata maini ni nahau ambao una maana ya ‘yanayokukera moyo’ au ‘yanayokuletea machungu moyoni.’ Nahau huu ni mwendelezo wa yaliyosemwa katika nahau uliotangulia. Bado mlalamishi katika muktadha wa wimbo huu wa *Modern Taarabu-Mipasho* anahisi kwamba, mpinzani wake ana wivu mwingi ambao unamkata maini kiasi cha kutaka kumuua. Mapenzi anayopata mlalamishi kutoka kwa mwanamume wanayezozania yanamtia mpinzani wake machungu moyoni. Mlalamishi anakiri kwamba, mpenziwe amempa mahitaji yake ambayo ni pamoja na chakula, vyombo vya thamani na hivyo hana shida yoyote. Hili linasababisha wivu kutoka kwa mbishi wanayezozania naye mpenzi kwani yeye hapati mahitaji haya kama ilivyo kwa mlalamishi.

Mlalamishi anamshauri mbishi wake ajiepushe na roho ya wivu ambayo haifai kamwe kwani hawatoshani mbele ya mpenzi wao. Wanawake wawili ambao wana uhusiano na mpenzi mmoja hutathmini kiwango cha mapenzi kutoka kwa mpenzi wao kwa kuangalia wanavyoshughulikiwa katika hali zote za maisha. Aghalabu, wataangalia aliyofanyiwa mwanamke mpinzani wake na kutaka wafanyiwe vivyo hivyo au hata zaidi ya hivyo. Hali kama hii ndiyo huzua uhasama baina yao kutokana na wivu unaoletwa na mmoja wao kutekelezwa majukumu yote na mpenzi wao kuliko yule mwanamke mwingine. Hii ndiyo hali ambayo ‘hukata maini’ kama ilivyo katika muktadha wa methali hii.

Hata hivyo, katika kiambatisho cha **2-NN-Nitadumu Nayo- Mzee Yusuf-** Mzee Yusuf ameapa akitumia nahau **Ona raha** kumaanisha kwamba, anafurahia penzi lao. Hapa, mhusika halalamiki kuhusu wenye wivu ila anajivunia penzi lao. Mzee Yusuf alikuwa anasifia penzi lao ambalo analithamini kiasi cha kuwa tayari kufa ili alilinde. Anadai kuwa jinsi wanavyopendana, hakuna la kuwatenganisha asilani. Anakiri kuwa haoni lolote baya kwa mpenzi wake. Ombi lake kwa Mungu ni kuwa awajalie yeye na mpenzi wake ili waweze kudumu katika penzi hili.

Siyo kila muktadha wa mapenzi katika muziki wa *Modern* Taarabu-Mipasho ambapo utapata wapenzi walilalamika. Wengine husifu uhusiano wao wa kimapenzi kutokana na namna wanavyofurahia uhusiano huo. Uhusiano kama huu huwa ni wa kuridhisha wapenzi husika. Anayependa na kupendwa kwa penzi la kuliridhisha huwa imara na hatetereki hata watu wengine wanapojaribu kumkosanisha na mpenzi wake. Hivyo, mhusika ameweza kudhihirisha hisia zake kwa kuingiza nahau wa ‘ona raha’ katika utendaji wa *Modern* Taarabu-Mipasho. Hali hii ndiyo inayobainishwa na kifungu kifuatacho:

- 36. *Oh, walahi naona raha raha kama nini*
- 37. *Kwake sioni karaha huyu wangu ayuni*
- 38. *Nitadumu naye kwa nguvu za Manani*
- 39. *Wan“ochonga tutakomaa nao*
- 40. *Na wachonge kimpango wao.*

(2-NN)

Vivyo hivyo, katika **4-PN-Penye Neema-** Miriam Mwinjuma katika kiambatisho hiki amedhihirisha mwingiliano tanzu wakati anapotumia nahau *Hata roho mkinitoa.* Mhusika ameutumia nahau huu ili kusesitiza kwamba kile alichomjalia mwenyezi Mungu atakihifadhi kwa lolote lile hata kama itamgharimu uhai wake. Anawashauri wanaomwonea kinyongo kwa neema aliyopewa na Mungu kuwa nao wamwombe Mungu awajalie neema yao. Alichopewa mja na Mungu hakiwezi kuondolewa. Aliandikalo Mungu kuhusu mja halifutiki. Hakuna anayeweza kuilalia bahati ya mwingine aliyopewa na Mungu. Juhudi zozote za kujaribu kumnyang’anya mtu bahati yake kutoka kwa Mungu katika muktadha huu, zitaambulia patupu. Kifungu kifuatacho kinaonyesha ulipotumika nahau uliojadiliwa:

- 30. *Jicho la ubaya kwangu,*
- 31. *Mnaloniangalia.*
- 32. *Mnaloniangalia,*
- 33. *Ndo mimi kanipa Mungu.*
- 34. *Ndo mimi kanipa Mungu.*
- 35. *Hata roho mkinitoa.*

(4-PN)

Nahau **Kaliwa kikao** umetumika katika kiambatisho kifuatacho- **5- SMH- Sina Muda**

Huo-Leila Rashid

38. *Yakunishughulisha kwako, mie sikijui,*
 39. *Yakunishughulisha kwako, mie sikioni*
 40. *We ni wa kuambiwa, hivi uso namacho,*
 41. *Si kikao kukaliwa, una nini chambilecho*
 42. *Muda nilopewa, wa kutafuta kinacho,*

(5-SMH)

Mhusika katika kiambatisho hiki, anawasilisha ujumbe kuwa hana wakati wa kupoteza kushughulika na mambo ya mtu asiye na thamani kwake. Anadai kuwa hata hana cha kumshughulisha au hata cha kukaa akimsengenyea mwenzake. Katika kifungu hiki, maneno haya ya mhusika yanadhihirisha kiburi na dharau kwa mrejelewa. Yaani ana nini cha kusemwa? Ana nini ili asengenye? Wakati alionao Leila ni wa kutafuta kinachomhusu, kushughulikia mambo yanayomhusu. Aidha, katika kiambatisho **3-MC-Mpenzi Chocolate-Mzee Yusuf**, nahau **malaika hunisimama mie** umetumiwa katika kifungu kifuatacho:

32. *Basi na ukweli, nakutamani wewe,*
 33. *Unifiche baridi, mwili joto uwe,*
 34. *Unaponukia udi, malaika hunisimama mie,*
 35. *Hamu hamu hizi, hebu nikumbatie*

(3-MC)

Malaika hunisimama mie, umetumiwa kwa maana ya 'kusionywa'. Katika ubeti husika, mhusika anakiri anavyomtamani mpenziwe ili amfae kwa joto na kwa baridi. Mtu anapopenda huvutiwa na mambo mengi ya yule ampendaye. Mojawapo ya mambo yale ni harufu nzuri ya mpenziwe. Mhusika katika kiambatisho hiki anakiri kuvutiwa na harufu nzuri ya marashi ya mpenziwe kiasi cha mwili wake kumsisimka! Anamwomba mpenzi wake amkumbatie ili kukidhi hamu yake kwake. Kukumbatiana ni mojawapo ya njia za kudhihirisha mapenzi ambapo mhusika katika kiambatisho hiki anasalitika

kimapenzi kiasi cha kutojizuia kuomba akumbatiwe na mpenzi wake ili aitulize hamu yake.

Nahau nyingine iliyodhihirisha mwingiliano tanzu katika semi na *Modern Taarabu-mipasho* imetumika katika kiambatisho **21-WGO-Wagombanao-Mzee Yusuf & Khadija Yusuf** katika kifungu kifuatacho:

- 29. *Khadija: Sisi bado,*
- 30. *Kiitikio: Tunasonga mbele, wanaona ghere.*
- 31. *Mzee: Hawaniwezi, ndo maana wananisema,*
 - a. *Wananchukia ndio maana wanaiteta sana.*
 - b. *Msinichafue.*

(21-WGO)

Ona ghere katika muktadha wa kifungu hiki ina maana ya ‘kuona wivu’. Nahau huu umo katika muktadha ambao unarejelea wafitini wanavyowagonganisha watu waliokuwa na umoja na waliokuwa wamependana. Baada ya waliogonganishwa kuwatambua waliowagonganisha, wanaamua kuridhiana na kuendelea mbele na ushirikiano wao. Hapa ndipo wanaposema kuwa waliowafitini wanaona ghere. Wanawaonea wivu kwa umoja wao. Hawahisi vyema kwani uhasama waliotaka uwepo umeisha. Waliowagombanisha wameamua kutupilia mbali tofauti baina yao na kusonga mbele na maisha yao kwa amani.

Aidha, katika kiambatisho **7-KMKV-Kila Mtu Kivyake Vyake-Khadija Kopa**, kuna matumizi ya nahau kama kiambatisho hiki kilivyodhihirisha:

- 5. *Ye kesho nawa mikono kwako, jua hatahadhirika*
- 6. *Hababaishwi na urembo wako, waudhi ye keshachoka.*
- 7. *Pita mbele usigeuke, kila mtu kivyake*

(7-KMKV)

Nahau huu **kesho nawa mikono** umetumika kwa maana ya ‘yeye amekwisha malizana nawe’ au ‘yake na yako yamekwisha’. Hana haja naye tena. Katika muktadha huu kuna mwanamke mmoja ambaye anamzomea mwenzake kuhusu mume wanayempenda wote. mhusika katika kifungu hiki anamshauri mwanamke wanayepishania mpenzi kuwa huyo

mume ameshamwacha. Mhusika huyu anadai kwamba hata huyu mwanamke mwenza akijipitisha pitisha mbele ya huyu mume, bado hatamchukua. Anamkejeli kuwa urembo wake haumshtui ila unaudhi na kumchosha yule mwanamume wanayezozania.

Kutoka kiambatisho **15-UKU-Umejuaje kama si Umbea** tunapata matumizi yafuatayo ya nahau: **Endelea kunichimba, nenda kwa wachawi omba, jua Mungu hapigi kwa fimbo,**

Nahau wa **kunichimba**, umetumiwa na mhusika katika muktadha huu kwa maana ya kufitiniwa. Kama yalivyo maudhui makuu katika kiambatisho hiki, mhusika anamshauri mfitini wake atie bidii kumfitini. Yeye hana shida na fitina hiyo kwani kwa sasa haimdhuru. Fitina hiyo haimhusu chochote kwa kuwa amepata afueni kutokana na hali yake kubadilishwa na baraka alizopokea kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hii ndiyo maana anaendeleza nahau hii kwa kumdhihaki mfitini wake kuwa hata asikomee kwa fitina tu, akitaka aende kutafuta msaada wa wachawi kwani mhusika anajua kuwa hatafaulu pale Mungu alipoamua kufungua milango ya baraka.

Katika kiambatisho kifuatacho cha **29-KM- Kazi Mnayo-Mohamed Ally**, kuna mfano mwingine wa katika Modern Taarabu-Mipasho.

7. Ndio maana mtoto shoo, yuko mikononi mwangu
8. Bure kuumia roho, kuwa na chuki dhidi yangu.

(29-KM)

Mhusika katika kiambatisho hiki ametumia nahau **mtoto shoo** katika kujigamba kuhusu mpenzi wake wa kike ambaye wanapendana sana. Anamwita mtoto shoo kwa maana ya binti mrembo na anaengezea kuwa hayuko tayari kuachana naye kwa sababu ya fitina za waja. Wamependana sana kiasi cha kutoacha nafasi ya sumu yoyote ya fitina kuwa sababu ya kuwatenganisha. Anaposema kwamba yuko na mtoto shoo mikononi anamaanisha kuwa yule binti ni wake na wala hamwachilii kamwe licha ya juhudi za wenye wivu.

32- SS - Sitaki Shari- Leyla Rashid

12. *Wewe chokonoa sana, mori hutanipandisha,*

13. *Ugomvi siko tayari,*

(32-SS)

Mhusika katika kiambatisho hiki anasisitiza kauli yake kuwa hana haja ya kujiingiza matatani na wanaotaka ugomvi naye. Hakuna juhudi zozote zile za kumchokoza ambazo zitamfanya kukubali kushikwa na ghadhabu na kugombana na yeyote yule **(mori hutanipandisha)**. Wanaotaka kuchokonoa yaani kumtafuta maneno na ugomvi na wafanye hivyo sana lakini yeye hatasalitika kuingia katika hasira ya aina yoyote inayoweza kuleta ugomvi.

Hizi ni baadhi tu ya semi kama zilivyoingiliana na *Modern* Taarabu-Mipasho. Misemo iliyotumika ina mafumbo ndani yake ambayo huhitaji kufumbuliwa na mtu anayeelewa lugha ya jamii husika. Katika sehemu inayofuata, ninachanganua namna mwingiliano tanzu unavyobainishwa kati ya utanzu wa mafumbo na *Modern* Taarabu Mipasho.

3.2.3 Utanzu wa Semi- kipera cha Mafumbo

Kwenye muktadha wa data ya utafiti huu, kuna mwingiliano tanzu kati ya mafumbo⁷, maigizo na nyimbo za *Modern* Taarabu-Mipasho. Hii ni kwa sababu kuwa mengi ya yaliyojitokeza katika sehemu ya maigizo pia ni mafumbo. Mifano ya jinsi mwingiliano tanzu kati ya *Modern* Taarabu-Mipasho na mafumbo ulivyodhihirika ni kama ilivyowekwa wazi katika ukokotaji ufuatao:

8. Hapandi farasi, mzoa punda,

9. Noti si karatasi, dereva si konda,

(6-FS)

⁷Muiruri (2006) ameeleza mafumbo kuwa ni maelezo yaliyoficha maana na kwa kawaida hutumika kama chemsha bongo. Huwa ni maelezo marefu yenye kuficha kitu kilichofumbwa. Hubuniwa na mtendaji kwa shabaha ya hadhira maalumu. Kufumbua huhitaji uchunguzi na kufikiria kwingi. Baadhi ya mafumbo huhitaji jibu la neno moja huku mengine yakihitaji maelezo mafupi ili kufumbua.

Sio kila mwenye kuvaa nguo nyeupe ni daktari, wengine ni wauza nyama katika **6-FS-Full Stop-Khadija Kopa** na *Hapandi farasi, mzoea punda* katika **14-Z- Zilipendwa-Khadija Yusuf**. Haya ni mafumbo yenye kumaanisha kuwa kila mja ana kile alichokizea, alichona ujuzi kwacho au akijuacho. Wauza nyama na madaktari huvalia nguo nyeupe kama mavazi rasmi wakati wa utendaji kazi wao. Hii ni kutokana na kwamba wanahitajika kudumisha usafi na hivyo ni rahisi kwa mavazi meupe kuonyesha uchafu yanapochafuka. Katika hali ya kawaida ya maisha, taaluma ya udaktari inaenziwa kuliko kazi ya kuuza nyama. Hivyo, ni vyema kuwa makini ili kutofautisha muuza nyama kutoka kwa daktari kwani ingawa ujuzi ni tofauti, mavazi yao yanafanana.

Katika muktadha wa kiambatisho hiki, kuna fumbo la farasi na punda. Licha ya kuwa hawa ni wanyama wafugwao nyumbani, thamani ya farasi iko juu kuliko ile ya punda. Ni familia chache sana tena za kitajiri ambazo huweza kufuga farasi. Hii ni kutokana na kwamba kiasili, huyu si mnyama wa Kiafrika kati ya wanyama waliofugwa nyumbani. Huwa na matandiko maalum ya kukaliwa pale anapobeba. Kinyume chake ni mnyama punda ambaye hufugwa na jamii nyingi za Kiafrika na hasa watu wa kipato cha kadri na cha chini. Punda hana gharama nyingi na ghali katika ufugaji wake. Mara nyingi hufugwa pamoja na mifugo wengine kama vile ngo'mbe na mbuzi. Aidha, kimaumbile punda wengi ni wadogo kwa kimo kuliko farasi. Hivyo, mtu aliyezoea kupanda punda atatizika kupanda farasi. Hii katika kiwango kingine ina maana kuwa mtu aliyezoea maisha ya hali ya chini hana uzoefu wa maisha ya hali ya juu. Atahitaji muda kuzoea maisha hayo.

Katika kiwango kingine kwenye kiambatisho hiki, kuna fumbo la noti na karatasi. Kama ilivyokuwa na fumbo la muuza nyama na daktari, noti na karatasi zimetumiwa kutokana na tofauti yake kidhamana. Ingawa noti huundwa kutoka kwa karatasi, thamani ya noti

iko juu ikilinganishwa na ile ya karatasi. Karatasi inayoundiwa noti huwa imetengenezwa kwa ustadi mkubwa wa kuweza kustahimili hali tofauti kuliko karatasi ya kawaida.

Fumbo la dereva na konda pia limetumiwa katika kiambatisho kilichorejelewa. Ingawa wote hufanya kazi katika gari lile lile moja, kazi zao zinatofautiana katika utekelezaji. Kimsingi, kazi ya dereva ni kuliendesha gari huku kazi ya konda (utingo) ikiwa ni kuwa msaidizi wa dereva. Utingo humwelekeza dereva anapotaka kurudi nyuma kwa kuangazia vizingiti vyovyote njiani. Aidha, katika gari la kubeba abiria utingo huwa na kazi ya kupanga abiria na mizigo katika gari, kuchukua nauli na kumjulisha dereva kila abiria anapofikia mwisho wa safari yake. Hivyo, watu hawa wawili wana kazi mbili tofauti kabisa.

Mafumbo haya yote yametumiwa kama tahadhari kwa mja kuwa makini katika kubainisha aina mbalimbali za ujuzi walionao watu. Katika uwanja wa kimapenzi, sio watu wote ni wa kuaminika. Wengine ni wanafiki na hawafai kamwe!

Paka mapepe katika ***11- PM- Paka Mapepe- Ashura Majaliwa*** kumaanisha mwanamke mwenye machachari. Paka huyu ana sifa zilizooredheshwa katika kifungu kifutacho:

16. *Paka huyo paka, paka mapepe paka,*
17. *Umpe kuku na bata, yeye hatotosheka,*
18. *Umpe japo steki huyo paka, hatakushukuru huyo paka,*
19. *Atakutoroka huyo paka, akimwona panya huyo paka,*
20. *Kila umtendeavyo, bado atalalamika paka,*
21. *Mrithi kwa kila njia, mwisho atakutoka paka,*

(11-PM)

Paka anayerejelewa ni mwanamke ambaye hatosheki na penzi analopewa. Hakomi kukimbilia wapenzi wengine kwani ana tamaa isiyo kifani (***17. Umpe kuku na bata, yeye hatotosheka***). Anaelezewa kama mwanamke ambaye hana shukrani licha ya kila anachopewa (***18. Umpe japo steki huyo paka, hatakushukuru huyo paka***). Ameyaangaza

macho yake akiwa chonjo ili asipitwe na vitamu vingine kama afanyavyo paka amwonapo panya (**19. Atakutoroka huyo paka, akimwona panya huyo paka**). Mwanamke mrejelewa humwacha mwanamume aliye naye hata kama amemfanyia kila kitu na kumpa vinono pindi tu amwonapo mwanamume mwingine (**21.Mrithi kwa kila njia, mwisho atakutoka paka**).

Fumbo lingine limeingiliana na *Modern Taarabu-Mipasho* katika kiambatisho **20-UJ-Utalijua Jiji-Afua Suleiman** kama ifuatavyo;

- 31. *Uroda kwa foleni, kwako wajipendelea*
- 32. *Wewe gumzo mjini, watu wanahadithia*
- 33. *Umeachika ndoani, kwa yako mbaya tabia*
- 34. *Unaogea jikoni, bafuni unapikia*

(20-UJ)

Unaogea jikoni, bafuni unapikia- Fumbo hili limetumiwa kumsuta mwanamke mshamba ambaye ameshindwa kumpendeza mumewe kama mke. Anafanya kila kitu visivyo na kuwa kicheko midomoni mwa watu vijijini. Anaonekana kutenda mambo kinyume, hali inayompa mwanamke mpinzani wake nafasi bora ya kumyang'anya mume. Fumbo hili limetumiwa kumuonyesha mwanamke mrejelewa kama asiyejelewa na mwenye tabia zinazoudhi sana. Anafanya mambo kinyume au isivyo. Jikoni ni kwa kupikia na bafuni ni kwa kuogea katika hali ya kawaida. Mtu akionekana akifanya kinyume, basi huwa amechanganyikiwa.

Aidha, mwingiliano tanzu mwingine kati ya mafumbo na *Modern Taarabu-Mipasho* unaonekana katika kiambatisho chenye anwani **4-PN-Penye Neema - Miriam Mwinjuma** sehemu ifuatayo;

- 9. *Binadamu mshumaa, unawaka huku unakwisha*
- 10. *Na dunia ni hatari, wahenga walisibitisha*
- 11. *Ukiendekeza njaa, huendelei maisha,*
- 12. *Mungu kakuashia taa, na afadhali ya maisha.*

(4-PN)

9.Binadamu mshumaa, unawaka huku unakwisha ni fumbo lililotumiwa kurejelea mkondo wa maisha ya mwanadamu. Maisha yake hunawiri kama mshumaa uwakao lakini hatima yake ni kifo kama ufanyavyo mshumaa uliowaka ukaisha na kuzima. Msisitizo katika fumbo hili ni kuwa hakuna anayeweza kudumu milele ila kwa neema yake Maulana. Mwenye uzima na uhai ni Mungu pekee hivyo binadamu ajihadhari na dunia ambayo ina hatari nyingi mno zinazoweza kumwangamiza. Aidha, kuna fumbo lililoingiliana na muziki wa *Modern Taarabu-Mipasho* kama ilivyo katika kiambatisho kifuatacho **32- SS-- Sitaki Shari- Leyla Rashid.**

29. *Nimefunzwa nimefunzika, dunia nyumba ya shari,*

30. *Mabaya kuyaepuka, niishi na watu vizuri.*

31. *Wewe bure neng'eneka, kubwa langu kukunyari,*

(32-SS)

Katika muktadha wa kiambatisho hiki, mhusika anatoa kauli kuwa hataki kujihusisha na balaa. Analalamika kwa mabaya aliyotendewa na mumewe na ndiyo maana anasema kuwa hataki shari. Anajitetea kuwa alilelewa katika hali ambayo alifunzwa kutojihusisha na matata. Pia katika malezi hayo, alifunzwa kwamba dunia imejaa mabaya (**dunia nyumba ya shari**). Hapa analinganisha dunia na nyumba iliyojaa mabaya. Mabaya haya ni kama vile ugomvi, fitina, uhasama na matusi. Kila mja ana hiari ya kuchagua atakavyoishi katika ulimwengu wa aina hii uliojaa mabaya. Mhusika anaona ni heri ajitenge na mabaya ili aishi na watu kwa amani.

Kutoka kiambatisho **18-ZZ-Zoa Zoa-Mwanaidi Shaaban** kuna fumbo lifuatalo.

13. *Tuliza boli kiwanja ni kidogo*

14. *Tuliza boli haya si madogo*

15. *Tuliza boli kiwanja mimi si mdogo*

16. *Tuliza boli hutikizi gogo*

(18-ZZ)

Kwa mujibu wa maneno katika kiambatisho hiki, mhusika anatumia fumbo la kuzozania mapenzi na hali inavyokuwa katika uwanja wa kuchezea mpira. Uwanja wa mpira huwa

umewekewa mipaka yake mahsusi ambayo mpira hautakikani kuvuka. Katika uchezaji wa mpira wa miguu, mchezaji akiupiga mpira kwa nguvu zaidi unaweza kutoka nje. Hii ndiyo hali inayorejelewa kama ‘mpira kuwa mwingi na kutoka nje’. Hivyo, anayecheza kwa namna hii hushauriwa ‘atulize boli’ kwa maana kwamba acheze kwa utaratibu kwa kuzingatia mipaka iliyowekwa ya uwanja huo.

Katika ushauri wake kwa mpinzani wake, kwanza mhusika anamwaambia aache kasi ya kurandaranda akitafuta mapenzi kwa kuwa uwanja ni mdogo na una mipaka yake ambapo lazima mpira uchezewe ndani yake (***Tuliza boli kiwanja ni kidogo***). Pili, anaposema (***Tuliza boli haya si madogo***), ni fumbo linalomaanisha kuwa uwanja wa mapenzi una mambo mengi. Hivyo, anapomshauri mpinzani wake atulize boli anamaanisha kuwa apunguze kasi ya anavyong’ang’ania mapenzi kwani uwanja huu wa mapenzi una masaibu mengi ya kushughulikiwa yanayohitaji utaratibu.

Tatu, kwa kusema (***15. Tuliza boli kiwanja mimi si mdogo***), ni tishio kwa mpinzani wake kuwa licha ya kutokuwa na nafasi ya kuwatosha wote wawili kugombania mapenzi, na ingawa kuna mambo mengi yanayohitajika katika uwanja huu wa mapenzi, yeye ni hodari. Ni bingwa wa kuogopwa. Ana ujuzi uanaohitajika kukabiliana na hali zote za uwanja huu wa mapenzi. Hatimaye anaposema (***16. Tuliza boli hutikizi gogo***), bado ni msisititizo kuhusu uhodari wake pale anapomshauri mpinzani wake kuwa apunguze kasi ya kubishana naye kwani yeye ni gogo. Yuko imara na hatetereki kamwe.

Kiambatisho kifuatacho **21-TKT- Tuacheni kama Tulivyo-Mohamad Ally** kina fumbo lifuatalo.

13. Kiiitikio: Sumu mpe paka mwenye roho ngumu.
- a. Usimpe mbuzi utamdhulumu.
 - b. Mi sitoachana naye,
 - c. Labda mje mtupangie,

(21-TKT)

Katika unukuzi huu, mhusika anaonekana kuwashauri wenye wivu kwa penzi lake. Anampenda mpenziwe sana kama anavyoeleza katika muktadha wa wimbo ulionukuliwa katika kiambatisho hiki. Mhusika anatumia fumbo la kumpa paka sumu kurejelea hali ya penzi lao ambalo liko imara. Kwa kawaida, si rahisi kumuua paka kwani inasemekana kuwa ana uhai mara tisa. Juhudi za kumuua paka zinahitaji kuwa kubwa ili kufikia ule uhai wa tisa na kumtoa uhai. Mhusika katika kiambatisho hiki anajaribu kuonyesha kuwa penzi lao limekita mizizi kama uhai wa paka na hivyo si rahisi kulisambaratisha ila pengine kwa kumpa sumu.

Aidha, kiambatisho kifuatacho **24- NM- Nilijua Mtasema- Khadija Yusuph** kinatupa mfano mwingine wa fumbo katika taraab ya mipasho.

47. Siku zote ndimu changa inakuwa haina maji,... No research, no right speech. Ukiona nanga inatoswa kwenye maji, ujue jahazi limefika hilo, (24-NM)

Katika muktadha huu, mhusika ametumia fumbo la ndimu changa ambayo daima kama anavyosema yeye, haina maji. Hili ni fumbo linalodhihirisha kujigamba kwa mhusika. Yeye anajiona kama mhusika aliyekomaa na mwenye ujuzi katika uimbaji wa *Modern Taarabu-Mipasho*. Wengine wote bado ni wachanga kama ***ndimu changa*** isiyokuwa na maji ambao katika muktadha huu ni ujuzi. Hivyo basi wanastahili kumpisha awaonyeshe alivyokomaa kwa ujuzi wa uimbaji wa *Modern Taarabu-Mipasho*. Hii ndiyo maana anasisitiza kuwa ***jahazi limefika hilo*** kumaanisha mwenye ujuzi ambaye ni yeye yuko uwanjani anawasilisha analolijua vyema.

Katika kiambatisho **30-TIT-Top in Town- Khadija Kopa** , mhusika anasema kwa njia ya mazungumzo:

104. (Mazungumzo; uzuri wa ndege manyoya, uzuri wa mwanamke kujiamini bwana. Mwanamke screensaver bavu la nyoka (30-TIT)

Kiambatisho hiki ni wimbo wa Taarabu ya mpasho ambayo Khadija Kopa ametumia katika kujisifu kwamba yeye ndiye bingwa nambari moja mjini (*Top in Town*) katika uimbaji wa *Modern Taarabu-Mipasho*. Anapomalizia kuimba wimbo huu, anausifu uzuri wake. Kama ulivyo uzuri wa ndege katika manyoya ndivyo ulivyo uzuri wa mwanamke katika kujiamini. Uso wa mwanamke aliyejiamini ni kama *screensaver* kwa maana kuwa ndiyo utatangulia kuonekana kabla ya makalio ambayo huja baadaye. Kwa kawaida wanawake katika jamii ya Waswahili huthamini makalio yao sana na ndiyo sehemu ambayo huichezesha huku wakijiangalia kila wanapoimba ngoma zao tofauti. Hata hivyo, mhusika anasisitiza kwamba mwanamke hapaswi kujiamini kwa sababu ana makalio ya kuvutia ila anahitajika kuwa na uso wenye kujiamini kwanza halafu mengine yafuate baadaye kama ndege anavyojiamini kutokana na urembo wa manyoya yake.

Kutoka **15-UKSU - Umejuaje Kama Si Umbea - Mwanaidi Shaaban** ni kifungu kifuatacho ambacho kinabainisha fumbo katika Modern Taarabu-Mipasho.

56. *Hataki biriani yako, kalichagua bada langu.*
57. *Sima ya bada hujui kusonga, hujui kusonga sima ya bada.*
58. *Sima ya bada tamu,*
59. *Ipate mpishi timamu.*
60. *Ipate papa adhimu,*
61. *Utie na tui gumu,*
62. *Pia chachandu ya ndimu*
63. *Ukila huishi hamu, huishi hamu kuila.*

(15- UKSU)

Kiambatisho hiki kinazungumzia mapishi ya biriani na sima ya bada. Hili ni fumbo linalorejelea aina za mapenzi. Mhusika katika muktadha huu anaeleza kuwa biriani imekataliwa na badala yake sima ya bada ikateuliwa. Biriani/biryani ni chakula chenye asili ya Kihindi ambacho hurejelea mchanganyiko wa wali, nyama na mboga zilizopikwa kwa viungo mbalimbali. Sima ya bada ni chakula kinachotengenezwa kutoka kwa unga wa muhogo uliokaushwa. Muhogo huu huvunwa shambani, ukaambuliwa maganda, kisha ukakatwakatwa katika vipande vidogo vidogo na kukaushwa juani kwa muda wa siku

tatu au zaidi kutegemea makali ya jua. Baadaye, vipande hivi vilivyokaushwa hutwangwa katika kinu na kisha kuchungwa ili kutoa unga ulio laini tayari kwa mapishi. Mapishi ya sima ya bada huhitaji ujuzi na pia huchukua muda mwingi. Sima hii huandaliwa kwa maji kuchemshwa kwanza. Kisha mpishi huongeza unga wa muhogo na kuendelea kukoroga hadi uwe kama uji. Hatimaye mpishi huongeza unga wa mhugo hadi mchanganyiko huo uwe mgumu na kuupika kwa utaratibu hadi uive.

Hivyo, kutokana na ufafanuzi huu, penzi lililochaguliwa ni la yule ambaye anajua kutoa penzi kama alivyo mpishi hodari wa sima ya bada. Kwa maneno yake mhusika, yeye anajua kuisonga sima ya bada kwa maana kuwa anajua kuonyesha mapenzi. Hii ndiyo maana anasema kuwa ***sima ya bada tamu, ukila hauishi hamu, hauishi hamu kuila.*** Aidha, anapotaja viungo vya kuambatana na upishi na ulaji wa sima ya bada (***papa adimu, tui gumu*** na ***chachandu ya ndimu***) anadhihirsha kuwa anafahamu kinachohitajika katika kuleta mapenzi ya kuridhisha. Hivyo, fumbo hili linasisitiza kuwa mapenzi yanahitaji kupaliliwa kwa kushughulikiwa kwa namna mbalimbali kama yalivyo mapishi ya sima ya bada.

Fumbo la kukata kobe kichwa limejitokeza katika kiambatisho **9- JZ- Jinamizi- Mwanaidi Shabaan**

- 13. Kukata kichwa kobe, kwataka timing wewe,
14. Hunayo timing wewe!*

(9-JZ)

Kobe ni mnyama mwenda pole kwa utaratibu. Kobe anatambulika kutokana na kuwa hubeba gwanda lake ambalo hulitumia kama kinga na nyumba yake. Kinyume na anavyojulikana kuwa wa mwendo wa pole, kila anapopata tishio kobe huwa mwepesi sana wa kurudhisha kichwa na miguu yake ndani ya gwanda lake. Hivyo mtu anayetaka

kumkata kobe kichwa anahitaji kuwa makini na kuvizia kwa utaratibu ili apate kama hajarejesha kichwa ndani ya gwanda lake. Mhusika katika muktadha huu ametumia fumbo hili kumshauri na kumdhihaki mwanamke mpinzani wake wa mapenzi kuwa anahitaji ujuzi katika kupata mapenzi (*Kukata kichwa kobe, kwataka timing wewe*) anayoyatafuta sana. Tatizo ni kwamba, hana mbinu za kupata penzi hili (*Hunayo timing wewe*). Atahitajika kuwa mwangalifu na mwenye mpangilio maalumu katika kusaka na kupata penzi analolitafula. Mapenzi hayahitaji mtu kuwa na pupa. Yanahitaji utaratibu katika hatua zote ili kuyapata.

Mafumbo yaliyojadiliwa katika sehemu hii yamepatikana katika mipasho mbalimbali iliyorejelewa. Huu ni ushahidi kwamba kuna mwingiliano kati ya mafumbo na *Modern Taarabu-Mipasho*. Mafumbo yamo katika utanzu wa semi ilhali *Modern Taarabu-Mipasho* imo katika utanzu wa ushairi simulizi katika fasihi simulizi ya Kiswahili. Tanzu hizi mbili zimeingiliana katika uwasilishaji wa ujumbe kwenye mipasho husika na hivyo kudhihirisha mwingiliano tanzu katika *Modern Taarabu-Mipasho*. Vivyo hivyo, mafumbo yaliyoingiliana na *Modern Taarabu-Mipasho* yamejitokeza katika sehemu nyingine chini ya tanzu na vipera tofauti ikiwa ni pamoja na majigambo na mazungumzo. Hali hii ya mfano mmoja kujitokeza chini ya tanzu tofauti inabainisha namna mwingiliano tanzu ulivyo hali halisi katika uwasilishaji wa *Modern Taarabu-Mipasho*. Sehemu inayofuata itaangazia mwingiliano tanzu kati ya *Modern Taarabu-Mipasho* na Lakabu.

3.2.4 Utanzu wa Semi- Kipera cha Lakabu

Muiruri (2006) ameeleza lakabu kama majina yanayopewa watu kutokana na wasifu au sifa zao za kimaumbile, kitabia, kimsimamo, kimatendo au sifa zozote zile ambazo

huhusishwa na watu hao. Lakabu huweza kutumia ufananisho kwa njia ya moja kwa moja kwa kumlinganisha mtu na mtu, mtu na kitu au mtu na mnyama, ndege au mdudu. Majina haya huwa ni ya utani ambayo pia huwa ni ya msimbo au kupanga. Lakabu hutumika katika kuficha jina asilia. Mifano ya matumizi ya lakabu katika *Modern Taarabu-Mipasho* ni kama inavyodhihirika katika kiambatisho **6-FS-Full Stop-Khadija**

Kopa

50. *Semasema, Musa Musa. Musa mipango.*

51. *Mfalme wa bezi Tanzania.*

(6-FS)

Kwa kuitwa ***mfalme wa bezi***, ina maana kuwa Mzee Yusuf anatawala katika uchezaji wa bezi katika uwanja wa *Modern Taarabu-Mipasho* kama anavyofanya mfalme katika himaya yake. Ni mwenye mamlaka na heshima yote katika uimbaji wa *Modern Taarabu-Mipasho*. Anatambulika sana kwa ujuzi wake wa kucheza bezi. Aidha, Mzee Yusuf anaelekea kupendwa na wengi kutokana na kazi yake nzuri na ya kuridhisha katika uchezaji wake wa ala za mipasho.

Katika kiambatisho hiki cha ***6FS -Full Stop- Khadija Kopa-*** tunapata matumizi mengine ya kilakabu katika ukokotaji ufuatao:

35. *Halafu wajifanya unalipa, hutafuti wako ukamweka.*

36. *Wewe huezi miliki yangu, baby cute wa Kiafrika*

37. *Kwanza mimi niko peke yangu, nimetulia sina shaka.*

38. *Nimetulia na mume wangu, mtoto wa uhakika.*

(6FS)

Katika unukuzi huu, mhusika amerejelewa kama ***baby cute wa Kiafrika.*** Jina hili la kilakabu limetumiwa kusesitiza urembo wake mrejelewa. Yeye anajivunia ngozi yake asili ya Kiafrika ambayo haijapata mabaka kutokana na kujipaka vipodozi vya kigeni vyenye kudhuru ngozi. Kwa maneno yake mhusika, yeye ni mtoto mrembo wa Kiafrika ambaye anajiamini hata anapotulia na mume wake (***Nimetulia na mume wangu, mtoto wa uhakika***). Hana wasiwasi (***nimetulia sina shaka***) kuwa wanawake waliojipodoa na

kuharibu ngozi zao asilia wanaweza kumnyang'anya mume wake. Anatumia jina hili la kilakabu ***baby cute wa Kiafrika*** kujivunia asili na utamaduni wake wa Kiafrika na pia kama njia ya kutolea nasaha kwa wanawake wenzake wenye asili ya Kiafrika kujivunia rangi yao nyeusi.

Mfani mwingine ambapo lakabu imetumika ni katika kiambatisho **22- TKT- Tuacheni kama Tulivyo-Mohamad Ally**

34.Asante sana mfalme baba, tajiri wa upeo, mpendwa na wengi. Dr love. Haya mfalme, vijana wana hamu sana na wewe .Usiku imeshaingia. Wavalishe nevi sasa wakalale. Najiskia nimeota nikiwa nimelala. Hei ni Juma wenda ulaya mtoto wa Mwanza, sharubaru wa jahazi, ni mwendo wa defender sasa. Kamata mwizi men.

(22-TKT)

Mfalme baba, tajiri wa upeo, mpendwa wa wengi na Dr. Love ni majina ya kilakabu yaliyotumiwa kumrejelea Mzee Yusuf ambaye ni bingwa wa muziki wa mipasho katika kutunga, kucheza ala ya kinanda na kuimba. Katika nyimbo za Taarabu, wasanii husifiwa kutokana na weledi wao katika uchezaji wa ala mbalimbali au uimbaji wao. Waaidha, Mzee Yusuf anaitwa ***mfalme baba***. Katika muktadha huu, Mzee Yusuf ni baba (kiongozi) kwa wanaoimba na kucheza *Modern* Taarabu-Mipasho. Katika kikundi chake cha uimbaji, Mzee Yusuf ndiye kiongozi. Pia, kuna wasanii wengine kama vile *The Machupas Family* miongoni mwa wengine ambao wameimba chini ya uongozi wake. Hivyo, yeye ni kama baba mlezi wa wasanii na kiongozi mwenye weledi katika muziki wa *Modern* Taarabu-Mipasho.

Isitoshe, Mzee Yusuf anarejelewa kama ***tajiri wa upeo***. Katika muktadha huu, ana ukwasi mwingi katika utunzi, uchezaji na uimbaji wa nyimbo za *Modern* Taarabu-Mipasho. Katika muktadha huu yeye ndiye anayeweka mipaka ya umbali wa muziki wa *Modern* Taarabu-Mipasho. Upeo unadhihirisha kiwango cha juu. Mzee Yusuf ni tajiri wa maarifa yanayouhusiana na uwasilishaji wa *Modern* Taarabu-Mipasho wenye kudhihirisha utajiri

wa uimbaji wake. Hii ndiyo maana analimbikiziwa majina yenye sifa tele kama tulivyoona katika mifano iliyofafanuliwa.

Hatimaye Mzee Yusuf anarejelewa kama **Dr. Love** kutokana na nyimbo anazoimba. Katika nyimbo hizi, Mzee Yusuf anashughulikia maudhui ya mapenzi kwa kiasi kikubwa. Mhusika huyu ana namna ya pekee na yenye kuvutia ya kueleza mapenzi yake kwa mpenziwe na hata mapenzi ya mpenziwe kwake. Uteuzi wake wa maneno ni wa kugusa hisia za hadhira yake. Kuna wimbo ambao ameimba wenye anwani hii ya *Dr. Love* ambao hueleza anavyotibu vizuri na pia anavyofanya operesheni vyema baada ya kumpa mgonjwa dawa ya nusukaputi akalala usingizi mwanana. Maudhui ya aina hii hutuliza nyoyo za wapenzi wengi wa nyimbo hizi kama ilivyo na tiba atoayo daktari katika kutibu magonjwa mbalimbali.

Matumizi mengine ya lakabu katika *Modern Taarabu-Mipasho* yamedhihirika katika kiambatisho-**26- NS- Nipe Stara-Rahema Machupa**

21. (Asante sana Chidi Boy. Mkono wa baraka.)- Chidi Boy ni mojawapo wa wachezaji maarufu wa ala za muziki wa *Modern Taarabu-Mipasho* katika kikundi kinachoongozwa na Mzee Yusuf. Chidi Boy ni mweledi wa kucheza ala aina ya gitaa katika kikundi chao cha *Modern Taarabu-Mipasho*. Wakati mwingi wale wachezaji ala husifiwa na wasanii huku wakitambuliwa kwa kutajwa na kupewa fursa waonyeshe ujuzi wao wakati wa uwasilishaji wa muziki wa mipasho. Ni kawaida kwa wachezaji ala hao kucheza kila ala na kwa kubadilishana zamu kila wanapotajwa. Hivyo katika muktadha huu, Chidi Boy anatambuliwa kwa kuwa na mkono wa uchezaji gitaa ambapo amerejelewa kama ‘mkono wa Baraka.’ Huenda ni *Mkono wa baraka* kutokana na namna anavyonogeza muziki wa mipasho na kupelekea kushabikiwa na hadhira kubwa hali inayofanya wapate baraka za kipato chao.

Mchezaji mwingine, Fatha Mauji, anasifika na kutambulika kwa uchezaji wa ala aina ya kinanda. Jina la kilakabu analopewa ni **26. mkono wa dhahabu, mwaga sumu.** Anaenziwa kama dhahabu kwa kuwa na ujuzi wa kucheza kinanda. Dhahabu ni mojawapo wa kito cha thamani. Dhahabu huoshwa kwa kupitishwa ndani ya tanuri ya moto mara saba ili iwe safi kabisa. Kwa mujibu huu basi, Fatha Mauji ana mkono ulioimarika na kubobea katika uchezaji wa kinanda. Haya yamewekwa wazi katika kiambatisho kifuatacho:

31-KM-Kazi Mnayo-Mohamed Ally

26. [*Fatha Mauji, mkono wa dhahabu, mwaga sumu.*]

27. *Kwa chuki zao, watajibeba wao watajibeba,*

28. *Siku ya leo, watajibeba wao watajibeba,*

(31-KM).

Kiambatisho **3-MC - Mpenzi Chocolate-Mzee Yusuf** kinadhihirisha matumizi ya lakabu katika unukuzi ufuatao.

9. *Yeye ndio chocolate wangu, na mimi kwake kali,*

10. *Moyoni adhiti wangu, anayenificha baridi kali,*

(3-MC)

Mhusika anamrejelea mpenzi wake kama *Chocolate*. Kama ilivyoelezwa katika sehemu ya maigizo, jina hili la kilakabu limetumika na mhusika katika kukiri vile anavyompenda mpenzi wake kwa hali zote. *Chocolate* ni kitafunio au kinywaji kilichotengenezwa kwa ustadi mkubwa kwa kutumia kakau. Katika desturi za kizungu, *chocolate* hutumiwa na wapenzi katika kudhihirisha mapenzi. Aidha, kama kinywaji, *chocolate* hutumiwa kuondoa baridi kama kiburudisho. Hivyo basi, mhusika anapomwita mpenzi wake *Chocolate*, anamaanisha kuwa yeye ndiye dhihirisho la penzi lake kama ilivyo *chocolate*. Humwondolea baridi ya kimapenzi pale kama kinywaji cha *chocolate* kinavyofanya kuondoa baridi katika hali ya kawaida.

Matumizi mengine ya kilakabu yamebainishwa katika kiambatisho **9-JZ--Jinamizi - Mwanaidi Shabaan**. Anwani ya kiambatisho hiki ni '**Jinamizi**'. Anwani hii imetumika kilakabu kumrejelea mke-mwenza katika muhtadha wa maudhui ya kiambatisho hiki. Jinamizi kwa mujibu wa Kamusi Sanifu ya TUKI (2004) ni ndoto ya kutisha inayomfanya mtu ahisi au afanye lolote kwa sababu ya hofu. Mhusika amempa mke-mwenza jina la kilakabu, jinamizi, kutokana na namna alivyoyahangaisha maisha yake ya ndoa. Kama ilivyo hamu ya kuondokewa na ndoto ya kutisha, mhusika anaonyesha furaha yake kutokana na kuondokewa na mke-mwenza aliyekuwa kama jinamizi kwake kama anavyonena katika kifungu kifuatacho;

1. *Bora sasa, bora sasa x4*
2. *Limeniondokea mama x 2*
3. *Jinamizi hili mama, limeniondokea mama x2*

(9-JZ)

Kama ilivyo na mivutano katika ndoto ya kutisha, mke-mwenza anayerejelewa kama mtu aliyekuwa ameleta hali ya mvutano na mashindano katika ndoa husika. Mhusika anakiri kutokuwa na amani wala raha. Anajawa na wasiwasi kama anavyojawa anayekuwa na jinamizi. (**Tulokuwa tukishindania, yamekwisha. Tulokuwa tukigombania, yamekwisha**). Hata hivyo, suluhu inapatikana kutokana na mke-mwenza kutoweza kutulia na kisha akaondoka (**Ulipoanza manoki, nilijua utakwenda**). Sasa mhusika ana uhuru wa kutosha wa mapenzi katika ndoa yake. Ameweza hata kuyatoa mawazo haya ya kutisha kutoka maishani mwake. Furaha yake ya kuondokewa na tishio kubwa la mke-mwenza (*Jinamizi*) inadhahirika katika ukokotaji unaofuata.

7. *Ninaye huyu wangu sasa, raha zote kwake napata*
8. *Wasiwasi sinao tena, pekee yangu mimi nanyeta*
9. *Raha kwangu hamna vutavuta, ninadunda nimeukata*
10. *Mvuto wewe nimekufuta, nimeshinda bila ya vita x2*
11. *Mungu kanifanya starring, mimi mbabe wa sinema*
12. *Ndipo najimwagamwaga,*

(9-JZ-)

Kwake ukewenza ulikuwa ndoto mbaya tu ambayo sasa imeisha. Anaweza kutawala katika ndoa yake. Mambo sasa yametulia katika maisha yake ya ndoa kama ilivyo na mtu anayetoka kwa jinamizi (*Kwangu wewe jinamizi tua , jinamizi tu x2*).

Mifano iliyoangaziwa katika sehemu hii ni dhihirisho la jinsi uwasilishaji wa muziki wa *Modern Taarabu-Mipasho* unavyohusisha tanzu nyingine katika mifanyiko ya mwingiliano tanzu. Sehemu ifuatayo imejikita katika mwingiliano tanzu uliopo kati ya kipera cha majigambo na mipasho.

3. 3 Mwingiliano kati ya *Modern Taarabu-Mipasho* na Ushairi Simulizi-Majigambo

3.3.1 Majigambo

Wamitila (2003) amefafanua kuwa ushairi simulizi ni sehemu ya utamaduni ambao hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Ushairi simulizi una utanzu wa kitambiko, utanzu wa nyimbo na utanzu wa kisimulizi. Aidha kuna mpangilio maalumu katika utendaji wa ushairi simulizi kama vile sauti na takriri ili kuyapa nguvu maneno na matendo ya kimatambiko. Lugha itumiwayo katika ushairi simulizi huwa nzito, iliyosheheni mafumbo na ishara ambazo hueleweka na kutambulika na wanajamii wanaohusika na imani na mielekeo inayorejelewa. Hoja hii inaambatana na ya Muiruri (2006) ambaye anasema kuwa ushairi simulizi hutumia lugha ya kishairi na ya kipekee ambayo ni tofauti na ilivyo katika tanzu zingine za fasihi simulizi. Hutumia taswira katika kuhakikisha kunaswa kwa makini ya hadhira. Husheheni tamathali za usemi kwa wingi katika kuleta mvuto zaidi kwa hadhira. Hivyo lililosalia ni kuweza kuchanganua namna matumizi ya Ushairi Simulizi yalivyoingiliana na *Modern Taarabu-Mipasho*.

Majigambo ni kipera mojawapo katika utanzu wa Ushairi Simulizi. Mulokozi (1996) anadahili kuwa majigambo hutungwa kwa ufundi mkubwa mno kwa nia ya kujisifu. Aghalabu, anayejigamba husifia uhodari wake katika mambo mbalimbali kama vile ushujaa wake vitani, jandoni, kazini na kadhalika. Muiruri (2006) anaongezea kuwa muundo wa majigambo hutegemea shabaha za mtunzi na jadi anayoiwakilisha. Bila shaka kuwa bingwa katika usanii ni tendo la hadhi na kishujaa.

Katika data ya utafiti huu, mafumbo hayakujitokeza yakiwa pekee katika *Modern Taarabu-Mipasho* ila yameingiliana na maigizo na kufafanulia zaidi katika mwingiliano wake na utanzu wa semi. Mifano ya namna mwingiliano tanzu huu ulivyojitokeza kati ya majigambo na muziki wa *Modern Taarabu-Mipasho* ni kama ilivyo katika kiambatisho cha **6-FS-Full Stop- Khadija Kopa**. Katika kiambatisho hiki mhusika anawanyamazisha wote ili yeye apate kusema. Mtu wa kuwanyamazisha wengine lazima awe na usemi na hivyo mhusika huyu anajaribu kuonyesha ubabe wake kwa kuwanyamazisha wengine wote ili yeye apate kuongea. Anajigamba kwa kusema kuwa anayetaka kuongea hana budi kuomba ruhusa kutoka kwake. Hivyo yeye ndiye wa kuwapa wengine nafasi ya kusema, kumaanisha kuwa yeye ndiye mwenye mamlaka. Haya anayasema kama inavyobainika katika kifungu kifuatacho:

16. *Fullstop wote kimya, zubaisha king'ori naongea*
17. *Fullstop acheni kelele, na si rukhsa kujitetea.*

(6-FS)

Pia mhusika anajigamba jinsi alivyo mrembo na mwenye ujuzi wa kunengua kiuno. Katika wimbo wake, mhusika anaigiza akinengua kiuno na kurembua macho. Anaonekana kuyatambua maumbile yake na kuyadhihirisha pale inapohitajika. Urembuaji wa macho hutumika na wanawake kama njia mojawapo ya kusisitiza urembo wao. Mhusika huyu anafahamu umuhimu wa kujisifu kwa kutumia urembo wake. Katika muktadha huu ametumia urembo wake vyema hadi mwanamume aliyempenda

amesalitika kimapenzi kiasi cha kuzimikia kwake. Haya yamejitokeza katika mishororo ifuatayo:

21. *Na ninajua kunengua. Kanipenda, kanizimikia ukweli,*
22. *Nahasa pale, naporembua.*

(6-FS)

Mhusika anaendelea kujigamba kuwa ana ladha tamu na ndiyo maana mwanamume husika katika muktadha huu hamwachi. Anatoa onyo kwa wote ambao wanapenda kuwaiba waume wa wengine kuwa wakati wa kukomesha tabia hii umefika. Hawatapata hii fursa tena na watawachwa kavu kwani yeye aliye bingwa wa kunengua kiuno amewasili uwanjani. Kwa kujiona kuwa bora, anawaita wanawake wapinzani wake kwa shindano ili apate kuwakomesha tabia yao mbaya ya kuiba mabwana wa wengine. Anawaambia haya katika kifungu kufuatacho:

28. *Nina ladha sweeti sana, ndio maana hataki kutoka*
23. *Sasa wezi wa mabwana, nawaambia mtawachwa katwaa.*

(6-FS)

Hatimaye, mhusika anawasuta kwa kuwakejeli anaowasema kuwa wao ni watu duni. Hata hawafai kupata penzi lolote la maana. Hivyo wa thamana na wa kupata penzi la maana ni yeye pekee! Kwa kuwaona kuwa duni, anawadharau kuwa wao wanafaa wapenzi duni wa vichochoroni. Hawa ni wapenzi wasiokuwa na fedha, wasiojua kupenda wala kupendwa kwenyewe. Kutokuwa na fedha kunawafanya wafanyie shughuli zao katika mazingira duni ya vichochoroni, machafu, yasiyofaa, yasiyokuwa na usTaarabuu na kwa bei duni. Hivyo, hata mapenzi wanayojihusisha nayo ni duni. Hii ndiyo maana mhusika akawaambia yafuatayo:

Nyie, taipu zenu za vichochoroni, ndio zinazowafaa. (6-FS)

Khadija Kopa anaongezea kuwa wapinzani wake hawamwezi hata waje na waganga lori nzima, wafanye hata na kafara na wachinje paka. Yeye anajigamba hapa vile amekita

mizizi katika uwanja huu wa mapenzi. Madawa ya uganga hayamwezi. Ni hodari kiasi cha kutodhurika na kuendewa kwa waganga. Alishasema kitambo kwamba, anajua kupenda kwa kunengua kiuno na kurembua macho. Mbinu zozote zile kutoka kwa wapinzani wake hazimtishi kwani yeye ni bingwa wa mapenzi. Haya ameyadokeza katika maneno yafuatayo:

29. *Hata mje na waganga lori nzima, himaya yangu keshafika*
30. *Mnilie mizimu na makafara, na mchinje hata paka.*

(6-FS)

Aidha, katika muktadha huu, mhusika anaonyesha imani katika itikadi ya mambo ya ushirikina katika jamii ya Waswahili. Kama anavyosema Sengo (1992), itikadi ni taasisi iliyo hai katika tamaduni za jamii zote za wanadamu. Ushirikina ni sehemu ndogo katika itikadi za watu. Uislamu na Ukristo hazifunzi wala kuhimiza itikadi hii. Lakini baadhi ya waumini hujikuta wameegemea uwanja huu wa maisha. Itikadi za Waswahili wa mwambao wa Kenya ni pamoja na imani ya kuwepo pepo - majini, mashetani; nguvu na uwezo wa pepo hao katika kulinda mashamba, mali, miji, kusaidia kutibu maradhi, na mashetani kuroga. Itikadi hizi zina nafasi katika upwa wote wa Waswahili. Ujuzi wake mhusika umemfanya mwanamume anayerejelewa kukatalia kwake. Anajigamba kuwa yeye ndiye *baby cute* (mrembo) wa Kiafrika mwenye rangi yake isiyokuwa na mabaka na bado anatamanika (*Wewe huwezi miliki yangu, baby cute wa Kiafrika*).

Wanawake waliojipaka vipodozi (vikarolaiti) huwa wamebadilisha rangi ya nyuso zao ili wawe weupe na waweze kuwavutia wanaume. Hata hivyo, wakati mwingine nyuso hizo huathirika na kupata vibakabaka vya rangi nyeusi na kahawia na hivyo kukosa kuvutia. Wanawake wanaojipaka mafuta tofauti tofauti ili kubadilisha rangi ya ngozi zao hufanya hivi kwa imani kuwa wale wenye ngozi ya rangi ya kahawia wanavutia zaidi. Pindi wanapofaulu kubadilisha rangi za ngozi zao, wanawake hawa hupata kujiona kuwa bora kuliko wenzao wenye ngozi ya rangi nyeusi na hata kujawa na kiburi. Hata hivyo

mhusika anawakosoa anapojivunia rangi yake nyeusi isiyokuwa na mabakabaka ambayo ni ya mtoto halisi wa Kiafrika. Anasema kuwa kamwe hatamani ngozi yenye vibaka ambayo imemuudhi. Anajigamba kuwa hata na rangi yake nyeusi bado anawavutia wanaume (**42.Mimi nina rangi yangu, na tena bado nawaka**). Mhusika anayasema haya kama inavyodhihirika katika ukokotaji ufuatao:

- 39. Vikarolaiti vyenu, vinavyowapa jeuri,
- 40. Hivyo vikarolaiti vyenu, nitavipiga marufuku hapa.
- 41. Mimi nina rangi yangu, sitaki uso wa baka.
- 42. Mimi nina rangi yangu, na tena bado nawaka.

(6-FS)

Katika kuonyesha alivyodhibiti penzi lake mhusika anajigamba vile lilivyo imara. Anaeleza alivyotulia na mume wake bila wasiwasi kwani yeye ni mtoto hakika. Katika muktadha husika, anaonyesha kuwa mapenzi hayajengwi kwa rangi ya ngozi iliyopakwapakwa ila hujengwa na mwanamke kama yeye mwenye ujuzi wa kimapenzi unaohitajika. Hata hana mtu wa kubishana naye kwa mpenzi wake. Yuko peke yake. Hana wasiwasi kwani anafahamu namna ya kulidhibiti penzi lao. Anajisifu kwamba hakuna anayeweza kubishana naye katika milki yake ya mapenzi kama ilivyo usemi wake katika muktadha ufuatao:

- 36. Wewe huwezi miliki yangu, baby cute wa Kiafrika.
- 37. Kwanza mimi niko peke yangu, nimetulia sina shaka.
- 38. Nimetulia na mume wangu, mtoto wa uhakika.

(6-FS)

Majigambo pia yamejitokeza na kuingiliana na maigizo, semi na Taarabu ya mpasho katika kiambatisho **15-UKSU- Umejuaje Kama Si Umbea- Mwanaidi Shaaban** Mhusika katika kiambatisho hiki anajigamba alivyo mrembo, asiyehitaji kujitangaza katika usemi wake, kwa mfano, **15.Japo mie sijatamba, wala sio wa kujigamba, lakini sifichi langu pambo**. Kisha anamkejeli mwenzake anayependa udaku kuwa hana lolote la kufanya na hawezi kuzuia neema aliyoipokea kama anavyonukuliwa akiimba katika

mshororo ufuatao: **16. Kasirika sasa vimba, bure jua hutaziba, wewe jifunze ujue mambo** ila awe tayari kukubali mabadiliko yaliyojiri.

Msemaji ambaye katika muktadha huu ni mhusika anajigamba hana lolote la kumtisha hata mpinzani wake mdaku akiamua kutumia njia zozote ikiwa ni pamoja na kwenda kwa wachawi. Wachawi huhusishwa katika masuala mbalimbali ya maisha ya binadamu kwa kuaminiwa kuwa wana nguvu za kiajabu za kufanikisha mambo. Katika muktadha wa wimbo huu katika sehemu ifuatayo, mhusika anajigamba kuhusu kutotishwa kwake na wanaomwonea kijicho hata wakiamua kwenda kwa waganga kumfungia dua yake. Anadai kuwa Mungu amemkumbuka na kumfanikisha katika maisha yake. Katika kifungu kifuatacho mhusika anawaambia maadui zake hivi:

17. Endelea kunichimba, nenda kwa wachawi omba, jua Mungu hapigi kwa fimbo,

18. Adabu yako elewa, nimefanikiwa mie, nimeongokewa mie, nimejaliwa mie

(15-UKSU)

Mhusika anadai kuwa amejaliwa kuvaa vizuri na si wa khanga moja tena. Khanga ni vazi la kitamaduni linalovaliwa na wanawake Waswahili wa pwani. Katika hali ya kawaida mwanamke anatakikana kuwa na khanga kadhaa, tena safi. Akiwa na moja basi ni ishara ya umaskini. Isitoshe, ameneemewa hadi sasa anapanda **Rav4**, gari ambalo ni kubwa la kifahari. Anashiriki pia katika kikundi sifika cha wanamodern taarabu- *Melody*. Haya yamejitokeza katika kiambatisho kifuatacho:

23. Unaona fi, uliona mie kuvaa

24. Siachi, kuvaa mie siachi.

26. Siachi, kupanda Rav4 siachi.

27. Unaona fi, mie kuenda melody,

28. Siachi, kuenda melody siachi.

(15-UKSU)

Katika muktadha huu mhusika anajigamba kwa ufanisi alioupata kwani Mwenyezi Mungu amemfungulia milango ya baraka. Kwa kauli mbiu yake anasema kuwa ni vigumu kuliziba jua kwa ungo kwa maana kuwa bahati yake kutoka kwa mwenyezi

Mungu haiwezi kuzuiwa kwa vyovyote vile sawa na jinsi jua haliwezi kuzuiwa kwa kitu au kifaa chochote. Jua liko juu sana na lazima liangaze wakati wake ukifika. Si rahisi kwa mwanadamu kulifikia jua ili alizuie. Hivyo baraka ya mhusika huyu iko juu imewekwa katika nafasi ambayo imeinuliwa na kuangaza. Hakuna anayeweza kuizuia kwa vyovyote vile. Hii ndiyo maana mhusika huyu anasisitiza kauli yake hii katika kifungu kifuatacho:

- 29. *Wataka kuliziba jua na ungo,*
- 30. *Huwezi kuliziba jua, huwezi kuliziba na ungo,*
- 31. *Huwezi kuliziba jua, huwezi kuliziba.*

(15-UKSU)

Mhusika anaendeleza majigambo yake kwa kumkejeli mdaku mrejelewa kuwa hata akifanya juu chini kutumia mbinu zote ili kuzuia baraka yake, hataweza. Anataja juhudi za kumfungia milango ya baraka, kuigongea milango hiyo misumari, kujenga ukuta kuizunguka na hata aweke walinzi kuichunga, yote haya ni bure kwa vile Mungu amemfungulia baraka. Hii itakuwa ni juhudi kubwa sana ya kutaka kuzuia baraka za mhusika ili kuhakikisha kwamba haimfikii. Hata hivyo, bahati yake haizuiliki na yeyote yule. Mhusika hapa ametumia chuku ya kujivunia jinsi alivyobarikiwa. Itakuwaje milango ambayo tayari imefungwa igongewe misumari, ijengewe ukuta na hata kuwekewa walinzi wa kuichunga! Anayeweza kutumia mbinu hizi zote katika kuzuia jambo labda awe ni mtu mwenye ghadhabu au chuki kubwa. Njia moja tu kati ya zote hizi inatosha. Mhusika anajaribu kueleza kuwa baraka iliyo wachiliwa juu yake na Mungu haiwezi kuzuilika kamwe! Ili kusisitiza ujumbe wake, mhusika anamkejeli mwenzake kama ilivyo katika kiambatisho kifuatacho:

- 34. *Milango uliyofunga, gonga misumari gonga, fanya ukuta ujenge pia,*
- 35. *Weka mtu wa kuchunga, hutaniona kusonga, sasa Mungu kanifungulia,*

(15-UKSU)

Kiambatisho **20- UJ- Utalijua Jiji- Afua Suleiman** kinaendeleza mwingiliano tanzu wa majigambo ya wasanii katika *Modern* Taarabu-Mipasho. Katika kiambatisho hiki, kuna wanawake wawili ambao mmoja anajigamba alivyofanikiwa kumpata mume wa mwenzake. Katika majigambo yake anataja sifa zake nzuri zilizompelekea mwanamume husika kumpenda huku akidondoa kwa kejeli kilichomfanya mwanamke mwenzake kuachiliwa mbali. Anajisifu jinsi alivyo na ujuzi pale anapomkashifu mwenzake kwa ukosefu wa ujuzi wa mapenzi, jambo lililomuudhi sana mumewe (**6. Mwenzangu huna ujuzi, mpenzi umemuudhi**). Hii ndiyo maana mhusika alimpokea mume huyu pale alipokimbilia kwake kama anavyoeleza katika ukokotaji ufuatao.

7. Kaja kwangu nimempokea, Kaja kwangu nimempokea. (20-UJ)

Badala ya kuomba msamaha kwa mwanamke aliyemkosea kwa kumnyang'anya mume, mwanamke huyu anazidi kujigamba kuwa hana la kumzuia kumchukua mwanamume husika (**Hata ukinilaumu, wako nishamchukua**), na kumkengeusha kwa kumpa yale aliyokosa kwa mwanamke wa kwanza. Aameamua kumpa vitamu na vyote alivyokosa kwa mwanamke wa kwanza. Baada ya mwanamume huyu kufanyiwa yote aliyoyahitaji katika penzi, alijisahau na akapata kuchanganyikiwa kama kifungu kifuatacho kinavyobainisha.

- 9. Hata ukinilaumu, wako nishamchukua,*
- 10. Penzi ulimdhulumu, visa ukamfanyia,*
- 11. Chachandu vitamutamu, wala hukumpatia,*
- 12. Bwana akapata wazimu, kashindwa kuvumilia,*

(20-UJ)

Mhusika anaendelea kujigamba vile amempagawisha mwanamume mhusika kwa kumpa tiba ya vitu ambavyo alikuwa hajawahi kupewa (**Kwangu akatia timu, tiba nikampatia**), hadi mwanamume mhusika akanyenyekoa na kutii kila aliloambiwa naye. (**Amri akasalimu, magoti kunipigia**). Anamsuta mwenzake kuwa baada ya mwanamume mhusika kupewa mapenzi motomoto, alifikia kujilaumu kuwa mapenzi yake ya mwanzo

hayakufaa, alikuwa amepotea njia. Haya ni majigambo ya jinsi alivyonogea katika kumpagawisha mwanamume mhusika kama ilivyo katika kifungu kifuatacho:

13. *Kwangu akatia timu, tiba nikampatia,*
14. *Nikampa vitu adimu, kwako hajajionea,*
15. *Amri akasalimu, magoti kunipigia,*
16. *Huku akijilaumu, kwako kapotea njia,*

(20-UJ)

Majivuno ya mwanamke huyu yanaonekana katika namna anavyoeleza jinsi mwanamume husika anavyomshughulikia. Yeye huketi akaletewa kila anachohitaji ndani ya nyumba. **(28a. Mimi naletewa ndani.)** Hahangaiki kamwe kutafuta kama anavyoeleza katika data iliyonukuliwa (**28b. Wewe watanga na njia, 29. Magomeni, Buguruni, ndara zakukatikia.** Katika hali ya kawaida, mwanamume aliyetoshelezwa kimapenzi humfanyia mpenziwe wa kike kila anachokitaka hadi kumletea kila kitu ndani.

Mwanamke huyu hakomei hapo ila anaendelea kujigamba kuhusu mapishi yake mazuri ya chai kama anavyosema mwenyewe katika **54.Nampikia maandazi, na chai ya tangawizi we mwenzangu.(20-UJ)**. Hii ndiyo hali inayompata mhusika katika wimbo huu kwani kama anavyojigamba, yeye ameweza kumtosheleza mpenzi wake kimapenzi kama vile anavyosema mhusika katika kiambatisho kifuatacho: **55. Kisha natoa dozi, impayo usingizi we mwenzangu.(20-UJ)**

Hata hivyo, hali ni tofauti na mwanamke wa pili. Mwanamke mtajwa hana wa kumtafutia riziki na kumletea nyumbani kwake. Inabidi ahangaike kutafuta; mahangaiko yanayotiliwa mkazo na namna ndara zinavyomkatikia njiani. Isitoshe, inamlazimu ajihusishe na shughuli za ziada kama vile ukahaba ili aweze kuyakimu mahitaji yake. Shughuli hizi za kutafuta zimemfanya asemwe na watu mitaani na hata kutodumu katika ndoa zake. Hali hii imeelezwa katika kiambatisho kifuatacho:

33. *Umeachika ndoani, kwa yako mbaya tabia,*
34. *Unaogea jikoni, bafuni unapikia,*

56. *Ohoo utalia, mwenzangu jiji utalijua.*

(20-UJ)

Kwa mujibu wa Finnegan (2012), sifa nyingine muhimu ya nyimbo za fasihi simulizi na ambayo pia inapatikana katika *Modern Taarabu-Mipasho* ni uwepo wa mhusika katika uimbaji wa nyimbo ili kuwasilisha ujumbe wa mhusika. Mhusika ana uamuzi wa kuelekeza wimbo kwa njia ya mwingiliano tanzu kama vile kuzungumza na hadhira katikati ya wimbo baada ya kusitisha wimbo ili kuteka nadhari yao na kuupitisha ujumbe sawasawa. Katika mifano ifuatayo, wasanii mbalimbali wa *Modern Taarabu-Mipasho* wamedhihirisha matumizi ya mwingiliano tanzu kati ya majigambo, mafumbo, semi na maigizo kupitia kwa mazungumzo katika nyimbo zao ili kufanikisha kujigamba kwao. Kwanza ni katika kiambatisho kifuatacho cha ***23- NM- Nilijua Mtasema-Khadija Yusuf*** Mhusika anasema,

“Haloo my dear braza, pandisha tanga hilo. Upepo ndio huo, si mbisho. Ni ya homo eh. Taanga moja tu. J4, vuta joshi hilo. Musa bezi, vuta jelali. Kepten Chidi boy, kaza ademani hiyo, usiachie. Kama ulikuwa hujui, hili ndilo jahazi bwana we. Mashine ikitimika inasafiri kwa tanga. Halilali njiani na safari huendelea.”

(23-NM)

Katika mazungumzo haya kwenye *Modern Taarabu-Mipasho*, mhusika anajigamba kuwa yeye ndiye chiriku wa ukweli mwingine hamna. ***Sikia Chiriku original, ukisikia mwingine, dupliketi huyo. (23-NM)***. Tanga kupandishwa juu ina maana ya kuwa sasa yeye yuko uwanjani na ni nafasi yake kuonekana. Anadai kwamba yeye ndiye jahazi ambalo lazima kila mtu alijue pale anaposema ***Kama ulikuwa hujui, hili ndilo jahazi bwana we. (23-NM)***. Ubingwa wake ni wa kutajika kama meli ambayo haiwezi kulala njiani. Inapoanza safari lazima ikamilishe mkondo.

Mhusika katika mistari hii bado anaendeleza majigambo yake kuonyesha kuwa ameboba katika uwanja huu wa mipasho. Yeye si ***ndimu changa ambayo haina maji. (23-NM)***.

Anajidai kwamba amekomaa katika uimbaji wake kama anavyosema ***No research, no right speech. (23-NM)***. Hapa ana maana kuwa nyimbo zake si za kubahatisha, ni nyimbo zinazotokana utunzi wenye ukwasi wa ujuzi na ubunifu mwingi. Ndio maana akasema kuwa nanga ikitoswa majini jahazi litakuwa limefika. ***Ukiona nanga inatoswa kwenye maji, ujue jahazi limefika hilo. (23-NM)***. Hapa, mhusika ndiye jahazi. Nanga hutoswa majini kuipa meli udhabiti wakati imefika ukingoni mwa bahari. Nanga katika muktadha huu yaweza kuwa ni ujuzi wake mhusika ambao unamwezesha kuzama ndani katika utunzi wa kusifika na hivyo kufanya jahazi (uimbaji) yake kuwa imara.

Vilevile mwingiliano tanzu kati ya majigambo na *Modern Taarabu-Mipasho* unadhihirika katika kiambatisho ***30-TIT-Top in Town-Khadija Kopa***. Mhusika huyu anajigamba kupitia kwa maneno haya: ***‘Watoto mmesema sana, gari kubwa linakuja sasa, lipisheni njia, pisha njia pisha njia.’*** Hapa mhusika anajigamba kuwa yeye ni gari kubwa linalokuja uwanjani sasa. Anawaita wengine ‘*watoto*’ kumaanisha hawajakomaa kama yeye katika uimbaji wa mipasho. Anasisitiza wampishe, yaani, wamwondokee, wampe nafasi yake kwani yeye si kama wao (*watoto*) ili aweze kuwaonyesha namna ipasayo ya kuimba.

Majigambo mengine katika *Modern Taarabu-Mipasho* yameelezwa katika kiambatisho **28-FK-Funga Kazi-Machupas Family** kwenye kifungu kifuatacho:

9. Hii ni meseji senti, fikie mwafulani,
10. Kinyago wa skauti, alovamia mjini,
11. Ni kweli sikutimia, ila sikuzidi wewe,
12. Unachekwa na mamia, unajisifu mwenyewe,

(28-FK)

Katika kifungu hiki, mhusika anajigamba kuhusu uhodari wake huku akijilinganisha na mwanamke mwafulani. Mhusika anampa mwenzake ujumbe kuwa yeye ni mfano (kinyago) tu aliyeparamia mji lakini watu wanamdharau kwa tabia yake duni. Mshororo ***Koma kukashifu wenzako, na wewe hujatimia***, ni onyo kwa Mwafulani. Kwa upande

mwingine,onyo hili linaashiria kuwa mhusika ndiye aliyetimia. Mhusika anajigamba kuhusu uwezo wake pale anapomwamrisha Mwafulani afunge kazi, ahame mji huo na kutafutia kwingineko ikiwa amemuudhi kama ilivyo katika mshororo ***Hii Sasa funga kazi, sitakuachia.*** Anajidai kuwa yuko tayari kupigania nafasi yake na yuko radhi kufanya lolote mradi amwondoe Mwafulani. ***Kupigana niko radhi, vita najua.*** Kisha anadokeza kwamba hatikiswi hata kwa upanga. Yeye amebarikiwa na Mungu na vitisho vyovyote havimtetereshi. Haya yamedokezwa na kifungu kifutacho:

- 23. *Hii Sasa funga kazi, sitakuachia,*
- 24. *Kupigana niko radhi, vita najua,*
- 43. *Hata ukija na panga, jua mpingo hukati,*
- 44. *Bure kwangu ukiwaka, katu la mungu hufutii,*

(28-FK)

Majigambo yamejitokeza katika *Modern Taarabu-Mipasho* iliyorejelewa na hivyo kudhihirisha mwingiliano wa utanzu wa majigambo na ule wa mipasho. Wasanii wameweza kutumia jukwaa la mipasho kujigamba na kuelezea sifa zao mbalimbali zilizowapa nafasi bora dhidi ya wenzao. Katika sehemu inayofuata, tutaangalia mwingiliano tanzu kati ya mawaidha na *Modern Taarabu-Mipasho*.

3. 3. 2 Fomula ya Ufunguzi na Fomula ya Kufunga

Mtindo wa fomula ya ufunguzi na fomula ya kufunga ni maarufu sana katika kuanza na kumaliza usimuliaji wa kisa katika utanzu wa masimulizi au hadithi. Lengo kuu la mtindo huu ni kuvuta makini ya hadhira na kuwajulisha kuwa huo ndio mwanzo wa usimulizi wa kisa kinachoelezwa. Katika utanzu wa hadithi, fomula ya ufunguzi hutumika kuitoa hadhira kutoka ulimwengu halisi na kuipeleka katika ulimwengu wa kidhahania. Aghalabu usimuliaji wa hadithi huanza kwa ‘Paukwa, hapo zamani za kale, siku moja, hadithi hadithi...’ Fomula ya kufunga hutumika na msimulizi katika kuashiria mwisho wa usimulizi. Pia ni njia ya kuinasua hadhira kutoka ulimwengu wa kidhahania

wa usimulizi hadi katika ulimwengu halisi. Masimulizi ya fasihi simulizi aghalabu yaliishia kwa ‘Wakaishi raha mustarehe, na huo ndio mwisho wa hadithi yangu, wakadumu milele na milele...’ Katika Modern Taarabu-Mipasho, fomula ya ufunguzi na ya kufunga imejidhihirisha katika kiambatisho **2- NN- Nitadumu Nayo- Mzee Yusuf** kama ilivyodhihirishwa na mshororo ufuatao: ***2.Yarabi iwe salama, salama usalimini.***

Ufunguzi huu hupatikana katika mashairi ya Kiarabu ambapo watunzi huanza utunzi wao kwa kurejelea jina la Maulana. Katika wimbo huu, mhusika amerejelea ‘Yarabi. Mianza ya aina hii husaidia kubaini mwanzo wa kisa. Licha ya kuwa hii ni njia ya kutambua nafasi ya kwanza anayoshikilia mwenyezi Mungu katika maisha ya mwanadamu, pia ni namna ya kuomba kibali chake katika kazi anayoelekea kufanya mhusika. Katika kuashiria mwisho wa wimbo wake, mhusika huyu anaimba maneno yafuatayo ambayo yanakuwa ndiyo fomula ya kufunga:

- 34. *Inshallah nitadumu naye,*
- 43. *Nitadumu naye kwa nguvu za manani*
- 47. *Labda afe nimzike au nife mimi,*
- 49. *Acha waseme wenyewe watachoka*
- 51. *Acha wachonge hao kimpango wao.*

(2-NN)

Katika kifungu hiki, mhusika ametumia neno *Inshallah* kwa maana ya ‘Mwenyezi Mungu akipenda’ na kuongezea kuwa ataishi na mpenziwe siku zake za uhai wake wote hadi watenganishwe na kifo. Hii ni baada ya kuwasilisha ujumbe kuhusu mapenzi yao na kuwasuta wanaowafitini na wanaowaonea kijicho huku akiwaambia waendele. Mifano mingine ya mwingiliano tanzu huu imedhihirika katika kiambatisho **4-PN-Penye Neema-Miriam Mwinjuma** ambapo mhusika ameanza kwa fomula ya ufunguzi kama ilivyodokezwa katika kifungu kifuatacho:

- 1. *Wacheni Mungu aitwe Mungu, mengi ayajua mapema,*
- 2. *Ameyapanga vizuri aliyoyaumba Mungu, na kila kilicho chema,*
- 3. *Wenye ni sisi walimwengu, Ni nusuru ya daima,*
- 4. *Yote sababu hujawahi ona Mungu, utaipata salama.*

(4-PN)

Katika kifungu hiki mhusika ameanza kwa kutambua ukuu wa Mungu katika kuyajua yote. Anamsujudu Muumba kwa kuwa na utaratibu mwafaka pale alipofanya kazi yake ya kuumba vitu vyote vizuri. Ufunguzi huu ni ishara ya unyenyekevu wa mwanadamu kwa Muumba wake kwa kutambua kuwa maisha yake yamo salama mikononi mwa yule (Mungu) aliye na mamlaka kumzidi binadamu. Hivyo basi, inamlazimu mwanadamu kumpa Mungu nafasi ya kwanza katika kila anachokitenda kama ilivyo katika kiambatisho hiki. Mhusika anaendeleza wimbo wake baada ya kupata kibali kutoka kwa Muumba wake mwenye uwezo wa yote.

Hatimaye, anapokamilisha uwasilishaji wa ujumbe wake katika wimbo huu, mhusika anaamua kutoa ishara ya kuhitimisha kupitia kwa maneno **bai bai** ambayo ni ya kuaga katika lugha ya Kiingereza **bye bye**. Katika kuaga, mhusika anawapa kwaheri waivu wake na wale walio na roho mbaya kwake na kumwachia Mola mweza wa yote awashughulikie. Hii inaashiria mwisho wa wimbo wake na hivyo kufuata muundo wa fomula ya kufunga katika masimulizi ya fasihi simulizi. Fomula ya kufunga ni kama inavyodhihirika katika kifungu kifuatacho:

43. *Wenye chuki bai bai,*
44. *Wenye roho mbaya bai bai.*

(4-PN)

Mfano mwingine wa mwingiliano tanzu kati ya *Modern Taarabu-Mipasho* na fomula ya kufungua na ya kufunga umejitokeza katika kiambatisho chenye anwani **19-VW-Viumbe Wazito- Mwanahawa Ally**: kwa njia ifuatayo

Utangulizi:

1. *Vile nilivyo wathamini, nikawawekeni usoni*
2. *Kumbe wakosefu wa imani, hata hamna shukurani*
3. *Viumbe msiochukulika viumbe wazito*

(19-VW)

Utangulizi huu umebeba lalama za mhusika kuwa amesalitiwa na wanadamu wenzake aliowathamini lakini wakamgeuka. Kawaida ya mahusiano ni kuwa hakukosekani wasaliti. Masahibu wakubwa anaowaamini mtu aghalabu ndio humgeuka. Kubadilika kwa marafiki wa mtu husababisha hali ya uchungu uletwao na ile hali ya kuhisi kuwa amesalitiwa na wale aliowaamini na kuwathamini. Hii ndiyo maana ya mhusika katika wimbo huu kukariri kuwa viumbe hawabebeki kutokana na kuwa wazito. Uzito anaourejelea unasababishwa na wivu na fitina zao kwake. Wanachosha moyo kila wanapobadilika na kumsaliti mwenzao ambaye amewaamini kama wasiri wake. Hatimaye katika kumalizia wimbo huu, mhusika anadokeza hisia na maamuzi yake kuhusu alilotendewa kupitia kwa kifungu kifuatacho:

- 29. *Wema nimefanya hamna shukrani, palipo bakia nashukuru Mungu*
- 30. *Nilidhani wenzangu kumbe maadui zangu*
- 31. *Sasa nimerudi kwangu wanadamu walimwengu*
- 32. *Tenda wema wende zako usingoje shukurani*
- 33. *Sipotezi muda wangu pikenii yenu majungu*
- 34. *Wala sioni uchungu nimeswafi moyo wangu*
- 35. *We nenda nisalimie mama*

(19-VW)

Mhusika huyu anaamua kufunga uimbaji wake kwa kuwasamehe wenzake. Msamaha ni mojawapo ya nguzo muhimu katika mafunzo ya kidini. Wanaomcha Mungu huamini kuwa msamaha kwa wenzao utawawezesha kupata msamaha kwa Mungu ili waweze kumpendeza Muumba wao. Asiyesamehe pia hukatiwa hukumu na Mungu. Mhusika katika wimbo huu ni mcha Mungu ambaye ameamua kutakasa nia yake mbele ya Mungu kwa kuwasamehe waliomsema au kumpikia majungu. Anamwachia Mungu kuwashughulikia waliomkosea kwa kukosa shukrani hata baada yake kuwatendea mema. Hivyo, anakamilisha wimbo huu kwa kutaja mwelekeo aliochukua wa kumwachia Mungu mambo haya yote. Inaaminika kuwa Mungu ndiye mwenye kuona yote na kuweka hesabu ya matendo ya mwanadamu. Hivyo basi kwa mja mcha Mungu, ni heri

kumwachia Mwenyezi Mungu kutoa hukumu kwani yeye ndiye pekee mwenye kutekeleza haki kwa waja wote bila ya ubaguzi wowote.

Katika kiambatisho kifuatacho **5-SMH-Sina Muda Huo-Leila Rashid** tunapata mfano mwingine kuhusu fomula ya kufungua na ya kufunga kama ilivyoingiliana na *Modern Taarabu-Mipasho*.

Utangulizi:

1. *Kansi na washikaji, wakti sinao,*
2. *Na yako mengi mahitaji, sina muda huo*
3. *Mimi naisaga tonge, ili iende kinywani,*
4. *Sitajitia mazonge, kuingia mashakani,*
5. *Ukiende huku, ukiende kule kuitafuta riziki,*
6. *Sio kupiga kelele, kujiongezea dhiki.*

(5-SMH)

Kama ilivyo na anwani ya wimbo huu, mhusika anafungua jamvi kwa kutangaza msimamo wake bayana kuwa hana muda wa kupoteza akiwafitini wengine-**wakti sinao**. Anasema kuwa ana mengi muhimu ya kumshughulisha badala ya kuketi akipiga kelele na kujiingiza katika shida. Waliokosa jambo muhimu la kuwashughulisha hujipata wakifanya umbea ili kupitisha wakati na hivyo kijiingiza mashakani pale wanaowafitini wanapogundua. Mtu mwenye shughuli muhimu huweka akili na makini yake yote kwa ayatendayo. Huwa hana muda wa kujishughulisha na mambo yasiyomhusu au kumfaidi. Badala ya kujiingiza katika fitina, mhusika anashauri ni heri ajishughulisha na kujitafutia riziki.

Katika kufunga usemi wake katika wimbo huu, mhusika anaamua kutomsengenya mwenzake. Si eti kwamba hawezi kufanya hivyo ila ameamua kujitenga na fitina ili kuepuka kufitiniwa pia. Anakiri kuwa hata yeye anajua kusema sana kiasi cha kumfanya mwenzake alie na hata kuzimia! Aameamua hatampa mfitini wake nafasi ya kupata habari zozote kumhusu ili akose ya kumsema. Hata hivyo, amejitenga na masengenyo kwani

anafahamu kuwa asengenyae naye husengenywa. Amemalizia wimbo wake katika maneno yaliyo kwenye kifungu kifuatacho ambayo ndiyo yanadhihirisha fomula ya kufunga mpasho huu:

Kimalizio:

48. *Una hamu nikuseme, Nikikusema utalia,*
 49. *Una hamu nikuchambe, Nikikuchamba utazimia*
 50. *Utabaki ati ati, la kwangu hulipati ng'o*

(5-SMH)

Mfano mwingine wa mwingiliano tanzu kati ya utanzu wa masimulizi na utanzu wa nyimbo za *Modern Taarabu-Mipashoni* katika **3-Mc Mpenzi Chocolate**- Katika kiambatisho hiki, mhusika anaanza uwasilishaji wake kwa kuja kwa ndege aina ya helikopta ambapo maandishi ya '*Presents*' yanaonekana kuashiria mwanzo wa uwasilishaji wa mpasho huu. Hivyo katika hali hii, mhusika amedhihirisha mwanzo wa mpasho huu na kuiandaa hadhira yake kwa uwasilishaji wake.

Anapomalizia uwasilishaji wake, anaondoka kwa helikopta huku akiipungia hadhira yake kwaheri. Maandishi '*The End*' yaani mwisho, yanaonekana pale anapokuwa kwenye helikopta akiondoka. Baadaye anapomaliza na kuiaga hadhira yake, anaitoa katika ulimwengu wa utendaji wa kimaigizo na kuwarejesha katika ulimwengu halisi. Mhusika hapa amefuata uwasilishaji wa kifilamu wa Kimagharibi ambapo anahusisha helikopta katika kazi yake. Hii ni sawa na fomula ya kufunga katika utanzu wa masimulizi kwenye fasihi simulizi. Hivyo, kunakuwa na mwingiliano kati ya *Modern Taarabu-Mipasho* na utanzu wa masimulizi hali ambayo inaleta mwingiliano tanzu katika uwasilishaji wa fasihi simulizi.

Huu ndio mtindo uliofuatwa katika nyimbo za mipasho ambapo kuna sehemu ya kwanza ya utangulizi na hatimaye sehemu ya kimalizio. Kama nilivyotaja pale awali katika ukurasa wa 82 wa utafiti huu, huu ni mtindo unaopatikana katika utanzu wa masimulizi na hivyo *Modern Taarabu-Mipasho* umeiingiza mtindo huu ili kuangazia mwanzo na mwisho wa nyimbo zake. Matumizi ya mtindo huu ni dhihirisho kwamba haifai kuziwekea mipaka maalumu tanzu za fasihi simulizi kwani zinaingiliana sana katika uwasilishaji wake. Utanzu niliojadili wa masimulizi umedhihirisha mwingiliano tanzu kati yake na utanzu wa maigizo katika utendaji wa utanzu wa nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho*. Katika sehemu ifuatayo, tutaangalia mwingiliano tanzu uliopo kati ya masimulizi ya khurafa na mipasho.

3.3.3 Kipera cha Khurafa

Masimulizi ya khurafa yana sifa ya wahusika wake kuwa ndege, wanyama, wadudu au mazimwi ambao huakisi tabia za binadamu. Khurafa hutajwa kuwa istiaru ndefu kwa sababu huweza kufumba. Pia huwakilisha mambo ambayo kwa kawaida ingekuwa muhali au aibu kuyasema hadharani. Mtambaji katika masimulizi ya khurafa huepuka kuudhi kwa kuonekana kumkashifu na kumwaibisha mtu hadharani. Matumizi ya wahusika wanyama ni aina ya jazanda ambayo wakati mwingine hukusudiwa kuwasilisha ujumbe wa mapenzi. Ujumbe wa aina hii ambao una ‘masuala ya aibu’ hukusudiwa watu wazima na hivyo kuna haja ya kuteua namna ya kuuwasilisha ili mwasilishaji adumishe adabu.

Khurafa katika *Modern Taarabu-Mipasho* inadhihirika katika mwingiliano wa utanzu wa masimulizi na utanzu wa semi katika kipera chake cha mafumbo ambapo ‘Paka Mapepe’ katika wimbo huu wa taarabu ni fumbo. Aidha, khurafa kutoka utanzu wa masimulizi imeingiliana na utanzu wa maigizo katika uwasilishaji wa wimbo huu wa *Modern*

Taarabu-Mipasho. Maelezo haya yamebainishwa katika kiambatisho cha **11-PM-Paka Mapepe- Ashura Majaliwa.**

Mhusika mkuu katika wimbo huu wa *Modern* Taarabu-Mipasho ni binadamu mwanamke ambaye amepewa sifa za ‘paka mapepe’ katika **1.Paka mapepe huyo na 2. Paka mapepe usimwandame, mapepe huyo.** Paka huyu anasemekana hamjui mume. Tabia zake hazipendezi kwani anaonekana kutotosheka na kila anachopewa kama ilivyodokezwa na maneno yafuatayo: **4.Huyo hamjui mume, mapepe huyo.** Amesawiriwa kama mhusika mwenye tamaa kubwa. Hata akipewa nyama mbadala kama vile kuku, bata, na hata steki, bado kila mara yuko mbioni kutafuta ‘panya’ yaani mawindo mapya ya wanaume. Haridhiki kamwe na yote anayotendewa. Yeye hubaki akinung’unika tu. Kwa kawaida chakula cha paka huwa ni nyama. Haijalishi ni kwa kiasi gani alichoshughulikiwa hata kama ni kupewa nyama ya ng’ombe mzima, apendwe hadi afanyiwe kila kitu, bado atatoweka akimwona ‘panya’. Maelezo haya yanajitokeza katika kifungu kifuatacho kama kilivyokokotwa:

17. Umpe kuku na bata, yeye hatotosheka,
18. Umpe japo steki huyo paka, hata kushukuru huyo paka,
19. Atakutoroka huyo paka, akimwona panya huyo paka,
20. Kila umtendeavyo, bado atalalamika paka,
21. Mrithi kwa kila njia, mwisho atakutoka paka,

(11-PM)

Kifungu hiki kinasisitiza juhudi zote ambazo mwanamke mtajwa (paka mapepe) amefanyiwa kwa lengo la kulipata penzi lake. Miongoni mwa aliyotendewa ni pamoja na kupewa kuku na bata, kupewa steki na bado hana shukurani. Katika kifungu kifuatacho 41-46, mhusika anashadidia kutoka nje kwa mwanamke mtajwa hata baada ya kupewa vitu vya kila aina kwa nia ya kumvutia. Anafanya hivi kwa kukariri neno “**huyo**” kila baada ya kutaja alichopewa ‘paka mapepe’. Hatulii ila pale tu anapopata vivutio vya aina nyingine. Anasisimkwa anapomwona ‘panya’. Katika muktadha huu, vivutio vingine ni

wanaume wengine wanaompagawisha mwanamke mtajwa kila awaonapo. Haya yameonyeshwa katika kifungu kifuatacho:

41. *Huyo paka mapepe huyo,*
42. *Hata umpende huyo,*
43. *Hata umlambe huyo,*
44. *Umchinjie ng'ombe huyo,*
45. *Akimwona panya, anachacharika,*
46. *Akimwona panya, ana akiringa*

(11-PM)

Mhusika Paka Mapepe ana tabia ya kuudhi pale anaposemekana kutojali na kuwa hata anaweza kuwachanganya kwa kuwagonganisha watu wenye uhusiano wa karibu kama vile wana, shangazi, kaka na baba. Katika mila na desturi za Kiafrika, huwa ni mwiko katika jamii nyingi kwa mtu kujihusisha katika mapenzi na watu wenye uhusiano wa karibu sana wa damu. Pindi tu jamaa waliochanganywa wanapogundua, hali ya taharuki, kukufuru mila na hata chuki na wivu huzuka kutegemea ukuruba wa uhusiano wao. Wakati mwingine suala kama hili linaweza kusababisha ugomvi mkubwa na watu wakakosana na kuumizana au hata kuuana. Hivyo, mwanamke huyu hana aibu wala hajali yale yatakayowapata wateja wake.

12. *Huyo atawachanganya, wana, shangazi na kaka*
13. *Tena akisha tapeli na baba atamtaka.*

(11-PM)

Aidha, mhusika huyu 'Paka' ana sifa ya kutokumbuka mema yote aliyofanyiwa. Hata si vyema kumruhusu kufanya ayatakayo kwani ni kama aliyepungukiwa na akili na ambaye ana shukrani za mateke kama za punda. Mtu mwenye tamaa nyingi kama Paka Mapepe huyu hana muda wa kushukuru. Haja yake huwa ni kufaidi kutoka kwa mhusika mmoja na kumtema punde tu anapompata mwingine wa kumfaidi. Mwanamke wa aina hii hana muda wa kufikiria mambo mema aliyotendewa. Muda alionao ni wa kutafuta mawindo mapya ya wanaume kama ilivyodokezwa katika kifungu kifuatacho:

23. *Mazuri kimfanyia, hisani hatokumbuka.*
 24. *Bure kumkubalia, kufanya anavyotaka.*
 33. *Muepuke hayawani, faudhila yake mateke.*

(11-PM)

Katika ukokotaji ufuatao, ***Usitazame gauni, japo ndo mavazi yake, tofauti we huoni, hana haiba ya kike***, ‘Paka’ ambaye ni mwanamke mrejelewa hana uzuri unaopatikana katika wana wa kike hata ingawa anavalia mavazi ya kike. Hata akiwa na wenzake, bado anadhihirisha tabia isiyopendeza kama ilivyowekwa bayana katika ***Japo yeye yumo kundini, mbovu desturi zake***. Katika maisha ya kawaida, panya huwa ni chakula chake paka kwani paka anapenda nyama. Mhusika Paka anawakilisha mwanamke mwenye tamaa isiyo na kifani licha ya kile anachopewa. Katika wimbo huu mhusika ameonyesha kuyafahamu mazingira yake vilivyo na matukio ya maisha yanayomzunguka. Anaelewa maisha ya paka ambaye ni mnyama anayefugwa na mwanadamu.

Mhusika wa pili ni Panya (mwanaume) ambaye amesawiriwa kama kitoweo chake Paka (mwanamke). Katika mpasho huu panya amesawiriwa kama kivutio kikubwa mno cha paka. Yeye ndiye sababu kubwa ya sifa zote hasi anazopewa paka. Panya ni mnyama ambaye hujulikana kwa tabia zake hasi za uharibifu. Mnyama huyu panya ni adui mkubwa wa mwanadamu na kila mara mwanadamu huwa mbioni kumwangamiza. Miongoni mwa madhara ya panya katika maisha ya mwanadamu ni kuharibu mimea na mazao, mavazi, vyombo na vitabu na hata vitu vya thamani. Paka hawezi kutulia amwonapo panya hata kama amechinjiwa ng’ombe mzima! ‘Panya’ (mwanamume) humfanya paka (mwanamke) hata akakosanisha watu wa jamii moja. Akimwona mwanamume ampendaye, huingiwa na maringo na kuwa kama aliyeingiwa na kichaa kama ilivyodokezwa katika kifungu kifuatacho:

12. *Huyo atawachanganya, wana, shangazi na kaka*
 13. *Tena akisha tapeli na baba atamtaka.*
 45. *Akimwona panya, anachacharika,*
 46. *Akimwona panya, anaringa*

(11-PM)

Mwishowe katika mpasho huu, mwanamke aliyemrejelea mwenzake kama ‘paka mapepe’ anadhihirisha nia yake ya kumtaka mwanamume husika pale anapomsihi aje kwake kwani anamdamini.

34. *Njoo kwangu mimi, nakuthamini,*
 35. *Sikupeleke puta huyo,*
 36. *Hafai huyo hafai, kwangu mimi nakurai*

(11-PM)

Wimbo huu umedhihirisha namna khurafa inavyoingiliana na *Modern Taarabu-Mipasho*. Matumizi ya Paka na panya katika mpasho huu ni mwafaka katika kusetiri ujumbe wa mhusika. Inaelekea kuwa kuna wanawake wawili wanaobishania mwanamume. Mmoja wao katika wimbo huu ameamua kutumia istiari ili kumkashifu mwanamke mpinzani wake kwa kulinganisha tabia zake na zile za paka ila katika mpasho huu, huyu ni paka asiyekuwa na shukrani. Paka katika maisha halisi hupenda sana kuandamana na wanawake. Si ajabu mwanamke huyu ameamua kutumia mnyama ambaye anamfahamu zaidi kitabia. Katika sehemu ifuatayo, tutaangalia mwingiliano kati ya aina nyingine za nyimbo na mipasho.

3.4 Mwingiliano kati ya Modern Taarabu-Mipasho na Utanzu wa Mazungumzo Kipera cha Mawaidha

Kutoka utanzu wa Mazungumzo kuna kipera cha Mawaidha. Mawaidha huwa ni maneno yaliyoteuliwa kwa uangalifu mkubwa kwa madhumuni ya kushauri, kuonya, kutoa suluhisho miongoni mwa malengo mengine. Aghalabu mawaidha hulenga maudhui mamoja maalumu. Kwa kawaida anayetoa mawaidha huwa ni wa umri wa juu, mjuzi au mtaalamu. Aidha, hulenga hadhira teule kwa kuwasilisha ujumbe kwa lugha sahili. Katika nyimbo zilizotumika kama data ya utafiti huu, mawaidha yameweza kuingiliana na utanzu wa semi, mafumbo na maigizo kwenye nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho*. Hili ni kama ilivyothibitishwa katika kiambatishochenye anwani **6-FS-Full Stop-**

Khadija Kopa-mhusika anatoa nasaha kwa vijana kwa kuwatahadharisha juu ya magonjwa ya zinaa na ugonjwa wa ukimwi. Kwenye mfano wa kwanza, Kopa anatoa mawaidha hususan kwa watoto wa kiume. Anawaomba wampe sikio apate kuwashauri kama kifungu kifuatacho kinavyoweka wazi:

87. *Watoto wangu wa kiume, nisikilizeni nyie,*
 88. *Mnaojiita masharobaro, nisikilizeni.*
 89. *Nyie mabarobaro, nisikilizeni.*

(6-FS)

Katika ushauri wake, anawaonya kuwa wanawake wanafahamu mengi. ***Nawaambia kina kaka, wanawake wanajua.*** Anapongezea kuwa ***Pale pana pa utamu, wamepapamba maua,*** anawaambia kuwa walipokusudia kupapata ambapo ni patamu paeremshwa kabisa. Hata hivyo, wajitahadhari na mahala hapo kwani pana magonjwa ya zinaa kama vile gonorrhoea na hata ukimwi. Ukimwi ni suala nyeti ambalo limeleta changamoto tele katika jamii ikiwemo mauti. Ndiyo maana anawashauri na kusisitiza kuwa ukimwi utawaua. ***Ukikosa gonorrhoea, ukimwi utakuuwa. Ukimwi utakuua, ukimwi utakuua.***

(6-FS)

Nasaha nyingine kwa wanawake imetolewa katika mpasho huu kuhusu vipodozi vya kigeni. Khadija kopa amechukua fursa hii kuwashauri akina dada dhidi ya kutoathiriwa na tamaduni za kigeni na kujipaka vipodozi visivyofaa kama anavyoimba katika ***Vikarolaiti vyenu, vinavyowapa jeuri.*** Khadija Kopa anaviita vikarolaiti. Anawaonya kuwa ngozi zao zitaathirika na kufanya vibaka baka kutokana na kujipika vipodozi hivyo. Anaonyesha kugadhabika kwake na tabia hii hadi anaapa kuipiga vita kwa kuifanya marufuku. Khadija Kopa anashangaa kwa nini wasichana waharibu ngozi zao kwa kujipaka vipodozi vya ughaibuni visivyofaa ilhali yeye ambaye hajavitumia, yungali mrembo, ana ngozi ya kuvutia na tena bado anang'ara kama ilivyodhihirika katika ukokotaji huu : ***41 Mimi nina rangi yangu, sitaki uso wa baka. 42 Mimi nina rangi***

yangu,na tena bado nawaka. Hapa ndipo anajiita ‘**Baby quite**’ wa kiafrika! Nasaha hii ameitoa huku akiigiza ghadhabu yake kuhusu wasichana wa kiafrika wanavyobadilisha rangi ya ngozi zao kama ilivyodhirishwa na sehemu ifuatayo:

- 39. *Vikarolaiti vyenu, vinavyowapa jeuri,*
- 40. *Hivyo vikarolaiti vyenu, nitavipiga marufuku hapa.*
- 41. *Mimi nina rangi yangu, sitaki uso wa baka.*
- 42. *Mimi nina rangi yangu,na tena bado nawaka.*

(6-FS)

Mfano wa mwingiliano tanzu mwingine wa nasaha na Modern Taarabu-Mipasho umo katika kiambatisho **34-TIT-Khadija Kopa kutoka kwa kikundi cha T.O.T.** Mhusika Khadija Kopa katika mpasho huu anaamua kuwapa wanawake nasaha. Katika jamii ya Waswahili, wanawake wana jukumu la kuwafunza watoto wao wa kike kukua wanawake wenye heshima katika jamii yao. Mafunzo hayo hunuiwa kuwashauri wanawake kuwa wenye tabia nzuri. Hufunza kuwa urembo wa mwanake ni zaidi ya sura nzuri. Huambatana na tabia njema pia kama vile upole, utulivu, unyenyekevu, ukarimu na mwenye mapenzi kwa mumewe na kwa wengine.

Uswahilini, ndoa na harusi ni taasisi ya kwanza kwa uzito wa maisha ya kila siku ya mtu. Ubikira ni ada kubwa sana kwa wasichana wa Kiswahili kabla ya kuolewa kwani ndoa ndicho kitovu cha maisha ya Waswahili. Ni desturi iliyoenea mwote Uswahilini, kwa wazazi kuwa washauri wakuu wa ndoa za watoto wao. Kuna hatua kadha wa kadha tangu mtu aposapo hadi kutoa mahari na kufunga harusi. Chuo hicho huwashirikisha makungwi na masomo katika kuwaelekeza na kuwafundisha wari harusi kabla na baada ya harusi.

Kwa waumini wa Kiislamu, sharia za Kiislamu huwa ndicho kigezo pekee cha kuendeshea maisha yao. Katika mpasho **34-TIT-Khadija Kopa**, mhusika anatoa nasaha kwa wanawake kama ilivyojitokeza katika ukokotaji ufuatao:

- 67. *Sasa nawapa usia kina dada msikie*
- 68. *Sasa nawapa usia mpendapo mtazame*

69. *Wengine si wanaume wengine magumegume*
 70. *Rusha roho taratibu tena nyuma utazame*
 82. *(Akugombanisha na ndugu zako) Si wanaume magumegume*
 83. *Si wanaume wana umeme*

(34-TIT)

Katika kifungu kilichorejelewa, mhusika anawapa wanawake nasaha kuhusu mapenzi. Wosia wake ni kuwa wanawake wawe waangalifu sana pale wanapopenda wanaume. Wasiwe na pupa ya kupenda bila kuchunguza historia ya wanaume watumainio kuwapenda. Wanatahadharishwa dhidi ya kuachilia penzi lao bila kwanza kuchunguza kwa makini mpokezi wa penzi. Nasaha yake kwao ni kuwa sio wote wanaowavutia ni wanaume. Wengine anawaita magumemgume! Hawatoshi kuitwa wanaume na hivyo akasisitiza kwa ilivyowekwa wazi katika sehemu ifuatayo kuwa:

- 75 *Kiitikio,*
 a. *Si wanaume magumegume*
 76 *(wengine) Si wanaume magumegume*
 77 *(wengine) Si wanaume magumegume*

(34-TIT)

Khadija Kopa hakomei hapo katika kutoa nasaha yake kwa wanawake. Wengi wa wanawake Waswahili huenda kufanya biashara ndogo ndogo ili kukimu mahitaji yao. Hata hivyo, kuna wanawake ambao waume zao wanajikimu kiuchumi. Wanawake hawa hawajihusishi na biashara ila husalia nyumbani ambapo mara nyingi huwa wameajiriwa wafanyikazi wa kuwasaidia katika shughuli za pale nyumbani.

Mhusika anaendelea kuwafungua macho akina dada kuwa hata na wale wasaidizi wa nyumbani ambao huwasaidia kazi mbalimbali za nyumba kama vile kufua hata na shuka za vitandani, ni hatari sana katika kuwaiba wananaume wao. ***Shuka zako azijua, ndani kwako ziko nne.*** Wanajua mienendo na mahusiano ya waajiri wao na hivyo wanaweza kuchukua fursa yoyote itokeapo ili kuwashawishi kimapenzi wale mabwana zao. Wanalinganishwa na paka shume ambaye ni mnyama anayefugiwa nyumbani. Paka huyu

huwa na tabia ya kunyemelea windo lake kama ilivyo na wasaidizi hawa wa nyumbani ambao hupenda kuwanyemelea waume wa waajiri wao. La mno ni kuwa hata baada ya kuwanyemelea waume wa waajiri wao, hulala nao vitandani mwa waajiri wao!

- 71. *Huyo unomkanyaga ndio anokuchukulia mume*
- 72. *Shuka zako azijua ndani kwako ziko nne*
- 73. *Tena mfanyakazi wako ukitoka paka shume*
- 74. *Tena alala kitanda chako mumeo ana umeme*

(34-TIT)

Wasaidizi hao huwa na fursa kubwa ya kuwaiba kimapenzi wanaume waajiri wao kwa vile wanafahamu siri zote za mle wanamofanya kazi. Mojawapo ya sababu zilizodokezwa kuhusu wajakazi kuwatwaa kimapenzi waume za waajiri wao ni unyanyasaji wanaotendewa. Khadija Kopa anawashauri wanawake kuwa kuna wengine wao ambao si wanawake ila ni makwekwerekwe! Wanawake wengine wametajwa kuwa na tabia ya kuwatwaa, wakubwa wao kazini aidha na ndugu za wanawake wenzao na hata kuwakosanisha nao. Pale mhusika huyu anapoimba kuwa wengine ni makwekwerekwe, anaigiza akifanya mfano wa kuku anayefurukuta mbawa zake. Nasaha hii imetolewa katika kiambatisho kifuatacho.

- 78. *(wengine) Si wanawake makwekwerekwe*
- 79. *wengine) Si wanawake makwekwerekwe*
- 80. *(Achukua ndugu zako) Si wanawake makwekwerekwe*
- 81. *(Amsomba bosi wako) Si wanawake makwekwerekwe*

(34-TIT)

Katika wimbo huu, mwanamke anashauriwa kuwa makini sana anapotafuta mpenzi mwanamume. Aidha, anatahadharishwa kuwa makini kuhusu kijakazi wake wa nyumbani. Ni jambo la kawaida wafanyakazi hawa na waajiri wao kukosana kikazi. Sababu imetolewa ya wajakazi hawa kufanya hivi. Unyanyasaji umetajwa kama mojawapo ya sababu za tabia tajwa. Hata hivyo dada hawa wanaonywa kuwa mfanyakazi wake ambaye anafahamu maisha ya ndoa yake na nyumba yake vyema ndiye

atakayemnyang'anya mumewe na kumpa machungu. Wanashauriwa kuwa wajihadhari kwani sio wote ni wanawake kwani wengine ni 'makwekwerekwe'!

Pia katika kiambatisho **25-WWW-Wasi Wasi Wako-Mzee Yusuf**, nasaha imetolewa na Mzee Yusuf kupitia kwa utanzu wa mazungumzo kama ifuatavyo:

"...Hata kama ni mswahili, unatakiwa usome Kiswahili ili upate kujua kanuni na na tashbiha, na mambo mambo. Hii sio hadithi rejea..."

(25-WWW)

Hapa Mzee Yusuf anazungumza katika wimbo wake huu akitaka wimbo ule usimamishwe kwanza, watu waache kupiga kelele na wawe makini kisha anawapa nasaha kuwa ni vyema wasome Kiswahili ili wamakinike. Hata kama ni Waswahili inapaswa ili wajue kanuni, tashbiha na mambo mengine mengi. Sehemu inayofuata imeshughulikia mwingiliano tanzu kati ya Modern Taarabu-Mipasho na utanzu wa masimulizi hususan, vipengele vya fomula ya kufungua na ile ya kufunga, khurafa, mwingiliano tanzu wa *Modern* Taarabu-Mipasho na tanzu nyingine za nyimbo.

3.5 Aina nyingine za Nyimbo katika *Modern* Taarabu- Mipasho

Muziki wa mipasho katika uwasilishaji wake umeweza kudhihirisha mwingiliano na ngoma nyingine za kitamaduni. Uchezaji wa nyimbo hizi umekuwa ni kwa lugha za kitamaduni huku wachezaji wakiwa wamevalia maleba ya kitamaduni. Katika nyimbo za *Modern* Taarabu-Mipasho zilizorejelewa, nyimbo hizi za kitamaduni hazikuimbwa kwa muda mrefu. Kwa ujumla zilikuwa fupi zenye ubeti mmoja au ikizidi mbili tu. Ngoma hizi ama ziliingizwa mwanzoni kama kitangulizi jinsi ilivyo katika ngoma ya Sebene kwenye wimbo wa anwani *Tenda Wema*, kati kama kiitikio mfano jinsi ilivyo katika wimbo wenye anwani **15-UKSU** au mwishoni mwa mpasho kama kimalizio jinsi ilivyo katika wimbo **25-WWW**. kama ifuatayo:

3.5.1 Sindimba katika *Modern Taarabu-Mipasho*

Utanzu wa *Sindimba* umedhihirika katika *Modern Taarabu-Mipasho* katika kiambatisho

25-WWW-Wasiwasi Wako-Mzee Yusuf

55. (*Huyo ndiyo Faza Mauji katupeleka kusini tucheze sindimba*)
56. *Che cheche che cheche cheza sindimba*
57. *Anachezesh mabega*
58. *Anachezesh mabega,*
59. *Sema zungusha zungusha*
60. *Anazungusha zungusha*
61. *Che cheche che cheche cheza sindimba*
62. *Aliyekula dona, na nguru wa kuchoma*
63. *Ado ado ado ado ado salali*
64. *Chinjiku chichilana*
65. *Nauliza nani kama mama, hakuna*
66. *Nauliza tena nani kama mama, hakuna*
67. *Okey, wamesikia hilo.*

(25-WWW)

Sindimba ni ngoma ya kitamaduni kutoka jamii ya Makonde kutoka Tanzania. Ngoma hii huimbwa kuadhimisha awamu mbalimbali za maisha ya binadamu. Katika ngoma hii, kuna uchezaji wa ngoma za kitamaduni ambapo wasanii wamevalia maleba meusi na meupe yenye madoadoa kama ngozi ya chui na shanga za kienyeji. Aidha, wamejifunga vibwebwe viunoni ambavyo wanavichezesh kufuatia midundo ya ngoma kubwa za kiasili zinazochezwa katika utendaji huu. Wasanii hucheza kwa mtindo wa kurusharusha miguu juu huku wakichezesh mikono yao upande upande. Kisha wanainama na kupiga magoti huku wakitikisa kiuno. Hatimaye wanainuka na kuendelea kutikisa kiuno. Aidha, mazingara walimochezea ngoma hii ni ya mashambani au kijijini tofauti na *Modern Taarabu-Mipasho* ambayo iliigizwa katika kumbi za burudani. Pia kuna wale waliobeba migwisho na firimbi ambazo ni ala zinazotumika katika ngoma za kitamaduni. Ngoma kubwa za aina tofauti tofauti huhezwa kwa wakati mmoja.

Kama uwasilishaji wa wimbo huu wa mipasho unavyodhihirisha, ngoma ya Sebene huhezwa na wanawake na wanaume. Uchezaji huhusisha kutikisa kwa mabega,

kuchezesha kiuno na hata kulala kwa kuinama chini kwa mtindo maalumu. Miongoni mwa wachezaji ni Mzee Yusuf na Faza Mauji ambao vile vile wanapatikana katika uimbaji na uchezaji wa Taarabu kabla na baada ya kuicheza hii sehemu ya ngoma ya sindimba. Mchakato huu unadhihirisha mwingiliano tanzu kati ya *Modern* Taarabu-Mipasho na ngoma ya kitamaduni ya sindimba katika utendaji na uigizaji wa Taarabu hii. Hivyo kuingiliana kwa ngoma hii ya sindimba na *Modern* Taarabu-Mipasho kunaleta hali ya ngoma ndani ya wimbo. Mara tu baada ya kucheza sehemu hii ya Sindimba, Mzee Yusuf anarejea katika kucheza wimbo wa *Modern* Taarabu-Mipasho. Inayofuata ni *Sebene* ambayo imedhihirika kuingiliana na nyimbo za *Modern* Taarabu-Mipasho katika data ya utafiti huu.

3.5.2 *Sebene* katika *Modern* Taarabu-Mipasho

Utanzu wa *Sebene*, ambayo ni ngoma ya kitamaduni kutoka Tanzania umejitokeza na kuingiliana kitanzu na *Modern* Taarabu-Mipasho. Katika uchezaji wa *Sebene*, wasanii wamevalia marinda ya mkonge, kanga na kofia za makuti. Wanacheza kwa mduara wakisonga mbele na nyuma katika midundo ya aina yake. Mmoja wao ambaye amevalia kofia ya makuti anaongoza uimbaji huu na kuwahusisha watoto pamoja na mzee mmoja ambao wanaonekana kuwa maskini kutokana na walivyovalia mavazi yaliyochanika chanika. Kutokana na maneno katika uimbaji wa kipande hiki cha *Sebene*, mhusika anaonekana kushughulikia maudhui ya umaskini. Anawatia moyo waliomo katika umaskini kuwa si kilema. Kiongozi wa wimbo huu wa *Sebene* anachangana maneno ya lugha ya kitamaduni na yale ya Kiswahili ambapo anasema kuwa umaskini si kilema, nia yake ikiwa ni kuwahimiza maskini. Baadaye uimbaji huu *Sebene* unakoma na mara moja waimbaji warejea katika uchezaji wa *Modern* Taarabu-Mipasho. Kunakuwa na mtiririko

mwanana katika mwingiliano tanzu kati ya sebene na *Modern Taarabu-Mipasho*. Wimbo ngoma ya sebene umewasilishwa katika kifungu kifuatacho **35 TW-Tenda Wema-**

1. *Eh mwana koibananga kurila,*
2. *Mwana mdodo bwe, Eh mwana koibananga kurila,*
3. *Lia uchungu bwe, Eh mwana koibananga kurila,*
4. *Alialia bwe, mwanangu mdodo bwe,*
5. *Eh mwana koibananga kulira,*
6. *Nyanya chungu na bamia, mimi ndio mboga yangu,*
7. *Masikini si kilema, mimi ndiyo jadi yangu.*
8. *Eh mwana koibananga kulira. Lia mwana bwe,*
9. *Eh mwana koibananga kulira,*
10. *Sangu mama kisangu, hata ukitia nazi,*
11. *Binadamu habebeki, kama mzigo wa mwizi.*
12. *Eh mwana koibananga kulira. mwana mdogo bwe,*
13. *Eh mwana koibananga kulira, Alia mwana bwe.*

(35 TW)

Aidha, chakacha katika *Modern Taarabu-Mipasho* kama inavyobainishwa katika sehemu inayofuata hata ingawa imetajwa kwa kifupi mno.

3.5.3 Chakacha katika *Modern Taarabu-Mipasho*

Kuna mshororo mmoja ambao unatokana na mtindo wa chakacha katika kiambatisho **18-ZZ-Zoa Zoa-Mwanaidi Shaaban - 40. Shilingi yang'ara yaua shilingi nyanga'ara.** Kiambatisho hiki ni kiungo cha chakacha chenye kusudi la kuonyesha alivyong'ara mhusika katika wimbo huo akilinganishwa na mwenzake. Ni njia ya kujisifu kwa mhusika kuhusu urembo na thamani yake. Kama ilivyo na shilingi, hung'ara pale inapomwezesha mja kupata mahitaji yake yote. Hata hivyo, shilingi yaweza kuua kupitia kwa njia nyingi. Mojawapo ni pale mtu anaweza akamuua mwingine ili apate pesa zake. Pia aliye na pesa anaweza kutumia pesa hizi vibaya kwa kuwaua wale ambao anawaona kama vizingiti katika kupata akitakacho maishani mwake. Hivyo kwa upande mmoja shilingi inang'ara kwa kuleta mazuri na kwa upande mwingine inaua. Mshororo huu kwa kawaida katika **chakacha** huimbwa kwa kurudiwa hivi :

*Shilingi yang'ara yaua shilingi nyanga'ara
Shilingi yang'ara yaua shilingi nyanga'ara
Nimepata dereva ajuaye gari, gari yangu yaenda mbio.*

(18-ZZ)

Kiambatisho **15-UKSU-** katika kimalizio chake pia kina mistari inayorejelea **goma, chakacha, lelemama** na **msewe** katika utamaduni wa Waswahili.

46Kimalizio

47. *Kalichagua goma, la Kiswahili goma,*
48. *Chakacha namchezea, habibi namchezea*
49. *Lele mama namchezea, habibi namchezea*
50. *Msewe namchezea, habibi namchezea,*

(15-UKSU)

3.5.4 Goma katika *Modern Taarabu-Mipasho*

Wachezaji katika uigizaji wa kanda hii wanacheza mitindo tofauti tofauti kulingana na jina la ngoma inayotajwa kila inapotajwa. Bazmaleh (2006) anafafanua kuwa goma ni ngoma ambayo huchezwa sana na Wabajuni. Ngoma yenyewe huchezwa bila vishindo wala harakati nyingi. Ni ngoma inayochezwa kwa ustaarabu na haiba ya juu. Wachezaji hucheza kwa umakini wa hali ya juu na kwa utilivu wakifuatia mdundo wa ngoma. Anayetaka kuona harakati za uchezaji wa goma ni lazima awe na umakini kutazama. Wachezaji huwa wamevaa kanzu nyeupe, kofia za vito na kubeba bakora katika mkono wa kulia. Bakora huwa imewekwa begani na huwa inainuliwa mara moja moja kufuatana na mdundo wa ngoma.

Wachezaji wa Goma huwa wamepambwa kwa shada la maua na pengine kosaja la pesa. Wapigaji ngoma huwa wanaelekeana na wale wachezaji. Goma inaweza kucheza kwa muda mrefu na huku watu wengine wakiimba nyimbo tofauti tofauti. Sehemu inayofuata itaangazia aina ya ngoma ya lelemama ilivyoingiliana na *Modern Taarabu-Mipasho* katika uwasilishaji wake.

3.5.5 Lelemama katika *Modern Taarabu- Mipasho*

Kwa mujibu ya Bazmaleh (2006), lelemama ni ngoma ambayo huchezwa na Wabajuni na wazaliwa wa Kiarabu. Ngoma hii sanasana huchezwa siku za harusi. Pia, kutegemea uwezo wa mtu anayecheza au anayeandaa harusi, ngoma hii inaweza kucheza kwa siku moja au tatu au zaidi lakini hazipitishi saba. Ngoma yenyewe huchezwa na wanawake wanaovaa kanga pekee. Kanga ndiyo nguo rasmi ya kucheza lelemama. Kawaida lelemama huchezwa ndani ya ua yaani boma lililojengwa kwa makuti. Wanaohudhuria ni wanawake pengine isipokuwa wale wapigaji ngoma ambao huwa waume. Lelemama huchezwa na wanawake wakiwa juu ya mabao wakiwa wamevalia lesa zao (kanga) zilizo safi na mara nyingi huvaa sare. Wachezaji huwa wamejipamba kwa vilua na mashada ya asmini yaliyofungwa vichwani. Kila mchezaji huwa ana vigongo viwili ambavyo urefu ni kama inchi 6.

Lelemamama huchezwa kwa makini kwa miondoko ya kuyumbayumba kulia na kushoto kwa kufuata mlilo wa ngoma. Lelemama pia huchezwa kwa makini na utulivu wa hali ya juu. Wanawake wengine huwa wamekaa chini kwenye majamvi wakipiga makofi na kuimba kufuata sauti ya zumari au tarumbeta. Katika kifungu kilichoambatishwa hapo juu, mhusika anahusisha kwa kuzitaja aina hizi zote za ngoma katika wimbo wa taarabu anaouimba. Hivyo, kumekuwa na mwingiliano tanzu kati ya aina hizi za nyimbo hali ambayo imedhihirika na kuboresha uwasilishaji wa ujumbe. Sehemu inayofuta itaangazia nyimbo za bembelezi zilivyodhihirika katika uwasilishaji wa *Modern Taarabu-Mipasho*.

3.5.6 Bembelezi katika *Modern Taarabu - Mipasho*

Bembelezi⁸ kama kipera cha utanzu wa nyimbo katika fasihi simulizi kimeweza kupata nafasi na kuingiliana na mipasho. Mwingiliano huu umejitokeza kati ya nyimbo za

⁸ Bembelezi ni nyimbo zinazoimbiwa watoto ili watulie au waweze kulala.

bembelezi, utanzu wa maigizo na nyimbo za *Modern* Taarabu-Mipasho. Katika data ya utafiti huu, nyimbo za bembelezi zimetumika katika mianzo, kiitikio au kimalizio. Nyimbo za bembelezi huwa na sifa ya mistari kukaririwa huku sentensi zikiwa fupifupi. Mfano wa wimbo wa *Modern* Taarabu-Mipasho uliotumia bembelezi kama kiitikio cha kati na kama kimalizio ni kama ilivyowekwa wazi katika kiambatisho **3-MC-Mzee**

Yusuf

38. *Halua, halua,*
39. *Halua, halua,*
40. *Halua, halua,*
41. *Halua, helua,*
42. *Halua halua,halua,*
43. *Halua, halua,*
44. *Haya ukitaka halua we chukua,*
45. *Halua, halua,*
46. *Ukitaka na tende pia chukua,*
47. *Halua halua*

(3-MC)

Halua ni aina ya chakula laini na kitamu kilichopikwa kutokana na viungo vya samli, unga na sukari. Ni chakula kinachopendwa sana na watoto na kinapotajwa, watoto hufurahi sana. Bembelezi hii imetumika kama kiitikio katika mpasho huu. Hivyo katika mpasho huu, Mzee Yusuf alihusisha bembelezi hii katika kumwonyesha mpenzi wake Chocolate mapenzi yasiyo mipaka na kumtuliza. Anamwambia akitaka anaweza kuchukua halua au hata tende, ambayo vile vile ni tamu kama *chocolate*. Uchezaji wa kifungu hiki wakati wa uimbaji unahusisha kuinama na kuinuka kwa zamu kulingana na midundo ya mpasho huku wachezaji wakiwa wanachezeshwa mikono yao kwa ishara ya kushangilia. Miondoko hii hufanana na namna mtoto anavyolalia bega wakati anapobembelezwā ili atulie. Aidha, pale wanapoimba sehemu hii, wanacheza wakiruka mbele na kurudi nyuma namna watoto wafanyavyo katika michezo yao mingi.

Bembelezi pia imeingiliana na utanzu wa *Modern* Taarabu-Mipasho kama kiitikio katika kiambatisho **17-NJ-Nalijua Jiji-Khadija Kopa.** Kwenye mpasho huu, bembelezi hii

yenye anwani **Nakuona Umechoka**, imejitokeza kama kiitikio. Wimbo huu huimbwa na watoto katika kushangilia timu zao pale wanapokuwa na michezo ya kubishana. Timu mbili pinzani huimbiana wimbo huu kwa kusudi la kuwasuta na kuwavunja moyo wenzao kwa kuwaambia kuwa wanaonekana kuchoka huku timu yao ikiwa bado na nguvu ya kuendelea na mashambulizi. Mashabiki huwakejeli kwa kuwaambia wapinzani wao maneno yafuatayo:

41. *Nakuona umechoka bao mezea tu,*
42. *Huku bado sijachoka bado mezea tu*
43. *Naona umeshuka posta bao mezea tu*
44. *Utaondoka chanika bado mezea tu.*

(17-NJ)

Katika sehemu ifuatayo, nitajadili kuhusu mwingiliano tanzu kati ya ngonjera na *Modern Taarabu-Mipasho*.

3.5.7 Ngonjera katika *Modern Taarabu-Mipasho*

Ngonjera ni aina ya nyimbo ambayo huimbwa na zaidi ya mtu mmoja kwa kupokezana. Utanzu huu umedhihirika katika utanzu wa *Modern Taarabu-Mipasho* kwenye wimbo ulioimbwa na Mzee Yusuf na Khadija Yusuf wenye anwani **Wagombanao ndio Wapatanao**. Kuthibiti hawa wawili wanaimba kwa kupokezana ili kudhihirisha umoja wao licha ya watu kudai kuwa walikuwa wametengana. Wanawakanya wanaowafitini wakome kwani kugombana kwa watu wenye uhusiano ni jambo la kawaida ambalo huishia kwa wao kupatana na kuendelea na shughuli yao.

Ngonjera hii ya Mzee Yusuf na Khadija Yusuf ni mfano wa namna nzuri ya kuchanganya tanzu mbalimbali za nyimbo. Inadhihirisha kuwa tunaweza kuwa na ngonjera- mipasho na mipasho- ngonjera ndani ya utanzu wa maigizo na ule wa semi. Hata hivyo, muziki huu unasalia na hadhi yake ya awali ya kuwa ni mpasho. Mwingiliano tanzu wa ngonjera na *Modern Taarabu-Mipasho* umedhihirika katika kiambatisho kifuatacho: **21-WGO**

Wagombanao-Mzee Yusuf & Khadija Yusuf

Utangulizi

- | | |
|--|-------------------------------|
| 29. <i>La mgambo limeshalia</i> | <i>Kwenu wapiga vuvuzela,</i> |
| 30. <i>Mungu katusaidia</i> | <i>Zimekwisha zenu hila.</i> |
| 31. <i>Wabaya tumewagundua</i> | <i>Zimeni zenu vuvuzela,</i> |
| 32. <i>Hizo ni za kombe la dunia</i> | <i>Na mambo ya futibola.</i> |
| 33. <i>Sisi tumeshaamua</i> | <i>Hakuna tena kunsila,</i> |
| 34. <i>Tena tunaomba dua tujalie Mola.</i> | |

(21-WGO)

Katika utangulizi huu, wawili hawa wanaimba pamoja wakikiri kwamba sasa wametambua wanaowagonganisha ili kuwakosanisha. Mradi wameshawagundua, sasa wanaamua kutokubali kutenganishwa tena na kuwashauri mahasidi wao wakome. Vivyo hivyo, wameamua kumuomba Mola awajalie heri njema katika umoja wao. Katika utangulizi huu vile vile wasanii hawa wametumia mfananisho wa kelele za vinywa vya wafitini na kelele zinazotokana na ⁹vuvuzela kupigwa. Mhusika wa pili anaanza kwa kutoa sababu za watu kugombana. Anasema kuwa kuna wale ambao hugombana kwa kutaka maendeleo na mara tu wanapoelewana, hutekeleza mambo yao kwa pamoja. Mhusika wa kwanza anaendeleza wazo hili la Khadija kwa kuonyesha mshangao wake kwa wafitini ambao wana fitina nyingi sana vinywani mwao :

35. *Khadija: Wengine wanagombana sababu maendeleo,
Na pale wakipatana wanafanya mambo yao.*
36. *Mzee: Nashangaa wenye laana na mavuvuzela yao,
Na maneno mengi sana metoka midomoni mwao.*

(21-WGO)

Kwa mujibu wa mhusika, ugomvi usio na maana ni wa zamani na ulitendeka hata kati ya wazazi, mabibi na babu zetu na kwa hivyo hili si jambo jipya. Hata hivyo, mwenzake katika mpasho husika anawasuta wafitini wao kwa kuwaita ‘ng’ombe watu’ na kuwauliza

⁹Vuvuzela ni kifaa kama baragumu ambacho hutumiwa zaidi na mashabiki kushangilia timu yao wakati wa uchezaji mpira wa kadanda. Ala hii hutumiwa sana katika uchezaji wa kadanda ya mashindano ya kombe la dunia. Wafitini wameulizwa wakomeshe kelele hizo hadi wakati wa kombe la dunia na uchezaji wa kadanda.

wawapishe kwani wamechoshwa na fitina zao. Anasema kwamba sasa wao wamo katika kikao kimoja cha mapatano. Wafitini wamewafitini kwa muda mrefu lakini sasa mapatano kati ya wasanii yamepatikana. Sasa wafitini wanatahayari. Haya yamewekwa wazi katika kifungu kifuatacho:

37. *Khadija: Wamegombana wazazi, mabibi na babu zetu,
Kwa viza vya kipuuzi, eti huyu mwari wetu.*
38. *Mzee: Wametujengea zizi, kaeni nyie ng'ombe watu,
Tumechoka na upuzi, na kuendekeza ya watu.*
39. *Mzee: Nyie ndio wapika sumu, mumezikaanga sana sasa mnaona haya.*
40. *Khadija: Na hao ndio wakaanga sumu, sisi maelewano hatuna huku
moto wachochea.*

(21-WGO)

Mhusika wa kwanza anarejea walipoanzia uimbaji wao kwa kumhusisha Mungu katika uhusiano wao. Anawaonya mahasidi wao kuwa watapata laana kutoka kwake Mungu kwa kuwakosanisha. Mhusika wa pili anakiri kwamba alikuwa amemchukia mwenzake kutokana na fitina nyingi aliyokuwa amepewa. Fitina huwakosanisha watu kutokana na maneno mengi ya uongo ambayo huleta machungu kwa waliofitiniwa. Wengine huwa hata hawataki kuongea na wenzao au hata kukutana na kukaa nao katika kikao kimoja.

Baada ya kugundua kwamba walikuwa wamekosana kwa sababu ya kufitiniwa, mhusika wa kwamza anaamua kumshukuru Mungu kwa kupatana kwao kwani amewawezesha kumjua aliyewakosanisha. Mhusika wa pili anaendeleza usemi wa mhusika wa kwanza kwa kumwomba Mungu awajalie neema ya kusonga mbele na ushirikiano wao kwani hata hatima ya watu waliogombana ni kupatana. Maoni haya yamedhihirika katika kifungu kifuatacho:

41. *Mzee: Mumeifanya haramu, kubwa mumezata laana Mungu atahukumia.*
42. *Khadija: Mie tena sina hamu nimeambiwa mengi sana mpaka
kukuchukia,*
43. *Mzee: Basi Mungu tumshukuru, mbaya tumemjua,*
44. *Khadija: Inshallah tupe nuru, mbele kutuangazia.*
45. *Kiitikio: Poleni wote wenye roho zoefu wa majungu,*

46. *Mzee: Wagombanao,*
 47. *Kiitikio: Ndio wapatanao,*
 48. *Khadija: Walisema,*
 49. *Kiitikio: Walimwengu.*

(21-WGO)

Kisha, mhusika wa kwanza anawashauri wafitini wao wote wawache kelele na mayowe yao na waje wajionee wenyewe walivyopatana. Anasema kuwa wafitini wao hawana lolote la kusema sasa kwani wao wamepatana. Mhusika mwa pili anasema kuwa wao wanaendelea mbele huku wafitini hawa wakiona wivu. Kawaida, wafitini hukosa kazi ya kufanya pale wale waliokuwa wakiwafitini wamepatana. Wafitini ni watu wa udaku wa kutafuta tafuta na kuingilia shughuli za watu wengine ili wapate kazi ya ufitini. Wanapokosa fitina za kueneza, husalia wakipiga porojo na makelele kama ilivyowekwa wazi katika kifungu kifuatacho:

50. *Mzee: Kelele,*
 51. *Kiitikio: Acheni kupiga kelele.*
 52. *Mzee: Mayowe*
 53. *Kiitikio: Njooni muone wenyewe.*
 54. *Mzee: Nyamazisha. Faza mauji, charaza charaza baba.(Mazungumzo)*
Hawana la kusema hawana.
 55. *Kiitikio: Hawana la kusema hawana.*
 56. *Khadija: Sisi bado,*
 57. *Kiitikio: Tunasonga mbele, wanaona ghere.*

(21-WGO)

Mhusika wa kwanza anaona kwamba sababu ya watu kuwafitini ni chuki waliyokuwa nayo kwake. Pia, hawamwezi ndio maana wanamsema. Mzee Yusuf ni anayeimba kama mhusika wa kwanza ni maarufu katika muziki wa Taarabu na hasa *Modern Taarabu*-mipasho ndiyo maana akaitwa *mfalme*. Khadija Yusuf ambaye ndiye mhusika wa pili katika mpasho huu pia ni mwimbaji hodari wa *Modern Taarabu* na ndiyo maana akaitwa *Chiriku* kutokana na sauti yake nyororo. Umaarufu wao huu ndio uliosababisha watu kuwafitini. Mzee Yusuf anawaonya wafitini wasije wakamchafua na kumtia ila kwa maneno matupu wanayoyasema. Kwake yeye hawana la kusema. Anawaonya kuwa

hatima ya fitina na ubaya wao ni aibu tu. Aibu hii itatokana na watu kugundua kuwa yote waliyoyasema kuhusu wasanii hawa ni ya uongo mtupu! Mhusika wa kwanza ameyaweka wazi malalamishi yake haya katika kifungu kifuatacho:

58. *Mzee: Hawaniwezi, ndo maana wananisema,
Wananichukia ndio maana wanaiteta sana.Msinichafue.*
59. *Kiitikio: Sitaki,*
60. *Mzee: Mtanitia doa*
61. *Kiitikio: Sitaki,*
62. *Mzee: Mtanitia doa*
63. *Mzee: Hawana la kusema hawana.*
64. *Kiitikio: Hawana la kusema hawana.*
65. *Mzee: Mwisho wa ubaya*
66. *Kiitikio: Aibu,*

(21-WGO)

Ngonjera hii ilivyowasilishwa imeweza kuonyesha ushirikiano mkubwa kati ya wasanii katika uimbaji wao. Ni kawaida kwa watu kuwakosanisha waimbaji mbalimbali kwa kuwafitini hasa wale wanaoonekana kunawiri katika fani hii. Maneno na matendo ya wasanii wawili hawa katika mpasho huu yamedhihirisha ujumbe wao mkuu kwamba wamepatana. Waliowatenganisha wanaulizwa wakae mbali kwani hawana la kusema sasa. Katika utendaji wa kanda ya Taarabu hii, wawili hawa wanapokezena uimbaji na hata kucheza pamoja wakikumbatiana ili kuonyesha umoja wao. Dhawabu ya wafitini ni laana kutoka kwa Mungu kama anavyosema Khadija Yusuf. Sehemu inayofuata itaangazia malumbano katika *Modern Taarabu-Mipasho*.

3.6 Malumbano ya Washindani katika *Modern Taarabu-Mipasho*

Katika ushairi wa Waswahili, malumbano¹⁰ yana historia ndefu ambayo ni ya jadi. Ni kawaida kupata malumbano hata katika mazungumzo ya kawaida ya Waswahili. Mazoea haya yamepenya hadi kwenye nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho*. Kuingizwa kwa

¹⁰Malumbano ya awali kabisa yaliyowahi kutambuliwa na Shaaban (1967) na Khatib (1992) katika ushairi yalikuwa kati ya Siti Binti Saad na waiyu wake. Kwa mujibu wa Ntarangwi (1998), malumbano hutumiwa na washairi katika kupimana nguvu za kiujuzi katika utanzu.

utanzu huu katika mipasho kumeyapa malumbano jukumu jipya la kudhihirisha ushindani wa ujuzi mkubwa wa usanii pamoja na umbuji wa wasanii katika nyimbo hizi. Washindani wametumia ubunifu mkubwa katika uteuzi wa maneno ili kuwapiku wenzao katika wanaloshindania na kuwakejeli. Malumbano yaliyojitokeza katika *Modern Taarabu-Mipasho* tuliyorejelea katika utafiti huu yameingiliana na utanzu wa maigizo, majigambo na hata utanzu wa semi. Haya yamedhihirishwa kupitia kwa nyimbo za Taarabu kwenye viambatisho vifuatavyo:

Katika utangulizi wa kiambatisho **20-UJ-Utalijua Jiji-Afua Suleiman**, mwanamke wa kwanza anamsuta mshindani wake kwa tabia zake za kishamba ambazo zimemfanya amnyang'anye mume. Tabia hizi ni pamoja na ufisadi, ujeuri, ukaidi, na ukali miongoni mwa nyingine kama ilivyo katika kiambatisho kifuatacho:

1. *Kazi yako ufisadi, jeuri ngebe na nongwa*
2. *Baraka ya ukaidi, ukali kama embe ngwangwa*
6. *Mwenzangu huna ujuzi, mpenzi umemuudhi*
7. *Kaja kwangu nimempokea*

(20-UJ)

Mhusika katika muktadha huu anamsema mwenzake kuwa ana vituko ambavyo ni kama vya mtu aliyerogwa. Hii ni kutokana na tabia yake ya kishamba ya kula andazi kwa togwa badala ya juisi au soda baridi. Juisi na soda baridi ni vinywaji vya mijini. Hivi ni vinywaji vya na matajiri mjini. Bei yake pia ni ghali kwa watu maskini kumudu kuvinunua. Kwa mujibu wa *Kamusi Elezo Huru ya Wikipedia*, togwa ni kinywaji baridi kinachotengenezwa kwa nafaka au maji ya matunda. Namna ya kutengeneza ni sawa na pombe ya kawaida ila tu haikubadilika bado kuwa na alikoholi. Hiki ni kinywaji cha kawaida ambacho hunywewa mashambani. Katika muktadha wa kawaida, andazi huliwa kwa chai na wala sio togwa. Matumizi ya togwa katika muktadha huu ni msisitizo wa ushamba alionao mwanamke anayerejelewa. Haya yamebainishwa katika kifungu kifuatacho:

3. *Vituko vya makusudi, si bure we umerogwa*
4. *Badala ya soda baridi, ama juice ya chungwa*
5. *Ushamba umekuzidi, andazi wanywia togwa*

(20-UJ)

Katika kujibu shutuma hizi, mshindani kwenye utangulizi wake katika kiambatisho **17-NJ-Nalijua Jiji**- anamjibu mwenzake kwa kumuuliza kuwa hata yeye ana nini? Mbona anauliza habari, kwani hana jibu. Maana yake katika muktadha huu ni kuwa sifa za mhusika huyu kulijua jiji zinajulikana kotekote, zimesambaa kote hata makonda (utingo) wanazijua. Hivyo, mshindani wake anauliza swali gani hilo lisilokuwa na jibu hadi watu wanamcheka? Makonda katika hali ya kawaida huwa waenezaji wa habari sana. Hii ni kwa sababu wao huwa na fursa ya kukutana na kutangamana na wasafiri kutoka sehemu mbalimbali katika vituo vya uabiraji magari. Hivyo, mshindani huyu anadai kuwa habari kuhusu yeye kujua jiji zinaweza kupatikana kotekote:

4. *Eti utalijua jiji?*
5. *Unauliza jibu huna habari, kawaulize makonda*

(17-NJ)

Asiye na ujuzi wa jiji ni huyu mshindani wake (mhusika wa kwanza) ambaye amelivamia jiji tu kama anayosema mhusika katika kiambatisho kifuatacho: **20-UJ-Utalijua Jiji-Afua Suleiman**

8. *Pokea chako kibomu* *shoga nakutumia*
9. *Hata ukinilaumu* *wako nishamchukua*
10. *Penzi ulimdhulumu* *visa ukamfanyia*
11. *Chachandu vitamtamu* *bwana hukumpatia*
12. *Bwana kapata wazimu* *kashindwa kuvumilia*

(20-UJ)

Mhusika wa kwanza katika muktadha huu anamlaumu mwivu wake kwamba alishindwa kutekeleza majukumu yake kama mke, hali iliyompelekea mumewe kukosa uvumilivu na kujipata ametwaliwa na mhusika wa kwanza. Hata hivyo mshindani katika kumjibu anasuta kuwa aliuvamia mji wakati usiokuwa na wake na kujitwalia wapenzi ambao ni

wa umri mdogo kuliko wake. Mshindani anamwonya mhusika wa kwanza aache kujigamba kwani mji huo si wake. Anamshauri asitische vituko vyake kwa vile Kopa analijua jiji hilo barabara kama ilivyobainika katika mishororo ifuatayo.

6. *Halua mji umeuvamia wala si wakati wako ewe,*
7. *Halua haflani watoto unawania wala si wa rika lako wewe,*
8. *Usijitie makuu bibi na mji huu si wako*
9. *Nalijua jiji bibi utakoma kwa vituko.*

(17-NJ)

Katika kiambatisho kifuatacho **20-UJ-Utalijua Jiji-Afua Suleiman,** mwanamke anayerejelewa anamkashifu mwivu mrejelewa katika mpasho wa Khadija Kopa kuwa amekuwa wa kuwapa wanaume uroda kwa foleni kule vijiwani na kuachwa ndoani kwa kuwa na tabia mbaya.

30. *Wasela wa vijiwani, nafuu wajipatia*
31. *Uroda kwa foleni, kwako wajipendelea*
32. *Wewe gumzo mjini, watu wanahadithia*
33. *Umeachika ndoani, kwa yako mbaya tabia*

(20-UJ)

Mwanamke mrejelewa katika mpasho wa Kopa anamjibu kuwa atulie kwani hayo ndiyo malimwengu katika kipande cha maneno kifuatacho ; ***Pole utapoa pole ndo dunia.*** Khadija Kopa anamsuta Afua kuwa kama anajisifu kuwa amesifika ajue mji huo si wake. Haya anayasema katika kifungu cha maneno kifuatacho ***13.Jamani mambo eti anatamba yeye na mji huu si wake.*** Majisifu yake hayafai kwa kuwa alifumaniwa na mkwewe mvunguni. ***11. Wafumbiwa wewe ulopatwa nalo mvunguni mtu na mkwewe.*** Hapa anajaribu kudhihirisha kuwa aliye na tabia potovu ni mrejelewa anayejisifu katika mpasho wa ***Utalijua Jiji.*** Isitoshe, anadai kuwa yeye ana mumewe ambaye anajulikana kama Esamboi ambaye anang'ang'aniwa na wanawake wengi. Haya anayasema katika mishororo ifuatayo:

20. *Koma kunifuatilia nina mume wangu ndani*
21. *Nadhani unamjua, Esamboi mjini*

22. *Wengi wamgombania, amewapiga na cheini*

(17-NJ)

Mhusika wa kwanza anamsuta mwivu wake kwa kumpaka matope kwa kujaribu kuonyesha sifa zake nzuri ambazo ni pamoja na nidhamu na utulivu nyumbani, ukarimu kwa ndugu na majirani, ucheshi na tabasamu na lugha tamu aliyojaliwa.

- 18..*Pamoja na ukarimu, kwa ndugu na majirani*
 19. *Ucheshi na tabasamu, kanijalia manani*
 20. *Nimepewa lugha tamu, nyoka hutoka pangoni*

(20-UJ)

Katika kumjibu, mshindani anajigamba kuwa yeye anajulikana mjini kwa urembo wake.

34. Najuli, najulikana kimwana. Anadai kwamba yuko sawa sana yaani **33.Unaniona*2 niko fiti?**, **35.Mtoto up to date natinga kama zamani,** akipita anavutia macho ya watu kumtazama. Yeye anajidai kuwa mjuzi wa jiji na anajilinganisha na gari kubwa ambalo lazima lionekane linapopita. **37. Nalijua jiji Bi. Shoti, ni gari kubwa utaumia.** Anajisifu vile ameweza kutembelea nchi zote na hivyo hawezi kupishana na mhusika wa kwanza. Anasema atamwacha kwa mataa, kwa maana ya kumwacha kwa taharuki au kama amezubaa.

38. *Ena nalijiua jiji Bi. Shoti, nitakuwacha kwenye mataa*
 39. *Nalijua jiji Bi. Shoti, nchi nzote nishaogelea*

(17-NJ)

Mshindani anaendelea kueleza kuwa anafahamu sababu za wivu kutoka kwa mhusika wa kwanza. Sababu anazotaja ni kuwa amekosa bwana wa maana. Pili, anadai kwamba mhusika wa kwanza ana umbo jembamba la jiti lisilopendeza. Tatu, havutii anapovaa nguo zinazombana. Aghalabu, wanawake huvaa nguo zinazowabana kwa nia ya kuonyesha uzuri na kuchongeka kwa maungo ya miili yao kwa nia ya kuwavutia wanaume. Mshindani anamsuta mhusika wa kwanza kuwa licha ya kuvaa nguo zinazombana, hakuna mwanamume anayevutiwa naye. Madai haya yanaendelezwa katika mishororo ifuatayo:

- 29. *Linokuuma Bi. Shoti, hupati bwana wa maana*
- 30. *Nahilo umbo la jiti, utahangaika sana*
- 31. *Hupendezi kwa taiti, hata nguo vao mapana*
- 32. *Nani atokudhibiti, shosti stara huana?*

(17-NJ)

Katika kujibu mhusika wa kwanza anadai kuwa ameshamtwaa mume wa mwenzake na wala mume huyu hatarejea tena. Anazidi kudai kuwa mwanamume huyu alikuja kwake kwa kudai bayana kuwa hamtaki tena yule mwanamke- mshindani wake. Kilichosalia kwa mshindani kama anavyokariri mhusika wa kwanza ni kilio na majuto kwa ushamba wake. Haya yamejitokeza katika mishororo ifuatayo :

- 46. *Kwako nishamchukua, kwako harudi tena we mwenzangu*
- 47. *Ohh utalia mwenzangu jiji utalijua.*
- 48. *Katamka waziwazi, kuwa hakutaki tena we mwenzangu*
- 49. *Ohh utalia mwenzangu jiji utalijua,*

(20-UJ)

Katika *Nalijua Jiji*, mshindani anamjibu mhusika wa kwanza na kujigamba kupitia kifungu kifuatacho kwamba:

- 25. *Mtoto wa boni town tena jiji naelewa*
- 26. *Nitapita uwanjani na wala sitakukimbia*
- 27. *In that case my dear, nishakupindua*
- 28. *Nalijua jiji tutapigana piku moja kwa kimaksudi*
- 44. *Oooh ajijua mtu hapa*
- 45. *Utamjulisha nimezaliwa mjini*
- 46. *Na kitovu changu kimezikwa Twaatugawe*
- 54. *Nalijua jiji bishoti ukirusha ngumi nitakurushia*
- 57. *Nalijua jiji pande zote.*

(17-NJ)

Kila mmoja wa wasanii hawa anajigamba kulijua jiji zaidi ya mwenzake. Ushindani wa aina hii ni wa kawaida katika utunzi na uimbaji wa Taarabu. Wakati mwingine malumbano huweza kugeuka na kuwa matusi baina ya wasanii. Hata hivyo, matumizi ya malumbano katika hali ya matusi ni mwiko katika jamii ya Waswahili. Malumbano haya huzungukia masuala tofauti tofauti ikiwa ni pamoja na salamu za kawaida hadi masuala ya kifalsafa. Maudhui katika malumbano hutegemea ujuzi wa lugha wa wasanii hali kadhalika masuala nyeti yanayoikabili jamii husika wakati huo (Kea, 2006).

3.7 Hitimisho

Sura hii imejadili na kufafanua kwa kutolea miktadha ya tanzu mbalimbali za fasihi simulizi kama ilivyojitokeza katika nyimbo za *Modern* Taarabu-Mipasho. Hata hivyo, tanzu hizi ni pana mno kwani zina vipera vingi kwa hivyo niliangalia baadhi tu ya vipera katika tanzu tulizorejelea. Tanzu hizi ni pamoja na maigizo, ushairi simulizi, ngomezi, masimulizi, mazungumzo na semi. Vipera vilivyojadiliwa ni pamoja na misemo, methali, lakabu, majigambo, mawaidha, khurafa, fomula ya kufungua na fomula ya kufunga na maigizo. Katika mbinu za utafiti, nilichanganua tanzu hizi kwa kukokota maneno, virai, vishazi, sentensi, aya na vifungu vya habari katika muziki teule wa *Modern* Taarabu-Mipasho ili kusisitiza uwepo na umuhimu wa mwingiliano tanzu katika *Modern* Taarabu-Mipasho. Sura inayofuata itaangazia dhima ya mwingiliano tanzu katika *Modern* Taarabu-Mipasho

SURA YA NNE

DHIMA YA MWINGILIANO TANZU KATIKA *MODERN TAARABU-MIPASHO*

4.0 Utangulizi

Sura ya nne imeainisha pamoja na kufafanua baadhi ya dhima ambazo ni pamoja na kupima ubingwa wa mhusika, kutumbuiza na kuchangamsha jamii, kuhifadhi na kuendeleza utamaduni, kuleta uhalisia, kuleta mtiririko wa ujumbe, kuimarisha mamlaka ya matini, kufikirisha na kumakinisha. Waaidha, dhima nyingine za mwingiliano tanzu ni kudhihirisha upekee wa mhusika, kupanua uwanda wa kina cha maudhui, kujitambulisha kwa fanani, kukuza na kufanya lugha ivutie, kuihamasisha jamii na nyenzo ya kuelewa hisia na mitazamo ya watu. Katika sehemu inayofuata, kila dhima iliyotajwa hapa itafafanuliwa kwa kutolewa mifano kutoka kwenye uchanganuzi wa data ya utafiti huu.

4.1 Kupima Ubingwa wa Mhusika

Kimsingi utafiti huu umebainisha kuwa mhusika hutumia mwingiliano tanzu kama fani katika kuisuka kazi yake kwa lengo la kutaka ipate kukubalika kisanii. Bulman (1989) anasema kuwa mwingiliano tanzu unaweza kutumika kama kipimo cha ubingwa wa mhusika. Hili huwezekana kutokana na namna mhusika huweza kudhihirisha mshikamano kati ya utanzu mmoja na mwingine na jinsi anavyoungiza mshikamano huo. Kupitia kwa dhima hii, mwingiliano tanzu umetumika kujenga muziki wa mipasho kutokana na vile tanzu mbalimbali ambazo ni pamoja na semi, khurafa, ngonjera, lakabu, fomula ya ufunguzi na ya kufunga, majigambo miongoni mwa nyingine zimeunganishwa kwa ustadi mkubwa katika kujenga na kufaulisha uwasilishaji wa nyimbo hizi. Mfano ni katika kiambatisho *3MC-Mpenzi Chocolate* ambapo mhusika ambaye ni Mzee Yusuf

ameweza kuanza kwa uigizaji akitua kutoka kwa ndege aina ya helikopta. Uigizaji huu unaingiza utanzu wa masimulizi kupitia kwa fomula ya ufunguzi. Mhusika anaendeleza mpasho huu kwa kuimba kwa lugha ya Kiswahili. Baadaye anachanganya na wimbo wa Kitanzania uitwao Sindimba kisha anaimba kwa lugha ya Kihindi. Isitoshe, mle ndani mwa kiambatisho hiki mna bembelezi ambayo inaimbwa kwa kuhusisha halua na tende, hali inayodhihirisha mwingiliano wa vipera tofauti tofauti vya utanzu wa nyimbo. Katika kiambatisho hiki pia Mzee Yusuf anatoa nasaha kwa wapenzi wa lugha ya Kiswahili ambayo imo katika utanzu wa mazungumzo. Mhusika anajigamba alivyopendwa sana na mpenzi wake anayemrejelea kama *Chocolate*. Hili hapa ni dhihirisho la ubingwa wa mhusika katika kuunganisha tanzu kwa namna inayoufanya muziki wake wa *Modern Taarabu-Mipasho* uvutie na ueleweke vyema.

4.2 Kutumbuiza na Kuchangamsha Jamii

Dhima iliyowekwa wazi na ya kimsingi ya *Modern Taarabu-Mipasho* ni kutumbuiza na kuichangamsha jamii. Mapigo ya muziki huu, miondoko yake, sauti za waimbaji na namna masuala mbalimbali yanavyojumuishwa katika muziki huu ni jambo lililoonekana kuvutia hadhira sana. Hadhira imeonekana kujumuika katika kila hatua ya uimbaji wa mipasho huku wakikariri mishororo mbalimbali katika nyimbo hizi ishara kuwa wanazifurahia na kujitambulisha nazo. Nyingi ya kanda za video zilizohusishwa katika utafiti huu zilidhihirisha umaarufu wa nyimbo za mipasho kutokana na jinsi kumbi za kuchezea nyimbo hizi zilivyofurika watu. Hadhira iliyotumbuizwa ilionekana kutambua dhima hiyo kwa kuwatuza wasanii mbalimbali jukwaani kwa fedha pale walipokuwa wakiimba. Hii ni mojawapo ya sifa za utendaji katika nyimbo za mipasho na Taarabu kwa ujumla. Wakati mwingine hadhira ilionekana kukosa hata nafasi ya kutosha kufanya miondoko mbalimbali pale walipokuwa wakijumuika kucheza nyimbo hizi. Burudani hii ni njia moja ya kuliwaza na kutuliza nafsi za hadhira.

4.3 Kuhifadhi na Kuendeleza Utamaduni

Kupatikana kwa bembelezi ndani ya *Modern Taarabu-Mipasho* ni ishara ya kukubalika kwa utamaduni na fasihi simulizi ya Waswahili ambapo nyimbo hizi zinapatikana. Aidha, zinaonyesha kuwa wasanii wa mipasho wanayaelewa mazingira yao sawasawa kiasi cha kuweza kukumbuka na kuhusisha nyimbo za watoto. Uhusishaji wa nyimbo hizi katika mipasho hunuiwa kuisisimua hadhira ambayo ni ya vijana na watu wa makamo pale wanapokumbushwa na kuimba nyimbo zao za utotoni. Ngoma za Kiafrika katika utamaduni wa Waswahili zinapata nafasi nzuri na kuingiliana na mipasho katika kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe. Uingizaji wa ngoma hizi katika mipasho ni dhihirisho kuwa wasanii wa mipasho wanaufahamu na kuenzi utamaduni wao. Wanajivunia nyimbo zao za kiasili ambapo wanaziwasilisha kwa watu wa tamaduni nyingine. Nyimbo hizi ni pamoja na chakacha, lelemama, goma.

4.4 Kuleta Uhalisia

Kipengele cha maigizo kimejidhihirisha zaidi katika kazi za fasihi simulizi na hasa *Modern Taarabu-Mipasho*. Dhima yake ni pamoja na kusisitiza matukio yanayotendeka katika jamii na kuleta uhalisia. Uhalisia umesisitizwa zaidi na maigizo kwenye nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho* ambazo zimetoa nafasi kwa jamii kuweza kujifunza kutokana na matukio yaliyoigizwa. Maigizo hayo mbali na kuleta uhalisia yametumiwa kuendeleza utamaduni wa jamii hasa kutokana na maleba yaliyotumika. Aidha, ala za muziki zilizotumika mfano ngoma, ni dhihirisho la utamaduni wa jamii husika. Isitoshe mavazi mbalimbali yaliyovaliwa katika nyimbo tofauti tofauti za mipasho kama vile kanzu za wanaume na nguo ndefu zilizovaliwa na wanawake zinadhihirisha na kuendeleza utamaduni wa jamii ya Waswahili. Pia kuna nyimbo kama vile *Tenda Wema* ulioimbwa na Mwanamtama ambapo wasanii wanapoanza kuimba wamevalia marinda yaliyotengenezwa kutoka kwa mkonge, yaliyopakwa rangi mbalimbali kuyarembesha,

kanga zilizofungwa viunoni na kofia iliyosukwa kwa makuti. Katika wimbo huu wanataja mnazi dhihirisho la mazingira ya pwani. Wimbo wanaoanza nao ni wa kitamaduni, miondoko yao pia siyo ya mipasho ila ni ya kitamaduni kwa lengo la kuonyesha utamaduni wao. Matumizi ya ngoma za kitamaduni ni muhimu katika kuendeleza na kudumisha utamaduni hali kadhalika kuboresha uwasilishaji wa ujumbe katika mipasho. Hivyo mwingiliano wa mipasho na nyimbo za kitamaduni umetumika kama kitambulisho cha jamii husika.

4.5 Kuleta Mtiririko wa Ujumbe

Semi katika *Modern* Taarab-Mipasho zimetumiwa katika kuleta mtiririko wa ujumbe uliokusudiwa na wasanii miongoni mwa majukumu mengine. Aidha, mwingilianotanzu kati ya semi na *Modern* Taarab-Mipasho umewasaidia walengwa kuhusisha kile kinachotajwa na maisha yao ya kila siku na hivyo kurahisisha na kuharakisha uelewaji wa ujumbe. Semi ni mafumbo ambayo hufumbwa kutokana na yale yanayopatikana katika mazingira ya jamii. Hivyo, ufumbuzi wa semi huhitaji mtu awe na ufahamu wa kile kilichorejelewa na semi zile. Maana, vilevile hupatiwa semi kulingana na ufahamu wa kinachorejelewa kwa mujibu wa ufahamu wa walengwa. Katika utafiti huu, utanzu wa semi umeingiliana na *Modern* Taarab-Mipasho kupitia kwa methali, misemo, mafumbo na lakabu kama ilivyoshughulikiwa katika sura ya tatu ili kufanya kuwe na mtiririko wa ujumbe katika uwasilishaji wa nyimbo za *Modern* Taarab-Mipasho.

4.6 Kuimarisha Mamlaka ya Matini

Pia, kuingiliana kwa semi na *Modern* Taarab-Mipasho kumetumika kuimarisha mamlaka ya matini inayozalishwa. Hii inatokana na sababu kuwa, kupitia kwa semi, msanii huweza kuipa sauti yake mamlaka na heshima kupitia kwa sauti za wahenga wanaowakilisha jamii (Wanjala, 2015). Semi kama utanzu wa fasihi simulizi ni mali ya

jamii. Hakuna msanii ambaye huzua semi kutoka kwa ombwe tupu. Hivyo semi huakisi mambo yanayopatikana katika jamii husika. Kwa kutumia semi, msanii huwa hawakilishi maoni yake mwenyewe ila hutumia maoni yanayokubalika na kupatikana katika jamii pana katika kujieleza. Kwa kutumia mafumbo yaliyojikita katika muktadha wa kijamii, ujumbe anaouwalikisha msanii hupata mamlaka kwa kuwa na msingi thabiti katika yaliyomo ndani ya jamii. Hivyo, semi zimetumika katika *Modern* Taarab-Mipasho kudhihirisha umahiri wa mafanani wa muziki huu wa mipasho pamoja kuuwasilisha usemi wa jamii pana ambamo wanatoka.

4.7 Kufikirisha na Kumakinisha

Dhima nyingine inayoambatana na mwingiliano tanzu katika mipasho ni ile ya kuifikirisha na kuimakinisha hadhira. Matumizi ya khurafa, mafumbo, methali na misemo huhitaji hadhira kufikiri sana ili kupata kiini cha linalozungumziwa. Maudhui huwa yamefumbatwa kwa maneno machache mateule katika nyimbo hizi. Yanayorejelewa aghalabu hutokana na mazingira ya jamii husika na matukio ya kila siku hivyo inakuwa rahisi kwa wanajamii kufumbua ujumbe. Hata hivyo, ujumbe uliofumbwa huhitaji mtu aliye makini katika kuutambua kama ilivyokusudiwa. Huu ndio utamu wa nyimbo za mipasho pale hadhira inapopata maana ya ujumbe uliofumbwa. Wengine huenda hatua zaidi ya kuuhusisha ujumbe ule na hali halisi au mtu halisi katika jamii ile na hivyo kuufanya muziki wa mipasho kukubalika na jamii zaidi. Mfano ni khurafa katika mpasho wa **11 PM-Paka Mapepe**. Inabidi hadhira itafakari kuhusu mhusika ‘paka’ anayerejelewa katika wimbo huu. Jibu litapatikana tu kwa kuhusisha tabia na matendo ya mhusika huyu ‘paka mapepe’ na yale ya wasanii wenye sifa kama hizo katika ulimwengu wao halisi. Hivyo basi katika muktadha huu, semi katika *Modern* Taarabu-Mipasho zimetumika katika kupunguza makali ya ujumbe uliokusudiwa kwani itahitaji hadhira kuzipa semi hizo maana.

4.8 Kudhihirisha Upekee wa Mhusika

Matumizi ya mwingiliano tanzu husaidia kudhihirisha upekee wa kila mhusika katika uwasilishaji wa kazi yake kwani kila mmoja ana mtindo wake wa kipekee. Upekee huu huwezesha na ubunifu wa fanani pale anapoitunga na kuiwasilisha kazi yake. Upekee huu pia huitwa mtindo, ambao ni namna ya pekee inayomtambulisha fanani mmoja kutoka kwa fanani wengine. Upekee humsaidia fanani kuwasilisha ujumbe wake kikamilifu kwa kuifikia na kuilenga hadhira yake. Fanani kama vile Mzee Yusuf ana upekee wa namna anavyotunga, kuimba na kucheza nyimbo zake ambao ni tofauti na ule wa Khadija Kopa ambaye ana namna yake maalumu ya kuwasilisha nyimbo zake. Upekee katika muziki wa mipasho ni jambo wanalojivunia fanani wengi katika kushindana nani bingwa na maarufu katika muziki huu. Upekee wa mhusika huwa na madoido muhimu katika kuifanya kazi yao yote kuivutia hadhira yao. Ubunifu wa kila mhusika katika mipasho umechangia katika kudhihirisha upekee wake na kuivutia hadhira kubwa. Hali hii pia imechangia kuwepo kwa umaarufu mkubwa wa nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho* kutokana na namna zinavyowasilishwa.

4.9 Kupanua Uwanda wa Kina cha Maudhui

Matumizi ya mwingiliano tanzu katika mipasho ni muhimu katika kupanua uwanda na kina cha maudhui yanayowasilishwa katika nyimbo husika. Kwa mfano, *Modern Taarabu-Mipasho* inapotumia mafumbo, misemo, methali na utanzu wa khurafa, maudhui yanayowasilishwa huweza kupata maana pana kwani vipera hivi vyote vinahitaji ufafanuzi wa kina ili vieleweke. Aidha, khurafa itumikapo, hadhira haina budi kuweza kuifafanua ili ipate maana iliyokusudiwa kuwasilishwa katika ule wimbo wa mipasho. Mfano mzuri ni khurafa ya **11 PM-Paka Mapepe** ambapo hadhira hupata maudhui mbalimbali kama vile ulafi na tamaa kama ilivyo katika kiambatisho kinachofuata:

16. *Paka huyo paka, paka mapepe paka,*
 17. *Umpe kuku na bata, yeye hatotosheka,*
 18. *Umpe japo steki huyo paka, hatakushukuru huyo paka,*
 19. *Atakutoroka huyo paka, Akimwona panya huyo paka.*

(11PM)

Adha, kuna maudhui ya kutoaminika miongoni mwa mengine kutokana na wimbo huu. Hii ndiyo maana fasihi ikaitwa sana inayotumia lugha katika kuumba, kusuka na kuwasilishia ujumbe wake kwa njia ya ustadi mkubwa. Hali hii huondoa uchapwa ambao ungepatikana ikiwa maudhui yangejitokeza kwa njia sahili isiyohitaji hadhira kufikiria kwa kina.

4.10 Kujitambulisha kwa Fanani

Mwinglianotanzu kati ya utanzu wa majigambo na *Modern Taarabu-Mipasho* umedhihirisha kuwepo kwa dhima ya kujitambulisha kwa fanani pale anapojisifu. Kwa mfano, katika wimbo wa **6 FS-Fullstop**, Khadija Kopa anajitambulisha kwa ubingwa wake wa muda mrefu kwa kusema ifuatavyo katika kiambatishi hiki:.. **hatukuingia juzijuzi jiji la Dar-es-Salama.** Hii ni namna ya kujitambulisha kuwa yeye si mgeni katika uwanja wa muziki wa aina hii. Ana ujuzi na uzoefu wa kutosha ama wa kutajika. Anasema kuwa yeye ni hodari anayesifika kote. Hivyo, anawashauri maadui wake wakome na wajipange upya kwani hawamwezi. Anaendelea kujisifu jinsi ametulia bila wasiwasi hata wakija na waganga lori zima, wachinje hata na paka hawamwezi. Pamoja na ukweli kuwa haya yote yanasemwa kwa njia ya majigambo, yanatueleza sifa mbalimbali anazopaswa kuwa nazo mwanamke anayesawiriwa katika muziki wa mipasho. Msingi wa majigambo haya ni mazingira na utamaduni wa Waswahili. Wengi wa Waswahili ni wa dini ya Kiislamu ambapo wanaume wanaruhusiwa kuoa hadi wanawake wanne. Kila mwanamke katika ndoa ya aina hii hung'ang'ania kumpendeza mumewe. Ukewenza huleta mabishano makali, chuki, na wivu baina ya wanawake ambao hujaribu kupata penzi la mume wao. Si ajabu malumbano mengi na majigambo baina ya

waivu huhusu urembo, wanavyojitunza, mapishi na hata kwenda kwa waganga kama anavyosema Khadija Kopa katika **6-FS**

1. *na nnajua kunengua kanipenda, kanizimikia ukweli,*
2. *nahasa pale, naporembua.*
3. *Sasa wezi wa mabwana, nawaambia mtawachwa katwaa.*
4. *Nawapa onyo 'full stop', hii ni challenge full gear.*
5. *Nyie, taipu zenu za vichochoroni, ndio zinazowafaa.*

(6FS)

4.11 Kukuza na Kuimarisha Lugha

Mwingiliano tanzu pia umetekeleza dhima ya kuikuza na kuinogeza lugha. Kuingiza tanzu mbalimbali katika utanzu mmoja kunahitaji ujuzi na ubingwa wa mazoea ya mhusika. Kuweza kuzichangana tanzu hizi ifaavyo ili kuwasilisha ujumbe huhitaji mhusika aelewe barabara lugha anayoitumia. Aidha, hadhira italazimika kupanua ujuzi wao wa lugha ikiwa watataka kupata ujumbe unaowalislishwa katika nyimbo za mipasho. Katika hali kama hii, wasanii na hadhira hawana budi ila kuimarisha ujuzi wao wa lugha husika. Matokeo ya mchakato huu ni msamiati mpya na wakati mwingine matumizi yake mapana kijitokeza. Kwenye uwasilishaji wa ujumbe katika baadhi ya nyimbo kama vile ***1-KCR-Kijiba cha roho***, ***6FS-Fullstop*** na ***3-MC-Mpenzi Chocolate***, matumizi ya mazungumzo, semi na hata majigambo yamedhihirisha ukwasi wa lugha iliyotumiwa na wasanii

4.12 Kuihamasisha Jamii

Mwingiliano tanzu wa *Modern Taarabu-Mipasho* na nasaha ulikuwa muhimu sana kwa vijana. Hali hii imesababishwa na changamoto kama vile UKIMWI, ukahaba, kutumia vipodozi vya kubadili rangi ya ngozi na hata mavazi. Kupitia kwa mipasho, Khadija Kopa ameweza kwa njia sahili kutoa nasaha kwa vijana na wanawake. Nyimbo za mipasho ni kivutio kikubwa sana kwa vijana na wanawake hasa tukirejelea kanda za

video zilivyodhihirisha kumbi zilivyofurika mashabiki wa mipasho wakati wa uwasilishaji wa nyimbo hizi. Hivyo basi, Khadija Kopa alitumia fursa hii vizuri sana katika kuwasilisha ujumbe wa onyo kuhusu suala la vipodozi vinavyowaharibu wasichana wa Kiafrika ngozi kama ilivyo katika kiambatisho kifuatacho:

- 39. *Vikarolaiti vyenu, vinavyowapa jeuri,*
- 40. *Hivyo vikarolaiti vyenu, nitavipiga marufuku hapa.*
- 41. *Mimi nina rangi yangu, sitaki uso wa baka.*
- 42. *Mimi nina rangi yangu, na tena bado nawaka.*

(6FS)

Kando na kuburudisha, nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho* zilidhihirisha mwingiliano wa maigizo na nasaha katika kuielimisha jamii ili kuitahadharisha dhidi ya hatari inayopatikana katika kushiriki ngono kiholela pamoja na suala nyeti la mapenzi katika ulimwengu wa wanawake na vijana. Kama ilivyo mojawapo ya sifa za nyimbo za mipasho, Khadija Kopa anaubwaga ukweli waziwazi kuhusu ugonjwa wa UKIMWI kwa kuitahadharisha jamii ijiepushe nao ili iepuke vifo. Haya yanajitokeza katika ukokotaji ufuatao:

- 87. *Watoto wangu wa kiume, nisikilizeni nyie,*
- 88. *Mnaojiita masharobaro, nisikilizeni.*
- 89. *Nyie mabarobaro, nisikilizeni.*
- 90. *Nawaambia kina kaka, wanawake wanajua.*
- 91. *Pale pana pa utamu, wamepapamba maua,*
- 92. *Ukikosa gonorrhoea, ukimwi utakuuwa.*
- 93. *Ukimwi utakuuwa, ukimwi utakuuwa.*

(6-FS)

Vivyo hivyo, ushauri mwingine sawa na huu umetolewa katika **28-FK- Funga Kazi-Machupas Family-** kuhusu ugonjwa wa UKIMWI ambao unaua.

- 16. *Umekuwa boda boda, hata huku kaa,*
- 17. *Dunia utaiaga, ukimwi unauwa.*

(28-FK)

4.13 Nyenzo ya Kuelewa Hisia na Mitazamo ya Watu

Dhima nyingine iliyotekelezwa na mwingiliano tanzu katika *Modern Taarabu-Mipasho* ni ile ya kuwa nyenzo ya watafiti kuelewa hisia na mitazamo ya watu kuhusu jamii zao na nafasi zao katika jamii zile. Aidha, watu wameweza kuelezea masuala nyeti yanayowaathiri katika jamii zao kwa ufanisi kama vile uganga, wivu, fitina na hata ubinafsi kupitia mwingiliano tanzu kwenye *Modern Taarabu-Mipasho*. Mfano mzuri ni katika **6FS-Fullstop-Khadija Kopa** ambapo suala la uganga na matambiko limetajwa:

33. *Hata mje na waganga lori nzima, himaya yangu keshafika.*
34. *Mnilie mizimu na makafara, na mchinje hata paka.*

(6FS)

Wasanii kama Mwanaidi Shabaan na Khadija Yusuf wamedhihirisha suala la wivu na madhara yake katika jamii. Katika **15-UKSU Umejuaje Kama Si Umbea- Mwanaidi Shaaban** anauliza:

1. *Umejuaje*
2. *Umejuaje nimefanikiwa umejuaje?*
3. *Umejuaje ukaona fi umejuaje?*
4. *Umejuaje kama si umbea umejuaje?*

(15-UKSU)

Swali hapa ni kuwa mrejelewa amepataje kujua yalimfanyikia Mwanaidi Shabaan kama si kupitia kwa umbea? Hii ni fitina au uzushi unaoendelezwa na watu katika jamii hasa baada ya maskini kuonekana kufanikiwa. Mwanaidi anauliza, mbona mrejelewa akahisi wivu baada ya kujua kwamba Mwanaidi Shabaan kafanikiwa? Ni jambo lipi linalimsumbua kumhusu Mwanaidi? Ndipo anamshauri aufyate ulimi wake kwani amesikika akisengenywa, awache wivu na fitina kwani wakati wa Mola kumbariki Mwanaidi umewadia. Mrejelewa hana uwezo wala nafasi ya kuizuia fanaka ya Mwanaidi. Haya yamejitokeza katika ya kifungu kifuatacho: **15-UKSU Umejuaje Kama Si Umbea- Mwanaidi Shaaban:**

13. *Umesikika waamba, wewe bado unagomba, lipi likusumbualo jambo?*

14. *Macho yako kama mamba, wala hujui kufumba, hakikupiti kitu kirembo,*
15. *Japo mie sijatamba, wala sio wa kujigamba, lakini sifichi langu pambo,*
16. *Kasirika sasa vimba, bure jua hutaziba, wewe jifunze ujue mambo.*
17. *Endelea kunichimba, nenda kwa wachawi omba, jua Mungu hapigi kwa fimbo,*
18. *Adabu yako elewa, nimefanikiwa mie,*

(15-UKSU)

Utanzu kama vile wa ngonjera na malumbano uliwapa wasanii fursa ya kueleza matatizo yao na kutoa suluhu yake katika nyimbo zao. Mfano sadifu ni katika **21-WGO-Wagombanao- Mzee Yusuf & Khadija Yusuf** ambapo wasanii hawa wawili wametumia ngonjera hii kueleza chanzo cha tatizo la kutengana kwao. Awali walikuwa wamependana sana na kushirikiana katika kila walilolitenda. Ushirikiano huo uliwaitea mafanikio makubwa. Hata hivyo, wasanii hawa waligombana na wakatengana baada ya kufitiniwa na watu. Baadaye wanatoa suluhu la kurudina na kushirikiana tena pale walipogundua kilichokuwa kimewatenganisha. Haya yamewekwa wazi katika kiambatisho kifuatacho:

1. *La mgambo limeshalia, kwenu wapiga vuvuzela,*
2. *Mungu katusaidia, zimekwisha zenu hila.*
3. *Wabaya tumewagundua, zimeni zenu vuvuzela,*
4. *Hizo ni za kombe la dunia, na mambo ya futibola.*
5. *Sisi tumeshaamua, hakuna tena kunsila,*
6. *Tena tunaomba dua tujalie Mola.*

(21-WGO)

4.14 Hitimisho.

Ufafanuzi ulitolewa katika sura hii umeangazia dhima mbalimbali zinazotekelezwa na mwingiliano tanzu katika *Modern Taarabu-Mipasho* kama ilivyodhihirika katika utafiti huu. Baadhi ya dhima hizi ni kuiburudisha jamii, kuelimisha jamii, kunogeza ujumbe, kumtambulisha mhusika, kuitambulisha jamii, kuhifadhi na kuendeleza mila na utamaduni wa jamii pamoja na kuifikirisha jamii. Nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho* ni mali ya jamii inayotokana na jamii. Hivyo basi mwingiliano tanzu wa nyimbo hizi

haufanyiki katika ombwe tupu na hivyo unatarajiwa kutekeleza majukumu mbalimbali katika jamii husika. Pia, maudhui, muktadha na utendaji wake wote umejikita katika yanayopatikana katika jamii.

SURA YA TANO

MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO

5.0 Utangulizi

Sura hii imetoa muhtasari wa tasnifu kwa kurejelea kila sura, matokeo na mapendekezo ya utafiti kutokana na ufasiri wa data iliyochanganuliwa katika sura ya nne. Yafuatayo ni maelezo kuhusu muhtasari wa kila sura ya utafiti huu.

5.1 Muhtasari wa Tasnifu

Tasnifu hii ina sura tano kwa ujumla ambazo zimeingiliana na kuchangiana katika kuikamilisha. Sura ya kwanza imeshughulikia usuli wa suala la utafiti, malengo ya utafiti na sababu za kuchagua mada. Pia imeshughulikia upeo na mipaka ya utafiti na msingi wa kinadharia ambapo tulijadili nadharia za mwingilianomatini na umuundo na mwisho ikajadili njia zilizotumika kukusanya, kuwasilisha na kufasiri data katika utafiti huu. Ufafanuzi umetolewa kuwa kuna aina mbili kuu za taarabu; Taarabu asili na *modern* Taarabu. Pia sura hii imeeleza kuhusu mitazamo miwili inayorejelea asili ya taarabu katika Afrika Mashariki. Mtazamo unaoshikiliwa na wataalamu wenye asili ya kigeni kama vile Topan unaeleza kuwa asili ya taarabu ni Misri huku wataalamu wa Kiafrika ambao ni pamoja na Khatib, Ntarangwi, Khamis na Mwamzandi miongoni mwa wengine wakieleza asili ya taarabu kuwa ni mtagusano wa tamaduni ya Waswahili na wageni kama vile Waarabu waliotembelea pwani.

Suala la utafiti huu lilizingatia kwa kina matumizi ya mwingiliano tanzu na dhima yake katika muziki wa *Modern* Taarabu- Mipasho. Hii ni kwa sababu mwingiliano tanzu katika fasihi simulizi una uamilifu mkubwa katika kuwasilisha ujumbe unaodhamiriwa na

mtunzi kwa hadhira. Aidha, matumizi mwafaka ya mtindo wa mwingiliano tanzu hufanya muundo wa kazi ya fasihi kuivutia hadhira lengwa kando na kutekeleza majukumu mengine muhimu. Suala hili la utafiti lilielekezwa na malengo matatu: kujadili mwingiliano tanzu kama unavyojitokeza katika *Modern Taarabu-Mipasho*, kuchanganua miktadha mbalimbali ya mwingiliano tanzu katika muziki wa *Modern Taarabu- Mipasho* na kutathmini dhima ya mwingiliano tanzu katika muziki wa *Modern Taarabu- Mipasho*. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya mwingilianomatini ambayo ilizalisha ile ya mwingiliano tanzu. Aidha, nadharia ya umuundo ilishirikishwa. Nadharia zote mbili kimsingi zinasisitiza umuhimu wa kuzingatia mwingiliano wa tanzu mbalimbali katika uchambuzi wa utanzu mmoja kwa kuondoa mipaka baina ya tanzu hizo ikiwa tunatarajia kupata matokeo mazuri.

Mengine yaliyoshughulikiwa katika sura hii ya kwanza ni ufafanuzi wa muundo wa utafiti, ukusanyaji wa data, sampuli ya utafiti na vifaa vya utafiti. Utafiti ulichukua muundo wa kimaeelezo. Katika kukusanya data, utafiti huu ulifanywa katika sehemu mbili kuu; maktabani na nyanjani. Sehemu hizi zilichangiana na kukamilishana na kuzalisha data toshelevu kwa utafiti huu. Uteuzi wa muziki wa *Modern Taarabu-Mipasho* uliorejelewa ulikuwa ni wa sampuli makusudi. Nyimbo zilizohusishwa katika utafiti huu ni zile zilizosheheni mwingiliano tanzu ambao ni kiini cha malengo ya utafiti huu. Kupitia kwa njia ya kisikiliza na kutazama, mtafiti aliweza kuteua kanda za mipasho zilizodhihirisha mwingiliano tanzu katika uwasilishaji wake.

Sura ya pili ilishughulikia uainishaji wa tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili, mwingiliano tanzu, uainishaji wa tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili, utanzu wa ushairi simulizi na utanzu wa *Modern Taarabu-Mipasho* kama ilivyojadiliwa katika mapitio ya maandishi yakiwemo vitabu, makala, tasnifu za maktabani na mtandaoni. Kutokana na mapitio ya maandishi mbalimbali, ilibainika kuwa ugiligili katika misingi ya uainishaji

wa tanzu za fasihi simulizi umesababisha tofauti za aina na idadi ya tanzu hizi kulingana na miainisho ya wataalamu mbalimbali. Hali hii pia ilichangiwa na historia ya uainishaji ulimwenguni ambayo iliegemea mtazamo wa Ki-Aristotle. Mtazamo huo ulipendekeza kila utanzu ushughulikiwe kwa kuwekewa mipaka maalumu. Baadaye wasomi wa kwanza Waafrika na fasihi ya Kiafrika walirithi mtazamo huu wa Kiaristotle na kuuendeleza hali ambayo ilikosa kuzaa matunda mema. Ilivyo ni kwamba fasihi ya Kiafrika ikiwemo ile ya Kiswahili huwa na tanzu ambazo ni vigumu mno kuzishughulikia kila moja kutokana na jinsi zinavyoingiliana, zinavyochangiana na kuumbana katika kuboresha uwasilishaji wa ujumbe.

Miainisho ya awali ya tanzu za fasihi simulizi haikuzingatia mwingiliano tanzu unaopatikana katika utendaji wa tanzu hizi. Pia sura hii imefafanua ugiligili uliopo kutokana na uainishaji huu. Maelezo yametolewa kuhusu utanzu wa ushairi simulizi pamoja na sifa zake ambamo nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho* zinapatikana. Mapitio ya maandishi yamebainisha kwamba kazi mbalimbali kuhusu muziki wa Taarabu zilikuwa na michango yake kwa utafiti huu na pia mianya iliyochochea kutekelezwa kwa utafiti huu.

Vile vile, katika sura hii ya pili asili ya nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho*, sifa zake, muundo wake, maudhui yake na utendakazi wake kwa ujumla umeweza kuelezewa kwa kina. Pia ni katika sura hii ambamo maana ya mipasho imeelezwa. Mipasho ni kipera cha *Modern Taarabu*, jina ambalo linamaanisha ‘nyimbo zenye urushianaji wa matusi na mabishano kupitia kwa utendaji wake.’ Jina *mipasho* linatokana na kitenzi cha Kiswahili *pasha*, chenye maana ya ‘kusababisha kupata’, ingawa katika muktadha huu kile anachopata mtu ni matusi na kejeli! Hata hivyo neno hili [mipasho] limetolewa katika maana ya msingi ya kimsamiati na limepewa maana ya ziada yenye kumaanisha kusema

ukweli au kusema bila ya kuogopa ili mhusika anayepashwa au anayesemwa aupate ujumbe wake vizuri sana na umwadilishe, umwelimishe au kumwadabisha.

Yaliyoshughulikiwa katika sura ya tatu ni pamoja na uchanganuzi wa data, uwasilishaji na maelezo kuhusu miktadha mbalimbali ambayo ilidhihirisha jinsi tanzu mbalimbali zilivyojitokeza katika nyimbo za mipasho. Data zilizokusanywa katika utafiti huu zilihaririwa kuanzia mwanzo hadi mwisho wa utafiti ili kuzichuja na kuhifadhi habari zilizokuwa na umuhimu katika utafiti huu. Uchanganuzi wa mwingiliano tanzu kutoka nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho* zilizokuwa zimeteuliwa na kunukuliwa umetolewa kwa njia ya maelezo ya kina na ya moja kwa moja. Ukokotaji wa mistari, mafungu ya maneno na beti mbalimbali zilizodhihirisha mwingiliano tanzu mbalimbali katika nyimbo zilizoteuliwa umehusishwa katika uchanganuzi wa data. Maelezo na ufafanuzi kuhusu tanzu zilizoingiliana yametolewa.

Katika sura ya nne, dhima inayotekelezwa na mwingiliano tanzu katika nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho* zilizochanganuliwa imejadiliwa. Miongoni mwa dhima hizi ni pamoja na kuchangamsha, kumtambulisha mhusika, kuhifadhi na kuendeleza historia na utamaduni, kudhihirisha upekee wa mhusika na kukuza lugha. Hatimaye, sura hii ya tano imetoa muhtasari wa kila sura, matokeo pamoja na mapendekezo.

5.2 Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii imeshughulikia matokeo ya utafiti kwa mujibu wa malengo ya utafiti.

Yafuatayo ni maelezo kuhusu lengo la kwanza.

5.2.1 Mwingiliano tanzu katika *Modern Taarabu-Mipasho*

Katika kushughulikia lengo la kwanza la utafiti huu, iliweza kubainika kwamba tanzu mbalimbali za fasihi simulizi zimeingiliana sana katika mianisho yake hali ambayo

imejidhihirisha katika *modern* Taarabu- mipasho. Hali hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na kukosekana kwa misingi thabiti ya kurejelewa katika kuainisha tanzu na vipera mbalimbali vya fasihi simulizi. Miongoni mwa misingi ambayo hurejelewa katika uainishaji wa tanzu na vipera vya fasihi simulizi ni kama vile maudhui, muktadha, ala na wasanii.

Vivyo hivyo, wasomi mbalimbali waliibuka na idadi tofauti ya tanzu na vipera vya fasihi simulizi kulingana na misingi waliyorejelea katika miainisho yao. Uainishaji uliofuatwa na wasomi wa awali ulijikita katika mtazamo wa Kiaristotle ambao ulizingatia kanuni za uainishaji wa tanzu za fashi simulizi kwa misingi ya fasihi ya Kizungu kwa kuziwekea mipaka maalumu. Hali hii ilikosa kuafikiana na hali ilivyo katika fasihi simulizi ya Kiafrika, ya Kiswahili ikiwemo, ambayo tanzu zake huingiliana sana kwa mhusika kujua au kutojua hasa inapowasilishwa. Hivyo katika utafiti huu, uchanganuzi katika uwasilishaji wa *modern* Taarabu- Mipasho ulifanywa kwa kuzingatia mwingiliano tanzu kama ilivyo na fasihi simulizi ya Kiafrika.

5.2.2 Miktadha Mbalimbali ya Mwingiliano tanzu katika *Modern* Taarabu-Mipasho

Utafiti huu uliweza kudhihirisha miktadha mbalimbali ya mwingiliano tanzu katika muziki wa *Modern* Taarabu-Mipasho na hivyo kutimiza lengo la pili la utafiti huu. Baada ya kuzichunguza nyimbo za mipasho, ilibainika kuwa hakuna utanzu unaoweza kujisimamia kivyake bila kuathiriana na tanzu zingine. Mwingiliano tanzu katika *Modern* Taarabu-Mipasho ulisababishwa na mchakato wa mwingilianomatini ambao uliwezesha kazi husika kukopa, kubashiri, kunukuu, kuiga na hata kurejelea tanzu zingine ama katika

fani au maudhui bila kuzingatia mipaka dhahania ya kitanzu. Katika nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho* zilizorejelewa katika utafiti huu, tanzu mbalimbali zilidhihirika kuumbana, kuchangiana na kujengana katika mwingiliano ulioimarisha uwasilishaji wa ujumbe.

Mchakato wa mwingiliano tanzu huu uliendelea kwa namna ambayo ama wasanii wa nyimbo hizi za *Modern Taarabu-Mipasho* walikusudia au ilitokea kwa wao kutokusudia. Mfano Mzee Yusuf katika *Mpenzi Chocolate* aliweza kuwasilisha mpasho ambao umo katika muundo wa shairi, akaigiza, akazungumza katikati ya wimbo, akaongezea mtindo wa kitamaduni wa aina ya sindimba, akahusisha ngomezi, akajigamba na wakati huohuo akatoa nasaha katika wimbo huo mmoja. Hali hii ilidhihirisha jinsi tanzu katika fasihi simulizi ya Kiswahili zilivyoubana na kuingiliana kwa namna ambayo kama tulivyotangulia kueleza awali, ni vigumu kuweka mipaka maalumu kwa kila utanzu. Katika uwasilishaji wake, tanzu hizi ziliingiliana na kubadilikabadilika katika uwasilishaji wa utanzu mmoja bila ya kuathiri hadhi ya utanzu huo.

Fomula ya ufunguzi na fomula ya kufunga ambayo hupatikana katika utanzu wa masimulizi, ilijitokeza sana katika mianzo na miisho ya nyimbo za mipasho. Kimsingi, fomula hizi zilitumika kuashiria kuanza na kumalizika kwa nyimbo zile. Katika masimulizi, fomula hizi hutumika katika kuteka nadhari ya hadhira na kuiweka tayari ama kwa kuanza au kumalizika kwa masimulizi. Vivyo hivyo katika mipasho, fomula hizi ziliashiria mwanzo na mwisho wa kila wimbo na hivyo kuiandaa hadhira vilivyo. Aidha, katika utanzu huu wa masimulizi, kipera cha khurafa kilidhihirika pale ambapo kishazi ‘paka mapepe’ kilitumika katika mojawapo wa mipasho. Katika mpasho huu, mwanamke kiruka njia anapewa sifa za paka mapepe ambaye hata apewe penzi la aina gani, hawezi kuridhika. Hii ni ithibati kuwa utanzu wa masimulizi unaweza kutumika

ndani ya utanzu wa nyimbo za *Modern Taarabu-Mipasho* katika kuboresha uwasilishaji wa ujumbe.

Utanzu wa semi ulidhihirika zaidi ambapo misemo, methali, lakabu na mafumbo yalitumika katika mipasho. Utanzu huu wa semi ulitumika kuupa uzito ujumbe uliokuwa ukitolewa kwa namna ya kimafumbo. Semi zitumikapo huhitaji mtu kuwa makini, afikirie sana ili apate maana ya kinachozungumziwa. Kila mtu anaweza kupata maana tofauti kutoka semi hizi na hivyo kuupa wimbo mmoja maana nyingi na inayotofautiana kutegemea msikilizaji na muktadha wake. Katika kutumia semi hizi mbalimbali, wasanii walifaulu kuonyesha ukwasi wao wa lugha ya Kiswahili pamoja na kuendeleza utamu wa lugha hii.

Mwingiliano tanzu ulidhihirika hata zaidi katika majigambo yaliyotumika katika mipasho. Wasanii walitumia utanzu huu wa majigambo katika kijitambulisha kwa kujimiminia sifa tele kuonyesha ubingwa wao. Miongoni mwa wasanii hawa ni pamoja na Khadija Kopa na Mzee Yusuf ambao katika nyimbo zao *Fullstop* na *Mpenzi Chocolate* walionyesha majigambo ya hali ya juu. Aidha, utoaji wa nasaha umeingizwa katika mipasho kwa namna ya kuvutia sana. Licha ya kuwa mhusika anaimba kuhusu mapenzi motomoto kati yake na mpenziwe, hasiti na wala hasahau kuwaonya vijana wa kisasa ambao anawatahadharisha dhidi ya kujiingiza katika mapenzi ya kiholela kutokana na kwamba watapata ugonjwa wa UKIMWI; wavulana na wasichana wawe makini wanapoteua waume na wake kwani wote si wanaume ila wengine ni magumegume! vile vile, wanaume wanaonywa kuwa si wote wawaonao ambao ni wanawake ila wengine ni makwekwerekwe!

Utafiti huu aidha uligundua kuwa kutokana na nyimbo za *Modern Taarabu- Mipasho* kuwa katika fasihi ya Kiafrika, kulikuwa na mwingiliano tanzu wa tanzu nyingine za

Kiafrika katika mipasho wakati wa uwasilishaji wake. Nyimbo za kitamaduni kutoka jamii mbalimbali za Kiafrika kama vile *sindimba* kutoka jamii ya Wamakonde na ngoma aina ya *sebene* zote mbili kutoka nchini Tanzania ziliingiliana na ile ya Taarabu ya mipasho na kusaidia kuumba maudhui na mnato katika muziki huu wa mipasho. Vivyo hivyo, katika uchezaji wake, baadhi ya wachezaji wa bendi walicheza kwa mtindo wa *lingala* na kwa midundo iliyolingana na ile ya mtindo wa lingala- mtindo kutoka Zaire. Mfano ni katika nyimbo za Mzee Yusuf- *Mpenzi chocolate* na *Wasiwasi Wako*.

Utafiti huu ulibainisha kuwepo kwa ufaraguzi kama sifa mojawapo muhimu katika nyimbo za *Modern* Taarabu ambapo waimbaji huwa na uhuru wa kufaragua wimbo fulani ili ukidhi mahitaji ya muktadha au sherehe tofauti na ile iliyotungiwa awali. Sifa hii ilidhihirika kupitia kwa namna wasanii mbalimbali katika nyimbo zote za mipasho zilizorejelewa na ambazo zilidhihirisha kuwepo kwa mwingiliano tanzu; wasanii walidhihirisha ubunifu katika kufaragua na kuchanganya ipasavyo tanzu mbalimbali katika uwasilishaji wao. Hili linashadidiwa hata zaidi na msingi mojawapo wa nadharia ya umuundo kuwa mtunzi anapaswa kuwa na uhuru wa ubunifu kwa kuingiza vipengele vipya katika kazi, mradi tu azingatie muundo wa kimsingi wa mfumo huo. Mwelekeo huu huingiza ujumi katika fasihi katika kupitisha ujumbe kwa urahisi maana kazi inakuwa ya kuvutia.

Wasanii wanafaa kuwa makini katika utunzi wao kwa maana jinsi kazi inavyowasilishwa pia ni muhimu katika usanii. Wasanii wa *Modern* Taarabu-Mipasho iliyorejelewa walibainisha ubunifu mkubwa katika utunzi na uwasilishaji wa kazi yao. Ili kufaragua ipasavyo, inabidi mhusika awe na ujuzi wa utunzi na uwasilishaji na pia afahamu namna anavyoitumia lugha husika. Wasanii katika *Modern* Taarabu-Mipasho waliweza kuwasilisha kazi zao kwa ufasaha huku wakionekana kuimudu lugha ya Kiswahili kutokana na jinsi walivyofaulu kuchanganya tanzu mbalimbali katika muziki wao.

5.2.3 Dhima ya Mwingiliano tanzu katika *Modern Taarabu-Miapsho*

Hatimaye, utafiti huu ulitimiza lengo la tatu la utafiti huu kwa kudhihirisha kuwa mwingiliano tanzu katika *Modern Taarabu-Mipasho* hutekeleza majukumu mbalimbali kama vile kuburudisha na kuchangamsha, kuelimisha na kumakinisha jamii, kuonyesha ubingwa na upekee wa wasanii, kutoa hisia mbalimbali za wasanii kuhusu jamii zao na kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii husika. Pia, kupitia kwa mwingiliano tanzu katika uwasilishaji wa *Modern Taarabu-Mipasho*, wasanii waliweza kueleza changamoto mbalimbali za kila siku zinazowakabili maishani mwao kama vile wivu, fitina, magonjwa, uchawi na matatizo katika ndoa. Hatimaye, wasanii waliweza kutoa suluhu kwa matatizo haya kwa kuwapa ushauri wanajamii kuhusu namna ya kuyakabili.

5.3 Mapendekezo

Baada ya kushughulikia na kupata kuwa kuna mwingiliano tanzu katika *Modern Taarabu-Mipasho* utafiti huu upendekeza kuwa utafiti mwingine unaweza kufanywa kwa kutumia nadharia hii ya mwingiliano tanzu katika vipengele vingine vya fasihi ili kuona matokeo yake yatakavyokuwa.

Pili, baada ya utafiti huu kuelekezwa na nadharia ya mwingilianomatini na ile ya umuundo, basi utafiti zaidi unaweza kufanywa kuhusu mwingiliano tanzu wa *Modern Taarabu-Mipasho* kwa kuelekezwa na nadharia nyingine za fasihi.

Tatu, licha ya tafiti ambazo zimefanywa kuhusu nyimbo za Taarabu mintarafu mtindo wake na mwingiliano tanzu katika Taarabu miongoni mwa zingine, utafiti huu unapendekeza kuwa tafiti zaidi zifanywe kwani uwanja huu wa Taarabu ni mpana na kuna mengi tu ya kushughulikiwa na watafiti wa fasihi.

Pia, data iliyotumiwa katika utafiti huu ni nyimbo 32 za *Modern Taarabu- Mipasho* kutoka Zanzibar. Hivyo basi utafiti zaidi unaweza kufanywa kwa kuhusisha data pana zaidi au hata data nyingine.

Baada ya kutumia mbinu ya kutazama na kusikiliza nyimbo za *Modern Taarabu- Mipasho*, utafiti mwingine unaweza kutendeka kwa kushirikisha mbinu zaidi au tofauti kama vile kushiriki moja kwa moja wakati wa uwasilishaji wa nyimbo hizi.

Mwisho, katika utafiti huu tuliteua nyimbo za *modern Taarabu* kutoka eneo la Zanzibar. Hivyo basi tunapendekeza utafiti mwingine ufanywe kwa kuteua nyimbo za *modern Taarabu* kutoka eneo lingine.

MAREJELEO

Allen, G. (2000). *Intertextuality*. London: Routledge.

Askew, K. M. (2002). *Performing the Nation: Swahili Music and Cultural Politics in Tanzania*. Chicago & London: The University Chicago Press

Askew, K. M. (1997). *Performing the Nation: Swahili Musical Performance and the Production of Tanzanian National Culture*. Tasnifu ya Uzamifu (Haijchapishwa), Harvard University. Ann Arbor: University Microfilms.

Bakhtin, M.M. (1981). *The Dialogic Imagination: Four Essays*. Ed. Michael Holquist. Trans. Caryl Emerson and Michael Holquist. Austin and London: University of Texas Press.

Bakhtin, M. M. (1984). *'Rabelais and His World'*. Mfas. Helene Iswolsky. Bloomington: Indiana University.

Bazmaleh, A. S. M (2006). *Winner of special category, Human Rights Award, 2006*, Malindi Museum – webb memorial library.

Best, J. W., na Khan, J.V. (2010). *Research in Education (10th ed)*. Pearson Education Ltd: India.

Beez, J., na Kolbusa, S. (2003). *Kibiriti Ngoma: Gender Relations in Swahili Comics and Taarabu-music. Stichproben. Wiener Zeitschrift für kritische Afrikastudien*.

Bryman, A. (2001). *Social Research Methods*. New York: Oxford University Press.

- Bulman, S. (1989). "The Buffalo –Woman Tale: Political Imperatives and Narrative Constraints in the *Sunjata* Epic", katika Barber, K. Na Farias, P. F. (1989). (Wah). *Discourse and it's Diguis: The Interpretation of African Oral Text*. Birmingham: Centre of West African Studies.
- Culler, J. (2003). *Structuralism and Literature*. London: May field publishing company.
- Finnegan, R. (2012). *Oral literature in Africa*. Open Book Publishers.
- Hawkes, T. (1997). *Structuring and semiotics*. London: Methuen.
- Hughes, A. (1989). *Testing for Language Teachers*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Ipara, I. O., na Maina, G. (2008). *Fani ya Isimujamii kwa shule za Sekondari*. Oxford University Press.
- Kavugha, F. S. (1977). *Desturi na Mila za Wapare*. Vuga Press.
- Kea, P. (2006). *Usemezano katika nyimbo za Taarabu*. Tasnifu ya uzamili (Haijachapishwa), Chuo kikuu cha Kenyatta.
- Kenguru, P. M. (2013). *Athari za Fasihi Simulizi katika Riwaya ya Utubora Mkulima: Tasnifu ya Uzamifu* (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi: Nairobi
- Khatib, M. S. (1981). Taarabu ni Fasihi Simulizi? *Makala ya Semina ya Fasihi Simulizi*. Chuo Kikuu cha Dar-es- salaam: TUKI.
- Khatib, M. S. (1992). *Taarabu Zanzibar*. Dar-es-salaam: Tanzania Publishing House.
- Kirkegaard, A. (1996). *Taarabu na Muziki wa densi. The popular Musical Culture in Zanzibar and Tanzania seen in relation to Globalisation and Cultural Change*. Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa), University of Copenhagen: Copenhagen.
- King'ei, G. K., na C, Kisovi. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Kothari, C. R. (2003). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley.
- Lodge, D. (ed.) (2005). *Modern Criticism and Theory*, (2nd ed). Pearson Education Ltd: India.
- Lyons, J. (1981). *Language and Linguistics*. London: Cambridge University Press.
- Marshalls, C., na Rossman.(1989). *Designing Qualitative Research*. Newbury Parcca: Sage Publishers
- Masinde, E.W. (2003). *Ushairi wa Kiswahili: Maendeleo na Mabadiliko ya Maudhui: Tasnifu ya Uzamifu* (Haijachapishwa), Chuo kikuu cha Kenyatta: Nairobi

- Mazigwa, S. A. (1991). *Fasihi ya Kiswahili*. Ndanda Peramiho: Benedictine Publishing Company.
- Merriams, S. (1998). *Quantitative Research and Case Study Application in Education*. San Francisco: Bass Publishers.
- M’Ngaruti, T. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Miles, B. M. (1994). *Quantitative Data Analysis*. Sage Publishers.
- Muiruri, P. K. (2006). *Maandalizi Mufti ya K.C.S.E Fasihi Simulizi, Maswali na Majibu*. Palco Enterprises Ltd.
- Mulokozi, M. M. (1989). Tanzu za Fasihi Simulizi. Katika, *Mulika*. Na. 21. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Mushengyezi, A. (2003). *Twentieth Century Literary Theory*. Literature Kampala: Makerere University.
- Mugenda, O. M., na Mugenda A, M. (1999). *Research Methods Quantitative and Qualitative Approaches*. Acts Press.
- Mugenda, O. M., na Mugenda A, M. (2003). *Quantitative and Qualitative Approaches*. Acts Press.
- Mwamzandi, I. Y. (2002). *Usemezano katika Umalenga wa Kiswahili: Mfano wa Taarabu*. Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa), Chuo kikuu cha Egerton.
- Mwamzandi, I. Y. (2002). *Majadiliano ya Tanzu katika Ushairi wa Kiswahili katika Utafiti wa Kiswahili*. Moi University, Eldoret: Moi University Press.
- Mwakasaka, C. S. (1977). *The oral Literature of Banyakyusa*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), University of Dar es Salaam.
- Ndungo, C. (2006). The Image of Women in the African Oral Literature: A Case Study of Gikuyu Oral Literature, katika *Gender Issues Research Report Series*. Na. 23. Ethiopia: OSSREA.
- Ngure, A (2003). *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Ntarangwi, M. G. (1998). *Taarabu Texts, Gender and Islam in Urban East African Context: Social Transformations among the Waswahili of Mombasa, Kenya*. (Unpublished). Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa), University of Illinois at Urbana Champaign
- Ntarangwi, M. G. (2001). “A Socio-Historical and Contextual Analysis of Popular Musical Performance Among the Swahili of Mombasa, Kenya” *Cultural Analysis*, (Volume 2).

- Njogu, K., na Wafula. R, M.(2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Jomo Kenyatta Foundation: Nairobi.
- Njogu, K., na Chimera, R. (2011). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation: Nairobi.
- Ogula, A. P. (2003). *Research Methods*. Department of Education: The Catholic University of Eastern Africa.
- Orodho, A. J. (2004). *Techniques of Writing Research Proposals & Reports in Education & Social Sciences*. Nairobi: Masola Publishers.
- Oyoyo, O. J. (2013). 'Uhakiki wa Fasihi katika Ngano Tano za Kiswahili'. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo kikuu cha Nairobi. Nairobi.
- Owen, C. E. (2010). *Taarabu and the Construction of Community Identity in Two Kenyan Towns*. The Robert D Clark Honors College of the University of Oregon
- Raman, S. P., W., na P, Broker. (2005). *A Reader' Guide to Contemporary Literary theory*. (5th Ed). Pearson Education Ltd.
- Robson, C. (1993). *Real World Research*. Blackwell Oxford UK and Cambridge U.S.A.
- Rono, P. (2013). *Uhakiki wa kimaudhui na kifani wa kidagaa kimemwozea*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi. Nairobi.
- Sarantakos, S. (1996). *Social Research*. Macmillan Education Australia: Moray Street, South Melbourne.
- De Saussure, F. (1916). *A course for General Linguistics*. Mac Graw Hill, New York.
- Khamis, A. M. S. (2001). *Redefining Taarab in relation to Local and global*
- Khamis, A. M. S. (2002). "Wondering about Change: The Taarab Lyric and Global Openness". *Nordic Journal of African Studies*. 11, 2: 198-205.
- Scholes, R. (1974). *Structuralism in Literature*. New Haven: Yale University Press.
- Sengo, T. Y. S. (1978). *Kudidimizwa kwa Fasihi na Wakoloni, Taamuli ya Fasihi Nadharia, Mtazamo na Mbinu za utafiti katika Fasihi Simulizi*. TUKI: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Sengo, T. S. Y. (1992). *Utamaduni wa Kiswahili: Wilaya ya Kusini-Unguja*, katika *Nordic Journal of African Studies* 1(1): 53–79 (1992). University of Dar-es Salaam, Tanzania.
- Senkoro, F, K. M. (1996). *Understanding Gender through Genre: Oral Literature as a Vehicle for Gender Studies in East Africa. A Paper Presented at The Annual African Literature Association*, Howard University, Washington DC.

- Senkoro, F. K. M. (2011). *Fasihi: Mfululizo wa Lugha na Fasihi*.KAUTTTL: Dar es Salaam.
- Shabaan, R. (1967). *Diwani ya 3: Wasifu wa Siti Binti Saad*. Dar-es-Salaam: Printpak Tanzania Ltd.
- Timammy, R. (2002). *Mombasa Swahili Women's Wedding Songs: A Stylistic Analysis*. Tasnifu (Haijachapishwa), University of Nairobi.
- Topan, F. J. (1992). 'Women and the Africanization of Taarabu in Zanzibar.' Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa), SOAS
- Topan, F. J. (2000). "Hot Kabisa! The Mpasho Phenomenon and Taarabu in Zanzibar", *Mashindano! Competitive Music Performance in East Africa*, ed. na Frank Gunderson katika Gregory F. Bartz, pp. 39-54. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.
- Traore, F. A. (2004). *Continuity and Change in Zanzibari Taarabu Performance and Swahili Forum*11: 75-81.
- Togwa-Wikipedia Kamusi Elezo Huru. kutoka <https://sw.wikipedia.org/wiki>
- Vuzo. A, S., N., na Njenga, M. (2011). *Upeo wa Insha kwa Shule za Upili*: Oxford University Press: Nairobi.
- Wainaina, M. (2002). *The Worlds of Gikuyu Mythology: A Structural Analysis*. Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta: Nairobi.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi : Focus publication Ltd
- Wamitila, K. W. (2006). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Focus Publishers Ltd.
- Wamitila, K. W. (2011). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: English Press.
- Wafula, R. M. (1992). *Nadharia kama mwongozo wa utunzi na uhakiki katika fasihi*, Staff seminar paper, University of Nairobi.
- Wanjala, W. F. (2015). *Mwingiliano tanzu katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika: Mfano wa Embalu na Mwaka Kongwa*. Tasnifu ya uzamifu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta Nairobi.
- Yego, E. K. (2013). *Nafasi Ya Mwanamke: Jinsi Inavyotetewa katika Nyimbo za Taarabu za Zanzibar*. Tasnifu ya uzamili (Haijachapishwa), Chuo kikuu cha Nairobi. Nairobi.
- Welleck, R. W. (1986). *Theory of Literature*, Harmondsworth: Penguin

KIAMBATISHO B: NYIMBO ZA TAARABU

Kiambatisho hiki kimehusisha nyimbo za mipasho zilizotumika kupata data ya utafiti huu. Asili ya nyimbo hizi ni sidii zilizounuliwa kutoka maduka yanayoziua. Nyimbo hizi zilinakiliwa baada ya kutazama na kusikiliza sidii husika.

1-KCR

Kijiba Cha Roho

1. Lo hasidi fisadi mkubwa, utakufa nacho kijiba cha roho
2. Kinakupekecha ndani kwenye moyo, utazikwa nayo roho mbaya na choyo
3. Utamwona hivi hivi mwana wa mwenzio, madagada na chititika mtoto

4. Roho ya kukereketa, kwa mambo yangu kufana,
5. Kuona nimempata, mvulana bomba sana,
6. Roho ya kukereketa, mifuko imejazana,
7. Kutwa kucha wanicheta, kunitilia fitina,
8. Nia kutupiga vita,tusipate kuona
9. Furusa hutoipata,yamiini tumelishana,
10. Nampenda muhi baka,na kwangu karoa sana,
11. Si muhini akitaka akitaka, nyama safi ilonona,
12. Utabakia kubweka, windo hulipati tena,

13. Utakufa nacho kijiba cha roho, utazikwa nayo roho mbaya na choyo
14. Acha we, acha nuksi, kila mtu na ndevu wake nenda katafute wako
15. Acha we, acha hasada, kila mtu na dili zake saka dema niko yangu
16. Wachwa we, acha fitina, kila mtu na riziki yakeugaga wa mafumbu.

17. Unachonga sana fulani,kuharibu jina langu,
18. Kwa mashoga majirani,wanipikia majungu.
19. Unachonga sana fulani, Mungu atakulaani,
20. Una hithni rohoni, una jelas mwenzangu,
21. Unaroga mapangoni,aje kwako bwana wangu,
22. Sito shea wanifitini,hadi kwa meneja wangu,
23. Ili nifutwe kazini,niharibikiwe mwenzangu
24. Hata ukifanya nini, fanya nini,hukati riziki yangu
25. Imeandikwa mbinguni, kasima ya fungu langu,

26. Utakufa nacho kijiba cha roho,utazikwa nayo, roho mbaya na choyo
27. Acha we, acha nuksi,kila mtu na ndevu wake, nenda katafute wako,
28. Acha we, acha hasada,kila mtu na dili zake, saka dema ndiko yangu.
29. Wachwa we, acha fitina,kila mtu na riziki yake,ugubaga wa mafumbu.

30. Utakufa nacho kijiti, cha kuchokoa rohoni,
31. King'asti humpati, kapoa kwangu nyumbani,
32. Utakufa nacho kijiti,wewe ameshakushiti.
33. Ananipa chakula chema,sina shida wala nini,
34. Na mavombo ya gharama,na fiwalo ya dhamani
35. Aidha ninamchuma,nachanulia mjini,
36. Ndo hayo yanokuchoma,yanokukata maini,
37. Unafanya kila jambo, kila jambo, unioe duniani
38. Ni bure zako hujuma,huniwezi mwafulani.

39. Utakufa nacho kijiba cha roho, utazikwa nayo roho mbaya na choyo.
 40. Acha we, acha nuksi, kila mtu na ndevu wake nenda katafute wako,
 41. Acha we, acha hasada, kila mtu na dili zake saka pema ndiko yangu.
 42. Wacha we, acha fitina, kila mtu na riziki yake, Mungu kagawa mafumbu.
 43. Achana na mie, sinijue jue, utakufa nacho kijiba cha roho
44. Achana na mie, sinijue jue, utazikwa nayo roho mbaya na choyo
 45. Achana na mie, sinijue jue, utaniona hivi hivi mwana wa mwenzio,
 46. Achana na mie, sinijue jue.

2-NN

Nitadumu Nayo- Mzee Yusuf

1. Utangulizi;
 2. **Yarabi iwe salamasalama usalimini**
 3. **Wasipate la kusema maadui asilani**
 4. **Mapenzi yawe ya daima yasiingiliwe na mtu,**
 5. **Waloomba tuachane wasipate kutucheka katu**
 6. **Nyoyo zao ziwaume kwetu wametoka patupu.**
7. Nimemzimia kichizi Ndio maana niko naye
 8. Namfagilia mpenzi Inshalah nitadumu naye
 9. Tunapendana azizi Iwe maisha mimi naye
 10. Anavyojua mapenzi Sijaona kama yeye
 11. Na kumkosa siwezi Mpaka nife na yeye
 12. Animaliza kwa pozi Na mapenzi yake yeye
 13. Kusema yote siwezi Hii siri yangu mie
14. Sijui nipewe nini Kwa huyu nishatosheka
 15. Huyu ndo wangu ayuni Hana hofu sina shaka
 16. Hata niambiwe nini Kwengine sendi teseka
 17. Kwake n"nakosa nini Napewa n"nachotaka
 18. Kikiwa cha bakulini Nakula pasi na shaka
 19. Kiwe ndani ya sahani Hunilisha muhibaka
 20. Simuachi asilani Wanochomwa nawataka
21. Wapo wanotia hila Ana hivi ana vile
 22. Nitadumu naye inshaallah Kwa Mola baraka tele
 23. Anajulia mashalah Tena ana sifa tele
 24. Kwa tabia hana hila Na umbo lake teule
 25. Nampenda kila mahala Nikienda huku na kule
 26. Penzi letu la muhala Si kama penzi la wale
 27. Kiulaini na kula na kula Furaha yetu milele
28. Wapo wanaotamani Penzi watuvurugie
 29. Hawawezi asilani Wala wasiingilie
 30. Labda nife nende kaburini Au afe nimzike yeye
 31. Mapenzi yetu ya shani Raha ya mambo yake oye
 32. Nampenda kama nini Mola jalie tutulie
 33. Kwake karaha sioni Raha pendo letu siye
 34. Cheko bashasha usoni Inshaallah nitadumu naye
35. Kiitikio;
36. **Oh, walahi naona raha raha kama nini**
 37. **Kwake sioni karaha huyu wangu ayuni**
 38. **Nitadumu naye kwa nguvu za Manani**
 39. Wan"ochonga **tutakomaa nao**
 40. Na wachonge **kimpango wao**
41. Ooh huyu ndo wangu ayuni kwani 42. **nampenda sana**
 43. Nitadumu nae kwa nguvu za Manani 44. **nampenda sana**
 45. Ooh nitakuwa na yeye maishani 46. **nampenda sana**

- | | |
|---|-------------------|
| 47. Labda afe nimzike au anizike mimi | 48. nampenda sana |
| 49. Acha waseme wao watachoka | 50. nampenda sana |
| 51. Acha wachonge wao kimpago wao | 52. nampenda sana |
| 53. Wacha wavimbe na wapasuke | 54. nampenda sana |
| 55. Hata niambiwe nini mimi simuachi | 56. nampenda sana |
| 57. Kwengine nifuate nini sitaki teseka | 58. nampenda sana |
| 59. Ooh huyu ndo wangu ayuni jama | 60. nampenda sana |

3-MC**Mpenzi Chocolate-Mzee Yusuf**

1. Utangulizi;
2. Imefika siku yenu, nyie kuwaambia kweli,
3. Huo unafiki wenu, na huo ufedhuli,
4. Hatuachani kwa maneno yenu, labda pindijalali,
5. Endeleeni na mirundo,
6. Sie tumependana,
7. Yeye ndio chocolati wangu, na mimi kwake kali,
8. Moyoni adhiti wangu, anayenificha baridi kali,

9. Basi naukveli, nakutamani wewe,
10. Unifiche baridi, mwili joto uwe,
11. Unaponukia udi, malaika hunisimama mie,
12. Hamu hamu hizi, hebu nikumbatie

13. Poleni nyie mafisadi, au wenye roho za ukaidi,
14. Yeye ndio wa uwaridi, raha zake kwangu huzidi,
15. Ananipa raha, ananipa raha ndani ya roho,
16. Nawapa karaha, nawapa karaha munaumwa roho,

17. Meseji zenu zenu zenu za karaha, Mie hazi, hazi nirushi roho,
18. Hamtaki sisi tule raha, tutazidi kuwaumiza roho
19. Kiwe kimoto ananipulizia, nikiwa na joto ananipepea,
20. Mzigo mzito huja kunitua, enye koroto ananifulia
21. Ye ndio kila kitu kwangu, mpenzi chocolate,
22. Ye ndio binti wangu sisikizi yoyote,
23. Kama ni tamu,
24. Nairamba, alivyotia,
25. Kama ni hamu,
26. Naipenda , aniswabilia
27. Ananitia nakshi, nakshi mahamumu,
28. Kumwacha sitaki, nitajidhulumu.
29. Kidonda tamu nzi ndo hufia,
30. Hapa patamu ndio maana nimetulia
31. Dhahari wazimu japari nimevua
32. Ananitia akshi, akshi mahamumu,

33. Kumwacha sitaki, nitajidhulumu.
34. Wanatamani tuachane,
35. wapi, shanshuu, Tuacheni tulale,
36. Na raha tuzile,
37. Ananitia akshi, akshi mahamumu,
38. Kumwacha sitaki, nitajidhulumu.
39. Halua, halua,
40. Halua, halua,
41. Halua, halua,
42. Halua, halua,
43. Halua halua, halua,
44. Halua, halua,
45. Haya ukitaka halua we chukua,
46. Halua, halua,

47. Ukitaka na tende pia chukua,
48. Halua halua
49. Uchungu moyoni unaniuwa,
50. Halua halua
51. Halua halua,halua,
52. Halua, halua,
53. Nakuona tu, unanifuatilia,
54. Mi nakuona tu, unaning'ang'ania,
55. Japo sitaki we wanifuatilia,
56. Japo sitaki we waning'ang'ania,
57. Nakuona tu, unanifuatilia,
58. Japo sitaki we waning'ang'ania,
59. Umerogwa wewe mwenzetu, Ulirogwa ama umetumwa,
60. Umerogwa.
61. Nei nei babuji,
62. Chuma chuma dede,
63. Nei babuji,
64. Chuma chuma dede,
65. Chuma, chuma,
66. Chuma chuma dede,
67. Ramaskhe babuji,
68. Chuma chuma dede,
69. Utanibeba leo, umekula hela zangu,
70. We utanibeba leo, umekunywa soda zangu,
71. Utanibeba leo, umekula hela zangu sana,
72. We utanibeba leo, siondoki peke yangu,
73. Utanibeba leo, umekula hela zangu,
74. Maneno maneno, mimi siwezi,
75. Kubishana bishana ovyo siwezi,
76. Kugombana gombana ovyo siwezi,
77. Kubishana bishana ovyo siwezi,
78. Nachokiweza labda ni kazi,
79. Hapo chacha,
80. Mimi ninasema ukweli,
81. Hapo chacha
82. Kimya wewe,
83. Helua, helua,
84. Helua, helua,
85. Helua, helua,
86. Haya ukitaka halua we chukua,
87. Halua, halua,
88. Ukitaka na tende pia chukua,
89. Halua halua
90. Haya ukitaka halua we chukua,
91. Halua, halua,
92. Uchungu moyoni unaniuwa,
93. Halua halua
94. Wanaonipenda wanipende,
95. Wanaonichukia na waende zao,
96. Ala, mpende akupendaye,
97. Asokupenda mtimue,
98. Mpende akupendaye, asokupenda usimng'ang'anie
99. Mpende akupendaye
100. Asokupenda mtimue,
101. Mpende akupendaye, asokupenda achana naye
102. Mpende akupendaye
103. Asokupenda mtimue,
104. Mpende akupendaye, asokupenda usimng'ang'anie
105. Mpende akupendayeasokupenda mtimue,

106. Haraka haraka haraka aende kule,Asije akakuua bure.
107. Halua halua, halua halua,
108. Haya ukitaka halua we chukua,
109. Halua, halua,Ukitaka na tende pia chukua,
110. Halua halua
111. Haya ukitaka halua we chukua,
112. Halua, halua,
113. Uchungu moyoni unaniuwa,
114. Halua halua

4-PN

Penye Neema-Miriam Mwinjuma

1. Wacheni Mungu aitwe Mungu,Mengi ayajua mapema,
2. Ameyapanga vizuri aliyoyaumba Mungu, Na kila kilicho chema,
3. Wenye ni sisi walimwengu, Ni nusuru ya daima,
4. Yote sababu hujawaiona Mungu,utaipata salama.

5. Penye neema ya Mungu,
6. Usta ya mja lazima, lazima.
7. Penye neema ya Mungu,
8. Usta ya mja lazima, lazima.

9. Binadamu mshumaa, unawaka huku unakwisha
10. Na dunia ni hatari, wahenga walisibitisha
11. Ukiendekeza njaa, huendelei maisha,
12. Mungu kakuashia taa, na afadhali ya maisha

13. Alo na husta ilomjaa, Huku yeye anakesha,
14. Anakuombea balaa,uyakimbie maisha
15. Unapojaliwa neema ya Mungu, lazima usla iweko,
16. Mabaya utaombewa, pia na majungu na nyingi chokochoko.
17. Mja hui kuwa imani ya Mungu Kwa kipato yako,
18. Ataomba dua, Amuombe Mungu iondoke kwako

19. Kama hakujaliwa, si aombe Mungu ataharibu chako
20. Hichi nilo nacho, kina waumiza roho,
21. Bure mtakufa nacho, kijiba cha roho.
22. Mnaikodolea macho, hema alonipa Mungu
23. Kama ninacho ninacho, uponyaji ni Mungu.

24. Jicho la ubaya kwangu, jicho la ubaya kwangu
25. Mnaloniangalia mnaloniangalia, ndo mimi kanipa Mungu
26. Ndo mimi kanipa Mungu, hata roho mkinitoa
27. Sina maringo ndogo, tabia yangu,

28. Wenye kinyongo na neema yangu
 - a. vimumu taa ya mumu,

29. Jicho la ubaya kwangu,
30. Jicho la ubaya kwangu,
31. Mnaloniangalia.
32. Mnaloniangalia,
33. Ndo mimi kanipa Mungu.
34. Ndo mimi kanipa Mungu.
35. Hata roho mkinitoa.

36. Wananiombea ili mradi nikose,
37. Wawe na njaa waradhi sote tukose,.
38. Ila Mola majaliwa, siku nipa kama wese,

39. Jicho la ubaya kwangu, jicho la ubaya kwangu,
40. Mnaloniangalia mnaloniangalia,
41. Ndo mimi kanipa Mungu,ndo mimi kanipa Mungu.
42. Hata roho mkinitoa.

43. Wenye chuki bai bai,
44. Wenye roho mbaya bai bai.

5-SMH

Sina Muda Huo-Leila Rashid

Utangulizi;

1. Kansi na washikaji, wakti sinao,
2. Na yako mengi mahitaji, sina muda huo
3. Mimi naisaga tonge, ili iende kinyawani,
4. Sitajitia mazonge, kuingia mashakani,
5. Ukiende huku, ukiende kule Kuitafuta riziki,
6. Sio kupiga kelele, kujiongezea dhiki.

7. Sina muda huo sina,
8. Wa kukaa viibarazani kumdiskasi mtu,
9. Sina muda huo sina,
10. Wa kukaa vipembeni nimsimange mtu
11. Na hamsini zangu, inanipeleka mbio,
12. Aloniamuru Mungu, siyamalizi kwa leo
13. Iwje ya walimwengu, mie sina muda huo,
14. Sinipikie majungu, mie si mke mwenzio
15. Muda huo sina, wakuchezea,
16. Naomba maulana, funguliwe njia

17. Kwanza tuheshimiane,
18. Mimi na we hatushei mume halau nikudiskasi,
19. Uongo tusizuliane,
20. Na vibaya usiniseme ukanitilia nuksi,
21. Usitake tuchapane, mi si wewe gume gume,
22. Ilokujaa mikosi, ukaya tusitafutane,
23. Huna kazi, si kalime, sema usinifosi

24. Huna haya muone, funga domo siniseme,
25. Niche sina nafasi, tafuta jambo nyingine.
26. La uongo usiseme, na wajinga usinimiksi
27. Kuna mengi ya kufanya sio kukudiskasi wewe,
28. Tafadhali nakukanya mie sina time na wewe

29. Sina muda
30. Wakupoteza.
31. Sina muda
32. Wakudiskasi mtu.

33. Yakunishughulisha kwako mie sikijui,
34. Yakunishughulisha kwako mie sikioni

35. Jialalie juu mpaka chini,
36. kisha nambie unanisumbua nini,
37. Hata nikae nikuseme pembeni.

38. Yakunishughulisha kwako, mie sikijui,
39. Yakunishughulisha kwako, mie sikioni
40. We ni wa kuambiwa, hivi uso namacho,
41. Si kikao kukaliwa, una nini chambilecho
42. Muda nilopewa, wa kutafuta kinacho,

43. Yakunishughulisha kwako, mie sikijui,
44. Yakunishughulisha kwako, mie sikioni

45. Mauji
46. Mauji anachana nyuzi
47. Kimalizio;
48. Una hamu nikuseme, Nikikusema utalia,

49. Una hamu nikuchambe, Nikikuchamba utazimia
50. Utabaki ati ati, la kwangu hulipati ng'o

6-FS

Full Stop-Khadija Kopa

Utangulizi;

1. Hamisi Simba, mwana nyamala, waambiena kuja.
2. Wamekataa corner wanakubali penalty.
3. kwa mara nyingine tena,
4. Mimi ni mtu wa watu, nisojua kunong'ona.
5. Jamani mapaparazi, mtajuta kuniona mnaingilia mapenzi,
6. Unayopeana na bwana mlianza na mizizi,
7. Penzi si la mwaka jana, hatukuingia juzijuzi jiji la Dar-es-Salama.
8. Umenipandia ngazi, ukashuka na milima.
9. Umelipiga mapenzi, joto joto lazizima.

10. Atayejitia bazazi
11. Ajue hana usalama.
12. Nitamfungia kazi,
13. Na mji atauhama
14. pamoja salamu klabu.
15. Twendekazi.
16. Fullstop wote kimya, zubaisha king'ori naongea.
17. Fullstop acheni kelele, na si rukhsa kujitetea.

18. Ole wenu mnaopita, njia za panya kunifuatilia.
19. Mimi niko majoha mando wa kike, hala ntawaarifu aaah!
20. Tena nalipa, Bishufi wa ukweli,
21. na nnajua kunengua. Kanipenda, kanizimikia ukweli,
22. nahasa pale, naporembua.

23. Sasa wezi wa mabwana, nawaambia mtawachwa katwaa.
24. Nawapa onyo 'full stop', hii ni challenge full gear.
25. Nyie, taipu zenu za vichochoroni, ndio zinazowafaa.
26. Sio wangu mimi, chumba na varanda tena ghorofani nampandia.

27. Fullstop jipangeni upya, hapa kwangu mumechemka.
28. Nina ladha tamu sana, ndio maana hataki kutoka.
29. Hata mje na waganga lori nzima, himaya yangu keshafika.
30. Mnilie mizimu na makafara, na mchinje hata paka.

31. 'Full stop' jipangeni upya, hapa kwangu mmechemka.
32. Nina ladha sweeti sana, ndio maana hataki kutoka.
33. Hata mje na waganga lori nzima, himaya yangu keshafika.
34. Mnilie mizimu na makafara, na mchinje hata paka.

35. Halafu wajifanya unalipa, hutafuti wako ukamweka.
36. Wewe huezi miliki yangu, baby cute wa Kiafrika.
37. Kwanza mimi niko peke yangu, nimetulia sina shaka.
38. Nimetulia na mume wangu, mtoto wa uhakika.

39. Vikarolaiti vyenu, vinavyowapa jeuri,
40. Hivyo vikarolaiti vyenu, nitavipiga marufuku hapa.
41. Mimi nina rangi yangu, sitaki uso wa baka.
42. Mimi nina rangi yangu, na tena bado nawaka.

43. Bandika bandika, mimi nabandua.
44. Nikuhidi maarifa, huna unalolijua.
45. Bandika bandika, mimi nabandua.
46. Tumependana wawili, wewe unajijua.
47. Hakutaki pesa mbili, hulijui takataka.
48. Bandikabandika, mimininabandua.
49. Bandikabandika, mimininabandua.

50. Semasema, Musa Musa. Musa mipango.
51. Mfalme wabesi Tanzania.

52. Wametoka kwa Harita .
53. Tumependa na wenyewe, maneno maneno ya nini.
 54. Eti Zera naughty boy, kwani mnataka nini?
 55. Sasa ninawaambia kijana yuko makini.
 56. Wala habitaji foja, maximum nikochini.
 57. Hahitaji msichana wa jezi, kiwanda anachondani.
 58. Anavyotua vifaa, kama yuko Marekani.
59. Kama yuko Marekani.
 60. Usigusemoto utapunguza.
 61. Napajuahapa Bongo, pameeneavituko.
 62. NakujuakuleZeni, kumeeneavituko.
 63. Na Mombasa mjini, pameeneavituko.
 64. Kina dada wakwambia, mambo nimpambaiko.
 65. Kama hujajipodoa, hapa Bongo hunasoko.
66. Hapa Bongo huna soko.
 67. nikwelezejehunasoko.
 68. Ninakuwekakipupa,nakupasahunasoko.
 69. Usigusemoto utapunguza, usigusemotoutapunguza.
70. Na kina dada wa bongo, wakweli wajanjasana
 71. Kina dada wa Mombasa, nanyiewajanjasana,
 72. Na kina dada waZenji, kwakweli wajanjasana,
 73. Mkifikauwanjani, macho mnatazana.
 74. Sasamkitokanje, mnawagobeamabwana.
 75. Mnagobeamabwana, mnagobeamabwana.
 76. Eeeh usiguse moto, utakuuguza,
 77. Eeeh usiguse moto utakuuguza.
78. Wapenzi wangu nawapenda, usifikiriutani,
 79. I love you so much, usifikiriutani.
 80. Nimewamiss, usifikiriutani.
 81. Wapenziwangu nawapenda, usifikiri utani.
 82. Hatamnapochizika, naposimama stejini,
 83. Na pale mnapopagawa, napokuwa uwanjani,
 84. Mungekuwa embe dodo, ningewala na majani.
85. Ningewala na majani, ningewala na majani.
 86. Usigusemoto, utapunguza, usigusemotoutapunguza.
 87. Watotowanguwakiume, nisikilizeninyie,
 88. Mnaojiitamasharobaro, nisikilizeni.
 89. Nyiemabarobaro, nisikilizeni.
 90. Nawaambia kina kaka, wanawakewanajua.
 91. Pale pana pa utamu, wamepapambamaua,
 92. Ukikosa gonorrhoea, ukimwiutakuuwa.
93. Ukimwiutakuuwa, ukimwiutakuuwa.
 94. Usigusemoto, utapunguza,
 95. Usigusemoto, utapunguza.
96. Kimalizio;
 97. Totimoto, watuache.
 98. Totimoto, tupishetupite.
 99. Totimpangomzima,
 100. Totimpangomzima.
 101. Loliondo kwa babu, sharubaru kapewa kikombe
 102. Akasema nangoja mrija boi.

7-KMKV

Kila Mtu Kivyake Vyake-Khadija Kopa.

1. Kila mtaka ni jina saba, kupata mwingi msiba,
2. Umepata uloyataka, pole dada yamekufika.
3. Mapenzi umeyafuja, na bwana amekuacha,
4. Kachoka vyako viroja, kaamua kukuacha,

5. Ye kesha nawa mikono kwako, jua hatahadhirika,
 6. Hababaishwi na urembo wako, waudhi ye keshachoka.
 7. Pita mbele usigeuke, kila mtu kivyake vyake,
 8. Yanini yako makeke, mimi sasa ndiye wake,

 9. Komuniketion yake kwako wewe ameshaikata,
 10. Hataki mashaka amechoka nawe kwa yalomkuta,
 11. Hatokurupuka kukufuata wewe, pengine kapata,

 12. Siutafute kila mtu vyake vyake,
 13. Usiuchunguze, kila mtu kivyake vyake,
 14. Usijisumbue, kila mtu kivyake vyake,
 15. Sinitilie, kila mtu kivyake vyake.

 16. Kwako hatorudi, humuoni tena.
 17. Anaye switi. Mtoto stadi,
 18. Mambo ka yangu, Kwako hayapati.
 19. Tuache tuspendi, twapendana sana,
 20. Ni wetu wakati.

 21. Amejaribu tepezi lake kwako, Sasa hana wasi,
 22. Hivi wamtafute kwa sasasi wako, simtie nuksi,
 23. Ameshakumbatwa na kwako hayuko, ni yangu nafasi.

 24. Siutafute kila mtu vyake vyake,
 25. Usimchunguze, kila mtu kivyake vyake,
 26. Usijisumbue, kila mtu kivyake vyake,
 27. Simfuatilie, kila mtu kivyake vyake.

 28. Japo alipenda, Akaoa
 29. Wala kushikika.
 30. Uliyomtenda, wala hakudhani,
 31. Mwisho amechoka.
 32. Leo unatenda, hata ukilaani
 33. Kwako hatofika.
 34. Kwangu karidhika.

 35. Utamaliza madawa, kwako harejei tena,
 36. Amepata maridhawa, mkuna,

 37. Atafute pa kuendea, habari nawe hana,
 38. Wewe kivyako vyako, naye kivyake vyake,
 39. Kila mtu kivyake vyake, kila mtu ki mpango wake,
- Kimalizio,
40. Unajipitisha pitisha kwake,
 41. Hakutaki.
 42. Unajichekesha chekesha kwake,
 43. Hakutaki.
 44. Unajishebedua shebedua kwake,
 45. Hakutaki.
 46. Unajichekesha chekesha kwake,
 47. Hakutaki.
 48. Unajitikisa tikisa kwake,
 49. Hakutaki.
 50. Ukijipodoa,
 51. Hakutaki.
 52. Ukijiremba,
 53. Hakutaki
 54. Ukijichubua,
 55. Hakutaki
 56. Ukienda kwa bafu,
 57. Hakutaki
 58. Ukienda kwa sangoma,
 59. Hakutaki

1. Jue uliacha ufizi ndio meno yakaja,
2. Namuamini mwenyezi, ndiye mtoa haja,
3. Sitakonda pozi, kwa ,
4. Na wenu chochezi, na hizo kwakwaja,
5. Kuharibu hamuwezi, alopangiwa mja,
6. Kazi ya mwenyezi, ni kwa mja.
7. Mabawa nipo nawangoja,
8. Kama ni wapwezi, fungueni m,

9. Heshima yangu imewatia kiburi, mnanipaka matope,
10. Na utu wangu umewatia jeuri, mnaona mdiripe
11. Basi wenzangu huo si ujabari, hayo ni maruperupe,
12. Maneno chungu na kuniwekea nadhiri, mie ili niogope,
13. Nyie si Mungu punguzeni munkari, na yenu mapepe,
14. Ni kosa langu kukaa nanyi vizuri, mi kuwarepa nikurepe

15. Mambo mingi neno na, washikaji hayapendezi,
16. Majina kuchafuliana, kwa sababu ya mapenzi
17. Japo ukweli hamna, mnamuudhi mwenyezi,
18. Mie mtalaamu sana, ila kwa huyu siwezi
19. Kama nina hamu sana, ninaye wangu mpenzi,

20. Wenyewe twapendana, nashona na darizi
21. Mumenikuta mungwana, nakuamini mwenyezi,
22. Hivi hivi mtaniona, kunishusha hamuwezi.

23. Mtaniona hivi hivi, Mtaniona.
24. zenu chamaa, nazotegemea ni nguvu za Rabana.
25. Mja nikiionga.

26. kwangu mtasubiri sana, ya bure ndo majungu.
27. Naogopa ya Sulbhana, si hofu ya mlimwengu.

28. Jabali Mungu anaona, si hofu zenu sina fundo,
29. Hivi hivi mtaniona, si hofu vyenu vishindo,
30. La kusema mimi sina, na moyoni sina fundo,

31. Kaniongoza sulbhana, taratibu wangu mwendo,
32. Ada ya mja hunena, humpa nani kitendo,

33. Anaonasi hofu zenu sina fundo,
34. Hivi hivi mtaniona, si hofu vyenu vishindo,

35. Sitajitia hashuo, kusema yaso na maana,
36. Msimamo ndio huo, Mungu anatosha sana,
37. Mungwana akivuliwa nguo, hasimami huchutama,

38. Mungu anaona, si hofu zenu sina fundo,
39. Hivi hivi mtaniona, si hofu vyenu vishindo,

40. Najibeba, nichukieni mwana zenu.
41. Najibeba, sijali vishindo vyenu.
42. Najibeba, sihofu porojo zenu.

43. Najibeba, mumenipandisha mizuka kaire.
44. Mzuka wangu umepanda kaire.

45. Najibeba nichukieni mwana zenu.
46. Najibeba sijali vishindo vyenu.
47. Najibeba sihofu porojo zenu.
48. Najibeba mumenipandisha mizuka kaire.
49. Mzuka wangu umepanda kaire.

9-JZ-

Jinamizi Mwanaidi Shabaan

Utangulizi;

1. Bora sasa, bora sasa x4
2. Limeniodokea mama x 2
3. Jinamizi hili mama, limeniondokea mama x2

4. Tulokuwa tukishindania, yamekwisha
5. Tulokuwa tukigombania , yamekwisha
6. Ninaye huyu wangu sasa, raha zote kwake Napata
7. Wasiwasi sinao tena, pekee yangu mimi nanyeta

8. Raha kwangu hamna vutavuta, ninadunda nimeukata
9. Mvuto wewe nimekufuta, nimeshinda bila ya vita x2

Kitikio,

10. **Ulipoanza manoki, nilijua utakwenda**
11. **Mungu kanifanya starring, mimi mbabe wa sinema**
12. **Ndipo najimwagamwaga, kwangu wewe jinamizi tua , jinamizi tu x2**

13. **Ulijisha utabana, mbona umeshabenua**
14. **Kwa marefu na mapana, hivi sasa natanua x 2**
15. **Kukata kichwa kobe, kwataka timing wewe,**
16. **Hunayo timing wewe!x2**
17. **Wasuasua wasuasua x2**

18. Umevuna ulichikipanda, usilie
19. Hiyo ndiyo faida ya uvuda , usilie
20. Ukeweza wako we mechi, mie sina namba kifuari
21. Watafuta pia na koti, unaweka mchawi ndani

22. Shoga siri hii sikufichi, huniwezi mi uwanjani
23. Wewe kwako bora ni pochii, kwa hilo mi hatufanani x2

10-FSH**Full Shangwe- Amingo**

1. Full Shangwe, tunashangilia,
2. Full shangwe, tunaliachia
3. Tupendana raha, na masikizano,
4. Kujiachia raha, bila mabishano,

5. Full shangwe leo, ni ya leo.
6. Fumzuka leo, achia leo,
7. Mambwembwe tunawatilia,
8. Na manakshi twajifagilia

9. Sana tu
10. Mwenzenu mi napendwa, mpaka naona raha,
11. Na raha ya kupendwa, penzi siwe na karaha
12. Sio kutendwa, moyo kakosa raha,
13. Mimi nalindwa, nisipatwe na jeraha

14. Boda to boda nakwenda,
15. Kujisoso mora raha,
16. Ama rumba kaniganda,

17. Nampenda sana
18. Labda afe nimzike au nife mimi,
19. Nampenda sana
20. Acha waseme wenyewe watachoka
21. Nampenda sana
22. Acha wachonge hao kimpango wao,
23. Nampenda sana

11-PM

Paka Mapepe- Ashura Majaliwa

1. Paka mapepe huyo
2. Paka mapepe usimwandame, mapepe huyo,
3. Usiache akutume, mapepe huyo.
4. Huyo hamjui mume, mapepe huyo,
5. Mwenye fedha kwake dume, mapepe huyo
6. Akisema msukume, tena asikusakame,
7. Mkomeshe akukome, abakie alalame
8. Habibi mimi niko, siku zote mimi wako,
9. Hanitoi mtu kwako

10. Fanya ufanyavyo fanya umuweke umwekavyo paka,
11. Nilikwisha kukuonya, huyo si wa kuridhika paka
12. Huyo atawachanganya, wana, shangazi na kaka,
13. Tena akisha tapeli na baba atamtaka.

14. Atafanya ya kufanya, mwisho atakasirikaa,
15. Hafai huyo hafai, kwangu mimi ni kurai

16. Paka huyo paka, paka mapepe paka,
17. Umpe kuku na bata, yeye hatotosheka,
18. Umpe japo steki huyo paka,hatakushukuru huyo paka,
19. Atakutoroka huyo paka, akimwona panya huyo paka,

20. Kila umtendeavyo, bado atalalamika paka,
21. mrithi kwa kila njia, mwisho atakutoka paka,

22. Alivyo abiri nia, hapo atakubandika,
23. Mazuri kimfanyia, hisani hatokumbuka.
24. Bure kumkubalia, kufanya anavyotaka,
25. Hafai huyo hafai, kwangu mimi ni kurai

26. Paka huyo paka, paka mapepe paka,
27. Umpe kuku na bata, yeye hatotosheka,
28. Umpe japo steki huyo paka,hatakushukuru huyo paka,
29. Atakutoroka huyo paka, akimwona panya huyo paka,

30. Usitazame gauni, japo ndo mavazi yake,
31. Tofauti we huoni, hana haiba ya kike,
32. Japo yeye yumo kundini, mbovu desturi zake,
33. Muepuke hayawani, faudhila yake mateke.

34. Njoo kwangu mimi, nakudhamini,
35. Sikupeleke puta huyo,
36. Hafai huyo hafai, kwangu mimi nakurai
37. Paka huyo paka, paka mapepe paka,
38. Umpe kuku na bata, yeye hatotosheka,
39. Umpe japo steki huyo paka,hatakushukuru huyo paka,
40. Atakutoroka huyo paka, akimwona panya huyo paka,

41. Huyo paka mapepe huyo,
42. Hata umpende huyo,
43. Hata umlambe huyo,
44. Umchinjie ng'ombe huyo,

45. Akimwona panya, anachacharika,
46. Akimwona panya, ana akirin

12-HM Huna Mambo-Afua Suleiman**Utangulizi;**

1. Utabaki kutamani kwa huyu huonekani,
2. Huna mambo halafani, anayekutaka nani?
3. Kwa vile huna thamani una bei ya dukani
4. Malipo yako ni duni bei ya vichochoroni,

5. Bi shoga utaumbuka utaumbuka kwa yako matamano,
6. Tena utaadhirika utaadhirika kwa kuyataka yasiyo,
7. Umrudie rabuka ukatubu madhambiyu,
8. Mi bure wachechetuka si maisha kwako hayo.
9. Watu wanakuepuka uwache tabia hiyo

10. Utabaki kutamani kwa huyu huonekani,
11. Huna mambo halafani anayekutaka nani?
12. Kwa vile huna thamani una bei ya dukani
13. Malipo yako ni duni bei ya vichochochoni,

14. Kipi unacsemagambahuko wewe uendako,
15. Huwa umeshika nambaakuna zaidi yako.
16. Unajidai kutamba kuwasumbua wenzako,
17. Kumbe wewe ni mshamba hupenda visivyo vyako
18. Umeshakuwa mtumba huna bei nenda zako,

19. Utabaki kutamani kwa huyu huonekani,
20. Huna mambo halafani anayekutaka nani?
21. Kwa vile huna thamani una bei ya dukani
22. Malipo yako ni dunibei ya vichochochoni,

23. Uzee umekukumba hata ukijipodoa,
24. Kutwa wajirembaremba upembe zinakwambia.
25. Mwili unanuka vumba bure unajichupua,
26. Wamtafuta mchumba ni nani atakuoa.
27. Unadansi unarumba nani utomuambia.

28. Utabaki kutamani kwa huyu huonekani,
29. Huna mambo halafani anayekutaka nani?
30. Kwa vile huna thamani una bei ya dukani
31. Malipo yako ni duni bei ya vichochochoni,

32. Sifa na vyako vitendo katu havikulingana,
33. Mwendu wako wavishindohaufai kuulizana
34. Ajabu ataka pendohata hujapendwa mbona,
35. Umetupwa huko kando bibi hutakiwi tena
36. Tuko si wenye midundo tuli tumetulizana

37. Utabaki kutamanikwa huyu huonekani,
38. Huna mambo halafani anayekutaka nani?
39. Kwa vile huna thamani una bei ya dukani
40. Malipo yako ni duni bei ya vichochochoni,
41. **Kimalizio;**
42. Una mambo we, hutakiwi tena we,
 - a. Hujui pendo we, akupende nani we,
 - b. Huna ujuzi we, akutake nani we,
 - c. Huna mpya we, uitoe wapi we.

13-MMUZ

Mlango Wa Mungu U Wazi- Swabah, Swalum

1. Mja hufiki popote, Nikule chako ,
2. Dunia ni yetu sote .
3. Juwa wabaya si wote, Wapo watonisitiri
4. Riziki hutoi wewe,mja usitaka habari

5. Unisusia wewe,
6. Sishituki moyo wangu
7. Nitapata mwengine we,
8. Hatojali shida zangu

9. Hasama mimi na wewe, sio kusudio langu,
10. Ukinibagua wewe, hanitupi mola wangu.
11. Kama wewe ni mbaya, nao wema wako tele

12. Jua mlango wa Mungu uwazi kaufungua,
13. Kama riziki ni yangu, huwezi kuiondoa.
14. Ufanyaje ulimwengu, usiyekuwa na haya,
15. Hujamaliza mizungu, la mola hutopangua

16. Madhali ni hai, sina wasiwasi kwa riziki yangu,
17. Kwa mola I lai, najua sikosi na langu fungu,
18. Taji hunivua, lilishapasi, sijipe uchungu,
19. Choyo hakifai, na chuki binafsi, ewe mlimwengu

20. Ukiufunga wa kwako mlango, jua wa mungu uwazi.

21. Umekaza uzi, kunichonganisha kwa mashoga zangu,
22. Nalijua wazi, linokukondesha, ni bahati yangu
23. Unajipa kazi, hutoiondosha, kudura ya mungu,
24. Hayo huyawezi, wajihangaisha, dawa chema jungu.

25. Sote wa kukadiriwa na mungu, Hatujitoshi kwa kitu
26. Hatowai nika ari kwa matamu na machungu
27. Usijipe ujabari kuvaa joho la mungu
28. Haufai ujeuri we kiumbe mwenzangu,
29. Tuendako ni shubiri mwana ndani letu fungu,
30. Joho la mwenyezi mungu mja likufae wapi?

31. Jua mlango wa Mungu uwazi kaufungua,
32. Kama riziki ni yangu, huwezi kuiondoa.
33. Ufanyaje mlimwengu, usiyekuwa na haya,
34. Hujamaliza mizungu, la mola hutopangua

35. Ya nini wewe,
36. Hukuniumba, umeumbwa,
37. Ume nini wewe,
38. Kiburi chako ni bure,
39. Mlango wa Mungu uko wazi,
40. Riziki Napata mimi,
41. Nina uzukiwa mimi,
42. Mungu amenisitiri

14-Z

Zilipendwa-Khadija Yusuf

1. Nimemtapika, sina hamu tena
2. Sikuambiwa yuko, nimeambiwa wako,
3. Kama umemchukua size yako,

4. Na mimi ni tayari, mwengine ninaye,
5. Wasi wasi sina, oyawe,
6. Niliyajua kitambo, kama huyo baka baka,
7. Sasa kama kwako yupo, wengine anapo, anapokwenda,

8. Hapandi farasi, mzoea ya punda,
9. Noti si karatasi, dereva si konda,

10. Kama huko ndo kupata, chukua ufaidike,
11. Halafu usije juta, ukifika mwisho kwake.
12. Na wala sitawafuata, awe wako uwe wake,
13. Yu pwalo anonifumbata, anofanya niridhike,
14. Msijibanze nakunta kivyangu vyangu kivyake

15. Mwenyewe nawatengeza, shoga sina shida hiyo.
16. Malighafi nimejaza, haitaki toti hiyo.
17. Unaniona natamba, na mpenzi wangu sambamba,
18. Natamba, na hiyo lela sambamba,
19. Bore hali, zilipendwa

20. S'Sijitie bure pepo, asompungaji wake,
21. Hukuambulia hapo, alipokuwa na chake

22. Na kwa watu atokapo, apendeza peke yake
23. Jicho hubakia papo, hutaki nitoke kwake
24. Sasa baki aliwepo, hana chake, hana lake

25. Mwenyewe nawatengeza, shoga sina shida hiyo.
26. Malighafi nimejaza, haitaki tochi hiyo.
27. Unaniona natamba, na mpenzi wangu sambamba,
28. Nikona boksi natamba, na hiyo lela sambamba,
29. Bure hali, zilipendwa

30. Fuataneni niwaone, wala usibabaike
31. Tena tusalimiane, kisa nisivunjike
32. Nimeshapata mwingine, nampenda peke yake
33. Si mwembamba, si mnene,aloshiha kwa mamake.
34. Tunalicheza sebene, shibe yangu shibe yake

35. Mwenyewe nawatengeza, shoga sina shida hiyo.
36. Malighafi nimejaza, haitaki toti hiyo.
37. Unaniona natamba, na mpenzi wangu sambamba,
38. Nikona boksi natamba, na hiyo lela sambamba,
39. Bure hali, zilipendwa
40. Sijanuna, sijakereka,

41. Vitindo vyake, vilinitosha, zilipendwa, kwangu zilipendwa,
42. Long time, nimemfurusha, nichanganyie, nicheki cheki,
43. Nachichitiza na ninatisha, hujatulua, hujapepewa,
44. Libukeni, unachekesha.

45. Jeuri mwenziwe kusudi, Sitaki mwenziwe basi,
46. Sina haja ya shahidi, si mfupi si mzasi.
47. Nishamtoa moyoni,

48. Aliposema mimi wa nini,
49. kuna wanosema watanipata lini.

50. Usione soo, sema naye,
51. Kwangu mimi no, sina haja naye.
52. Zilipendwa sina haja naye

15-UKSU

Umejuaje Kama Si Umbea- Mwanaidi Shaaban

1. Utangulizi;
2. Umejuaje*3
3. Umejuaje nimefanikiwa umejuaje?
4. Umejuaje ukaonafi umejuaje?
5. Umejuaje kama si umbea umejuaje?

6. Umeyatafuta, umeshayapata, sasa walialia
7. Vizurivyakupita, wavikodolea macho,
8. Vinono vyakupita wavikodolea macho
9. Vitamu vyakupita wavikodolea macho
10. Wakufuma tumefuma, fuma,wakukosa umekosa, kosa
11. Swadakta, umepata swadakta,
12. Swadakta, nimefanikiwa swadakta,

13. Umesikika waamba, wewe bado unagomba, lipi likusumbualo jambo?
14. Macho yako kama mamba, wala hujui kufumba, hakikupiti kitu kirembo,
15. Japo mie sijatamba,wala sio wa kujigamba,lakini sifichi langu pambo,
16. Kasirika sasa vimba, bure jua hutaziba, wewe jifunze ujue mambo.
17. Endelea kunichimba, nenda kwa wachawi omba, jua Mungu hapigi kwa fimbo,
18. Adabu yako elewa, nimefanikiwa mie,

19. Kiitikio;
20. Jahaza yako elewa nimefanikiwa mie
21. Nimeongokewa mie,

22. Nimejaliwa mie,
23. Unaona fi,kuniona mie kung'aa,
24. Siachi*4, kuvaa mie siachi.
25. Unaona fi,mie kupanda Rav.4 ,
26. Siachi*4, kupanda Rav4 siachi.
27. Unaona fihii,mie kuenda melody ,
28. Siachi, kuenda melody siachi.
29. Wataka kuliziba jua na ungo,
30. Huwezi kuliziba jua,
31. huwezi kuliziba na ungo,
32. Huwezi kuliziba jua,
33. Huwezi kuliziba.

34. Milango uliyofunga, gonga misumari gonga, fanya ukuta ujenge pia,
35. Weka mtu wa kuchunga, hutaniona kusonga, sasa Mungu kanifungulia,
36. Ulie ukining'ong'a, ati mi wa moja kanga, hali ishanibadilikia,
37. Jahazi kutoka Manga, kwangu limetia nanga, neema sasa nailalia.
38. Hebu domo lako funga, kwangu mimi hutachonga, jua Mungu, ameshanilipia

39. Kiitikio;
- 40. Jaza yako elewa, nimefanikiwa mie,**
- 41. Nimeongokewa mie, nimejaliwa mie.**
- 42. Unaona fi, uliona mie kung'aa,**
- 43. Siachi, kung' aa mie siachi.**
- 44. Unaona fi,mie kupanda Rav4 ,**
- 45. Siachi, kupanda Rav4 siachi.**
- 46. Unaona fi,mie kuenda melody ,**
- 47. Siachi, kuenda melody siachi.**
- 48. Wataka kuliziba jua na umbo,**
- 49. Huwezi kuliba jua, huwezi kuliziba na umbo,**
- 50. Huwezi kuliziba jua, huwezi kuliziba.**

- 51. Kimalizio;**
52. Kalichagua goma, la Kiswahili goma,
53. Chakacha namchezea, habibi namchezea
54. Lele mama namchezea, habibi namchezea
55. Msewe namchezea, habibi namchezea,
56. Hatakibiriani yako, kalichagua bada langu.
57. Sima ya bada hujui kusonga, hujui kusonga sima ya bada.
58. Sima ya bada tamu,
59. ipate mpishi timamu.
60. Ipate papa adhimu,
61. Utie na tui gumu,
62. Pia chachandu ya ndimu
63. Ukilahuishi hamu, huishi hamu kuila.

16-MA

Mnaungulika-Aisha Othman

1. Hatua tulofikia, si vyema kutendeanana,
2. Sisi wa pakata moya, kijicho kuoneana
3. Yangu yakininyokea, wenzangu wivu mwaona,
4. Mumesahau ya kuwa mtoaji sumu hana.

5. Makafara mumetoa, kuzamisha langu jina,
6. Mola hakuwapa njia, hilo likashindikana,
7. Nazidi kubarikiwa, kama mnavyoniona,
8. Mungu akitaka kupa, hakuletei barua,

9. Usijizidi hukupa, bila mwenyewe kujua
10. Wacheni kubabaika, haya ni majaaliwa,
11. Mkono kuenda kinywani, nyie hampendelei,
12. Imewatoka imani, kudura hamtambui

13. Mnataka niwe duni, roho zenu zifurahi,
14. Hilo haliwezekani, maadamu niko hai
15. Kusuda zenu nyoyoni, mimi hazinishitui
16. Mlopangalo pangeni, haliwi katu haliwi,

17. Kukicha mimi na wingi,hadhi hamunishushii
18. Mungu akitaka kupa, hakuletei barua,
19. Usijizidi hukupa, bila mwenyewe kujua
20. Wacheni kubabaika, haya ni majaaliwa,

21. Hebu kazeni moyo, haja msiadhirike,
22. Kwa haya niliyo nayo, imani isiwatoke
23. Tusiendeane mbio, mtu huridhia chake,
24. Alichochacho mwenzio, kione kama matope,

25. Sitara kwangu ni ngao,acheni nisitirike,
26. Bahati mezaliwa nayo, bure msiungulike
27. Msijiumize roho, sitahama la mukeke

28. Mungu akitaka kupa, hakuletei barua,
29. Usijizidi hukupa, bila mwenyewe kujua
30. Wacheni kubabaika, haya ni majaaliwa,

31. **Mnavyoniona,**
32. **Mnaungulika,**
33. **Shida sina tena,**
34. **Mnaungulika,**
35. **Mambo yangu yakifana,**
36. **Mnaungulika,**
37. **Choyo mnaona,**
38. **Mnaungulika**

17-NJ

Nalijua Jiji-Khadija Kopa

Utangulizi,

1. Eeeh! Anani dege lisoliwa anajikoti kama ye si wa mjini
2. Eti utalijua jiji?
3. Unauliza jibu huna habari, kawaulize makonda
4. Kuna kituo mwananyamala, tutapigana vikumbo humohumo
5. Unalijua hilo? Wanakucheka watu
6. Halua mji umeuvamia wala si wakati wako ewe

7. Halua haflani watoto unawania wala si wa rika lako wewe
8. Usijitie makuu bibi na mji huu si wako
9. Nalijua jiji bibi utakoma kwa vituko
10. Pole utapoa pole ndo dunia
11. Wafumbiwa wewe ulopatwa nalo mvunguni mtu na mkwewe
12. Haya mambo*2
13. Jamani mambo eti anatamba yeye na mji huu si wake.

14. Uwahi nifanyizia umezaliwa mjini
15. Wewe unauliziwa kwani umekuja lini?
16. Kipi unacho vutio shoga ukatake nani?
17. Mabwana ulodandia, siazi yangu katuni
18. Bwana uolgombaria, siazi yangu katuni
19. Koma kunifuatilia nina mume wangu ndani
20. Nadhani unamjua, Esamboi mjini
21. Wengi wamgombaria, amewapiga na cheini
22. Nalijua jiji Bi Shoti nimezaliwa Usheroni
23. Tena nalijua jiji Bi Shoti Kariako nimekulia
24. Nalijua jiji Bi Shoti Gereza wananielewa

25. Kiitikio;
26. Mtoto wa boni town tena jiji naelewa
27. Nitapita uwanjani na wala sitakukimbia
28. In that case my dear, nishakupindua
29. Nalijua jiji tutapigana piku moja kwa kimaksudi

30. Linokuuma Bi. Shoti, hupata bwana wa maana

31. Nahilo umbo la jiti, utahangaika sana
32. Hupendezi kwa taiti, hata nguo vao mapana
33. Nani atokudhibiti, shosti stara huana?
34. Unaniona*2 niko fiti?
35. Najuli, najulikana kimwana
36. Mtoto up to date natinga kama zamani
37. Mavazi yanifiti, nikipita natizamwa
38. Nalijua jiji Bi. Shoti, ni gari kubwa utaumia
39. Ena nalijua jiji Bi. Shoti, nitakuwacha kwenye mataa
40. Nalijua jiji Bi. Shoti, nchi nzote nishaogelea

41. Nakuona umechoka bao mezea tu
42. Huku bado sijachoka bado mezea tu
43. Naona umeshuka posta bao mezea tu
44. Utaondoka chanika bado mezea tu
45. Oooh ajijua mtu hapa
46. Utamjulisha nimezaliwa mjini
47. Na kitovu change kimezikwa Twaatugawe

48. Mji una masharti, mpaka ufanikiwe
49. Siyo kuvaa mashati, ukajiona ni wewe
50. Mwanamke abiuti, manukato uyajue
51. Na hasa uwe na hati, kwawanaume wenyewe
52. Mume wangu humpati, hangaika upagawe
53. Mwenyewe ni mahabubu, si mchafu kama wewe
54. Mtoto wa Asimilati jijini natamba mie
55. Nalijua jiji bishoti ukirusha ngumi nitakurushia
56. Tena nalijua jiji ukikta nitafunua
57. Tena nalijua jiji bishoti nchi zote nishaongelea

58. Kiitikio cha katikati;
59. Nalijua jiji pande zote
60. Nala vinono nimetemete
61. Huwahi nifanyia lolote
62. Ooh yes my dear nishakupindua

18-ZZ

Zoa Zoa-Mwanaidi Shaaban

Utangulizi;

1. Humpati huyo*2
2. Utasota sana humpati huyo we

3. Hunitishi umedoda, si wewe wa kunipiku
4. Bei yako wewe soda, chipsi na nusu kuku
5. Kama kuna la ziada, basi umepewa buku
6. Kwa lipi utanishinda huna bao zoa zoa
7. Kupanga pangua bandika bandua
8. Nyakua nyakua si kwa wangu mimi

9. *Kiitikio;*
10. Kujipendekeza wajihangaisha
11. Itajikomboa dada umechina
12. Dada Umechina ooh dada umechina
13. Tuliza boli kiwanja ni kidogo
14. Tuliza boli kiwanja si madogo
15. Tuliza boli kiwanja mimi si kidogo
16. Tuliza boli hutingishi gogo

17. Uninyang'anyi ukunda
18. Nimetulia waranda
19. Unashuka mi napanda
20. Uko moja niko kenda

21. Jitangaze vikaoni, jitangaze harusini
22. Mwishowe kichochoroni, kwa wangu huoni ndani

23. Jitangaze gazetini, jitangaze redioni
24. Mwishowe kichochoroni, kwa wangu huoni ndani
25. Mke mwanamke gani, umezoea kombaini?
26. Mi na we hatushindani, huna bao zoa zoa.

27. Najua kiruka njia, pa kulala wapangia
28. Waume wawania, yeyote kwako sawia
29. Huchagui wafagilia, siti konsen nyuma pia
30. Wivu we utanitia, huna bao zoa zoa.

31. *Kimalizio;*
32. Washindana na budege wazoazoa wazoazoa
33. Washindana na kikapu wazoazoa wazoazoa
34. Waheshimiwa wataka wewe
35. Wakurugenzi wataka wewe
36. Muuzaji wataka wewe
37. Muuza duka wataka wewe
38. Muuza karanga wataka wewe
39. Kwako bora shilingi, bora shilingi
40. Shilingi yang'ara yaua shilingi nyanga'ara.

19-VW

Viumbe Wazito- Mwanahawa Ally

Utangulizi;

1. Vile nilivyo wathamini, nikawawekeni usoni
2. Kumbe wakosefu wa imani, hata hamna shukurani
3. Viumbe msiochukulika viumbe wazito

4. Mlikusudia nini enyi wenzangu, mwenzenu kunihimiki
5. Mwanitia ubayani si hulka yangu, mjue sifedheheki
6. Hamdhamini hisani wala nguvu zangu, viumbe hamchukuliki
7. Nimejenga imani dhabiti moyo wangu katu sitotaharuki
8. Ninaamini hakika iko siku itafika tope mnazonipaka zote zitatakasika
9. Wala donge sitoweka maumini nina nia njema kwenu nyie.

10. Kiitikio;
11. Sijui niwaweke fungu gani viumbe muhesabike
12. La faraja dhiki jema kwenu huwa baya
13. Wenzangu hamchukuliki ndivyo mlivyo zoea

14. Unanifuja kwa watu uso na fadhila eti nina roho mbaya
15. Wanipigia upatu kila mahali mbaya mimi mbaya
16. Navumilia sikitu najua yenu nia wenzangu nimezoea
17. Muhukumu Mola wetu naamini inshala huko tutayatambua
18. Wema wangu haozi milele utabakia
19. Nifanyavyo roho radhi kinyongo sitowekea
20. Fadhila mfadhili mbuzi binadamu ana maudhui kweli huyoooo

21. Sivui ubinadamu kwa mliyontendea
22. Ingawaje ni vigumu kwa mja kuvumilia
23. Sitojenga uhasimu moyo umetulia
24. Kitu hicho kwangu sumu wala sitomfanyia
25. Nitawatendea wema mimi ninajali utu
26. Wala sitorudi nyuma siwezi hilo kutu
27. Nyie palilieni chuki siku mtajuta.

28. *Kimalizio;*
29. Wema nimefanya hamna shukurani, palipo bakia nashukuru Mungu
30. Nilidhani wenzangu kumbe maadui zangu
31. Sasa nimerudi kwangu wanadamu walimwengu
32. Tenda wema wende zako usingoje shukurani
33. Sipotezi muda wangu pikenii yenu majungu
34. Wala sioni uchungu nimeswafi moyo wangu
35. We nenda nisalimie mama*2

20-UJ**Utalijua Jiji-Afua Suleiman**

Utangulizi;

1. **Kazi yako ufisadi Jeuri ngebe na nongwa**
 2. **Baraka ya ukaidi Ukali kama embe ngwangwa**
 3. **Vituko vya makusudi Si bure we umerogwa**
 4. **Badala ya soda baridi Ama juice ya chungwa**
 5. **Ushamba umekuzidi Andazi wanywia togwa**
 6. **Mwenzangu huna ujuzi Mpenzi umemuudhi**
 7. **Kaja kwangu nimempokea.**
-
- | | |
|-------------------------|---------------------|
| 8. Pokea chako kibomu | Shoga nakutumia |
| 9. Hata ukini laumu | Wako nishamchukua |
| 10. Penzi ulimdhulumu | Visa ukamfanyia |
| 11. Chachandu vitamtamu | Bwana hukumpatia |
| 12. Bwana kapata wazimu | Kashindwa kuvumilia |
-
- | | |
|------------------------|--------------------|
| 13. Kwangu akatia timu | Tiba nikampatia |
| 14. Nikampa vitu adimu | Kwako hajajionea |
| 15. Amri akasalimu | Magoti kunipigia |
| 16. Huku akijilaumu | Kwako kapotea njia |
-
- | | |
|---------------------------|------------------------|
| 17. Kapenda yangu nidhamu | Na utulivu nyumbani |
| 18. Pamoja na ukarimu | Kwa ndugu na majirani |
| 19. Ucheshi na tabasamu | Kanijalia manani |
| 20. Nimepewa lugha tamu | Nyoka hutoka pangoni |
| 21. Sifa hizi ni muhimu | Na mengi mengine ndani |
| 22. Wewe mkaanga sumu | Kwako hazipatikani |
| 23. Na mapishi yako bomu | Kitimutimu jikoni |
| 24. Wali wautia ndimu | Hayo ni mapishi gani |
| 25. Bwana imemwisha hamu | Katimua nyumbani |
-
- | | |
|--|--|
| 26. Unaningoja njiani Madhila kunifanyia | |
| 27. Usitake ushindani Hunishindi nakwambia | |
| 28. Mimi naletewa ndani Wewe watanga na njia | |
| 29. Magomeni BuguruniNdala za kukatikia | |
| 30. Wasela wa vijiwaniNafuu wajipatia | |
| 31. Uroda kwa foleni Kwako wajipendelea | |
| 32. Wewe gumzo mjini Watu wanahadithia | |
| 33. Umeachika ndoa niniKwa yako mbaya tabia | |
| 34. Unaogea jikoni Bafuni unapikia | |
-
- | | |
|-------------------------|----------------------|
| 35. Kwako kaachia ngazi | Kwangu kaweka makazi |
| 36. Sasa akaa mbalizi | Kachoka yako maudhi |
| 37. Utamaliza mizizi | Waganga na waganguzi |
| 38. Talasimu na hirizi | Ongeza na vipodozi |
| 39. Kwake hupati nafasi | Mimi ndio yake pumzi |
-
40. **Sasa ndo utalijua jiji mwenzangu**
 41. **Chajio utakunywa uji mwenzangu**
 42. **Na juice utakunywa maji mwenzangu**
 43. **Huyu kwako harudi tena mwenzangu**
 44. **Najinafasi najinafasi**
 45. **Utajiju wewe utajiju**
 46. Kwako nishamchukua Kwako harudi tena we mwenzangu
 47. **ohh utalia mwenzangu jiji utalijua**
 48. Katamka waziwazi Kuwa hakutaki tena we mwenzangu
 49. **ohh utalia mwenzangu jiji utalijua**
 50. Bwana kanipa nafasi Nimuonyeshe ujuzi we mwenzangu
 51. **ohh utalia mwenzangu jiji utalijua**
 52. Nami sifanyi ajizi Mpenzi namuenzi we mwenzangu
 53. **ohh utalia mwenzangu jiji utalijua**
 54. Nampikia maandazi Na chai ya tangawizi we mwenzangu
 55. **ohh utalia mwenzangu jiji utalijua**
 56. Wali wa nazi kwa ndizi Mavitus kama kazi mwenzangu we mwenzangu
 57. **ohh utalia mwenzangu jiuu utalijua**
 58. Mwisho natoa dozi Impayo usingizi we mwenzangu

59. **ohh utalia mwenzangu jiji utalijua**
 60. Mwenzangu huna ujuzi Rudi tena kajifunze we mwenzangu
 61. **ohh utalia mwenzangu jiji utalijua**
 62. Bibi acha upuuzi Kuishi na mume kazi we mwenzangu
 63. **ohh utalia mwenzangu jiji utalijua**
 64. Mume ataka malezi Sio mambo ya kihuni we mwenzangu
 65. **ohh utalia mwenzangu jiji utalijua**
 66. Ngebe na jeuri zako Leo zimekuishia we mwenzangu
 67. **ohh utalia mwenzangu jiji utalijua**
 68. ohh utalia mwenzangu jiji utalijua wee

21-WGO

Wagombanao-Mzee Yusuf & Khadija Yusuph

Utangulizi;

7. **La mgambo limeshalia** **Kwenu wapiga vuvuzela,**
 8. **Mungu katusaidia** **Zimekwisha zenu hila.**
 9. **Wabaya tumewagundua** **Zimeni zenu vuvuzela,**
 10. **Hizo ni za kombe la dunia** **Na mambo ya futibola.**
 11. **Sisi tumeshaamua** **Hakuna tena kunsila,**
 12. **Tena tunaomba dua tujalie Mola.**

13. **Khadija:** Wengine wanagombana sababu maendeleo,
 i. Na pale wikipatana wanafanya mambo yao.*2

14. **Mzee:** Nashangaa wenye laana na mavuvuzela yao,
 a. Na maneno mengi sana metoka midomoni mwao.*2

15. **Khadija:** Wamegombana wazazi mabibi na babu zetu,
 i. Kwa viza vya kipuuzi eti huyu mwari wetu.*2

16. **Mzee:** Wametujengea zizi kaeni nyie ng'ombe watu,
 a. Tumechoka na upuzi na kuendekeza ya watu.*2

17. **Mzee:** Nyie ndio wapika sumu, Mumezikaanga sanasasa mnaona haya.

18. **Khadija:** Na hao ndio wakaanga sumu, Sisi maelewano hatuna huku moto wachochea.*2

19. **Mzee:** Mumeifanya haramu,kubwa mumepata laanaMungu atahukumia.

20. **Khadija:** Mie tena sina hamu nimeambiwa mengi sanaMpaka kukuchukia,*2

21. **Mzee:** Basi Mungu tumshukuru, mbaya tumemjua,

22. **Khadija:** Inshallah tupe nuru, mbele kutuangazia.*2

23. **Kiitikio:** Poleni wote wenye roho zoefu wa majungu,*2

24. **Mzee:** Wagombanao,

25. **Kiitikio:** Ndio wapatanao,

26. **Khadija:** Walisema,

27. **Kiitikio:** Walimwengu.*2

a. Inshallah*2 Salama, Sote twaomba salama.

b. Kwenu wote wenye chawa, msotuumbea salama.

28. **Khadija(mazungumzo):**Haya sasa, Mohammed Mauji, wapandishe milima watoto hawa wadogo hawa wamezoea kubebwa. Chidi boy, washa chombo hicho.Hakina msaada kwenye maji,Musa besi, mngurumishe samba huyo wasikie. Habari ndio hiyo.

29. **Mzee:**Kelele,*2

30. **Kiitikio:** Acheni kupiga kelele.
31. **Mzee:** Mayowe *2
32. **Kiitikio:** Njoooni muone wenyewe.*2
33. **Mzee:** Nyamazisha. Faza mauji, charaza charaza baba.(Mzungumzo)
a. Hawana*2 la kusema hawana.
34. **Kiitikio:** Hawana*2 la kusema hawana.
35. **Khadija:** Sisi bado,
36. **Kiitikio:** Tunasonga mbele, wanaona gere.*6
37. **Mzee:** Hawaniwezi, ndo maana wananisema,
a. Wananchukia ndio maana wanaiteta sana.*2
b. Msinichafue.
38. **Kiitikio:** Sitaki,
39. **Mzee:** Mtanitia doa
40. **Kiitikio:** Sitaki,*3
41. **Mzee:** Mtanitia doa
42. **Mzee:** Hawana*2 la kusema hawana.
43. **Kiitikio:** Hawana*2 la kusema hawana.*
44. **Mzee:** Mwisho wa ubaya,
45. **Kiitikio:** Aibu,
46. **Mzee:** Ukiona manyoya usiulize, nyamaza kimya. Watu

22-TKT

Tuacheni kama Tulivyo-Mohamad Ally

Utangulizi;

2. Najua mnyapita yangu hakika, ngoma isimame safarini,
3. Safari hii yenu ya uhakika, safari yetu I mapenzini.
4. Najua Mungu hatoyataka, wenyewe yatawarudieni.
5. Ubaya mnaotaka, hutopati asilani.
6. Hamkatazwi umbea, hua mnasema kweli.
7. Japo vitabu vitabu vimetwambia, ni mbaya kweli kweli.
8. Hilo mlokusudia, penzi letu kulikatili,
9. Hapo sitawaachia, kuupitisha ufedhuli.
10. Na mlivyodhamiria, kututenganisha wawili,
11. Penzi kututibulia, ndo ushindwe kula asali.
12. Kwa hapa mtazimia kama tulivyo tuacheni,
13. Wenye meno wametuliananyi vibogoyo tuacheni,*2
14. **Kiitikio:** Sumu mpe paka mwenye roho ngumu,
a. Usimpe mbuzi utamdhulumu,*2
b. Mi sitoachana naye,
c. Labda mje mtupangie,*2
15. Mwajuana mpa nini au yeye anachonipa,
16. Kinonikata mainina mwili nikanenepa,*2
17. Visa visavi tuacheni msifanye mambo kwa pupa,
18. Huruma nawaoneni hivyo mnvayo tapatapa.
19. Pole, nawapa poleni nyie mafisadi papa,
20. Hata mpange foleni hamuambulii kitu hapa.*2
21. Kilo baki karogeni, maana mshatoka kapa,
22. Mkashinda hiri geni, sisi tunapata sapa.*2
23. Sumu mpe paka mwenye roho ngumu,
24. Usimpe mbuzi utamdhulumu,*2 Mimi sitoachana naye,
25. Labda mje mtupangie,*2

26. Kiitikio;

27. Sisi tumejizatiti, hamtuumizi kichwa,
 28. Kwa lolote tuko fiti, mtakesha kutwa kucha.
29. Mimi ninaye ni wangu, na mimi ni wake,
 30. Acheni yenu majungu, na vineno ya uhehe*2
 31. Fanyeni kafara za vyungu, mtajuta mwisho wake,
32. Kiitikio;
 33. Sisi tumejizatiti hamtuumizi kichwa,
 34. Kwa lolote tuko fiti mtakesha kutwa kucha.

35. *Asante sana mfalme baba, tajiri wa upeo, mpendwa na wengi. Dr love. Haya mfalme, vijana wana hamu sana na wewe. Usiku imeshaingia. Wavalishe nevi sasa wakalale. Najiskia nimeota nikuwa nimelala. Hay ni Juma wenda ulaya mtoto wa Mwanza, sharubaru wa jahazi, ni mwendo wa defender sasa. Kamata mwizi men.*

36. Kimalizio;

37. Majungu yenu ya bure, wenzangu Mumedoda.
 38. Fitina zenu za bure, wenzangu Mumedoda.
 39. Majungu yenu ni bure Mumedoda.
 40. Kanyaga*4 Koboa
41. Kwetu ndio kwaza mkoko Naalika maua,
 42. Nye msitutie joto Mtasumbua.*2
 43. Kanyaga*4 Koboa*2
44. Haya majungu yenu Tunawatesa.*2
 45. Na fitina zenu Tunawatesa.*2
 46. Haya maneno yenu Tunawatesa.*2*2
 47. Kanyaga*4 Koboa*2
48. Majungu yenu ya bure, wenzangu Mumekonda.
 49. Fitina zenu za bure, wenzangu Mumekonda.
 50. Majungu yenu ni bure Mumekonda.
 51. Kanyaga*4 Koboa
52. Kwetu ndio kwaza mkoko Naalika maua,
 53. Nye msitutie joto Mtasumbua.*2
 54. Kanyaga*4 Koboa*2
55. Haya majungu yenu Tunawatesa.
 56. Na fitina zenu unawatesa
 57. Haya maneno yenu Tunawatesa.
 58. Kanyaga*4 Koboa*2
59. Asimoliwa na mwezi usigombane na mkwezi.

23-MH**Mkamilifu hakuna-Fatma kassim**

Utangulizi;

1. Kila mja na kasoro zake, Alopangilia*2 yupo.
 2. Kila jambo kina kikomo chake, Liso na mwisho, *2 halipo.
 3. Kila hisi kaumbiwa lake, Wa kukadaa hayuko.
 4. Na anaye sifiwa mzuri, pia ana kasoro zake.
 5. Na anyeambiwa mshari, kumbe njema roho yake.
6. Hakuna alotimia, kuanzia utosini,
 7. Mpaka mwisho wa vidole, au aliyetimia,
 8. Mwenye uzuri wa shani, hapati hata upele.*2
9. Sinichukulie poa, kwa kejeli mdomoni,
 10. Kunipigia kelele, huwezi kunidomoa,
 11. Kukosea mitihani, kwa mja yeyote Yule,*2

12. Mmoja ametimia, si mwingine ramani,
13. Hakuna asiyekosea, labda malaika samawini.*2

14. Hakuna mkamilifu binadamu, sote tuna mapungufu.
15. Alotimia raufuKwa lolote lake lile.
16. Mja acha majisifu aso hili ana lile.*2

17. Ubinadamu wa mtu hutimia kwa vitendo,
18. Si mdomo na maneno hebu angalia utu,
19. Tabia na wake mwendo punguza kiromoromo.*2

20. Usimkashifu mtu kwa kukosa moja tendo,
21. Unauchonga mdomo au ni roho ya kutu,
22. Limekuingia fundo kwangu yaliyomo yamo.*2

23. Wewe kubagua watu, hujui yao matendo,
24. Ila mimi si sumutu, ya bure vyako vishindo.*2

25. Hakuna*2 mkamilifu binadamu sote tuna mapungufu.
26. Alotimia raufu kwa lolote lake lile.
27. Mja acha majisifu aso hili, ana lile.*2
28. Kinachokuumanimeshakijua,
29. Ndo maana umesema sana, nilipokosea,*2
30. Yanakutoka maneno, kwa moja nilokosea,
31. Mema yangu mia tano, unayafukia.*2
32. **Kimalizio;**
33. Si walimwengu, makosa tumeumbiwa,
34. Alo kamili ni Mungu, acha kujiashua,*2

24-NM

Nilijua Mtasema-Khadija Yusuf

1. Nilijua mtasema*2,
2. Kama maneno yangelikuwa njaa, yangalitesa tumbo langu.
3. Na kama yangelikuwa tindi kali, yangebagua ngozi yangu.
4. Na kama yangelikuwa sumu kali,yangeutoa uhai wangu.

5. Lakini hayana virusi hayanibabaishi.*2
6. Nilijua mtasema, semeni.*2
7. Siwakatazi kusema, midomo kawapa mwenyezi.
8. Semeni yote mtosema, hamnitii maradhi.*2
9. Nimerudi kwa mwadhama,profesa wa mapenzi,
10. Kwenu nimekwisha hama, mumeshindwa kunienzi.*2

11. Huku ninalishwa nyama ya mishakaki ya mbuzi,
12. Mnachojua ni lawama, si utengaji wa kazi.*2
13. Siyajali mnosema, ngao yangu ni mwenyezi.*2

14. Binadamu ng'amba, huishi kwapa,
15. Nilijua mtasema.*2 Semeni.
16. Hamshushi hadhi yanguSemeni.
17. Simwachi mpenzi wanguSemeni.
18. Buheri sasa niko kwangu,*2

19. Nilijua mtasema, semeni.*2
20. Sijali mavuvuzela, mnoyapuliza kwangu,
21. Sasa mambo wera wera, nakamua laifu yangu,*2
22. Mkinisema kila mara, mie ndio uzima wangu,
23. Bure zenu biashara, ya majungu dhidi yangu, *2
24. Semeni sina hasara, atanilipia Mungu,
25. Najua kinowakera, kurudi kwa hani wangu*2

26. Sijasaka haira, mi napata kula yangu
27. Binadamu ng'amba, huishi kwapa,
28. Nilijua mtasema.*2 Semeni.
29. Hamshushi hadhi yanguSemeni.
30. Simwachi mpenzi wanguSemeni.

31. Buheri sasa niko kwangu,*2
32. Mdomo nyumba ya maneno, nilijua mtasema,*2
33. Longo longo la waswazi, hazinipi mthani,
34. Hazininyimi usingizi wa kulala na mwandani,
35. Nimerudi kwa mpenzi, sasa maneno ya nini.

36. Mdomo nyumba ya maneno, nilijua mtasema,*2
37. *Haloo my dear braza,pandisha tanga hilo. Upepo ndio huo, si mbisho. Ni ya homo eh. Taanga moja tu.J4, vuta joshi hilo. Musa bezi, vuta jelali. Kepten Chidi boy,kaza ademani hiyo, usiachie. Kama ulikuwa hujui, hili ndilo jahazi bwana we. Mashine ikitimika inasafiri kwa tanga.Halilali njiani na safari huendelea.Sikia Chiriku original, ukisikia mwingine, dupliketi huyo.*

38. Tunawarusha roho*2
39. Wanovimba wapasuke, wapasuke.
40. Tunawarusha roho
41. Wanochomwa nawachomwe, nawachomwe.
42. Tunawarusha roho
43. Wanoumwa nawaumwe, nawaumwe.
44. Tunawarusha roho
45. Tunawapita uwanjani na mpenzi,
46. Tunawarusha roho*2
47. *Siku zote ndimu changa inakuwa haina maji,La bamia likikomaa linazidi kushuka thamani.No resach, no right speech. Ukiona nanga inatoswa kwenye maji,ujue jahazi limefika hilo,*

48. Tunawarusha roho*2
49. Wanovimba wapasuke, wapasuke.
50. Tunawarusha roho
51. Wanochomwa nawachomwe, nawachomwe.
52. Tunawarusha roho
53. Wanoumwa nawaumwe, nawaumwe.
54. Tunawarusha roho
55. Tunawapita uwanjani na mpenzi,
56. Tunawarusha roho*2

25-WWW

Wasi Wasi Wako-Mzee Yusuf

1. Wasi wasi ndio wa akili, waswahili wamesema,
2. Ila mwamini Jalali, ndo kila kitu kwa umma,
3. Wewe ukisikia hili, moyo unapiga ngoma,*2
4. Huipati afadhali, mwili wakuchomachoma,*2
5. Mie ndo wako wa kweli, nilotibu yako homa*2

6. Hebu lala uamke,nikiwa mbali na we,
7. Tena kula kikushuke, ukipenda jishebedue,*2
8. Wasikutishe wahepe, akili wasikutimue,
9. Wanoleta sekeseke, waambie ho,
10. bibi unitue.*2

11. Utapewa maneno na wapekepeke,ukose raha usichangamke,
12. Wasiwasi wako pembeni uweke,mimi ndo wako ntakufanya ucheke,*2
13. Subira umesubiri sana, umesubiri sana, nini sijakuridhisha,
14. Kupenda nakupenda sana, nakupenda sana, kipi chakupa presha?*2
15. Kupenda nakupenda sana, nakupenda sana/I love you so much, kipi chakupa presha?*2

16. Ama meseji nyingi sana,ndizoo zinazokutisha,
17. Misti koli mingi sana,roho zakupaparisha,*2
18. Kama ni hamu ushanimaliza, huo utamu mpaka nasaza,
19. Kama ni hamu ushanimaliza, huo utamu mpaka nasaza, nakula kesho
20. Kwengine sumu itaniumiza,*2

21. Sijitie presha, hayuko zaidi yako,
22. We ndo unayeniponya, inatosha huba zako*3
23. Tuangalie maisha, achana na choko choko,
24. Zama zao zimekwisha, alikula raha zako,*2

25. *(Mgeni Kisoda, simamisha. Simamisha wanapiga kelele. Piga kinanda Geni Kisoda. Kwenda kwenda, acha kelele. Kimya kimya, punguza kelele. Hata kama ni mswahili, Unatakiwa usome Kiswahili ili upate kujua kanuni na na tashbiha, na mambo mambo. Hii sio hadithi rejea. Kisoda. Musa Mibango. Babake.)*
26. Tumbo iweke mabano, wa mjini si wa kuja,
 27. Elewa ni vigumu mno, vinyume kukaa pamoja,
 28. Kama stirio na mono, kuelewana ni vioja,
 29. Kula andazi aso meno, mate tu yatamvuja,
30. Nasema mate yatamvuja, mate yatamvuja,
 31. mate yatamvuja, mate yatamvuja,
 32. Nasema mate yatamvuja, mate yatamvuja,
 33. Kibogoyo hana meno, mate yatamvuja,
34. *(Musa Mibango yah. Geni Lisoda.)*
35. Usiogope lolote, usiogope yeyote*3
 36. Ogopa ya Mungu tu, la mtu never.
 37. *(Aminia mkubwa. Gedi, Kisoda.)*
 38. Usiogope lolote, usiogope yeyote*3
 39. Ogopa ya Mungu tu,
 40. *(Gedi, Kisoda mpasie fatha Mauji. Awaambie wote walionuna, wananunia mapenzi yetu. Eti kwanini hatujaachana.)*
41. Wabambe wamenuna nasema, wabambe wamenuna.
 42. Wanafiki wamenuna nasema, wanafiki wamenuna.
 43. Mafisadi wamenuna nasema, mafisadi wamenuna.
 44. Na wambea wamenuna nasema, wambea wamenuna.
 45. Sisi hatutaachana na wanune, wambea wamenuna.
 46. *(Saluti five. Screen masters.)*
47. Msinione nakonda, mwenzenu ninapenda sana,*2
 48. Yamenogea, yamenogea.
 49. Mapenzi yake, yamenogea.*2
 50. Yamenogea, yamenogea.
51. Kanigusa hapa, kanigusa pale mie, mwenzenu nimepagawa,
 52. Akinifanya hivi, akinifanya vile, mwenzenu nimepagawa.*2
 53. Akisimama hivi, Akisimama vile, mwenzenu nimepagawa.*2
 54. Akinishika hivi, Akinishika vile, mwenzenu nimepagawa.*2
 55. ***(Huyo ndiyo Faza Mauji katupeleka kusini tu cheze sindimba)***
 56. ***Che cheche che cheche cheza sindimba***
 57. ***Anachezesh mabega***
 58. ***Anachezesh mabega,***
 59. ***Sema zungusha zungusha***
 60. ***Anazungusha zungusha***
 61. ***Che cheche che cheche cheza sindimba***
 62. ***Aliyekula dona, na nguru wa kuchoma***
 63. ***Ado ado ado ado ado salali***
 64. ***Chinjiku chichilana***
 65. ***Nauliza nani kama mama, hakuna***
 66. ***Nauliza tena nani kama mama, hakuna***
 67. ***Okey, wamesikia hilo.***
68. Nipe*2 Nikikupa utalewa.
 69. We nipe, mimi nipe. Nikikupa utanogewa.*2
 70. Kama gari, gari lako wewe, ntaapanda daladala.
 71. Kama pesa pesa zako wewe, hata chini ntalala.*2
72. Cheza, sema tu cheze. Haya nacheza mie. Sote tu cheze.
 73. *(Sema tulki wangu, lolote nitafanya kwa ajili yako. Lolote? Hilo tu?)*
74. Unajua nakupenda*3, lolote lile ntatenda kwa ajili yako ntatenda,*3
 75. Niguse/nishike/tabasamu/hebu cheka kidogo nione raha mwenzio, mpaka nipagawe,*4
 76. Kumbe wanaona gere*3
 77. Kutwa wananuna bure* 2 na kuvimba bure,*2

78. Hii ni ya masantula, gomo la pwita.Ndo mwanagu mwanajuma,namtafuta.
79. Ye akaninunulie, kitu mafuta.Kwa bahati nzuri akayakuta.
80. Kwa bahati mbaya akayapita.*2
81. Okota maganda, peleka Uganda. Yamepanda bei, sukuma.

26-MB

Mambo bado-Fatma Yusuph

Utangulizi;

1. Nimewastahimilia sana, naona mtanipanda kichwani.*2
2. Maneno hayeshi,hata nikiwapuuza.
3. Riziki ninayopata,nyoyo yawanyong'onyeza.
4. Eleweni wenzangu, riziki haiwaniwi.
5. Kama yako itafika, mwenyewe haujijui.

6. Nikipata mie, nyie munanuna,
7. Nia yangu safi mie, kwenu mbaya sina.
8. Basi mambo bado,Wasiwasi sina,
9. Ndo kwanza niko gado.*2

10. Nimewagundua, bado mnacho kinyongo,
11. Si bure, msingerusha madongo.*2
12. Kweli sasa nimeamini,penye riziki hapakosi fitina,
13. Leo nilowadhamini, wananidhihaki kwa maneno yaso maana,*2

14. Kama riziki anatoa binadamu, mie ningetoka kapa,
15. Mngenidhalilisha na kunidhulumu hata tonge msingenipa.*2
16. Lakiniwapi riziki ni kwa hesabu, mola anazisusha,
17. Naye hanitupi,yote ndo majaribu mie ameshanivushia,
18. Watapi tapi ustadha atawaadhibu, mie huninenepeha,*2

19. Mwakumbuke yaliyopita, mawazo yamewasonga,
20. Si bure msingekuwa na nongwa.*2
21. Nawaeleza mambo pleni, mie habari sina, hata mkiniteta.
22. Inshallah sitoanguka chini na bure zenu fitina,kwa raha nakula bata,*2

23. Wanaonichukia hasara kwao,wanjikata maini,
24. Wanaoninunia imekula kwao,mazali hamnipi pumzi sini*2
25. Mla mla leo, namfaidi mie,nyie yenu yamekwisha,
26. Punguzeni choyo, bata boy ninaye, nakula naye maisha.
27. Mkubali matokeo, siachani naye,mnajipandisha presha.*2

28. Mwenzenu kinyongo sina, kiroho safi mjue,
29. Hata mkinitukana, mnajitusi wenyewe,
30. Kisicho riziki hakiliki,silazimisha,
31. Na pia mpewa hapoponyeki, basi na aeshe,

32. Nuneo na mhamaki, mambo bado*2
33. Riziki hutoa Mungu, choyo mtakufa nacho,
34. Na hamuipati yangu,bure kodoeni macho.

35. Msipaparike kila mtu akajua,jikazeni kike japo kuwa mwaumia*2

36. Mume yatupa mkumbuke bahati mliichezea.
37. Riziki hutoa Mungu, choyo mtakufa nacho,
38. Na hamuipati yangu,bure kodoeni macho.

27-HS

Hatuna Habari

1. Stori za majirani tuzifunge sasa hani,
2. Wanasema chini chini kujua wetu u gani,
3. Acha tutoke gizani,Mambo yawe hadharani.
4. Wa kuandika andikeni,Wa kuongea ongeeni,*2
5. Semeni semeni, maredio katangazeni,
6. Magazeti andikeni, habari zisambazeni,*2

7. Tujitokeze mpenzi mbele za watu watujue,
8. Kwa swala zote na pozi, manafiki tuwasumbue,*2
9. Huba na yangu mapenzi ntakupa utosheke,
10. Sina mapenzi ya wizi mwenzangu nitumie,*2
11. Na mimi nitakuenzi,raha zote nikupatie habibi,
12. Ziwashe simulizi wambea,nimeshakupenda wajue,*2 Wewe forever.
13. Sifikirii mimi, sifikirii karaha,
14. Nimezichoka amini, nimechoka nilikotoka,
15. Kwako nataka mimi, kwako ninataka raha,
16. Niyasahau maisha na karaha zilizopita*2
17. Mpaka nimekuchagua, ujue umenishika,
18. Kamwe sitokusumbua, kwangu huwezi kujuta,*2
19. Nafasi nakupatia, ujue kuitumia,
20. Wengi wananililia, wewe nimekuchagua*2
21. Funga mkanda hani, tumeingia vitani,
22. Yapasa kuwa makini, binadamu wafitini,*2
23. Watakayosema hani, sisi tuachane nao,
24. Watakayo sema fabi, na kimpango wao*2
25. *(Wanamuita Ally B, mwarabu wa Dubai*2,we black beauty.Tunasema huu ni buchi, sio njaa.)*
26. Tulopendana ni sisi, nini kinawasumbua,
27. Acheni chuki binafsi, majungu kutuwekea,*2
28. Mimi nishampenda, nayeye amenipenda,
29. Tena nimemganda,naye ameniganda,*2
30. Tulopendana ni sisi, nini kinawasumbua,
31. Acheni chuki binafsi, majungu kutuwekea,*2
32. Kwa mahaba alonayo, sijui kama nitamwacha,
33. Mapenzi anipeayo, sifikirii kumwacha*2
34. Tulopendana ni sisi, nini kinawasumbua,
35. Acheni chuki binafsi, majungu kutuwekea,*2
36. (Najua mtasema, lakini itafika wakati mtanyamaza.Utakubali ndugu yangu kimoyomoyo. Tunacheza wote. Kila mmoja).
37. Cheza *4 tara dansi,*3
38. Lasema na wanafiki msikie,
39. Watu wakishapendana mtulie,
40. Acha hani acha bebi wewe,
41. Walimwengu tuwazoe mam,
42. Tena sitaki maneno kwetu sie,
43. Fanyeni yenu ya kwetu mtuachie,
44. Nyamaza bebi nyamaza hani wangu,
45. Wacha waseme yote wawezayo,
46. Chukua*3, yote yako,*3
47. (Ai jamaa, Chukua yote yako. Apana kubali mwenzako. Nipe.
48. Jua kwetu limeshachomoza, mie leo naeleza,
49. Kutufitini hamtoweza, wenyewe tumeshapendana,
50. Wambea wambea mkae pembeni.
51. Mi nafunguka nishakupenda, nitakupa unachokipenda,
52. Hutopata tena kidogo, tuombe Mungu atupe kinga,
53. Wambea wambea mkae pembeni.
54. Mama kaniita, baba kaniita,wanataka wanipe wosia mamayo,Nenda upate,
55. Duniani kuna majanga ya kila aina ngoja, Nenda upate*2
56. Wanasema nisiwe mjuaji, kila jambo nilishikie bango,
57. Anayejifanya mjuaji, mimi niachane naye,

58. Niepuka vishawishi,kauli njema iwe silaha kwangu,*2
59. (kauli ya mzazi haipingwi na mja. Mapenzi ya kweli hayana kificho. Wakali wa Soweto, mumepitishwa na jamii.Hapana chezea Soweto.

28-FK

Funga Kazi-Machupas Family

1. Kwa vile na gumo, kusikiliza na mitihani,
2. Kajishuku yumo, jiwe karusha gizani,*2
3. Koma kukashifu wenzako, na wewe hujatimia,
4. Jichunge mdomo wako, utakuweka pabaya,*2

5. Na sisi tuna ya kwako,kosa kazi unatarajia,
6. Hupendezi kisonoko, vishindio ukivaa,*2
7. Tena shukuru wazungu kwa kuleta hayo ukashonea,
8. Ukingoja ndugu yangu kwa hicho kichwa cha boti,watu tungekumbia,*2

9. Hii ni meseji senti, fikie mwafulani,
10. Kinyago wa skauti, alovamia mjini,*2
11. Ni kweli sikutimia, ila sikuzidi wewe,
12. Unachekwa na mamia, unajisifu mwenyewe,*2

13. Hii Sasa funga kazi, nimekuamulia,
14. Baya sitolihifadhi ulilonifanyia,*2
15. Umekuwa boda boda, hata huku kaa,
16. Dunia utaiaga, ukimwi unauwa.*2
17. Unajifua Magamba, uonekane msafi,
18. Asili yako ushamba, shetwani mjaa nuksi.*2
19. Utaburuza hao washamba,ulopanda nao basi,
20. Nilimfunga mkanda, kwenye ndege bila wasi*2

21. Hii Sasa funga kazi, sitakuachia,
22. Kupigana niko radhi, vita najiua,*2
23. Umegeuka kisoda, unalala baa,
24. Walevi wanakukanyaga, tunakushanga*2

25. Na kama nimekukera, hama mji katafute hifadhi,
26. Hii nnyiponza subira,ili wewe upate mtaji,*2
27. Kusudi haina pole, nawe pokea ya kwako,
28. Umegeuka nguruwe, kujikaanga kwa mafuta yako*2

29. Hii Sasa funga kazi, nimejiandaa,
30. Ziko wapi zako pozi, acha kujiashua*2
31. Bibi umekuwa hoja, unakwanguniwa,
32. Wakubwa na waso na rika, wanakununua*2
33. (Hapo, we mchai karaba jianda kuchomolewa mwiba.Malope Hapo sasa.Mzee wa kifimbo cheza,charaza bakora)

34. Unatushangaza sana, kama uso na riziki,
35. Kila kona na mabwana na riziki haupati,
36. Unajipachika vyeo, mwenzetu haueleweki,
37. Ofisi yako haiyo, unalenga kwa manati.
38. Waki savu maini hutozoea,
39. Nenda mvimba mashavu, mshamba hujabobea*2
40. Hauwezi kula mbivu, sababu hukuzoea,
41. Unatushangaza sana, kama uso na riziki,
42. Kila kona na mabwana na riziki haupati,

43. Hata ukija na panga, jua mpingo hukati,
44. Bure kwangu ukiwaka, katu la mungu hufutii,
45. Kama vaze kanga, casino huna nafasi,
46. Unajipachika vyeo, mwenzetu haueleweki,
47. Ofisi yako haiyo, unalenga kwa manati.

48. Utazimaliza ngoma zako na ziso zako,
49. Hazitoacha kusema, bahati yangu siyo yako,*2
50. Ukicheza tukunyema, mi nacheza kwainto,
51. Unatushangaza sana, kama uso na riziki,
52. Kila kona na mabwana na riziki haupati,

53. Mapacha, mpango mzima*3
 54. Rahma Machupa mapacha, mpango mzima,
 55. Zainabu Machupa mapacha, mpango mzima,
 56. Ashura Machupa mapacha, mpango mzima,
 57. (Utalala hoi.sasa)
 58. Hajatulua huyo, huyu demu mapepe,
 59. Amefulia huyo, kiasi tumchenge,*2
 60. (Ala, hii kweli funga kazi)

29-KM

Kazi Mnayo-Mohamed Ally

- 21 Haiui nyoka fimbo ya mbali,usemi wa mababu zetu,*2
 22 Bure mtachonga wafedhuli,kufuatilia penzi letu,
 23 Tatizo tunapendana, vigumu sumu kupita,
 24 Pia kuvumiliana, heshima twaitafuta.
 25 Mie si maproso kutalazia mali zangu,
 26 Katu sikuona so, kumwambia hali yangu,*2
 27 Ndio maana mtoto shoo, yuko mikononi mwangu,
 28 Bure kuumia roho, kuwa na chuki dhidi yangu.*2
 29 Ushindi wenu ni roho, mkija uwanjani kwangu,
 30 Na mapigo ya kileo, habanduki mpenzi wangu,*2
 31 Sumu ya penzi maudhi, sie hatuudhiani,
 32 Au kumwacha siko radhi, na yeye wala sidhani*2
 33 Imepanda yetu hadhi, hebu tuangalieni,
 34 Ndo maana tumelihali, wapambe mbali kaeni,*2
 35 Roho zikikuumeni, nyie njama fanyeni,
 36 Ila kwetu tambueni,kazi takupateni*2
 37 Ni choyo tu, na roho mbaya zenu,
 38 Ni usta tu, kunichukia mwenzenu,
 39 Ila kazi mnayo,ya kutugonganisha,
 40 Ila kazi mnayo,mbinu zote mtazisha.
 41 Mkitaka mistake jahazi iko juu,*3
 42 [walikuwa hawajui. Kisoda.]
 43 Wenu presha juu, wetu raha tu,
 44 Hatutoachana hata mtupige vita,
 45 Hatutotengana hata mtupige visa,*2
 46 [Fatha Mauji, mkono wa dhahabu daktari wa meno,mwaga sumu.]
 Kwa chuki zao, watajibeba wao watajibeba,
 Siku ya leo, watajibeba wao watajibeba,
 47 Na wanune, na wanune sana,
 48 Na wavimbe, hatutoachana sie,*2
 49 Waseme mcha na usiku watalala na usiku*2
 50 Wapo waliogombana, ikisha wakapatana,
 51 Wapo waliopigana, mikono wakapeana,*2
 52 Na ugomvi utakwisha, rahasana*3
 53 [Asante sana fatha Mauji,safisha jiji baba limejaa chafu.]
 54 Wote walo nuna, na wanune na wanune,
 55 Wenye wivu wajinyonge, wajinyonge,
 56 Na walovimba wapasuke wapasuke,*2

30-TIT

Top In Town-Khadija Kopa

2. Top*2 in town, mama wa madoidoni,
3. bado yuko uwanjani,*2
4. Wasaka wako hoi, hawajui wafanye nini,
5. Amewatoa nishani ,wako hoi taabani.*2

6. Anatambisha Tanga, chezsha mchaka mchaka*2
7. Yu alopewa kipaji kwa uwezo wa Rabuka,
8. Kawasha taa kwa maji na utambi na ushawaka

9. Eeeyeya mama wa kitanzania bado niko uwanjani
10. Ndiyo mimi mama wa kizanzibari, maskini naaja
11. Ssh, mtoto wa kidonge, niacheni nilonge
12. Ssh kazaliwa Makadara, nimesimama imara

13. Mama wa kualila tu na simdharau mtu
14. Mi hiyo ndo hulka yangu mimi napenda utu
15. Mama wa viunit niko gado niko fiti
16. Kimama mkula kinondoni kimala masala mjini
17. Basi dubliketi maperesheni hupiga saluti
18. Kichuna wa Kizaramu nisyekwisha utamu

19. Sweety wa Mwananyamala hekoti amekwara
20. Sweety wa Mwananyamala wewe unasema nini
21. Mtasema usiku mtalala na bwana niko naye ndani
22. Tena na heshima sjarura bado naitwa queeni

23. Mimi top in town ooh
24. Asiyenijua nani ooh
25. Tena nawapagawisha ooh
26. Afrika na Marekani ooh

27. Mimi top in town ooh
28. Asiyenijua nani ooh
29. Na nimewacha gunzo ooh
30. Comoro na huko London ooh

31. Kiitikio,
32. Nimebahatika Mungu amenipa nuru mie
33. Hata mkitaka hamwezi kunidhuru mie
34. Hamwezi kunivua joho alonipa Mungu
35. Mwenzenu nimeshapewa wacheni yenu majungu

36. Si mwengine top in town
37. Top in town*2
38. Top top top,
39. Top in town*2

40. Hei hei hei mi sigombe mwanamume nikajita mashaka
41. Mwanamke najiamini nipatacho naridhika
42. Sh namrusha roho nani una nini wewe msaka
43. He na maziwa ya Kichina juu umeyapandisha

44. Mimi nikikuachia ujue nimemchoka
45. Na kam ni msTaarabuu ujue sitobanduka
46. Na hasa awe muugwana rohoni anoridhika

47. Ela mimi sipendi taabu wala sitaki mashaka
48. Wameshushwa kwa vitabu chagua unoridhika
49. Nampenda tabibu mwenye vitu vya uhakika
50. Sitaki teksi bubu polisi wakanishika

51. Nasajili bila taabu ooh
52. Gari lenye uhakika ooh
53. Gegi yangu si mbovu ooh
54. Leseni nimeshakata ooh

55. Nimekoshewa wanukanuka jasho lako likanuka

56. Wala sijakoshewa mkaratusi nikafuliwa matusi
57. Nimekoshewa mpenda fedha mie
58. Mambo yangu hamtayaweza mie
59. Tena na chenji ikabaki mie
60. Watoto yatima wakapewa mie
61. Si mwengine top in town
62. Top in town*2
63. Top top top,
64. Top in town*2
65. (Mazungumzo) *Watoto mmesema sana, gari kubwa linakuja sasa, lipisheni njia,pisha njia pisha njia).*
66. Kiitikio,
67. Nasema toti kimeo mbona mnacheza*3
68. Sasa nawapa usia kina dada msikie
69. Sasa nawapa usia mpendapo mtazame
70. Wengine si wanaume wengine magumegume
71. Rusha roho taratibu tena nyuma utazame
72. Huyo unomkanyaga ndiyo anokuchukulia mume
73. Shuka zako azijua ndani kwako ziko nne
74. Tena mfanyakazi wako ukitoka pakashume
75. Tena alala kitanda chako mumeo ana umeme
76. Kiitikio,
a. Si wanaume magumegume
77. (wengine) Si wanaume magumegume
78. (wengine) Si wanaume magumegume
79. (wengine) Si wanawake makwekwerekwe
80. (wengine) Si wanawake makwekwerekwe
81. (Achukua ndugu zako) Si wanawake makwekwerekwe
82. (Amsomba bosi wako) Si wanawake makwekwerekwe
83. (Akugombanisha na ndugu zako) Si wanaume magumegume
84. Si wanaume wana umeme
85. Timbwiri timbwiri na shamberere*4
86. Dereva akifanya polepole mkono na paja*2
87. Shika sukani yako polepole mkono na paja
88. Dere akisogea kwa huku polepole mkono na paja
89. Dereva akifanya leo polepole mkono na paja
90. Zingatia yako sukani polepole mkono na paja
91. Mume wangu yu karibu hapo polepole mkono na paja
92. Sijaleta sokomoko polepole mkono na paja
93. Tucheze kisomoka jamaa do! Haya jama
94. Kama hutaki ondoka jamaa do! Haya jama
95. Sasa hutoki ndani jamaa do! Haya jama
96. Mpenzi wako yu ndani jamaa do! Haya jama
97. Hapa ndiyo uwanjani jamaa do! Haya jama
98. Dada usiwe kaniki jamaa do! Haya jama
99. Mapenzi yako ya wigi jamaa do! Haya jama
100. Mume wangu hakutaki jamaa do! Haya jama.
101. Nimelipanda basi jamaa do! Haya jama
102. Mpaka Bagamoyo jamaa do! Haya jama.
103. Nimeubwaga wangu moyo jamaa do! Haya jama
104. Nawe bwaga wako moyo jamaa do! Haya jama.
104.(Mazungumzo; uzuri wa ndege manyoya, uzuri wa mwanamke kujiamini bwana. Mwanamke screensaver bavu la nyoka makalio yanafuata baadaye)

31-TW-Tenda Wema-

14. Eh mwana koibananga kurila,
15. Mwana mdodo bwe, Eh mwana koibananga kurila,

16. Lia chungu bwe, Eh mwana koibananga kurila,
17. Alialia bwe, mwanangu mdodo bwe,
18. Eh mwana koibananga kulira,

19. Nyanya chungu na bamia, mimi ndio mboga yangu,
20. Masikini si kilema, mimi ndiyo jadi yangu.
21. Eh mwana koibananga kulira. Lia mwana bwe,
22. Eh mwana koibananga kulira,

23. Sangu mama kisangu, hata ukitia nazi,
24. Binadamu habebeki, kama mzigo wa mwizi.
25. Eh mwana koibananga kulira. mwana mdogo bwe,
26. Eh mwana koibananga kulira, Alia mwana bwe.

27. Ah wema huo, Ah wema huo,
28. Tenda wema uende zako, usingoje shukurani,
29. Itafika muda wako , Utalipwa na manani.

30. Ninawapa notice, mwisho wenu ndio leo,
31. Munajitia nuksi, roho zenu zina choyo.
32. Sibadili sibatili wema wangu, sibatili wema wangu ndio dini.

33. Nawatendea wema, mnatengeneza,
34. Naichapa salama, sibatili ishari,

35. Nimerudi mimi ndiye mama lao,
36. wale wazushi wakome umbea wao,
37. Wala mimi sitishiki kwa hivyo vitisho vyao,
38. Na wala sitetereki, nazijua njama zao.

39. Kama mimi nina dhiki, wenye uwezo ndo wao,
40. Mniacheni sasa bibi, mnanikalia mwao.
41. Mnanijengea chuki, nifanyalo si jema kwao,
42. Mkome mimi sitaki, Nawaba la aibu leo.

43. Kibanda changu, ghorofa mnazo nyie,
44. Chakula changu, siwaombi msinizulie,
45. Kuniwekea viao, vya kunijadili mie,
46. Waso haya wana mji wao, jirani zao ni nyie.

47. Na funguo ya riziki, mungekuwa nayo nyie,
48. Mimi ningepata dhiki, singepata kitu mie,
49. Ninamuomba Razaki, mema anijalie,
50. Mpaka siku ya haki, baraka nizidishiwe.

51. Sitaki sitaki maneno yenu, sitaki,
52. Sitaki sitaki hasada zenu, sitaki,
53. Mnajipa dhiki kwa maongezi yenu, sitaki.

54. Malewa, malewa male tucheze malewa,
55. Male, malewa, male tucheze malewa.
56. Mja wa heri, hulipwa heri,
57. Mja wa shari, hatumlipi shari.

58. We nenda tu, ukae ukifikiri,
59. Ukumbuke Mungu wako akuondolee shari.
60. Nasi tunakuomba Mungu atakustiri,
61. Uzidi kuendelea akuepushe nari.

62. Magemba ge, magemba ge, sema baba

32-SS

SITAKI SHARI-LEYLA RASHID

1. Nimejua azma yako, azma yako wanitafuta shari,
2. We zifanye njaro zako, hutanipandisha mori,
3. Vitoka na kejeli zako, nitakuonyesha biasharieuri,

4. Ntakupandisha ntakushusha, natkutia ndani ya dustbin.
5. Chonga uchongavyo jidomo lifike kule,
6. Bwatuka ubwatukavyo mi maisha yaenda mbele,*2
7. Ropoka ovyo uwe mstari wa mbele, mie sikuogowi,
8. Fanya ndaro ufanyavyo zijae gunia tele,naapa sikukohoi,*2

9. Jokonoa uwezavyo, unitoneshie upele,
10. Wala riziki huondoi, mi nakuona ovyo,
11. Una janzanzi tele, sauti yangu siitoi,*2
12. Wewe chokonoa sana, mori hutanipandisha,
13. Ugomvi siko tayari,
14. Ukinitibua sana nitakupandisha ntakushusha,
15. Sana sana ntakunyari,*2

16. Funguka tukana sana, mzuka hutonipandisha,
17. Sina makolea shari, bwatuka bwatuka sana,
18. Nia hutoiondosha, natumaini kahari,*2

19. Mie shari na hasama, baadam sivitaki,
20. Kichwa chini nainama, yupo hakimumu wa haki,*2

21. Nimezaliwa na mama, sijatokea shinani,
22. Siendekezi hasama, tunapita dunia*
23. Sitaki sitaki shari, sione nimetulia,
24. Sitaki sitaki shari, ugomvi sikuzoea,*2

25. [We hani we, naumiza roho yangu.I love you nyang'a nyang'a. Hili ndilo jahazi tulishusha kaze.Haya sasa.]

26. Sitaki sitaki, maneno na wewe,
27. Sitaki sitaki, ugomvi na wewe,
28. Sitaki sitaki, ukali wa mwao,

29. Nimefunzwa nimefunzika, dunia nyumba ya shari,
30. Mabaya kuyaepuka,niishi na watu vizuri.*2
31. Wewe bure neng'eneka, kubwa langu kukunyari,

32. Ukitaka kuishi vizuri, kwanza nenda na wakati,
33. Usabasi na ushari, umepitwa na wakati,*2